

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 13Agosti, 2011

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Nishati na Madini

(Majadiliano yanaendelea)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. KISYERI W. CHAMBIRI: Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni zaidi ya miaka kumi, umeme umepita katika maeneo ya Maweni, Majengo, Mukuyuni A, Mukuyuni B, Ari Halaa, Singu, Signo. Umeme huo ni wa msongo wa KV 33. Hakuna juhudzi zozote zimefanywa kuwapatia wananchi umeme katika maeneo hayo. Nataka kufahamu lini wananchi wa maeneo hayo watapatiwa umeme?

Mheshimiwa Spika, pili, katika bajeti ya *TANESCO* ya mwaka huu, fedha zimetengwa kupeleka umeme mtaa wa Muruki, Babati Mjini. Meneja wa Mkoa amekataa kupeleka umeme Muruki kwa kisingizio kuwa hakuna njia. Halmashauri ya Mji wameandika barua *TANESCO* na kuthibitisha njia ipo. Lini wananchi wa Muruki watapata umeme?

Mheshimiwa Spika, tatu, ingawa tayari wameleta nguzo kwa ajili ya umeme Mamagha, Banga, Himiti, Haraa, hoja sasa ni muda mrefu sana, lini umeme utawekwa katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, nne, muda mrefu sasa tumeomba umeme upelekwe Vijiji vya Imbilili, Mtuka, Malangi na Kiongozi. Lini maeneo hayo yatawekwa katika mpango na kupelekewa umeme?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hoja hizo hapo juu, nimeomba Meneja wa Mkoa atayarishie makisio ya maeneo hayo kupata umeme. Naomba ahimizwe kufanya kazi hiyo.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri yenye matumaini "kimipango" katika kutatua matatizo ya umeme. Miradi yote ya umeme alioitaja katika hotuba yake itachukua muda. Katika miaka mitatu ijayo, matatizo haya yatapungua. Kinachotakiwa kufanya ni kuwa na timu ya ufuutiliaji wa miradi hiyo. Bajeti hii

ikipita, tunaanza mchakato wa bajeti mpya ya 2012/2013, inabidi Wizara ijipange katika kutekeleza miradi yake ambayo ni mingi na ya thamani kubwa.

Mheshimiwa Spika, umeme wa maji, ili kuweza kutoa nafuu ya bei ya umeme, ni vema tukaendelea kutumia umeme wa maji ili ku-*balance tariff* kwa umeme wa *gas na thermal* lakini hili linahitaji *TANESCO* kusaidia katika kutunza vyanzo nya maji. Maji ni malighafi muhimu kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme vijiji. Asilimia 80 ya Watanzania wanaishi Vijiji ambapo uzalishaji unafanyika. Fedha zinazotengwa katika *Rural Energy* ni ndogo na kwa bajeti hiyo halitawenza kuleta umeme Vijiji kwa haraka. Katika bajeti ya mwakani, ni lazima *REA* ipatiwe bajeti ya kutosha ili kumaliza matatizo ya umeme Vijiji hasa kwa miradi ambayo mwaka huu haikutengewa fedha kama miradi ya Mkwaja – Mkalamo ya Wilaya Pangani. Hii itapunguza manung'unko ya Waheshimiwa Wabunge ambapo mwaka huu hatukupata miradi hata mmoja.

Mheshimiwa Spika, madini, hapa kuna tatizo hasa katika kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika na madini yao. Ni vyema kuhakikisha kwamba makampuni makubwa ya madini yanatekeleza *corporate social responsibility* kwa wananchi kama maji, shule na zahanati.

Mheshimiwa Spika, Sheria, kwa vile nchi yetu imepata madini ya *uranium*, ni vyema kukawepo na Sheria kuhusu uchimbaji wa *uranium* ambapo ni madini mapya yanayotawaliwa Kimataifa. Ni vizuri tukajifunza toka nchi kama Namibia na Malawi ambao tayari wana sheria nzuri tu kuhusu *uranium*. Sheria hiyo iletwe haraka Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mafuta, ni lazima Sheria ya Mafuta ikaletwa hapa Bungeni. Nchi ya Saudi Arabia na za Gulf zina Sheria Maalum ya Mafuta, si vizuri suala hili likabakia katika Sheria Mpya ya Madini. Sasa ni wakati wa kuwa na Sheria *specific tusiwaachie TPDC* peke kusimamia Sheria hii.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia 100/100.

Mheshimiwa Spika, nianze na Madini ya Chumvi. Madini ya Chumvi huchimbwa Mikoa 10 nchini Tanzania ambayo ni Lindi, Mtwara, Tanga, Pwani, Dodoma, Shinyanga, Singida, Mbeya, Dar es Salaam, Zanzibar na Ukanda wa Pwani. Chumvi ni madini hafifu sana katika madini yote nchini, hupata matatizo sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma, wasiitoze tozo kama madini ya dhahabu au almasi. Madini ya chumvi yanakumbwa na matatizo 12 yafuatayo:-

(1) Haina soko na ikipata soko haina bei, ni shilingi 1,200/= mpaka shilingi 1,500/= kwa kilo 50.

(2) Serikali iliongeza mzigo mbiti kwa wakulima kwa kuwataka wakulima hao waweke madini joto kwa faida ya wananchi. Serikali ilitumia madini ya chumvi kuweka *Iodine* (Madini Joto) ili wananchi wengi watumie *Iodine* kupitia chumvi baada ya kuona kuwa wanadamu wengi Tanzania wana upungufu wa *Iodine* mwilini, kuweka Madini Joto katika chumvi ni mzigo sana kwa mkulima. Tunaomba madini haya na mabomba yake yatolewe bure. Chumvi inaweza kuliwa bila madini joto, hili liangaliwe upya. Serikali itoe Madini Joto kwa wakulima wa chumvi.

(3) Mzalishaji wa chumvi anatakiwa kodi ya Wizara ya Madini na Nishati kila mwaka. Anatakiwa aliye ushuru wa Maliasili kwa ajili ya mikoko ya shilingi 80,000/= kila mwaka kwa hektaki 2.5 hata kama hatumii eneo lote alilopewa.

(4) Anatakiwa aliye mrahaba wa asilimia tatu (3%) ya bei ya chumvi atakayouza.

(5) Anatakiwa aliye ushuru wa shilingi 50,000/= kwa kila pakti ya kilo 50.

(6) Mkulima wa chumvi anatakiwa aweke Madini Joto ambayo huuzwa shilingi 30,000/= kwa kilo na huweka pakti 320 tu. Gharama hii huibeba mkulima kwa niaba ya wananchi wanaokula chumvi.

(7) Kila mwaka anatakiwa afanye usajili kwa shilingi 200,000.

(8) Anatakiwa awe na zana za kuchimbia madini.

(9) Haijulikani ni wa Wizara ya Kilimo, Afya, Madini au Maliasili, wote wanadai kodi. Chambueni upya yupi ni yupi.

Mheshimiwa Spika, katika suala la chumvi, tunaomba yafuatayo yatekelezwe:-

(i) Serikali igawe bure Madini Joto kwa wakulima wa chumvi kwani zoezi la kuweka Madini Joto ni zoezi la Serikali baada ya kuona kuwa watu wengi hawana Madini Joto katika mili yao. Chumvi unawenza kula bila Madini Joto, hivyo zoezi la kula Madini Joto litapungua ila watu wanawenza kuumwa magonjwa 100 kwa kutokula madini joto. Kwa hiyo Madini Joto ni muhimu.

(ii) Serikali iondoe baadhi ya tozo ya kila mwaka angalu itoze tozo mara moja tu. Angalieni suala la tozo.

(iii) Wapewe pembejeo bure.

(iv) Kuwe na Bodi ya Chumvi.

(v) Tusaidiwe Kiwanda cha Kusaga Chumvi Lindi.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la soko ya zao hili la chumvi kwa sababu mwekezaji wa aliyenunua Kiwanda cha Karatasi Mgogolo ananunua chumvi kutoka nje badala ya kununua chumvi Tanzania. Zamani chumvi yote ilikuwa ikinunuliwa na Kiwanda cha Mgololo, sasa chumvi yote ipo tu haina soko. Chumvi za kula zinatoka Mombasa, tunataka aliyekeza Mgololo anunue chumvi Tanzania pia tunataka soko la chumvi.

Mheshimiwa Spika, madini ya gesi. Tutaka Vijiji vinavyopitisha bomba la gesi vipewe umeme. Vijiji hivyo ni Miteja, Njenga, Mkwanyule, Mpara, Nyamwage na Kilwa Kisiwani.

Mheshimiwa Spika, madini. Katika Wilaya 93 zilizotajwa kuwa zina madini, Wilaya ya Ruangwa haikutajwa kama ina madini hivyo kutotambuliwa na Serikali. Kwa taarifa Ruangwa kuna madini ya *Green Garnet*, *Green Tourmalines*, Dhahabu, *Blue Safaya*, Marakati na rangi za kupaka nyumba. Kwa hiyo, Ruangwa pia wasaidiwe nyenzo za kufanya, wapimiwe viwanja, wafanyiwe upembizi na pia watambuliwe na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa 100/100.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nashukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kunijalia Afya njema na kunipa uwezo wa kuchangia machache katika Wizara hii kwa maendeleo ya nchi yetu na watu wake.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu sahihi zinaonyesha mgao wa umeme umeanza muda mrefu sana nchini toka mwaka 1992 mpaka sasa ni takriban miaka 20. Ni wazi kuwa Serikali haiko makini na haina dhamira ya kweli ya kutatua tatizo la nishati kwa ujumla wake. Mahitaji ya umeme nchini ni 1200 MW na vyanzo vyote 10 vinavyotegemewa kutoa umeme vinazalisha 818 MW tu na hata hizo 818 hazipatikani! Ni dhahiri kabisa Serikali haina dhamira ya dhati kumaliza tatizo la nishati ya umeme kwani miaka 20 ya tatizo hili ni mingi sana. Serikali haiko makini hata kidogo! Badala ya kuchukua hatua madhubuti kumaliza tatizo, Serikali inaingiza siasa na kulifanya mzaha tatizo pale Waziri anapotoa kauli kuwa "umeme utakuwa historia kabla ya 2010". Waziri au Serikali inatoa kauli hiyo kimzaha mzaha bila ya kusikiliza ushauri wa wataalam, kutokuwa na sera na nia njema ya kutatua tatizo na kutopanga bajeti ya kutosha/kutafuta mwekezaji makini. Badala yake

Taifa linabebeshwa mzigo wa umaskini zaidi kwa watu wake kutokana na mkataba mibovu ya uwekezaji katika nishati ya umeme kama ya *DOWANS*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tafiti mbalimbali kuonyesha kuwa nchi yetu ina vyanzo vingi vyta umeme vikiwemo vya maji kama Ruhudji -358 MW, Ruwakali - 222 MW, Stieglers Gorge- 1200 MW, Masigira - 118 MW, Mpanga - 114 MW, Kakumo-58 MW, Malagarasi-20 MW. Julmla ni 2085 MW.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya umeme wa gesi. Mnazi Bay - 300 MW na Kinyerezi- 240 MW. Jumla 540 MW.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya umeme wa makaa ya mawe. Mchuchuma - 600 MW na Kiwira - 400 MW. Jumla 1000 MW.

Mheshimiwa Spika, pia kuna vyanzo vingi vyta kuzalisha umeme wa upopo vikiwemo vya Singida na Makumbuko.

Mheshimiwa Spika, Serikali haiko makini na haina dhamira, nia wala adhma ya dhati ya kutatua kero na adha ya nishati ya umeme ili kuwapunguzia umaskini wananchi wetu na kulifanya Taifa lisonge mbele kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, wakati sasa umefika Serikali kubadilika, mikataba ya madini irekebishwe ili wananchi wanufaikie na rasilimali zao walizojaliwa na Mwenyezi Mungu anayewapenda sana Watanzania. Majuto ni Mjukuu, tuisubiri kuja kujuta hapo badaye, watoto wetu watatuombea laana kutoka kwa Mwenyezi Mungu ikiwa hatutawatendea haki ya kupata manufaa ya madini yao.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini hasa dhahabu hapa nchini ni wa gharama nafuu zaidi ukilinganisha na nchi kama Angola lakini Angola pamoja na kuwa gharama ya uchimbaji ni kubwa, Serikali ya Angola inapata hadi 30% ya dhahabu inayochimbwa huko. Ni jambo la aibu na fedheha kwa rasilimali watu tuliyonayo kuyaachia madini yetu yakichukuliwa kiholela na sisi tukiachiwa ucharibifu mkubwa wa mazingira. Ushauri wangu mikataba ya madini irekebishwe haraka sana na Serikali ipate angalau asilimia 20% ya faida inayopatikana kutokana na uzalishaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, nawaomba kuwasilisha.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, ukosefu wa umeme wa kutosha ni janga linaloturudisha nyuma na kutafuna mafanikio yote tuliyopata tangu uhuru.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* igawanywe mara tatu na kuWE na Mamlaka tatu tofauti na zinazojitegemea za Uzalishaji umeme, *Transmission and Distribution*.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya umeme na jukumu la uzalishaji vikabidhiwe JWTZ wavilinde, wasimamie na kuondoa hujuma kwenye vyanzo vya nishati.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyoweza kutoa ufanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusiana na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kuomba maelezo juu ya ratiba kamili ya lini Wilaya Mpya na Jimbo la Mbogwe itapatiwa umeme wa uhakika kuitia mradi wa *Electricity (V)* unaofadhiliwa na Benki ya Afrika kutokea eneo la Bulyanhulu (Kahama Mine) kuitia Vijiji vya Lunguya, Ushirika, Mbogwe, Nanda, Kagwe, Bukombe, Lubeho, Masumbwe, Mzambarauni, Cagil Ginnery, Nyakafuru, Kakumbi na Lugunga.

Aidha, naomba Wakala wa Usambazaji wa Nishati ya umeme Vijijiini (*REA*) iweke katika mpango wake kuweka umeme katika maeneo ya Vijiji vya Iboya, Nambubi, Bwendanseko, Ilolangula, Bugalagala, Kashelo na Lulembela. Mheshimiwa Waziri, tunaomba umeme.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapokuwa katika dharura tuliyomo kwa sasa, Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha tunaondokana na tatizo hili ambalo linaigharimu nchi yetu hasa katika sekta ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme ndiyo *engine* ya ukuaji wa uchumi, imani yetu watu wa Jimbo la Mbogwe tutapiga hatua kimaendeleo endapo Wilaya yetu itapatiwa umeme. Hatua hii itavutia wawekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo vinu vya kuchambulia pamba, ukoboaji wa nafaka na kwa matumizi ya nyumbani. Umeme kwa kifupi ni ukombozi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imepata neema ya kuwa na madini ya aina mbalimbali yakiwemo Makaa ya Mawe, upopo na nguvu ya jua, hivi vinaweza kuwa vyanzo vya uhakika vya umeme au nishati. Kwa mara nyingine nchi yetu imejaliwa kupata gesi na madini ya *uranium* ambayo pia yanaweza kuwa chanzo cha uhakika cha umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa rasilimali ya madini, nashauri nchi yetu isifanywe kuwa ya watu wasiojua thamani ya utajiri wa madini. Kwa mantiki hiyo, naomba Serikali ifikirie kwa makini juu ya uwezekano wa kushiriki kikamilifu kuwekeza katika sekta hii muhimu kwa kupitia Shirika la Madini la Taifa *STAMICO*.

Mheshimiwa Spika, tutazame sasa ni kwa jinsi gani sheria zinavyoweza kurekebishwa na kuhakikisha Serikali yetu inakuwa na hisa na kumiliki migodi mikubwa nchini na kwa migodi ambayo tayari inafanya kazi ambayo ni *Geita Gold Mine, Resolute Golden Pride, North Mara, Tulawaka, Buzwagi na Kahama Mine* pindi muda wake wa mkataba kama ni miaka ishirini na tano (25) basi muda wa mkataba unaofuata Serikali ipate hisa za kutosha. Nasema haya kwa kuangalia Mataifa ya Kiafrika kama vile Afrika Kusini, mgodi wa Johannesburg na mgodi wa Obwasi huko nchini Ghana, uchimbaji wao dhahabu umekuwa ukiendelea kwa zaidi ya miaka mia moja. Kwa mantiki hiyo, upo uwezekano wa uchimbaji wa madini ya dhahabu ukaendelea kwa miaka mingi ya uchimbaji wa dhahabu nchini mwetu. Nchi yetu ni tajiri jamani utajiri wa rasilimali ya madini utumike kuujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, napenda nianze kuunga mkono hoja na kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini, ni moja ya Wizara yenye changamoto kubwa sana na inapaswa itende haki kwa kuzingatia kwamba maendeleo yanapaswa kwenda kwa uwiano ulio sawa kwa Mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, napata tabu sana kwamba je ni kweli Mheshimiwa Waziri hajui kwamba katika nchi ya Tanzania kuna Mikoa ya pembezoni ambayo kutokana na *geographical allocation*, Mikoa hii imekuwa *disadvantaged* na hivyo kuwa nyuma kimaendeleo katika nyanja zote kwani hakuna mtumishi hata mmoja ambaye yuko tayari kwenda kufanya kazi maeneo ya giza.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa sana nashindwa kuelewa kwamba imekuwaje Wizara hii imeshindwa kuelewa jinsi ambavyo Mkoa wa Rukwa hususan katika Jimbo na Wilaya Mpya ya Kalambo hakuna hata Kata moja kati ya jumla ya Kata kumi na saba (17) ambazo zimepewa umeme na ukizingatia Makao Makuu ya Wilaya Mpya, Mji Mdogo wa Matai na Mji Mdogo wa Kasanga kuna kazi nzuri ya upanuzi wa bandari ya Kasanga na ujenzi wa soko la kimataifa la samaki. Nashindwa kuelewa ni jinsi gani umaana wa bandari na soko la kimataifa la samaki vitawenza kufanya kazi bila ya umeme.

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini vipi Wilaya Mpya ya Kalambo tutaendelea kulinda nyaya za umeme zikipita kwetu kwenda Sumbawanga Mjini na hali sisi tukiwa kwenye giza totoro.

Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba katika Jimbo langu la Kalambo yapo maporomoko ambayo ni ya pili kwa ukubwa Afrika na zaidi ya kuwa kututio cha watalii, Serikali ni vizuri ikatafuta namna ya kuweza kuzalisha umeme kwa ajili ya Wilaya ya Kalambo na Vijiji vya jirani vya Kasanga, Kisumba, Kituo cha Afya Ngorotwa, Mpombwe na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri azingatie haya katika majumuisho yake atoe majibu sahihi ya mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele ya Bunge hili. Hoja hii ni ya msingi sana kwani ndiyo nguzo pekee inayotoa fursa kubwa ya ajira na pato kubwa la Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, suala la wachimbaji wadogowadogo limekuwa jambo ambalo utekelezaji wake umekuwa wa ahadi pasipo utekelezaji. Leo hii vijana wetu wengi wanaumizwa migodini kwa kupigwa risasi, kufukuzwa hovyo na wengine kupata ulemavu wa kudumu. Ukiangalia hali ya wanachi ilivyo na mazingira yao kwa ujumla hawafaidiki na migodi hii. Leo hii wananchi hawa ndio inaonekana wanavamia maeneo ya mgodi, suala la kujuliza hapa katи ya mwekezaji na mwananchi nani aliyekutwa kwenye eneo la machimbo?

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Biharamulo Magharibi kuna mgodi wa dhahabu wa Tulawaka, vijana wengi wameumizwa katika mgodi huu, vijana wengi wamepata ulemavu katika mgodi huu na hakuna ajira iliyosmi kwa vijana hawa. Hivi Serikali ilisaini vipi mikataba na hawa wawekezaji? Eneo hili hakuna eneo lilitengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogowadogo. Matokeo yake vijana hawa wanapojajiri kwa kuchekucha mchanga ambaa umeshatupwa, inaonekana vijana hawa wanavamia mgodi, hivi Serikali inawajali kweli wananchi wake au tafsiri ya neno migodi haieleweki? Niombi Serikali itenye eneo la wachimbaji wadogowadogo na wapewe nyenzo za kufanya kazi ili vijana hawa waweze kujajiri na wasibughudhiwe.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji hawa hawawatendei haki wananchi hususani wale wanaozunguka eneo la mradi. Leo hii maeneo haya bado shule hazina madawati, Zahanati zetu hazina vifaa vya kutosha, barabara bado ni mashaka sana. Hata mrahaba unaolipwa ndani ya Halmashauri hauonekani umefanya kazi gani, bado ni kiasi kidogo na hajulikani ni utaratibu gani unaotumika katika malipo haya. Niombi Wizara ya Nishati ya Madini waweke utaratibu wa kisheria na kuhakikisha kuwa katika mikataba yao iwe shirikishi kwa wananchi na izingatie utoaji wa huduma za jamii na vilevile ilenge kutoa nafasi za ajira kwa vijana wetu. Pale inapotokea wawekezaji wanapokiuka masharti haya na kunyanyasa wananchi basi hatua kali zichukuliwe dhidi yao na Serikali ilisimamie hilo.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara yenye matatizo makubwa ya kisheria, kisera na uongozi kwa sababu mbalimbali. Mimi kwa kutambua uwingi wa wachangiaji na uzito wa hoja zilizotolewa naona nichangie kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukubwa wa Wizara. Kama walivyoshauri wachangiaji wengine, naomba nishauri kwa Wizara hii igawanywe, Wizara ya Nishati pekee na Madini peke yake. Hii itarahisisha utoaji huduma. Ili kutoongeza ukubwa wa Serikali, Wizara nyingine ziunganishwe kama Kilimo na Maji iwe Wizara moja au elimu iwekwe pamoja.

Mheshimiwa Spika, hali mbaya ya umeme. Kwa vile tatizo limeshajulikana, iliyobaki ni kututia ufumbuzi (*solution*) ya muda mfupi, muda wa katи na muda mrefu. Hapa ndipo inapendekezwa kuundwa Kikosi Kazi (*Task force*) siyo Tume. Nashauri na kuisihi Serikali kukubali ushauri wa kuundwa Kikosi Kazi chenyе kuhusisha sekta binafsi kwani hii ni sera ya Serikali kupitia PPP, wadau wakiwemo wenye viwanda na mahotelii wako tayari.

Mheshimiwa Spika, matatizo kuhusu madini ni mikataba mibovu kuhusu uchimbaji Dhahabu na *Tanzanite*. Ili kutatua tatizo hili pamoja na Serikali kukosa malipo makubwa ya kodi kwa sababu ya madini kusafirishwa nchi za nje bila thamani yake kujulikana, nashauri mapendekezo yaliyoko kwenye Tume ya Mheshimiwa Jaji Bomani yatekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumzia *Gold Rash*, naomba wakati wa kujibu hoja za Wabunge, Mheshimiwa Waziri anieleze katika ruzuku ya Shs.2,978,330,000/= iliyopangiwa Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Mbulu imepangiwa kiasi gani na ni ya shughuli gani? Fedha za Mradi wa Umeme wa Haydo-Maghang ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, *Gold Rash*. Mwaka 2011, mwezi Machi, dhahabu ilipatikana katika vijiji vya Masienda, Tsawa, Gehandu na Hhasama katika Wilaya ya Mbulu. Dhahabu ilipatikana katika Maji (*Alluvial gold*). Wachimbaji walivamia ardhi na mali ya watu hadi vita vya kutumia silaha za jadi zikaanza. Vita hivyo havijakoma hadi leo kwa sababu Serikali inasita kuchukua hatua. Wakazi hao wamekosa maji na amani kwa sababu Mkuu wa Wilaya anawatetea wavamizi. Naomba Waziri anipe maelezo kwa nini?

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, naomba maelezo kama *REA* imetenga fedha za maporomoko ya Lingatuta Wahanje.

Mheshimiwa Spika, ni lini *TANESCO* watafikisha umeme katika Taasisi za umma za Peramiho zifuatazo:-

- (i) Maposeni Secondary
- (ii) Peramiho Hospital
- (iii) Chuo cha Madaktari Peramiho
- (iv) Masoko ya Peramiho

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Rural Lighting Tanzania 2010*, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya Peramiho (Jimbo) chini ya mradi huo? (*Led Tech Solar System*), ni vijiji vingapi vitanufaika?

Mheshimiwa Spika, *Item 10 Lighting Rural Dispensaries* mbona Songea haipo na hasa Songea Vijijini? Ni Tunduru na Mbinga.

Mheshimiwa Spika, *Item 10* tena ya Miradi ya kuhamasisha matumizi ya taa za mwanga bora vijijini (*Lighting Rural Tanzania* inarudia tena Mbinga, kwa nini sio Peramiho Songea)? Kwa nini hatugaiwi hiyo neema wote?

Mheshimiwa Spika, *Item 15* tena 116, *Family lighting* inarudia tena Mbinga, Namtumbo Tunduru, kwa nini sio Songea Jimbo la Peramiho? Sielewi Kabisa kwani huko hakuna wahitaji, kuna nini? Nahitaji majibu.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, kwanza, katika bajeti ya mwaka 2011/2012, Jimbo la Mbozi Magharibi halijaainishiwa usambazaji wa umeme wa Gridi ya Taifa hata kijiji kimoja wakati katika Jimbo zima lenye Kata 14 ni Kata moja tu ndio inayopata umeme wakati Kata 13 hazijawahi kupata umeme tangu tupate uhuru miaka 50 iliyopita. Hivyo wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi wanaomba maelezo ya kutengwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara ituambie ni Kampuni gani inayofanya utafutaji wa madini katika Kata ya Ivuma, Jimbo la Mbozi Magharibi maana tumejaribu kutafuta jina lakini watu/watafutaji hao hawako tayari kujieleza wao ni nani. Hivyo tunaamini utapeli huu unafanywa

ilhali Wizara ya Nishati na Madini inajua. Kwa hiyo, Serikali/Wizara iwareleze Watanzania ni kampuni ngapi imezajiri katika utafutaji wa madini ikiwemo Jimbo la Mbozi Magharibi, Kata ya Ivuma.

Mheshimiwa Spika, tatu, tatizo la umeme. Katika Kata ya Tunduma, Jimbo la Mbozi Magharibi, ni Kata pekee yenye umeme lakini mpaka sasa wananchi hawapati umeme wa uhakika. Hivyo basi kama Serikali inashindwa kusambaza ama kugawa umeme wa uhakika ijiuzulu kwani mpaka sasa watu wenye vipato vya chini vinavyotegemea umeme kama vile Salon na kadhalika hawafanyi kazi yoyote hali inayopelekea wao kuishi maisha magumu. Kwa hiyo, Serikali itueleze ni lini tatizo hili la umeme litakwisha na wala sio kututangazia miradi.

Mheshimiwa Spika, nne, hasara ya Taifa iliopatikana/iliyotokana na Taifa/Serikali kuingia mikataba feki ya madini pamoja na Serikali kusamehe kodi makampuni yote yanayochimba madini nchini. Hili linatakiwa liwekwe wazi ili sasa Tanzania iingie katika hoja ya kuamua kuendelea na hao wawekezaji katika sekta ya madini ama kuwaondo, kwa hiyo Serikali tunaomba itupe taarifa kamili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Spika, juhudzi za Serikali za kuachana na utegemezi wa umeme unaotokana na maji zilianza kipindi cha mwaka 2005 – 2010. Serikali ilibuni miradi minne (4) iliyokusudiwa kuongeza kiasi cha MW 645 za umeme kwenye Gridi ya Taifa ambayo ni:-

- | | | |
|-------|-------------------------------|--------|
| (i) | Kiwira – Makaa ya mawe MW 200 | |
| (ii) | Mnazi Bay | MW 300 |
| (iii) | Ubungo | MW 100 |
| (iv) | Tegeta | MW 45 |

Mheshimiwa Spika, kati ya 645MW ni mradi wa Ubungo 100MW na Tegeta MW 45 ndiyo ambayo imekamilika, miradi ambayo inazalisha kidogo ambapo MW 500 zimeshindwa kuzalishwa kwa sababu kimsingi yamechangiwa na kutokujibika vya kutosha na dhamira ya dhati kwa Serikali kujikita kwenye kuondoa tatizo la umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu nchi iliingia kwenye ukame tangu mwaka 2005 hadi sasa mwaka 2011, pia kutokana na athari za mazingira ni ukweli usiofichika kwamba athari za ukame zitaendelea kuwepo na kuendelea kung'ang'anira miradi inayotegemea mvua iwe ya umeme au kilimo hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza bado Serikali inaita janga la umeme ni la dharura wakati kwa sasa ni mwaka wa sita tangu kutokea tatizo hilo ambalo limepelekea hadi Baraza la Mawaziri kuvunjwa na aliyejewa Waziri Mkuu kijiuzulu, lakini bado Serikali hajifunzi na kuchukua hatua za utekelezaji za kununua mitambo ya majenereta ya kutosha na kuachana na urasimu wa kukodi mitambo ambayo inaiingiza hasara nchi na kutumia vibaya pesa wa walipa kodi (wananchi).

Mheshimiwa Spika, historia inaonyesha mikataba yote ya kukodisha mitambo imelenga kufishwa juhudzi za *TANESCO* kujitegemea na kuzalisha umeme hasa malipo ya *capacity charge* kwa mitambo na *TANESCO* kununua mafuta ya kuendesha mitambo hiyo, lazima viongozi tuwe wazalendo na kuoneea huruma upotevu wa rasilimali hasa fedha bila sababu na kutengeneza mazingira wananchi wakapoteza imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze leo sababu za kutotumia mitambo ya Symbion ilipokuwa inaitwa *DOWANS*. Haya mambo ndiyo yanababisha hasira kwa wananchi na kukifanya Chama cha Mapinduzi kinachounda Serikali kuchukiwa na wananchi. Naomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu mikataba ya Symbion na Aggreko ili wananchi waone endapo kuna unafuu wowote kwenye mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuititia kauli ya Waziri Mkuu kwamba Sheria ya Manunuzi italetwa Bungeni kutenguliwa baadhi ya vipengele. Hii itasaidia Serikali kununua mitambo mikubwa kama ya umeme, vichwa vya treni, ndege na kadhalika. Ombi langu, Serikali itenje fedha za kutosha za kununua majenereta ya kutosha ya kumaliza tatizo la umeme. Kutokana na hotuba ya Waziri ya bajeti, miradi 10 imenorodheshwa lakini yote itakamilika mwaka 2013, 2014, 2015 na 2016. Nchi haiwezi kuendelea kukaa gizani, shughuli za uzalishaji kusimama, wananchi wajasiriamali washindwe kurudisha mikopo kwenye mabenki na kuendelea kufilisiwa mali zao, makusanyo *TRA* kuendelea kushuka, waendelee kusubiri mwaka 2016 ili kupata umeme wa uhakika! Haya ni maajabu ya Mussa. Wanafunzi vyuoni wataandamana wakikosa umeme. Wafanyakazi wataandamana kwa kupewa *redundancy* kazini na mahospitali yatafungwa na wananchi watakosa huduma. Tujiulize ni wagonjwa wangapi wanakufa kwa kukosa *operation hospitalini*?

Mheshimiwa Spika, kwa heshima ya Chama changu CCM na Serikali yangu, ili CCM iendelee kubaki madarakani, narudia kuiomba Serikali itafute fedha zinazohitajika shilingi 1.7 triliioni kuweza kununua mitambo ya majenereta kutatua tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba niorodheshe miradi iliyotajwa na Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake cha bajeti na muda wa kukamilika ili wote tuwe na uelewa wa pamoja kwamba nchi haiwezi kuendelea kukaa katika giza kwa miaka mingine mitano (5) ambapo kwa sasa tumeshakaa miaka (5) tangu mwaka 2005.

- (1) Kinyerezi MW 240 utakamilika mwaka 2013/2014.
- (2) Mnazi Bay MW 300 utakamilika mwaka 2014/2015
- (3) Somanga Funga MW 230 utakamilika mwaka 2013/2014.
- (4) Ruhudji MW 358 utakamilika mwaka 2015/2016
- (5) Kiwira MW 200 utakamilika mwaka 2013/2014
- (6) Ngaka MW 400 utakamilika mwaka 2014/2015
- (7) Mchuchuma MW 600 utakamilika mwaka 2014/2015
- (8) Stiglers Gorge MW 2100 Mradi haujaanza kabisa bado Serikali inaongea wa Wawekezaji binafsi.

Mheshimiwa Spika, nadhani utakubaliana na mimi kwamba hakuna hatua zozote za dharura za kumaliza tatizo, hivyo naomba Serikali itafute shilingi triliioni 1.7 kwa ajili ya kununua majenereta. Serikali iachane na zana ya kusema ni gharama kuleta majenereta, gharama hizo zinalinganishwa na nini? Nchi kuendelea kukaa gizani?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika eneo la usambazaji wa umeme *vijiji*. Imekuwa ni kero, kila miradi inayopangwa Mkoa wa Lindi na Mtwara ambayo inatoa Mnazi Bay na Songosongo lakini *Vijiji* vya Mikoa hiyo havimo katika program ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na kigugumizi cha kuwalinda wafanyabiashara wanaochakachua mafuta. Najaribu kuuliza, wachakachuaji wa mafuta wako wapi? Je, wamefanyiwa au kuchukuliwa hatua gani na wako wapi? Haya ni matatizo yasiyofaa na kulinda maovu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea jinsi madini yanavyoporwa Mkoa wa Lindi na hakuna juhudzi zozote zinazofanywa. Maeneo ya madini ni kama haya yafuatayo:-

- (1) Nditi, Kiegei, Ikungu – Nachingwea.
- (2) Mnacho, Nandagala, Nambilanje, Nangowe – Ruangwa
- (3) Kilanjelanje, Makangaga – Kilwa

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yote yanatoa madini aina ya dhahabu, *Gypsum*, je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru uporaji wa madini yetu kiholela?

Mheshimiwa Spika, mwisho, sitaunga mkono hoja mpaka niambiwe kwa nini Mkoa wa Lindi haumo katika Mradi wa Usambazaji Umeme Vijiji.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi kubwa wanayopambana nayo katika suala la kusimamia na kuhakikisha kuwa umeme unapatikana katika nchi nzima. Aidha, wamekuwa wavumilivu pamoja na vishindo vya malalamiko ya kukosa umeme. Tunawaambia sisi tuko nyuma yao, tunawaombea Mungu awafanyie wepesi katika kazi zao za kila siku na awaepushe na yote maovu na awalinde daima.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu, naomba sasa nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme ni tatizo sugu na watu wengi wanakerwa na kukatikakatika kwa umeme. Utaratibu huu unaharibu biashara za watu na kusababisha hasara na kufanya mitaji kupungua au kwisha. Hali hii inawapata wale wanaotegemea umeme katika shughuli zao. Vilevile kutokuwa na uhakika wa umeme kunachelewesha umeme kufikishwa vijiji ambapo wanavijiji wanausubiri kwa hamu. Kwanza niipongeza Serikali kwa mpango walionao wa kuzalisha umeme ili kupunguza tatizo hilo kama sio kumaliza.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itafute fedha mahali popote katika vyando vyake na hata kwenye matumizi ambayo sio muhimu na yasipofanyika hakuna athari kama ujenzi wa nyumba za kuishi viongozi na kadhalika. Mpango wa kupata fedha, tunaomba Waziri atueleze mpango mzima wa kununua mitambo na kazi hiyo ifanyike mapema na si kama walivyopanga kwani mpango huo utachelewesha kupatikana kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali iache kutegemea umeme wa maji ila iwepo mipango mizito na mikubwa ya kuhakikisha tunazalisha umeme wa *gas* na mkaa. Naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni fedha kiasi gani zitatafutwa ili kuzalisha umeme huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, *Kikuletwa Power Station* – Kijiji cha Chemka, Kata ya Masama Rundugai - Wilaya ya Hai, inayomilikiwa na *TANESCO* imefungwa siku nyingi na mali zake zikiwemo nyumba, ardhi, mashine na miundombinu ziko katika hali mbaya. Nahitaji kujua ni lini *station* hii itafunguliwa/kufufuliwa. Aldha, ni vipi uwezekano wa *station* hii kukabidhiwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai kwa ajili ya kuendelezwa/kufufuliwa kwa kushirikiana na *REA*?

Mheshimiwa Spika, umeme Wilaya ya Hai. Miradi ya Wilaya hii imekwama katika hatua mbalimbali. Bajeti ya Wizara haionyeshi fungu lolote kwa mradi wowote wa Wilaya ya Hai. Miradi iliyo katikati itafanywaje? Miradi ambayo haijaanza itaanza lini? Miradi ya Wilaya ya Hai ambayo imekwama ni kama ifuatavyo:-

- (a) Miradi ya Umeme Iliyofika Nusu.
 - (i) Losaa Kitongoji cha Mungu Amaye - Mradi unaendelea, nguzo tayari zimebekwa bado waya.

- (ii) Bomang'ombe – Kingereka - Mradi unaendelea, nguzo ndogo 60 pamoja na transfoma mpya tayari bado waya.
 - (iii) Fiderisi - Nguzo 17 zimewekwa, mradi unaendelea bado waya.
 - (iv) Masama Mashariki – Monjulu - Mradi mdogo nguzo 30, bado waya.
 - (v) Kware Korongoni - Nguzo 30 zimewekwa, mradi unaendelea bado waya.
 - (vi) Kawaya - Nguzo 12 tayari zimewekwa, mradi unaendelea bado waya.
 - (vii) Bomang'ombe Uzunguni - Nguzo 17 zimeshapelekwa bado hazijasimamishwa, bado waya.
 - (viii) Mroma – Ufishi - Nguzo 10 zimewekwa, mradi unaendeleam bado waya.
 - (ix) Kitifu – Kwa Sadala - Nguzo 24 tayari mradi unaendelea bado waya.
 - (x) Tema – Masama Mashariki - Nguzo 28 tayari, mradi unaendelea bado waya.
 - (xi) Lemira Kati - Nguzo 19 tayari mradi unaendelea, bado waya.
- (b) Miradi ya Tanesco iliyoko kwenye Mpango
- (i) Machame Ndernyi A – Nguzo 10 pamoja na waya na transfoma.
 - (ii) Machame Ndernyi B - Nguzo 10 pamoja na waya.
 - (iii) Uswaa – Mbweera - Nguzo 24 na waya.
 - (iv) Kia Junction - Nguzo 15 na waya.
 - (v) Kwa Sadala - Nguzo 24 na waya.
 - (vi) Bomang'ombe Gezaulole - Nguzo 12 na waya.
- (c) Miradi Iliyokwama Kupitishwa Kutokana na TANESCO Kushindwa Kumudu Gharama
- (i) Lemira – Isuki – Kirumbiu - Nguzo 40, transfoma moja na waya.
 - (ii) Tema Juu - Transfoma moja ipo nguzo na waya bado.
 - (iii) Uboro - Nguzo 30, transfoma na waya.
 - (iv) Mbosh Parish - Nguzo 60 zilihitajika zimepelekwa nguzo 30 na waya, bado nguzo 30 na waya.
 - (v) Bomang'ombe – Magadini - Nguzo 40 transfoma moja na waya.
 - (vi) Kwa Somali - Nguzo 30 transfoma moja na waya.
 - (vii) Mungushi – Kambi ya Maziwa kuelekea Sanya Juu - Nguzo 40 transfoma moja na waya.
 - (viii) Chemka – Ngulu - Nguzo 30 na waya.
 - (ix) Longoi – Nguzo Nne - Nguzo 70 transfoma na waya.
 - (x) Ngosero - Nguzo 80 transfoma na waya.

(xi) Bomang'ore Kwa Kiriwe - Nguzo 60 transfoma na waya.

(xii) Roo Secondary - Nguzo 40 transfoma na waya.

(xiii) Mashua - Nguzo 60 na waya.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi yenye miundombinu ya umeme sasa imechakaa sana na nyaya za umeme nyangi ni wazi (yaani haziko *insulated*) na kwa hali ya uoto wa sehemu za milimani nyaya hizi hupita katikati ya migomba na miti. Mimea hii sehemu nydingine husababisha *Short Circuit* na hivyo kuongeza tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara. Aidha, mara kadhaa nyaya hizi zimesababisha vifo au majeraha makubwa kwa wananchi. Ni lini TANESCO itaanza ukarabati wa miundombinu hii?

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waziri, Naibu na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tumechoshwa na hadithi, maneno, orodha ya miradi na kadhalika, Watanzania wanahitaji umeme. Hatukubaliani na porojo zinazotolewa na Watendaji wa Wizara hii huku Watanzania wakiteseka na kuendelea kutaabika na maisha magumu.

Mheshimiwa Spika, sababu zinazotolewa kwamba mabwawa yamepungua kina cha maji, inaonyesha wazi kwamba waliopewa dhamana ya kuongoza Wizara hii nyeti wameshindwa kuwa *proactive*. Sio wabunifu hata kidogo. Nani asiyeelewa kwamba suala la mabadiliko ya hali ya hewa ni *global issue*? Ni leo hali ya hewa imeanza kubadiliika? Tusidanganye Watanzania.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo yanayoonyesha jinsi gani Serikali haiko makini kuondoa tatizo la umeme. *IPTL* ina uwezo wa kuzalisha umeme *megawatt* 100, cha ajabu Serikali ilishindwa kutoa pesa ya mafuta mtambo ukawa unazalisha *megawatt* 10 tu! Leo Serikali inasema itatoa pesa ya kununua mafuta ya mwezi mmoja tu, je, *what next?*

Mheshimiwa Spika, wafungwa walioko Gerezani wanahitaji mwanga wa umeme kama raia na Watanzania wengine. Gereza la Kilimo la Urambo ni Gereza linalozalisha chakula cha kulisha hata Magereza mengine, ni Gereza linalofuga na wanazalisha mifugo na mazao yake. Naiomba Serikali ielete Bunge hili ni kwa nini Gereza hili ambalo liko umbali wa kilometra 12 tu kutoka mjini Urambo halina umeme. Nitakamata shilingi ikiwa Serikali haitatoa maelezo ya kina na kutoa ahadi hapa lini umeme utakwenda pale.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kuongeza ushuru kwenye mafuta ya taa, bei imepanda vibaya sana na tumemmaliza huyu maskini wa nchi hii ambaye hana uwezo wa kutumia umeme lakini pia mafuta ya taa ndiyo tegemeo lake. Kwa uchumi duni hawawezi kununua mafuta kwa Shs.2200/= . Hili ni tatizo. Serikali lazima irudi nyuma na kuangalia nini kifanyike ili suala la mafuta ya taa liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha sana katika kitabu cha Waziri, Wilaya ya Urambo hakuna kijiji chochote kilichopewa mradi chini ya REA. Mradi Na. 26 umetaja Vijiji sita (6) vya Urambo na Mradi Na. 27 kuboresha njia ya umeme Kaliua. Hakuna pesa yoyote iliyotengwa kwa miradi hii na hakuna maelezo yoyote na hatua za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atoe maelezo ya kina juu ya miradi hii.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Spika, taarifa ya Wizara kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na MCC ambayo inatekelezwa na TANESCO katika Mkoa wa Dodoma, Jimbo la Mpwapwa, maeneo ya Ng'ambi – Kisoko, Pwaga, Lupeta na Wotta. Naomba kutoa ufanuzi wa maeneo hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ng'ambi – Kisoko na Lupeta, ni maeneo ndani ya Jimbo la Mpwapwa. Pwaga na Wotta ni maeneo ndani ya Jimbo la Kibakwe. Kwa kuzingatia jiografia ya maeneo yalivyo kwa kila Jimbo, sielewi utekelezaji wake utakuwaje, kwa sababu ya umbali kati ya eneo na

eneo (kwa kila Jimbo). Naomba wakati wa utekelezaji, ukarabati na uongezaji wa njia za usambazaji umeme (*distribution system, rehabilitation and extension project*), wataalamu waangalie jiografia ilivyo. Nasema hivi kwa sababu watakaonufaika na mradi huu ni wachache, wengine ambaao ni jirani hawatanufaika kabisa, wakati uongezaji wa njia za usambazaji umeme huu, hauunganishi baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa upande wa Jimbo la Mpwapwa pamoja na maeneo yaliyopendekezwa, tatizo lillopo ni njia ya umeme inayopeleka umeme Jimbo la Kibakwe. Njia hii inapita milimani kutoka Jimbo la Kongwa (Sagala) badala ya njia hiyo ya umeme kupitia barabara kuu inayopitia Mbande – Kongwa – Ng’ambi – Chunyu, Iyoma – Idilo hadi Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napendekeza maeneo yaliyomo katika barabara kuu nayo yafikiwe, kuongeza njia ya umeme na vijiji vingi vilivromo katika barabara kuu vitanufaika sana, kuliko kupitisha njia ya umeme milimani kusiko na watu. Wakati wa msimu wa mvua, nguzo za umeme zinazopita milimani huanguka mara kwa mara na kuleta usumbuwa wa kukatika kwa umeme katika mji wote wa Mpwapwa. Hali hii inaleta matatizo kwa mafundi wa *TANESCO* kugundua haraka kulingana na ugumu wa njia yenye.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi napendekeza uongezaji wa njia za umeme uelekezwe kupitia Ng’ambi – Kisoko, Chunyu, Iyoma, Idilo kuelekea Mji wa Mpwapwa.

MHE. LOLESEA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri. Pia natoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano mkubwa nilioupata kutoka kwenye Wizara yake. Aidha, nawashukuru Nailbu Waziri na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata wakati wote.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Busanda, Wizara imekusudia kuleta umeme wa *MCC* katika Kata za Bukoli, Rwamgasa, Nyarugusu na Katoro. Juhudi tumeziona na wananchi wamefurahia sana kwa hatua zinazoendelea. Niombe Serikali iharakishe utekelezaji wa miradi hii maana imekuwa ni ahadi ya muda mrefu sana. Pia Serikali itoe taarifa za mara kwa mara kwa wananchi kuhusiana na hatua zilizofikia. Pamoja na juhudi za mradi huu wa umeme kukusudia kuleta umeme ndani ya Jimbo la Busanda, lakini mradi huu unakwenda kwenye Miji Mikuu ya Kata na kuacha baadhi ya huduma za kijamii kama Kituo cha Afya Kashishi na Shule za Sekondari. Naiomba Serikali kupitia *REA* iangalie uwezekano wa kupanua usambazaji wa umeme katika vijiji vilivyo karibu na njia kuu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, upande wa madini, nazidi kuiomba Wizara itengete maeneo ya wachimbaji wadogowadogo katika maeneo ya Nyarugusu, Rwamgasa na Kaseme. Maeneo waliyotengewa Nyarugusu yapo ndani ya makazi ya watu na kwa upande wa Rwamgasa maeneo waliyopewa hayawatoshi kulingana na mahitaji yaliyopo. Kwa Kata ya Kaseme wale wachimbaji wadogowadogo walioondolewa Tembo Mine wapewe eneo jipya kwa ajili ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho Mfuko wa Wachimbaji wadogowadogo bado hatujaona utekelezaji wake na wananchi wanafuatilia sana na kuulizia kuhusu Mfuko huu. Naomba katika bajeti ya mwaka huu Mfuko huu uwafikie hata wachimbaji wadogowadogo waliopo Rwamgasa, Nyarugusu, Nyakagwe na Kaseme.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri na timu yake kwa hotuba yao nzuri waliyowasilisha leo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwenye hotuba yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa wote tunatambua tatizo la umeme ni janga la Kitaifa na kwa hiyo lazima lishughulikiwe Kitaifa na kwa umujimu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hali yoyote ile, umaskini wetu wa kipato kwa wananchi wa Taifa hili unachangiwa kwa 100% na tazito la umeme. Hivi sasa Watanzania wote waliokuwa wanapambana na kujinua kimaisha kwa shughuli zisizo rasmi kama Salon, biashara za vinywaji, mahindi, usindikaji wa vyakula na kadhalika vyote hivi vimefungwa na wakati huo wengi kati ya hawa walichukua mikopo katika taasisi za kifedha wanarudishaje na hawafanyi kazi?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara tuendelee kuwa wa pembezoni hata katika kile ambacho Mwenyezi Mungu ametujalia mpaka lini? Gesi ya Mnazi Bay, wananchi wa Mtwara wamekuwa wavumilivu, ahadi waliyopewa ya kuunganishiwa umeme kwa Shs.60,000/= imeyeyukia wapi? Kama kosa la kiutendajji liliosababisha mradi huo kutoiva kwa wakati kwa nini waadhibiwe Wanamtware? Utekelezaji wa mradi mpya wa ujenzi wa bomba la gesi utoke Mnazi Bay hadi Somanga – Tanga wakati wana Mtwara hawa jaunganishiwa? Inawezekanaje? Tunataka wananchi waendelee kuwa mashuhuda wa kuangalia mabomba ya miradi ya gesi bila wao kutumia? Kwa sasa kwa utaratibu uliopo Wanamtware hawawezi kutumia umeme huo, katika Wilaya zake zote ukitaka umeme nguzo Shs.500,000/= na kuendelea, hivi kwa namna yoyote ile Serikali haina namna ya kupunguza bei za kuunganisha umeme unaotokana na gesi ya Mnazibay?

Mheshimiwa Spika, kwa namna gani wananchi wa Mtwara watalinda mazingira kwa *product* ambayo haiwanufaishi moja kwa moja? Wakati mradi unaanza, wale waliojenga nyumba na kuomba umeme *TANESCO* waliambiwa wasubiri umeme utatoka Mnazibay, sasa wanaambiwa bado, kwa miaka miwili (2) wasubiri mpaka mwaka wa ngapi? Wadai uhuru wa gesi yao?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Wizara ikaona namna ya kuweka taratibu na viwango nafuu vya kuunganishiwa umeme kwa Wanamtware.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ABUU H. JUMAA: Mheshimiwa Spika, nina heshima kubwa kupata fursa hii kuweza kuchangia bajeti ya mwaka 2011 – 2012 ya Wizara ya Nishati na Madini. Bajeti hii imeandalila kwa makini sana na kwa utaalamu mkubwa ikizingatia kwamba sasa hivi wananchi wanalamika sana kuhusu kero kubwa ya ukosefu wa umeme ambaeo upo katika mgao usiokuwa na mpangilio. Hivyo Wizara lazima ifanye juhudhi za ziada kuhakikisha huduma ya nishati ya umeme inaboreshwu ili kuondoa adha na kero kwa wananchi wote wanaoishi mijini na wale wa vijijini ambaeo ni wengi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mtiririko mzima wa bajeti hii umelenga kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, upo upungufu ambaeo unatakiwa kurekebishwe ili kukidhi mahitaji ya wananchi na kuifanya llani hii ya Chama cha Mapinduzi katika sekta hii ione kane inalenga kutoa huduma bora kwa wananchi na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia nishati ya umeme, tunagusa kuathirika kwa huduma katika nyanja mbalimbali. Ili kuweza kuzalisha katika viwanda, migodini na hata maofisi lazima kuwepo na umeme wa kuaminika kwa muda wote (*reliable power/electricity*). Katika mahospitali, tunahitaji huduma za umeme kukamilisha uchunguzi wa maradhi, utunzaji damu na madawa katika majokofu, matibabu kama upasuaji na hata kuhifadhi maiti. Vinu vya kuhifadhi na kusambaza mafuta, huendeshwa na umeme kama hakuna umeme itakuwa vigumu sana kutia mafuta katika magari. Taa za kuongoza magari barabarani pia hutumia umeme. Bila umeme huduma mahospitalini zinazorota na kuhatarisha maisha. Mashuleneni kadhalika umeme ni muhimu sana katika mabaara, madarasani, mabwenini pia huwezesha wanafunzi kusoma bila bughudha. Huduma ya umeme inaraisisha huduma majumbani kwani hutoa mwanga, kupikia, kuhifadhi vyakula na kadhalika. Nishati ya umeme pia hutumika kuraisisha umwagiliaji mashambani, hivyo ni muhimu sana kwa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuonyesha mifano hiyo utaona ni kwa nini huduma hii inapokosekana kunakuwepo na malalamiko mengi toka kwa wananchi. Shirika pekee la kuzalisha na kusambaza umeme *TANESCO*, pamoja na kuwepo kwa ukosefu au mgao wa umeme lakini pia wafanyakazi wa Shirika hili wanawakera sana wananchi. Utakuta *TANESCO* wamefanya uzembe wa kutokusanya fedha kwa wateja wao kwa muda mrefu kama miwili na hata mitano,

mteja huyu anahama nyumba iwe ya kampuni fulani au ya Shirika la Nyumba (*NHC*) anapoingia mpangaji mpya na kupeleka mkataba wake *TANESCO* ili asomeke kama mteja wao mpya, ndipo wanaposhtuka na kukata huduma ya umeme wakimlazimisha mpangaji huyu mpya kulipa deni aliloacha mpangaji wa zamani au vinginevyo hapewi huduma.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi wengi sana ambao wanapata adha hii ya kunyimwa huduma na wengine wamekwenda Mahakamani kuishaktaki *TANESCO* ili haki ilazimishe kupata huduma. Tendo hili la uzembe wa kuikosesha Serikali na Shirika mapato na kisha kumnyanyasa mteja mpya anayetaka huduma, asiye na hatia, hii si sawa kabisa, wafanyakazi wa *TANESCO* ni lazima wabadilike na wawajibike ipasavyo ili hata hiyo huduma ya mgao basi wananchi wasiwe na malalamiko yasiyo na msingi.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe mawazo na mchango wangu kwa jinsi gani tatizo la mgao wa umeme linaweza kufanyiwa kazi kupunguza makali ya adha hii kwa wananchi. Bwawa la Mtera ndilo bwawa kubwa ambalo linategemewa sana katika kuzalisha nishati ya umeme hapa nchini. Bwawa hili tangu limetengenezwa hakuna kumbukumbu kama limewahi kutolewa tope (*drenching*) ili kina chake kiweze kuhifadhi maji mengi ya kuweza kuzalisha umeme mwangi. Pia bwawa hili liko katika nyanda za chini, Serikali ichukue hatua za makusudi kuzuia kilimo katika nyanda za juu ambapo mmomonyoko wa ardhi unajaza tope katika mto na bwawa la Mtera kadhalika. Kuna haja pia Serikali kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi waishio kando ya bwawa kutokaza miti ovyo, kutoharibu uoto wa asili kwa kulisha wanyama kando ya vyanzo vyaa maji na badala yake waoteshe miti na kuzuia mmomonyoko wa ardhi, kwa kifupi kutunza mazingira kando ya mito inayotiririsha maji katika bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaweza kufanya jitihada zaidi katika kubuni vyanzo vingine vyaa kuzalisha umeme kama kutumia maporomoko na maanguko ya maji yaliyoko katika mito mingi ya hapa nchini. Mkaa wa mawe na *gas* badala ya kutegemea bwawa la Mtera na vyanzo vinavyotumia mafuta mazito. Mtambo wa kufua umeme katika kiwanda cha *PTL* kilichoko Tegeta kinatumia mafuta mazito, kinaendeshwa na wageni na pia umeme wake ni ghali sana. Serikali ichukue hatua za ama kununua au kuwezesha wananchi kupata ubia katika mtambo huo ili kudhibiti uzalishaji na gharama zake. Badala ya kutumia mafuta mazito basi itumike *gas* ambayo inazalishwa hapa nchini ili kuzalisha umeme kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukumbushia kilio cha wananchi wa Jimbo la Kibaha *Vijiji* kuhusu matatizo ya umeme. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa ziara yake aliyoanya katika Jimbo la Kibaha *Vijiji* mnamo tarehe 11 Januari, 2011 kujiona mwenyewe matatizo ya umeme yanavyoathiri maendeleo ya Jimbo. Katika ziara yake alitembelea Kata ya Gwata na Magindu. Pia Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu, alitoa ahadi kwa wananchi wa Kata ya Ruvu kupatiwa umeme katika bajeti hii. Naamini ahadi za Mheshimiwa Rais zitatekelezwa kwani matatizo ya umeme yanaathiri sana shughuli za maendeleo katika mashule, nyumba za ibada, zahanati na shughuli binafsi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda nipongeze juhudi za Wizara ya Nishati na Madini katika kudhibiti sekta ya madini hapa nchini. Pamoja na kazi kubwa iliyofanyika, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kwamba wageni wanaokodishwa migodi ya madini hawawatendei haki wananchi wanaishi jirani na migodi. Wamekuwa wachafuzi wa mazingira na vyanzo vyaa maji na kupelekea wananchi kupata madhara ya afya zao. Kutohana na mikataba mibovu, wamiliki hao wamekuwa wakiinyima Serikali mapato yake halali kutoka katika madini yanayozalishwa katika migodi hiyo. Napenda kushauri Serikali iangalie upya mikataba ya wamiliki wa migodi ili mapato yanufaishe pia wananchi. Ama Serikali iwawezeshe wananchi waweze kuingia ubia katika kuiendesha migodi hiyo. Sheria iwepo ya kunyima wageni kumilikishwa migodi bila kuwa na ubia na wazawa, hii itasaidia kuwapa uwezo wazawa katika kuhakikisha migodi inatoa ajira kwa vijana wetu, migodi inakidhi hali bora za kufanya kazi (*conducive working environment*) na Serikali inapata mapato sahihi kuliko kutegemea mirahaba.

Mheshimiwa Spika, migodi inayomilikiwa na wageni inasemekana ni madini mengi sana yanatoka nje ya nchi bila Serikali kujua kwa kuwa hakuna uangalizi kwa kile kinachoalishwa. Serikali ibuni ulinzi wa kitaalamu na uimarishe kuhakikisha kiwango na ubora wa madini

yanayozalishwa na kwamba mrahaba au pato linalokwenda Serikalini ni sahihi. Inasikitisha sana kuona kwamba nchi yetu ina madini ya aina nyingi kama Almasi, Dhahabu, *Tanzanite*, *Emerald* na mawe mengine ya vito vya thamani lakini ni maskini tofauti na nchi nyngine zilizotajirika kwa madini yake kama Botswana, South Africa na nynginezo zenyenye madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke Sheria ya kwamba wawekezaji katika sekta ya madini ni lazima wajenge viwanda vya kukata (*process*) vito vya madini hapahapa nchini badala ya kupeleka madini (*raw*) nje ya nchi. Kwa kufanya hivi, Serikali itasaidia kudhibiti na kufahamu thamani ya madini yanayozalishwa hapa nchini, kuongeza ajira na ujuzi katika sekta hii na kupata mapato sahihi yatokanayo na madini na hivyo kuendeleza huduma za muhimu kwa wananchi. Hii pia itazuia nchi zinazochukua sifa ya kujitangazia madini yanayopatikana hapa nchini pekee kama *Tanzanite* kuwa yanatoka nchini mwao. Hii inasababishwa na nchi yetu kutokuwa na wananchi wenye ujuzi na viwanda vya kukata madini katika viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri atakumbuka kilio cha matatizo ya umeme alichokisikia na kukiona katika Jimbo la Kibaha *Vijiji* na pia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwapatia umeme wananchi wa Kata ya Ruvu itatekelezwa mapema katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme nchini limekuwa wimbo wa kila siku. Sasa tunapaswa kujiuliza ni nini hasa chanzo cha tatizo hili? Nchi yetu tumejaliwa neema kubwa ya kuwa na vyanzo vingi zaidi ya kutegemea maji tu. Tuna gesi asilia, upepo, juu, makaa ya mawe na kadhalika. Tusiogope kusema ukweli, Serikali haina dhamira ya dhati kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, je, bajeti inayotengwa kwa Wizara hii ni ya kutosha? La hasha! Ukiangalia bajeti ya Wizara hii kiasi kilichotengwa kwa Miradi ya Maendeleo ni kidogo sana. Hivyo Serikali inapaswa kuongeza fedha katika Wizara hii nyeti kwa sababu kukosekana kwa umeme nchi imepata hasara kubwa sana na ni fedheha/aibu/adha kwa nchi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati *Vijiji* (*REA*). Watanzania wengi wanaoishi *vijiji* nao hawanufaiki na umeme. Serikali iwekeze zaidi katika mipango ya usambazaji umeme *vijiji* vikiwepo *vijiji* vya Kambi ya Simba, Slahhamo, Kitete, Upper Kitete, Lositeti Kata ya Mbolumbulu na *Vijiji* vyote vya Tarafa ya Lake Eyasi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini mradi wa umeme kutoka barabara kuu ya Karatu – Mbulu kwenda Endamararieki utakamilika?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kitabu cha Taarifa kwa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wakala wa Nishati *Vijiji* vya Mei, 2011, Dar es Salaam, ukurasa wa 11-12, chini ya kifungu cha 60, mikakati ya Wakala kwa mwaka 2011/2012, kipengele kidogo cha (h) na kiambatisho Na.6, ukurasa wa 20, *List of New Grid Extension Projects – item No. 4, power supply to Mang’ola (Lake Eyasi) and Mbolumbulu ambako zimetengwa jumla ya Tshs. 2,361,000,000 (2.361 Bilioni)*. Ukiangalia kitabu cha bajeti, ukurasa wa 103, jedwali Na.3, miradi katika Mpango kabambe wa kusambaza umeme wa Gridi *Vijiji* katika Mikoa 16, *vijiji* vyangu vya Mang’oka (*Lake Eyasi*) na Mbolumbulu havipo. Nahitaji maelezo ya kutosha maana hii inanipa hisia ya upendeleo au uchakachuaji kinyume chake nashika shilingi. Naomba Waziri anipe majibu.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na mikakati mizuri yenyenye kuleta utatuzi mkubwa wa janga la umeme na usuluhishi mkubwa kwenye baadhi ya migodi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, naomba kuleta malalamiko yangu juu ya masuala mawili (2) ambayo napenda sana kwa niaba ya wananchi wangu wa Tarime na Mwibara nipewe majibu yenyenye kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, tangu Mgodi wa Nyamongo uanze na kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na migogoro mingi baina ya wananchi waishio kandokando ya mgodi huu na wawekezaji wa kampuni ya *Barrick Gold Mining*. Nilitarajia kabisa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ingezungumzia mgogoro huu na hatua za haraka ambazo Wizara imejipanga kuzichukua kusitisha migogoro hii ambayo imesababisha vifo vingi na madhara makubwa kwa wananchi wa Nyamongo – Tarime. Kwa masikitiko makubwa nalazimika kusema Wizara haijaona kama hili ni tatizo. Nilitegemea kabisa Wizara ingejuja na suluhu ya nini kitafanyika kuondoa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kabisa yale madhara yaliyosababishwa na kemikali inayotirishwa kwenye Mto Tigite, yatakuwa yamepatiwa ufumbuzi. Nilitegemea kabisa Wizara ingejuja na mikakati kabambe ya uchimbaji wa malambo yatakayoweza kuwapatia maji safi na salama wananchi wetu wa Nyamongo ili waweze kuondokana na utumiaji wa maji ya Mto Tigite kwao wenyewe na mifugo yao. Nilitegemea pia Wizara kwa kupitia hotuba yake ingetueleza kwa uwazi kabisa ripoti ya Tume zote zilizoundwa kwa ajili ya kuchunguza madhara ya kemikali hiyo kwenye Mto huo. Nilitegemea pia Waziri angelleleza Bunge lako Tukufu ni fidia kiasi gani wahanga wa janga hili liliosababishwa na kemikali watalipwa kwani wahanga wote tayari wanafahamika.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri atueleze ni kwa nini suala hili hajalizungumzia kabisa na je, tuamini ile nadharia ya kwamba Serikali inawakumbatia hawa Barrick na kusahau wananchi wake? Je, ni lini ripoti za uchunguzi wa suala hili zitawekwa bayana ili kuondoa hofu kwa wananchi hawa wa Nyamongo? Je, ni kwa nini Wizara haioni umuhimu wa kuwachimbia wananchi wa Nyamongo malambo na mabwawa ili waondokane na utegemezi wa maji toka kwenye mito iliyopo karibu na mgodi ambayo imeonekana inawaleta madhara kutokana na kemikali?

Mheshimiwa Spika, umeme katika Jimbo la Mwibara. Naomba pia nieleze masikitiko yangu juu ya ahadi hewa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwa wananchi wa Mwibara wakati akizindua umeme Wilayani Ukerewe mwaka jana 2010. Umeme wa Ukerewe umepita katika Jimbo la Mwibara lakini kwa masikitiko makubwa umeliacha Jimbo hilo bila umeme na kuwafanya wananchi wabakie kulinda nguzo za umeme uendao Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni kwa nini Waziri hajatekeleza ahadi yake kwa mwaka huu wa fedha kama alivyotamka wakati wa uzinduzi kule Ukerewe na badala yake ameamua kupeleka umeme Jimbo la Bunda kwenye mashule jambo ambalo Wizara ingeamua kupunguza gharama kwenye shule hizo kwa kufunga *solar*. Je, ni lini hasa wananchi hawa wa Jimbo la Mwibara watapatiwa umeme ili waondokane na hii kero ya kulinda nguzo na hali umeme hawana?

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara yake ya Nishati na Madini vizuri. Mungu ampe afya.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Wizara hii ikawa moja tu, Nishati iwe peke yake na Madini iwe ni Wizara nyingine kwani Wizara ya Nishati ni Wizara nyeti sana na inabeba uchumi wote wa Taifa hili na Madini ibaki Wizara ya Madini peke yake kwani Wizara hii ni ya utafiti tu. Ili kuipunguzia kazi Wizara ya Nishati ibaki Nishati tu.

Mheshimiwa Spika, nikija katika vyanzo vya umeme, tumezoea umeme wetu unapatikana kwa njia ya mvua ambayo mvua zenyewe ni za msimu. Kwa nchi inayoendelea ni lazima kubuni njia mbadala, kabla ya tatizo hili kujitokeza kwa nini tunashindwa kusoma alama za nyakati? Hivi sasa miongo imebadilika mwisho mvua hazinyeshi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haiwezi kutoa maamuzi magumu kwa kufumba macho kidogo kwa kutafuta wataalamu wa kuleta umeme kwa mawimbi ya bahari ingawa ni gharama kubwa sana lakini matumizi yake ni daima na ndio maana nikasema ni maamuzi magumu sana. Katika kuongea na wadau pale Karimjee Dar es Salaam, kuna mdau mmoja ambaye alitoa wazo hili la umeme wa mawimbi ya bahari. Sasa kwa nini tusifumbe macho?

Mheshimiwa Spika, nikija katika kanuni zinazokataza Serikali isinunue mitambo chakavu/*used*, kanuni hizi zibadilishwe ili ikitokea hali ya dharura kama ya sasa inayolikabili Taifa hili iweze kusaidia hali ya dharura iliyopo nchini. Ajira zinapotea, uchumi unadidimia, Serikali inakosa mapato. Kanuni sio msahafu jamani kwamba hazibadiliki kanuni zimetungwa na sisi wanadamu. Katika ripoti imetajwa miradi mingi sana ya umeme lakini ukamilikaji wake hadi 2013/2014. Haiwezekani kwa hali ya sasa na ndio maana nikasema hizo kanuni zibadilishwe na kuna miradi mingine ilikuwa ikamilike pia nayo hajakamilika katika kipindi alichosema katika ripoti yake.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumejaliwa kuwa na rasilimali nyingi sana lakini bado tunaendelea kuwa maskini. Ni jambo la kusikitisha sana kwa Tanzania yenyne neema tele.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa masikitiko makubwa sana siungi mkono hoja.

MHE. ANNE K. MALECEL: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuanza kushukuru Watanzania kwa upendo wa dhati wa kusali mchana na usiku wakimwombea Mume wangu John Samwel Malecela aliyefanyiwa *Bypass Operation* ili apone na Mwenyezi Mungu amezisikia sala zangu, Mheshimiwa Malecela amerejea Tanzania akiwa mzima na anaendelea kupona.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema nitakuwa sijawatendea haki Watanzania na wapigakura wangu iwapo nitaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nilichangia nikiwa mchangiaji wa kwanza nikasema sitaunga mkono hoja na naona niweke kimaandishi kwani Serikali haikutendea haki wananchi wangu haswa baada ya Serikali kuititia Waziri wake wa Nishati kuniahidi mara nyingi na akanifanya na mimi niwandanganye wananchi wangu na kuniweka njia panda.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia vizuri kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ukurasa wa 103, nimefadhaishwa sana na kitendo cha kuandika kwamba Same Mashariki imepewa umeme wakati vijiji vyote vilivyoorodheshwa ni vijiji vya Same Magharibi.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa Mbunge ninayeongea sana na Mheshimiwa Waziri kwa karibu, ahadi zote alizokuwa ananipa kama Serikali ndizo nilizotumia kuombea kura. Leo hii naona Serikali inapeleka fedha za umeme Wilaya ya Same, zote zinapelekwa Same Magharibi lakini wanadanganya Bunge na kuandika Same Mashariki.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizopelekwa Mkoa wa Kilimanjaro zikagusa Majimbo matatu yote ni ya Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Nishati amejipa umeme Jimbo lake, Mheshimiwa Naibu Waziri amejipa umeme Jimbo la Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la Mawaziri kupendeleana wenyewe kwa wenyewe inatuumua sana sisi Wabunge. Uonevu unaofanywa na Wizara hii kutojali Majimbo ya Wabunge na kujali Majimbo yao na Mawaziri wenzao itatufikisha mahali pa sasa kuwaachia Mawaziri wao ndio wapitishe bajeti hili.

Kwanza Mheshimiwa Spika, nimeumizwa sana na bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini na naomba niweke kimaandishi kwamba sitaunga mkono hoja hii iwapo Mheshimiwa Waziri hatabadili na kuwatia matumaini wananchi wangu.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

MHE. ABDULSALAAM S. AMEIR: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nachoomba ni umeme katika Jimbo langu kama swalilangu Na.2 nilivyojibowi. Kata hizo nilizozitaja ndio itapita barabara ya lami toka Kilosa hadi Mji Mdogo wa Mikumi. Ni vijiji vinavyozalisha chakula takribani asilimia sabini (70%) ya chakula katika Wilaya ya Kilosa. Ili kuleta maendeleo ya wananchi na kuondoa umaskini kama llani ya chama chetu inavyoeleza, naomba umeme katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna taasisi ya kidini wapo katika mchakato wa kuweka *Hydropower* katika maporomoko ya Mto Yovi. Naomba Serikali itie mkono wake ili waweke mtambo mkubwa utakaoweza kusambaza Kata kama sita, naamini Wizara ina nia nzuri ya kuboresha sekta hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, naamini maombi yangu yatafanyiwa kazi na nipo tayari kushirkiana na taasisi hiyo pamoja na Serikali kufanikisha mradi huu.

Mheshimiwa Spika, shukrani, naunga mkono hoja.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, madini. Mwaka 2007, Rais aliunda Kamati ya Bomani kushauri kuhusu Sekta ya Madini. Taarifa ya Kamati ilioa mapendekezo yake na moja ya mapendekezo hayo ni mrahaba kuwa 5% (Sheria ikataka 4%) na kubadili formula (*netback value to GNPS*) na asilimia sitini (60%) ya mauzo ya madini nje fedha hizo zirudi nchini ili kuimarisha thamani ya shilingi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yote hayajatekelezwa. Serikali imesema inazungumza na Kampuni za Madini zilizopo ili wahamie Sheria Mpya. Mchakato huu uendelee ili mrahaba utozwe kwa mujibu wa Sheria Mpya. Kampuni tatu za Madini zina madai yao Serikalini kuhusu VAT, Serikali itumie hili kama *strategy* ili kampuni *zi-migrate into Mining Act 2010*.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kurejesha nchini fedha za kigeni zinazotokana na mauzo ya madini litekelezwe haraka kwa kufanya marekebisho ya kanuni. Hili likifanyika, uchumi wetu utakuwa na fedha za kigeni za kutosha na hivyo kuimarisha Shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia nchini ni Taasisi muhimu sana kwenye Sekta ya Madini hapa nchini. Hata hivyo, Wakala hawapewi fedha za kutosha licha ya umuhimu wake. Lazima tuwe na picha pana kuhusu *GST*. Huko siku za usoni *GST* ndio inapaswa kufanya kazi ya kugawa vitalu vya madini kama ilivyo *TPDC* kwa sasa *GST* inapaswa kufanya *survey* nchi nzima kupata aina za madini, kutenga maeneo na kisha kufanya mnada na hivyo nchi kufaidika na ugawaji huu wa vitalu. Nashauri kuwa katika bajeti ya TMAA, Tshs. 1 billioni zipunguzwe zipelekwe *GST* ili kuwawezesha kufanya kazi hii nyeti. Tujenge uwezo wa kitaasisi wa *GST* kwa kuwapa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, nishati. Kiwira. Serikali imetangaza kuwa tutapata mkopo kutoka China ili kuwzesha mradi wa Kiwira kuanza kazi. Nimeshaongelea sana *mentality* hii ya Serikali ya kila kitu China. Wakianza mazungumzo tu, China! Wanasa hau China ndio walipewa Kiwira kabla? Mazingira yaliyowafanya Wachina washindwe yamebadilika? Kwa nini hatujifunzi kutokana na makosa ya nyuma? Nina uhakika miaka mitano (5) itapita bila Kiwira kuzalisha chembe ya makaa au umeme. Serikali iangalie upya mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya *POAC* kuhusiana na Kiwira. *NSSF & STAMICO is the right approach to Kiwira project*.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya mkataba wa Gesi kati yake na *Orca Company* kuhusiana na kodi ya mapato. Pia mkataba wa umeme kati ya *TANESCO* na *Songas*. Vilevile uchunguzi ufanywe kuona mahusiano ya Orca na *PanAfrica Energy Corporation* (Mauritius) na *Pan Africa Energy* (Tanzania) kama ni mahusiano ya kukwepa kodi (*tax avoidance*). *Offshore registered companies* ziangaliwe sana kuhusiana na mambo ya kodi. *Orca (offshore)* na *PAE Corp (offshore)*.

Mheshimiwa Spika, umeme. Nashauri *pension funds* money zitumike kununua mitambo ya 500 MW ndani ya miezi hii miwili kabla ya sherehe za uhuru. *Malaysia Tenaga Company* wana mitambo hawatumii. Mawaziri wafanye mazungumzo nao. Wahusishe *pension funds* kuleta mitambo, wapewe *PPA* na *TANESCO* bila *capacity charge*. Hili linawezekana tukiamua.

Mheshimiwa Spika, *REA*. Ushuru wa mafuta ya taa unaokusanywa uende kuzalisha na kusambaza umeme vijijini. Ushauri huu umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya KFWA inataka kuwekeza 50 MW Solar. Tunaomba Serikali ikubali mahusiano yetu na Ujerumani yawe katika nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kesi ya *Dowans*, katika hotuba ya Waziri hakugusia kabisa *contingent liability* ya 94 bilioni kwa Kampuni ya *Dowans*. Taarifa zilizopo (sina uhakika nazo) zinasema kuwa *Judge* wa Uingereza anaweza ku-enforce the *ICC award* na hata kama atachelewesha *TANESCO* watatakiwa kuweka mamilioni ya pesa kama *security*. Hizi zitamaliza kabisa Shirika letu. Kama Mahakama ya Uingereza ikitoa maamuzi ya kushika *assets* zetu maana yake ni kwamba mali za *TANESCO* au hata Serikali zitashikwa huko Ulaya na Marekani. Mfano juzi hapa Ndege ya Rais Kabila zilishikwa. Serikali inachukua hatua gani kulinda mali za Serikali au *TANESCO* nje? Serikali itoe kauli kuhusu ilipofikia kesi ya *Dowans* hapa nchini na huko Uingereza (hii kesi ya UK ndio hajulikani kabisa).

Mheshimiwa Spika, kuhusu *IPTL*. Nimepata taarifa kwamba Mahakama imeamuru Kampuni ya *IPTL* iwe *woundup*. Wizara inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa mchakato wa kugawa mali unafanyika haraka? Tukichelewa wale *Standard Bank* watakimbia Mahakamani kuzuia, Wizara ishirikiane na RITA kwa haraka ili *windingup process* ifanyike na nchi iondokane na mzigo wa *IPTL*.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Waziri waliwaahidi wananchi wa Mtwara Vijiji kuwaunganishia umeme kwa gharama za Shilingi 60,000 tu. Wananchi wa Msimbati na vijiji vya mradi wa awamu ya kwanza umeme umefika lakini gharama imebadilika kuwa Shilingi 400,000 hadi 500,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufuatailia tunaambiwa kuwa fedha ambazo zingegharamia/saidia uwekaji umeme hazikupatikana kutohana na uzembe wa *EWURA*. Sasa napenda kufahamu *EWURA* wamechukuliwa hatua gani kwa kuwakosesha wananchi wa Mtwara Vijiji na Taifa kwa ujumla Euro 28 million?

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wanatoa kauli gani kwa wananchi wa Mtwara Vijiji ambao *gas* inatoka Jimboni kwao lakini hawajanufaika na *gas* hiyo wala umeme wa *gas* yao? Ni hatua gani zimechukuliwa kuhakikisha wanapata umeme kwa gharama wanayoimudu badala ya kuanzisha miradi ya umeme kwenda Singida na Bomba la *Gas* kwenda Tanga?

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo yafuatayo:-

- (i) Serikali ifanye tathmini ya miradi ya *MCC* ili kujua so far tumefikia wapi.
- (ii) Serikali *i-subsidize* gharama za nguzo kwa mtumiaji wa mwisho.
- (iii) Bei ya umeme kwenye maeneo ambayo wanazalisha umeme wapate kwa gharama nafuu kuliko maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero ina migodi miwili ya kuzalisha umeme Kihansi na Kidatu lakini inasikitisha kuwa bado kuna tatizo kubwa la umeme, napendekeza Wilaya hii ipewe kipaumbele katika kupata miradi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, katika Jedwali Na. 3, miradi katika Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme wa Gridi Vijiji katika Mikoa 16, katika Ukurasa 106, Mkoa wa Morogoro, Wilaya Kilombero imetajwa Malinyi, Mji huu haupo Wilayani Kilombero, upo Ulanga. Naomba kufahamu je, Mji au Kijiji gani cha Kilombero kitakachopata umeme? Ni kwa nini iwe Mji au Kijiji kimoja wakati tunazalisha umeme?

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, nchi yetu ilikumbwa na janga la uchakachauaji mafuta, licha ya kuikosesha nchi yetu mapato lakini pia kulikuwa na uharibifu mkubwa wa injini za

magari kutokana na mafuta yaliyochakachuliwa. Ni kweli kwa kupandishwa bei ya mafuta ya taa tatizo la uchakachuaji litapungua kwa kiasi kikubwa, lakini nitoe tahadhari, uchakachuaji unaweza ukaendelea kama haikuchukuliwa tahadhari ya mafuta ya ndege (JETIA) yanawenza yakatumika katika uchakachuaji. Licha ya hofu ya mafuta ya ndege, Serikali iwe macho na Mikoa inayopakana na nchi ya Kenya kwani nchi hiyo bei ya mafuta ya taa iko chini na kama mafuta ya taa hayo yatavushwa kuja Tanzania basi uchakachuaji utaendelea.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu katika Bunge hili linazungumzwa suala zima la wachimbaji wadogowadogo wa madini na wao kupatiwa eneo la uchimbaji na misaada ya vifaa vya kufanya kazi. Mpaka leo utekelezaji wa maagizo hayo ni hadithi. Je, ni lini wachimbaji wadogo wa madini watapatiwa haki hiyo katika nchi yao?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, gesi asilia liko katika Muungano ambapo Zanzibar ni sehemu ya Muungano huo. Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepatiwa gawio la fedha zinazotokana na gesi asilia?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina tatizo kubwa la umeme, kinachoshangaza Serikali ina miradi mingi midogomidogo ya kufua umeme. Kwa nini Serikali hajikiti kwenye miradi mikubwa mfano Stiegler's Gorge katika kuondoa tatizo la umeme?

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inategemea sana ubora wa mazingira katika kupata maji na hatimaye kupata umeme wa maji. Wizara hii imechangia nini katika utunzaji wa mazingira katika maeneo ambayo kuna vyanzo vya maji. Wizara ilipaswa ioneckana waziwazi katika uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, wauzaji mafuta wana tabia, bei ya mafuta inapopanda basi hapo bei hupandishwa leo mafuta bei imepunguzwa lakini bei iko pale pale. Ni lini bei hizi za mafuta zitatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme nchi hii limekuwa ni la muda mrefu sana. Miradi mingi ya maendeleo haiendi, makampuni yanakuwa, yanashindwa kufanya kazi kutokana na tatizo hili. Mapato ya Serikali yanapungua siku hadi siku na nchi inazidi kudidimia.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu tusitegemee umeme unaopatikana kwa njia ya maji, ambayo hatuna uhakika nayo. Wakati mwagine maji yanapungua na wakati mwagine yanaongezeka, tunakuwa hatuna umeme wa uhakika. Ni vyema tungeliangalia vyanzo vingine vya upatikanaji wa umeme kama vile makaa ya mawe au gesi. Nchi yetu imejaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa gesi asilia, ingetumika kwa kuzalisha umeme kuliko kutegemea vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nzungumzie kuhusu sekta ya madini, hawa wachimbaji wadogowadogo wasidharauliwe, wapewe kipaumbele ili na wao wafaidike na rasilimali ya nchi yao. Hawa wawekezaji wakubwa wanawanyanyasa sana wachimbaji wadogowadogo. Wachimbaji wadogo wapewe maelekezo ili wafuate sheria na taratibu za Serikali. Serikali ichukue jukumu kila kwenye Wilaya zilizo na migodi wapewe elimu ili waweze kujajiri na kuepukana na ugumu wa maisha.

MHE. MBAROUK SALIM ALI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwepo hapa leo hii na kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, umeme ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya jamii kwani bila ya umeme hatuwezi kutaja maendeleo ya jambo lolote lile katika nchi. Sasa inasikitisha kuwa hali ya umeme Tanzania inazidi kuwa mbaya kadri siku zinavyosonga mbele.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumekuwa tukitumia sana maji kwa uzalishaji wa umeme na kwa mujibu wa Serikali, hali ya umeme na mgao wa umeme unoendelea unatokana na kina cha

maji kupungua au kushuka katika mabwawa ya uzalishaji kati ya mwaka 2004 – 2011 na kuilazimu Serikali kutegemea umeme ghali wa mafuta. Japo suala la ukame na mabadiliko ya hali ya hewa Tanzania kumechangia kupunguza kina hicho, lakini tatizo kwa mujibu wa tafiti binafsi za mtu mmojammoja ni kwamba mabwawa yote yamejaa ama mchanga au tope, hivyo hata mvua ingenyesha kwa kiasi gani kina hicho cha maji lazima kiwe kidogo kutohana na mchanga au tope zilizopo kwenye mabwawa hayo. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho aweze kuuthibitishia umma wa Watanzania kuhusiana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei 2011, Serikali kuititia Shirika la *TANESCO* lilitangazia umma kwamba kutakuwa na mgao wa umeme wa muda mfupi kwa ajili ya matengenezo ya mitambo. Tokea muda walioahidi kwamba umeme ungerudi katika hali yake ya kawaida, mgao umekuwa ukiongezeka mpaka kufikia masaa 12 na 18 kwa siku. Kwa taarifa zisizo rasmi ambazo Waziri anatakiwa athibitishe ni kwamba vinu vya gesi vimeisha gesi na mategemeo ya kuzalisha gesi nyingi hakuna tena na uwezo wa vinu kutoa gesi mwisho ni 2018. Labda Waziri angethibitisha hili na kulifanua kwa umma wa Watanzania ili watu waweze kuelewa. Tatizo kubwa ni usiri wa Serikali, kwa nini Serikali haiko wazi kwenye mambo makubwa na magumu kama haya? Nashauri Serikali iwe wazi kwenye masuala ya umeme ili watu waelewe kinachoendelea badala ya kudanganywa na kuwapa Watanzania tamaa kila siku.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nashukuru.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Spika, napenda na mimi kuchukua fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, tatizo sugu la mgao wa umeme ambalo sasa limekomaa na kuwa janga la Taifa limetokana na ufisadi, udhaifu, uongozi na utendaji amba o umeikabili sekta ya nishati nichini kuanzia Awamu ya Pili. Je, Serikali na Wizara haioni sasa ni wakati muafaka iundwe Tume Maalum ambayo itashirikisha wadau, wanasiasa na amba o sio wanasiasa tuangalie kwa makini, tuondoshe itikadi za kisiasa kwa sababu tatizo hili ni janga la Taifa zima. Tuchunguze kwa makini kabisa kama kuna mafisadi wanaotafuna sekta hii ya nishati na madini wafukuzwe kazi na tuajiri wafanyakazi wengine amba o ni wataalam. Naishauri Serikali iepuke mikataba mibovu ya wawekezaji ambayo inasababishia Taifa hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili la umeme limewaathiri Watanzania wengi na pato la Taifa limeshuka. Viwanda havifanyi kazi hivyo hatuingizi mapato ya Serikali na wananchi wamekuwa wakiteseka kwa sababu shughuli zao zinategemea umeme. Hata lengo hili dogo la MW 1788, ambalo ni sawa na ongezeko la wastani wa MW 360 kila mwaka, halijaanza kutekelezwa kwa ukamilifu. Hii ni kwa sababu katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali imepanga katika bajeti kuongeza MW 160 ambazo kimsingi zilipaswa ziwe zimekamilika mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu suala zima la wachimbaji wa madini wadogowadogo. Wawekezaji wamekuwa wakiwanyanya hawa wachimbaji wadogowadogo, hawafaidiki na rasilimali za Taifa hili. Vijana hawa wamekuwa wakipoteza maisha na kuishia jela kwa ajili ya rasilimali za Taifa lao. Naishauri Serikali ipitishe Sheria kwa wawekezaji amba o wanakuja kuwekeza kwenye migodi ili kuwalinda wananchi wanaozungukwa na migodi na vijana amba o wanajipatia riziki zoa katika migodi hii. Wananchi hawa waliozungukwa na migodi ni maskini sana hivyo basi migodi hii imekuwa ikinufaisha wawekezaji na Watanzania wengi wanabaki kuwa ni maskini, hawanufaiki na rasilimali zao. Naomba Waziri atakapokuja kuhitimisha aniambie ni vijana wangapi wameajiriwa kwenye migodi hii?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aniambie wawekezaji hawa wamewasaidia vipi wananchi amba o wamezungukwa na migodi hii na ni watoto wangapi walioweza kusaidiwa kama katika suala la elimu, je, wamejengewa shule? Pia suala la afya, wananchi hawa waliozungukwa na migodi wamejengewa hospitali? Naomba Waziri aniambie wananchi hawa wamenufaika vipi na rasilimali za Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu suala la mafuta. Tarehe 15 Juni 2011, wananchi walishukuru Serikali kwa kutoa kauli ya kupunguza tozo kwenye bidhaa za mafuta ili

kupunguza bei na gharama za wananchi na kuonyesha mashaka kuhusu kiwango ambacho kitaondolewa na Serikali. Mashaka hayo yalidhihirika kwenye kuitisha Muswada wa Sheria ya Fedha tarehe 22 Juni 2011 ambapo Serikali haikuonyesha kivitendo dhamira ya kupunguza kodi kwenye mafuta kwa kiwango cha kuwapunguzia ugumu wa maisha wananchi badala yake ikajikita kwenye kupunguza tatizo la uchakachuaaji pekee ambalo limedumu kwa sababu ya Serikali kushindwa kusimamia utawala wa sheria. Ushahidi ni kwamba katika marekebisho ya kodi, Serikali haikupunguza hata senti moja kati mzigo wa kodi kwenye *petrol*. Aidha, Serikali ilipunguza kodi ya dizeli kwa shilingi 99 tu huku ikiongeza kodi ya mafuta ya taa kwa shilingi 358.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hili ni mzigo kwa wananchi walipa kodi masikini, je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kupunguza kodi ya tozo kwenye bidhaa za mafuta ili kuwapunguzia gharama wananchi hawa wa kipato cha chini ili nao waweze kujimudu kimaisha?

Mheshimiwa Spika, ukiondoa kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia na ukubwa wa kodi zinazotozwa na Serikali, bei ya mafuta inakuwa juu kutokana na mfumo mzima wa uagizaji, usafirishaji, uingizaji na usambazaji. Mfumo uliopo sasa unanufaisha makampuni makubwa mengi yakiwa ya kigeni na wafanyabiashara wachache wa ndani pamoja na baadhi ya viongozi wa Serikali wasiokuwa waadilifu kwa kulinyonya Taifa na kuongeza gharama za maisha kwa Watanzania walio wengi. Kwa kuwa athari kubwa ya kasi ndogo ya ushushaji wa mafuta bandarini kutokana na ufinyu wa miundombinu, je, Serikali sasa haioni ni muda muafaka kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo na kujenga Boya kubwa la kupakua mafuta baharini (*SPM*) na kujenga *KOJ*mpya?

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linaathiri Watanzania wengi na linanufaisha matajiri wachache wasiokuwa waadilifu katika Taifa hili. Kwa hiyo, Serikali na Wizara ihakikishe wafanyabiashara hawa wa mafuta wasiokuwa waadilifu katika bidhaa za mafuta wanachukuliwa hatua za kisheria na kufutiwa leseni zao na biashara hii inabaki kwa wafanyabiashara waadilifu wenyewe uchungu na Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka nipatiwe majibu ya kutosheleza kwa haya niliyoyasema.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake nyingi alizonijalia na kuweza kupata wasaa wa kuchangia kwa maandishi hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja asilimia 100 na nampongeza sana Waziri Ngeleja kwa hotuba yake nzuri. Pia nawapongeza Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao na umahiri katika masuala yote ya utendaji kazi wao, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuchangia kwangu, nitajikita zaidi upande wa umeme. Umeme kwa kweli ni tatizo kubwa sana hasa maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, sehemu nayotoka katika Mkoa Mpya wa Geita na ni Wilaya Mpya ya Nyang'hwale, katika Wilaya hii hakuna umeme kabisa, tuko gizani licha ya nguzo za umeme zilizopita kutoka Nyamtukuza kwenda kwenye machimbo Kakola. Nguzo hizi zimepita kwenye mashamba ya watu na pia kwenye vijiji ambapo ni makazi ya watu na pia kuna Shule na *Dispensary*.

Mheshimiwa Spika, natoa masikitiko yangu kwa Waziri wa Nishati na Madini kwa sababu hawa wawekezaji kweli wanashindwa hata tu kupeleka umeme kwenye shule ambamo nguzo zao zimepita? Basi niombe Waziri ajitahidi kutupatia umeme maeneo haya katika vijiji vya Nyamtukuza, Kakora, Kitongo, Ikangala na Karumwa. Maeneo haya nguzo zimepita zikienda kwenye machimbo.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru Serikali kwa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Najua Wizara hii inasimamia sekta nyeti yenye migogoro mingi kwa sababu Watanzania wengi wanaihitaji. Hata hivyo, napenda kupongeza mipango inayoendelea hususani ya umeme katika Mkoa wa Simiyu, katika kitabu cha bajeti nimeona jinsi utaratibu wa

usambazaji umeme vijiji ulivypangwa kutekelezwa lakini pia katika utendaji halisi nimeshuhudia jinsi nguzo zinavyosambazwa na nyaya kutandazwa katika maeneo mengi ya Mkoa wa Simiyu mfano Kata ya Bariadi – Nkolola, Bariadi – Kilala na Bariadi Sapiwi – Mkula – Lamadi. Hii ni hatua njema hasa ukizingatia maeneo mengi ya Mkoa wa Simiyu yanakaribia kuwa jangwa kutokana na kuisha kwa misitu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Simiyu kuna Viwanda vingi vya Pamba hivyo kupatikana kwa umeme wa gridi kutapunguza gharama ya uendeshaji wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, tatozo kubwa linaloikabili nchi hii sasa ni kukatika kwa umeme na migao. Hii ni matokeo ya kutegemea zaidi umeme wa maji, naomba tutoke huko kwa haraka sana tuweke nguvu kuzalisha umeme usiotegemea maji. Iwapo tukifanikiwa hili, nchi yetu itawezekujikombua na kuimarishe uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. SEIF S. RASHID: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Kitaifa, suala la umeme ni zito na ni changamoto ambayo nathubutu kusema tumekosa mipango iliyokuwa inatakiwa kutekelezwa miaka mingi iliyopita. Nasema ni kushindwa kutekeleza mradi wa umeme wa MW 2100 na Stiglers' Gorge na kuachana na miradi mingi midogomidogo ambayo siyo tu haitoshelezi bali inapoteza fedha za umma kwa kulipia utawala wa miradi mingi isiyotosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la umeme Wilaya ya Rufiji. Kwa miaka hamsini Warufiji walichangia kwa uchumi wa nchi katika kilimo na wamekuwa wakisubiri kupatiwa umeme. Kwa vile umeme unaozalishwa Somangafunga ni wa MW 7.5 na ukweli kwamba maeneo yaliyopatiwa umeme hadi hivi sasa unatumia MW 2.5 tu na kufanya maeneo mengi yasiosambaziwa umeme kuendelea kuwa kiza wakati umeme wa MW 5 ukipotea bure.

Mheshimiwa Spika, nimeomba umeme kusambazwa kwa vijiji vya kutokea Nyamwage kuelekeA Mtwara na Nambonjo na hivyo kufikisha umeme katika Sekondari ya Mtwara. Naomba Serikali kutupa nafasi ya kusambaziwa umeme ambao upo Ikwiriri ili ufkiele vijiji 14 vilivyo katika barabara moja hadi Mloka na hivyo kuwanufaisha watu wengi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, sipo tayari kuona miradi ya umeme iliyowezeshwa na Serikali ikifanyika maeneo mengi na kwa vile tunaomba vijiji 18 hivi, basi pamoja na jibu la Serikali kuwa mradi huo utahitaji Shilingi bilioni tatu hivi, hiyo sio sababu ya kuwaambia Warufiji wanaofahamu kwamba Serikali inapata zaidi ya shilingi bilioni tano kwa mwaka kwa ajili ya mapato ya hifadhi ya Selous peke yake. Nitasakiiza na kuunga mkono hoja ikiwa Serikali itanipa angalau ahadi ya kufikisha umeme katika vijiji vya Kata hizo za Mtwara, Mkongo, Ngorongoro, Kipugira na Mwaseni vyote hivi vikiwa na vijiji takribani 18.

Mheshimiwa Spika, katika vijiji vilivypatiwa umeme vya Muhoro, Utete na Bungu, umeme huo umesambazwa katika mitaa mitatu tu na kuacha wananchi wengi wakiuangalia wakitakiwa kulipia fedha nydingi sana na kwa kuwa hawana kipato cha kutosha hawatamudu kulipia gharama hizo. Naomba Serikali kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vilivyofikiwa kama vile Muhoro, Nyamwage, Utete, Bungu na Kibiti ili wananchi wengi zaidi wanufaika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali katika kufikisha umeme na ni matumaini ya Warufiji kuwa Serikali itasakiiza kilio chao kama nilivyo eleza hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya mabadiliko katika tozo ya mrahaba kwenye Kampuni za Madini kutoka asilimia tatu hadi asilimia nne, lakini Sheria hiyo haiyagusi Makampuni ya zamani. Ni sababu zipi Sheria hiyo isianze kutumika na kuyagusa makampuni ya zamani hasa ukizingatia mikataba ya madini inachukua muda mrefu. Kwa sasa

kwa kutumia asilimia tatu Serikali inakusanya shilingi bilioni 63, lakini kwa ongezeko la asilimia moja kama asilimia nne ikianza kutumika Serikali itakusanya shilingi bilioni 126.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, Halmashauri zimepewa mamlaka ya kukusanya ushuru (*service levy*) lakini Halmashauri zinashindwa kukusanya ushuru huo kwenye makampuni ya madini kutokana na mikataba ya madini kuwa siri. Mbali na hilo, Serikali ilingia makubaliano ya hiari na Makampuni ya Madini kinyume na MDA lakini si makampuni yote yanayotoa tuzo ya Dola 200,000 na hata zile Halmashauri zinazopata ile asilimia 20% haifiki chini kwenye mitaa au vijiji ambavyo ardhi yake ina madini.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni ni wakati muafaka kwa vijiji ambavyo ardhi yao ina madini viwe na hisa moja kwa moja kwenye Kampuni za Madini? Hii itachangia kupunguza matatizo yanayotokea kwenye makampuni ya madini na wananchi wanaozunguka migodi. Hii itasaidia vijiji hivyo kujinua kiuchumi, kuboresha miundombinu yao na hata kuwasaidia wachimbaji wadogowadogo.

MHE. MANSOOR S. HIRAN: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia kwa mdomo kwa sababu muda haukutosha, naomba niweze kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, madini. Tafadhali Waziri angalie upya mikataba ya migodi mikubwa ya dhahabu. Mimi nashangaa wawekezaji wakubwa wanakuja nchini, wanafanya utafiti halafu wanakwenda kwenye mabenki kuomba mikopo ya fedha, hii inathibitisha kwamba migodi inaanizhwa kwa sababu kuna dhahabu. Hii migodi ina wawekezaji wawili, Mtanzania ametoa ardhi na dhahabu, mwekezaji amekuja na pesa ya uendeshaji, je, kwa nini sisi hatuna ubia ndani ya migodi hii?

Mheshimiwa Spika, dunia inatushangaa sisi tunauza madini yetu au dhahabu yetu bure tunachotoza ni ushuru au *royalty* ya 3.4% je, ile dhahabu haina bei? Saudi Arabia wanauza mafuta, wawekezaji wapo wa kuendesha mitambo ya kuzalisha mafuta, lakini Serikali inauza mafuta kwa hizo kampuni na hiyo kampuni hutoza gharama za uzalishaji tu. Naomba kujua dhahabu inauzwa kwa bei gani na Serikali ya Tanzania? Je, mbona wanashindwa kuleta hapa Bungeni hiyo mikataba ya migodi mikubwa?

Mheshimiwa Spika, umeme. Nashauri muelekeze Mifuko mikubwa ya Fedha ya Wafanyakazi, wawekeze kwenye miradi ya kuzalisha umeme, mfano kujenga bomba la gesi kutoka Kusini mpaka Dar es Salaam ambayo yake ilikuwa ni USD 120 Millions. Hii inaweza kujengwa na NSSF au mifuko mingine yoyote, hizo pesa wanazo, hata kununua mitambo ya uzalishaji umeme wangenunu na kuingiza umeme TANESCO.

Mheshimiwa Spika, mafuta. Nashauri 6PSifanyiwe utafiti wa ndani zaidi na pia makampuni ya Watanzania pia yapewe kipaumbele kwa hii miradi mipya ili sisi Watanzania tuweze kumiliki miradi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA OTHMAN ALI: Mheshimiwa Spika, suala la umeme ni mtihani hapa kwetu Tanzania. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu katoa tamko rasmi hapa Bungeni, naomba hilo suala lifanyike pindi itakapofikia ule muda alioahidi ili Watanzania wapunguze midomo kwa suala hili.

Mheshimiwa Spika, bili za umeme haziendani na matumizi tunayotumia majumbani. Unakuta bili umeletewa kama nyumba ni kiwanda au tunaponunu Luku inakimbia sana kutumika (harakaharaka). Naomba suala la umeme litakapokaa sawa na hili pia liangaliwe sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifuatilie umeme kule Zanzibar pale palipoharibika mwaka jana ili tatizo kama lile lisije kutokea tena.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, ukipima katika wasemaji wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi, malalamiko yao ni nishati ya umeme na kidogo wachimbaji wadogowadogo wa madini. Leo mimi nitajikita katika suala zima la uzalishaji umeme Mtera na Kidatu, hasahaha *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba Mheshimiwa Waziri ameordhesha miradi mingi itakayozalisha umeme ili kukabili upungufu uliopo kwenye gridi kama alivyoainisha MW 100 Aggreko zitapatikana Agosti, MW 160 Ubungo na kadhalika lakini katika hotuba yake hakuna mahali panapozungumzia kitakachotokea endapo mitambo ya Mtera na Kidatu itakapozimwa kutokana na kina cha maji kwenye mabwawa kumalizika. Hadi Jumamosi 16/7/2011, Bwawa la Mtera lilibakiwa na sentimita 74 tu usawa wa bahari kwa maana ya 690.74 ambapo kina cha chini kabisa ni sentimita 690 na hiki kikifikiwa lazima mitambo izimwe, kina cha juu ni sentimita 698.50. Mtambo wa Mtera ukizimwa baada ya wiki moja au mbili ni lazima mitambo ya kituo kikubwa cha Kidatu nayo izimwe.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya kina endapo mitambo hiyo itazimwa, *TANESCO* wanadhani nini baada ya siku 38 zilizobaki kwa matumizi ya sentimita mbili kila siku. Je, kutakuwa na athari gani ya uzalishaji wa umeme kwenye gridi ya Taifa, hatujui mvua zitanyesha lini ili kuongeza maji katika mabwawa hayo. Hii miradi mipya ya Aggreko itakapokuwa tayari kupeleka katika gridi ya Taifa umeme mwingi utakuwa haupatikani kwa sababu Mtera na Kidatu imekauka, je, Serikali imejipanga vipi kujinasua na balaa hili? Napenda kujua hivi ni kweli Bwawa la Mtera limejaa matope ndiyo maana halitunzi maji?

Mheshimiwa Spika, hali mbaya ya kifedha ya *TANESCO*. Nimekuwa Bungeni tangu 1995, sijawahi kusikia Serikali ina hali nzuri ya kifedha labda miaka ya 1980. Tatizo la kifedha linatuathiri sana sisi Wabunge na wananchi kwa kukosa fedha za kununulia vifaa kama vile nyaya, *transformer*, nguzo na kujenga mitambo mipya ya kupozea umeme. Hivi sasa usambazaji umeme vijijini umesimama na hapa Waziri aniambie hii ni ahadi ya siku nyingi alishaitamka, nilipouliza hivi karibuni aliniambia mpango wa kupeleka umeme kutoka Tallo - *Kabila Centre* utatekelezwa mwaka huu wa fedha, naomba nipate kauli yake leo ndani ya Bunge kuhusu mradi huo. Mkurugenzi anaufahamu vizuri, Waziri, Naibu pia Afisa Habari Badru Masoud anaufahamu, naomba majibu lakini pia naiomba Serikali mambo yafuatayo iyatazame ili kuiimarisha *TANESCO* kifedha.

(i) Serikali ifikirie kutoa msamaha wa kodi ya kuagiza mafuta, vipuri vyta mitambo na vifaa vyta kuunganishia umeme mteja (*Import & Excise duties*). Hii itapunguza gharama za kuwaunganishia umeme wateja. Wabunge tunalalamika gharama za kuunganisha umeme ziko juu, hivyo Serikali iondoe kodi kwa vifaa hivyo.

(ii) Kwenye mikataba, Serikali ijivue "gamba". Ipo mikataba hadi leo ina utata, haina maelezo, mikataba ya kifisadi, haielezeki, migumu, jamani kisichobadilishwa ni Kur'an na Biblia tu, vingine vyote vinabadilishwa lakini hapa lazima kuwr na utashi wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya Songas na *IPTL*, naomba ipitiwe upya (*Reviewed*) kwa faida ya nchi yetu. Gharama zitozwazo, *capacity charges* ni kubwa mno. Vituo viwili Songas na *IPTL* hupokea si chini ya 10.985 bilioni kila mwezi kutoka *TANESCO* na hii ni balaa zaidi yaani wawe wametoa umeme kwa *TANESCO* au hawakutoa lazima walipwe, ukijumlisha na gharama ya ununuzi wa umeme (*energy charges*) kutoka makampuni hayo, Shirika linatumia zaidi ya 35% ya mapato yake yote kuilipa Songas na *IPTL* japo umeme ambao *TANESCO* inaonunua haufiki 30% ya umeme wote. Nashauri mikataba iwe *reviewed* ili iwe na tija,

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali ina tatizo gani kuamua baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara ya Nishati na Madini 2006 na 2009 wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa Ubungo akizindua *Ubungo Gas Plant*, Ngeleja aliambiwa '*live*' alisema *Diesel* ni ghali *IPTL* itumie gesi kupunguza gharama ukitumia gesi kwa kila *unit* zingepungua nusu (1/2) mfano tungenunua MW 20 badala ya kutoa 50 tungetoa 25, lakini Wizara na *TANESCO* siku zote imekuwa na kigugumizi. Jamani nami nauliza swalii nani mtu mzito yuko nyuma ya hilo ambaye hataki kulitekeleza? Ikumbukwe kama ni kweli yanayosemwa siku zao zimeishaanza kuhesabika.

(iii) Mheshimiwa Spika, *TANESCO* inafilisika kutokana na gharama za uendeshaji kwene vituo na Mikoa ambayo haina umeme wa gridi. Vituo hivyo ni kama Kigoma, Songea, Mpanda, Biharamulo, Ikwiriri, Ngara, Kilwa Masoko, Masasi, Ludewa, Liwale na kadhalika. Vituo hivi vinazalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito ya *Diesel*. Mitambo yake mingi imechakaa inahitaji vipuri na ukarabati wa mara kwa mara. *TANESCO* inatumia pesa nyingi kuhudumia vituo hivyo wakati uzalishaji wa mapato ya vituo hivyo ni mdogo. Gharama za uzalishaji umeme Mikoa minne ya Kigoma, Ruvuma, Rukwa na Kagera mwaka 2009 zilikuwa shilingi 48 bilioni wakati mapato baada ya wateja kulipa bili yalikuwa Shs.14 bilioni, *TANESCO* ilipata hasara ya Shs.34 bilioni (2009). Mwezi Juni mwaka jana (2010) *TANESCO* Songea ilitumia shilingi 729 milioni, mapato ni shilingi 171 milioni, Rukwa gharama Shs.236 milioni mapato Shs.165 Milioni. Huu utaratibu tutaendelea nao mpaka lini, lakini kwa utaratibu huu hali ya kifedha *TANESCO* itakuwa nzuri lini? Tutawalaamu *TANESCO* bure kibashara hawaendelei kumbe biashara yenye ni kichaa.

Mheshimiwa Spika, asilimia 85 ya wananchi hasa waishio vijiji hawana umeme, wanatumia mkaa, kuni, mafuta ya taa, mabaki ya mazao (*crop waste*) kama za pamba, katani, nazi, miwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwenye kitabu cha Waziri, vifungu 67, 71, 157(e), vimezungumzia *Biofuel*, kimiminika, *biogas* na nishati mbadala. Mfano Tanzania ina akiba ya karibu MW 600 za umeme wa Joto Ardhi lakini sioni mpango wa kuendeleza nishati hiyo wakati nchi ya jirani wanatumia sana Joto Ardhi. Sioni mpango kamambe wa kuendeleza *Solar* wakati nchi yetu juu ni kila siku, miaka michache ijayo tutakuwa jangwa endapo ukataji miti kwa ajili ya kupikia utaendelea badala ya kutumia nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, najua suala la wachimbaji wadogowadogo amelikuta, wapo waliomtangulia lakini Mheshimiwa Rais alikmpeleka hapo kutatua migogoro ya wachimbaji madini, kutafuta suluhisho la muda mrefu la umeme, akiondoka aache alama (*legacy*) ya kuwa hapa alipokuwepo Ngeleja matatizo ya umeme na wachimbaji aliyamaliza kama siyo kuyapunguza. Kumbuka Rais amekuamini, alikuweka umsaidie na siyo umuanguushe, tumia ujuzi wako, chota na uzoefu toka kwa wazoefu ili utuokoe Watanzania katika giza, tumechoka kutukanwa. Nakutakia kila la kheri katika majumuisho, naomba nipaye majibu kwa yale niliyouliza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARET S. SITA: Mheshimiwa Spika, Serikali ileze mpango mkakati wa muda mfupi, wa kati na muda mrefu wa kumaliza tatizo sugu la ukosefu wa umeme unaoathiri uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina rasilimali nyingi za kuwezesha kumaliza tatizo la umeme nchini. Ni vema kukawa na mpango mkubwa badala ya midogomidogo mingi.

MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH: Mheshimiwa Spika, nimekipitia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, sikuona sehemu yoyote ile ambayo sisi kama Wilaya ya Mafia Wizara ina mpango wa kuondoa tatizo la umeme katika Wilaya ya Mafia. Pamoja na Mheshimiwa Rais alipokuja Mafia na kuahidi kuondoa na kuleta majenereta yenyewe uwezo wa kuzalisha *megawatt* nne lakini bado Serikali au Wizara haikuona umuhimu wa kuondoa tatizo hilo angalau kwa *megawatt* mbili. Hivyo naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja za Wizara yake aweke bayana kuhusu mpango huo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja hii.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, tatizo la mgao wa umeme katika Jiji la Dar es Salaam limekuwa kubwa sana na kusababisha shughuli mbalimbali zinazowapatia kipato wananchi walio wengi kusimama, hivyo kuzorotesha uchumi wa wananchi wetu na Taifa kwa ujumla. Baya zaidi ni kukosekana kwa umeme katika Hospitali ya Mwananyamala hivyo kusababisha kukosekana kwa huduma mbalimbali hasa za upasuaji, maabara, mochuari na kadhalika. Naomba sana Wizara kupitia *TANESCO* waliangalie jambo hili kwa makini sana ili

Hospitali hii ya Mwananyamala inayohudumia wagonjwa zaidi ya 150 kwa siku iweze kupatiwa umeme wakati wote. Pia TANESCO waangalie uwezekano wa kupunguza makali ya mgao katika maeneo ya Mwananyamala, Kinondoni, Magomeni, Mwenge na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, napenda nami kuchangia kwenye hotuba hii kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa umeme ni mhimili wa maendeleo ya Taifa, je, Serikali sasa haioni kuwa kuna haja ya kutunga Sheria kali na kuhakikisha kuwa vyanzo vya maji *especial* mito na mabwawa haviharibiwi?

(ii) Kwa kuwa tumekuwa na janga hili kwa kipindi kirefu sasa, je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kutumia ueme wa upepo na hasa ukizingatia kwenye nchi yetu tuna upepo wa kutosha?

(iii) Mwisho kabisa napenda kujua Serikali imejipanga vipi kuwafidia wananchi ambao wamechukua mikopo benki kwa ajili ya kufanya biashara ambazo *directly* zinategemea umeme hivyo kushindwa kulipa madeni hayo kutokana na hali halisi. Mheshimiwa Waziri Watanzania wanapenda kujua utawaambia nini katika suala hill hasa ukizingatia Serikali ni sikivu!

MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA: Mheshimiwa Spika, kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri inayoendelea kuchangiwa amezungumzia kuboresha maeneo yanayopatikana madini ili yaweze kusaidiwa kwa kuwawezesha wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Waziri katika orodha yake ya maeneo yanayotoa madini hajaonyesha maeneo yanayotoa madini yaliyopo Wilaya ya Ruangwa ambayo hutoa madini ya aina mbalimbali kama ninavyoonesha hapo chini licha ya Naibu Waziri kuja Ruangwa na kuona uzalishaji wa madini ya aina mbalimbali. Maeneo yanayozalisha madini:-

- (1) Namingo – Dhahabu, *Green Tourmalines*.
- (2) Nambilanje – Dhahabu.
- (3) Nandagala – Dhahabu.
- (4) Nankonjela – Copper, *Garnet*.
- (5) Manokwe – Safaya.

Mheshimiwa Spika, kwenye orodha yake maeneo haya hayajatajwa. Kama hayatambuliki, Serikali ina mpango gani wa kuyatambua maeneo haya ili wachimbaji wadogo waliopo huko waweze kunufaika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri kwani Wizara yake ni ngumu sana, ina mambo mawili makubwa na ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Naomba nami nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme. Historia ya mgao wa umeme Tanzania. Mgao wa umeme haukuanza leo kwa mujibu wa takwimu za TANESCO, mgao wa umeme ulikuwa katika miaka ya 1992, 1995, 1997, 2000, 2010 na mpaka hii leo, ni hatari sana. Kwa Serikali iliyo makini toka mwaka 1992 ingeanza kujipanga kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, umakini na nia njema ya Serikali bado haionekani katika sekta hii hasa katika suala la kuondokana na mgao huu wa umeme unaokwamisha maendeleo ya Taifa mfano:-

(i) Mwaka 2008/2009, Bunge liliidhinisha fedha za ununuzi wa *generator* 17 ili kuondokana na mgao wa umeme katika kipindi hicho lakini cha kushangaza Serikali ilitenga fedha za kununulia *generator* 5 tu.

(ii) Pia katika mradi wa Stiglers George, kwa Serikali makini hii sehemu ingekomboa uchumi wa Taifa katika nyanja zote. Stiglers Gorge ni chanzo cha maji kinachotosha kuhimili mahitaji ya nchi nzima kwani kina uwezo wa kuzalisha *megawatt* 1200 MW ambazo ndio mahitaji muhimu ya nchi kwa sasa. Jicho jingine la Taifa limulike Stiglers George kwa sababu kama Serikali itaamua kweli kuwekeza basi Taifa halitakaa kuzungumzia mgao tena.

(iii) Mtambo wa Ubungo (Dar es Salaam) jirani na *TANESCO* Makao Makuu. Ujenzi wake uligharimu jumla ya Shs.Bilioni 99.45 na ulianza rasmii kufua umeme tarehe 30/7/2008. Kituo hiki kina injini 12 zenye uwezo wa kutoa *megawatt* 102.5 (MW 102.5). Mpaka kufikia mwaka huu tarehe 30/7 kituo kitakuwa kina umri wa miaka mitatu tu toka kianze kufua umeme. Inasemekana kituo hakizalishi tena MW 102.5 kama ilivyokusudiwa na hii inatokana na uchache wa gesi toka Songosongo. Aidha, uwezo wa kutoa gesi kama ilivyokusudiwa haupo tena, kuna vinu havtoi gesi kabisa na vingine vinatoa gesi chache tofauti na kusudio. Naomba Waziri anipe ufanuzi kwa nini mambo haya yako hivyo?

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa za juujuu inasemekana gesi haitoki vizuri kwa sababu mabomba toka ardhini yanayosafirisha mpaka Dar es Salaam yamejaa kutu (*Rust*) tupu na suluhisho pekee ni kubadilisha mabomba hayo kuweka mapya, je, uvumi huu ni kweli? Naomba ufanuzi. Kama ni kweli ina maana kuwa vifaa hivyo vya awali ni feki vingekuwa imara Serikali isingekuwa na jukumu la kuingia hasara nytingine kubwa hivi.

(iv) Mheshimiwa Spika, *IPTL* imepunguza uzalishaji wa umeme na kwa mujibu wa Serikali ni kwamba kuna upungufu wa mafuta mazito. Wakati ikisema hayo imesahau kwamba inajenga kituo cha MW 60 Nyakato Mwanza kwa kutumia mafuta hayohayo mazito ambayo kwa Dar es Salaam ambako ni karibu na bahari *IPTL* imeshindwa kuyapata sijui Mwanza itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, kuna kila dalili Serikali itashindwa kuendesha mradi huu wa MW 60 Mwanza kwa sababu umbali wa Mwanza – Dar es Salaam, kwa usafiri tunaotegemea wa barabara ni gharama na shughuli ngumu kusafirisha mafuta mazito kupeleka Mwanza kwa kutumia barabara wakati wa hapa Dar es Salaam tu mafuta hayapo. Hapa inaonekana ni mradi mwngime unaolekeea kultitia hasara Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ulazima wa kuwa na mitambo ya kutumia mafuta mazito, swali la kujuliza kwa nini ipelekwe mbali sana (Mwanza)? Kwa nini isingejengwa Kibaha, Mlandizi au hata Chalinze ambako hata usafirishaji wake ungekuwa nafuu?

Mheshimiwa Spika, wakati nchi ikiwa bado haijajua nani mmiliki halali wa *Dowans* na nani wameitia hasara nchi kupitia mikataba ya kifisadi ya *Dowans*, tumeshuhudia mitambo ile wakiuziwa kampuni mpya ya *Symbion* na kubarikiwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Bi. Hillary Clinton. Watanzania wanahoji katika hili je, ni taratibu gani zilifuatwa? Ni taratibu zipi zilifuatwa kutangaza zabuni mpaka *Symbion* wakaibuka washindi na kuchukua mradi? Tafadhali Mheshimiwa Waziri naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla tumeshindwa kuliokoa Taifa katika uhaba wa umeme kwa Serikali kupuuuza mambo yafuatayo:-

(i) Kutosikiliza ushauri wa wataalamu wetu, Dkt. Idrissa Rashid alisema nchi itaingia gizani, je, sasa hivi tuko wapi?

(ii) Kutotenga bajeti mbadala kutatua tatizo.

(iii) Kuingiza siasa katika mambo ya msingi mfano ni kauli za Waziri kama umeme utakuwa historia wakati hana uhakika wa kitaalam.

(iv) Kutokuwa na sera na nia njema ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iimarishe Shirika la *TANESCO* kwa kuteua Bodi huru na Menejimenti ya wataalamu wenye uzoefu katika shughuli za umeme na kuwapa mkatuba wenye malengo yanayopimika (*management performance contract*). Sanjari na uboreshaji wa Menejimenti, Serikali izingatie uzoefu na mafanikio yaliyopatikana kwa nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwe na mgawanyiko ufuataao:-

- (1) Kuwepo kwa kampuni inayoshughulikia uzalishaji pekee (*electricity power generation*).
- (2) Kampuni nyingine kushughulikia usafirishaji pekee (*electricity power transmission*).
- (3) Kampuni nyingine zishughulikie usambazaji, masoko na mauzo ya nishati ya umeme (*electricity power distribution*) ili kuleta tija na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, madini. Eneo hili la madini lina matatizo makubwa sana. Baadhi ya matatizo ya Wizara katika sekta ya madini ni haya yafuatayo:-

- (a) Wizara kutoifanya marekebisho Sheria ambayo ingezuia makampuni ya Madini kutumia sehemu kubwa ya uwekezaji wao kama mkopo (*debt financing*), makampuni yaruhusiwe kama yana angalau mtaji wa 30%, 40% au 50%.
- (b) Athari za mazingira na afya ya wanadamu na wanyama vipewe kipaumbele, pale inapotokea wawekezaji kutojali maisha ya binadamu na viumbe wengine kwa mfano North Mara.
- (c) Zaidi ya kutekeleza Sheria, Serikali (*Local Government Authorities*) ambako migodi ipo, ijaribu kuratibu masuala baina yao na wawekezaji kwa njia rasmi ya kisheria kwa mfano mgogoro wa North Mara kwa mujibu wa ripoti, ilichangiwa na uzembe wa watendaji Serikalini ambao hawakuratibu makubaliano kimaandishi kati ya wamiliki wa leseni ndogo pamoja na Serikali za vijiji kwa upande mmoja na mwekezaji wa awali kwa upande wa pili. Hivyo kupelekea makubaliano hayo kutotambuliwa na makampuni yaliyokuja kumiliki maeneo hayo.
- (d) Fidia inapotolewa kwa wananchi inabidi iwe *realistic* katika mantiki kwamba wamiliki wa maeneo wafaidike na maliasili zao maana lengo la Serikali ni kuhakikisha wanapata haki zao na sio ubabe kwa mfano kijiji cha Pande B ambako wawekezaji wa Saruji (Tanga Cement) wamechukua eneo la kijiji heka 371 kuchimba mchanga ambao unatumika kwenye kutengeneza *cement* pesa zimeshalipwa takribani milioni 424, watu wa Mipango Miji wakishirikiana na uongozi wa Kata na Kijiji wamezila sasa wanakijiji wanadai haki yao. Jeshi la Polisi wanaenda usiku wanakamata wanaume kwenye kijiji hicho na kuwabambilika kesi, sasa hivi kijiji kizima hakina wanaume, wote wanalala porini kujificha, je, hii ni haki? Huo ndio uongozi wa kidemokrasia? Huku ni kutengeneza bomu ambalo litakapokujalipuka kuzimika kwake itakuwa ni shida sana.
- (e) Serikali/Wizara kutokuwa na mapitio endelevu ya Sheria za Kodi katika sekta ya madini (*on going review of Mining fiscal regime*).

- (f) Madini kutokuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa mfano mwaka 2008 ilichangia 2.6% na mwaka 2009 ilichangia 2.5% tu katika pato la Taifa. Mchango huo haulingani kabisa na madini tuliyonayo, yanayovunwa na uharibifu wa mazingira unaofanywa kwa uvunwaji huo.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapa pole, Mheshimiwa Ngeleja, Waziri pamoja na Nailbu wake, Mheshimiwa Adam Malima kwa kuongoza Wizara ngumu kama hii ambayo wamerithi matatizo matupu, kutoka kwa Mawaziri

waliowatangulia. Tunachowaomba wafanye kazi kwa juhudini na maarifa, ni imani yangututafanikiwa. Cha muhimu ni kuchambua hoja zenyetija na kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, pia ni muhimu kuwajali watu wetu ambao wanawapisha wawekezaji, kuhakiki kama wamelipwa fidia zao. Kwani katika mgodi wa *GGM*, kunaonekana kuna dhuluma ya wazi kwa wananchi. Maeneo ya Kata ya Mtakuja, Kijiji cha Nyakabale, kuna watu ambao walihamishwa na kupisha mgodi mnamo mwaka 2004. Uthamini huo ulishuhudiwa na wananchi (wenye mali), Afisa Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji cha Nyakabale, Afisa Ardhi wa Wilaya ya Geita, Mwakilishi wa Mgodi wa *GGM* na Mthamini, zilihesabiwa na kushuhudiwa na pande zote mbili, yaani wafidiwa na wafidaiji na viongozi wa Serikali nao wakashuhudia.

Mheshimiwa Spika, mfano Bwana Hamis Mgaja alithamanishwa mali zake kama hivi:-

- (1) Migomba (M) kiasi kilichotakiwa kulipwa 253 kiasi kilicholipwa 56 mazao ambayo hayakulipwa 197.
- (2) Migomba (Y) 106 iliyolipwa 56 pufungu 82.
- (3) Miti ya kuni 131 iliyolipwa 29 pungufu 102.
- (4) Miti ya mbao 330 iliyolipwa 73 pungufu 257.
- (5) Milonge 126 iliyolipwa 26 pungufu 100.
- (6) Katani 357 iliyolipwa 85 pungufu 272.
- (7) Nanasi 856 iliyolipwa 189 pungufu 662.
- (8) Mwembe mmoja iliyolipwa mmoja.
- (9) Nyumba mmoja haikulipwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo ndivyo alivyotendewa Christina Odira, huu ni udhulumati mkubwa, tunawafunza nini wananchi wetu? Au huu ndio usemi wa amani na utulivu au amani na uvumilivu. Mtu kudai haki yake kwa muda wa miaka saba? Waraka wa malalamiko uko mezani kwa Mheshimiwa Waziri. Naomba wakati wa majumuisho atoe kauli ya suala hili. Kwa kuwa viongozi wote wa Serikali wa chini, wameshaandika barua mbalimbali kwa Mkurugenzi Mtendaji wa mgodi wa *GGM* ambazo zilipitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Nyakabale, *WEO* wa Kata ya Mtakuja, Katibu Tarafa, Mkuu wa Wilaya ya Geita, tarehe 7/3/2008 lakini pamoja na hayo hakuna mafanikio. Ni nani ambaye atasikilizwa na wawekezaji hao ili wananchi hawa wapate haki zao? Kamishna wa Madini analijua hilo. Tafadhalni naomba majibu ya kina ni lini wananchi hawa watalipwa fidia zao. Siku hiyo naomba nami nitaarifiwe ili niwe shuhuda.

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Wizara hii kutufikiria umeme eneo la Kiseke, Wilayani Illemela, kwani nyaya za umeme mkubwa zimepita na eneo la Kiseke shulenii hapana umeme. Umeme umeenda *PPF* na hapa kati pamerukwa. Naiomba Wizara kuliangalia hilo, hawa nao wapate umeme, kwani ni machungu kuona umeme nyumba ya jirani yako nawe unauhitaji, pesa unayo lakini huupati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umeme mitambo yake kufungwa eneo la Nyakato, Jijini Mwanza lakini cha ajabu baadhi ya maeneo hayo maji hakuna tatizo umeme mdogo hauwezi kuendesha pampu kusukuma maji katika matenki ya maji. Matatizo hayo yamelikumba eneo la Nyasaka, Kangara na mengineyo. Pia huko kuna shule za bweni, wanafunzi 600 maji ya kusomba kwa gari, mabomba yapo tatizo ni umeme aibu. Stesheni ya umeme ipo Nyakato wananchi wa Nyakato hawapati maji kisa umeme hauna nguvu ya kuweza kusukuma maji, ni aibu tena fedheha.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kina, imeelezea malengo yenye kuhusisha maeneo takribani yote kuhusiana na madini, pia nishati. Mimi naona jambo muhimu sana ni kutia maanani suala la umeme Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya uzalishaji wa umeme (*energy power project*) ni vyema iwe *plant* kubwa zenyenye kuzalisha umeme mwingi na sio kuzalisha umeme kidogo na hivyo kufanya kuwa na vituo vingi vya uzalishaji wa umeme. Napendekeza Kusini Tanzania kuwe na *project* moja. Kaskazini Tanzania kuwe na *project* moja na Kati Tanzania kuwe na *project* moja ili kwa ujumla wake kuwa na utoshelevu wa mahitaji yote ya umeme Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inapata hasara kubwa sana kwa ukosefu wa umeme. Uchumi unashuka na uzalishaji unashuka. Kutokana na hali hiyo basi ni vyema kutumia vyanzo vyote vya uzalishaji wa umeme ili kuondokana kabisa na upungufu wa umeme na uwezo huo upo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme kule Zanzibar pia ni vyema kuwa na vyanzo vyake vya umeme kwa kutumia maji ya bahari, kwani Zanzibar imezungukwa na bahari tena zenyenye kina kikubwa cha maji hivyo, hakuna sababu hata moja ya kukosa umeme kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuna haja kabisa ya kuzalisha umeme kwa biashara na wa akiba nchini kwetu. Mpango huu ni muhimu sana kuingizwa kwenye bajeti ya Taifa. Rais wetu linamkera hili Mheshimiwa Waziri fanya juhudi kwa kuwatumia wataalam ili kupata ufumbuzi wa kudumu.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kutoa maoni yangu juu ya Wizara hii ya Nishati na Madini ambayo ni mionganoni mwa Wizara nyeti na muhimu sana juu ya kuendeleza uchumi wa nchi lakini pia na uhuishaji wa maisha ya Watanzania kiajira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na dhana nzima ya kwamba Wizara ya Nishati na Madini ni Wizara muhimu kwa Watanzania lakini utendaji wake ni mbovu na umekatisha matumaini ya Watanzania juu ya kuwafikisha kwenye maendeleo. Wizara hii illikuwa ni jicho la Watanzania juu ya kuona Tanzania imefikia wapi kimaendeleo lakini wapi Watanzania wanaangamia, wanapaza sauti kwenye chupa nyeusi iliyofungwa hawasikiki wala hawaonekani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ama inaingia mikataba mibovu na wawekezaji au kuna wajanja wanaingia mikataba na wawekezaji huku wakiwa na hisa zao katika mikataba hiyo kwa nyuma ya pazia wanafaidika na kujinufaisha wakiwasaliti Watanzania kimaendeleo. Daima wakibaki vinywani mwao na msamati wa Tanzania ni maskini kumbe ni Watanzania walio maskini lakini Tanzania sio maskini kuna wajanja wanaila.

Mheshimiwa Spika, utaamini vipi kuambiwa kwamba Tanzania ni maskini wakati nchi hii imejaliwa kuwa na madini ya *Tanzanite* ambayo ni madini pekee na hayapo katika nchi nyingine yoyote duniani. Ukiacha madini hayo, tuna Dhahabu, Almasi, *Uranium* na hata Shaba, hivyo umaskini wa Watanzania uko wapi kama si kwamba unatengenezwa kwa makusudi?

Mheshimiwa Spika, umefika wakati wa kuwaeleza ukweli Watanzania hatuwezi kuendelea kuishi kama hali ilivyo baada ya miaka 50 ya Uhuru na miaka 47 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Ni aibu na fedheha kubwa Tanzania leo kushindwa kimaendeleo na Seychelles ambayo inaendesha nchi yake kwa kutumia bahari na viwanda tu.

Mheshimiwa Spika, watu wanaendeleza nchi zao kwa kuzitumia rasilimali za Tanzania, wanachukua hapa mawakala, wanaotumika kuwapelekea ni sisi wenyewe Watanzania wanasafishia kwao na wanjitangaza wao kwamba ni wazalishaji wa Dhahabu, Almasi, Uranium na Shaba kama Wakenya wanavyojitangaza kwamba ni wazalishaji wa Karafuu wakati hakuna hata shina moja la Mkarafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusiwatake wawekezaji hawa kujenga viwanda vyao vya kusafishia hapahapa Tanzania ili kuendeleza kumpatia ajira Mtanzania? Hivyo kutakuwa na kosa gani kwa mali inayochimbwa na kupatikana Tanzania ikasafishwa Tanzania? Hivyo hatuoni kwamba ni dhahiri kuna watu wananaufaika na uwekezaji huu?

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nichangie suala la nishati na napenda niseme kwamba inaonekana suala hili la kukosekana kwa nishati ya umeme na kuendelea kuwa na umeme wa mgao kwa kipindi cha nusu karne na ushee tokea Uhuru ni la makusudi. Tusidanganyanye kama watoto sisi sote ni watu wazima na hili halihitaji taa wala tochi kwani lipo kweupe na analiona kila mmoja wetu lakini Tanzania tuna tabia ya kulindana sasa tutalindana hadi lini tena kwa dhuluma ya wazi wanayofanyiwa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina vyanzo vingi vya kuzalisha umeme na tukawa na umeme wa ziada ambao tungeweza hata kuwauzia majirani zetu lakini ajabu kubwa ya Tanzania tumebarikiwa na amani ambayo imetufanya tuwalinde hata wezi na wabadhirifu wa hicho kitu kinachoitwa amani. Tanzania tuna Mito, Maziwa, Bahari, Makaa ya Mawe na Gesi, vyote ni vyanzo tosha vya kuzalisha umeme lakini kutokana na kwamba tukishughulikia vyanzo hivyo maendeleo yatapatikana, mgao wa umeme utaondoka na Watanzania walio gizani miaka nenda miaka rudi watahoji ilikuwaje na waliozoea kulindana watakuwa hawana hoja za kujibu ndio ukaona bado wanang'ang'ania kwamba nchi iende kama ilivyo yaani kuondokana na mgao wa umeme Watanzania wakapata maendeleo kwao ni kosa.

Mheshimiwa Spika, ukiacha Mito, Maziwa, Bahari, Makaa wa Mawe basi hata hali ya hewa tuliyonayo Tanzania inaweza kuzalisha umeme wa kutosha lakini kwa sababu hatuna nia njema na Tanzania na Watanzania tumeshindwa kufanya la maana. Leo tunadiriki hata kupiga makofi kutaka Tanzania kuingizwe mitambo chakavu wakati Sheria hii ilipingwa katika Bunge hili hili mwaka 2004. Sheria hii imeletwa tena katika Kamati ya Uchumi na Fedha na haikuletwatwakati Bunge hili nasema kwamba endapo Serikali itaileta Sheria hii ili ipitishwe katika Bunge hili basi Watanzania waelewe rasmi kwamba Serikali hii ina malengo ya kuwamatiliza na kuwadumaza kimaendeleo na sio kuwakomboa na kuwatoa katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanataka maendeleo hawataki tena maneno ya ulaghai ambayo hayana tija kwao wala vizazi vilivyopo na vijavyo ni aibu kwa Tanzania ya leo kuendelea tena na umeme wa mgao, umeme usio tija, umeme ambao unaendelea kuua hata vifaa vichache vya wananchi wanavyojipatia angalau riziki zao katika makazi yao kwa kuzimiwa umeme wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba hata Naibu Waziri wa Nishati na Madini alipokuwa akijibu swal li nyongeza juzi ljumlaha asubuhi alisema kwamba mashine chakavu ya kusindika nyama haikidhi viwango vya kimataifa na hivyo haisafishwi tena kwenda nchi za Ulaya, hivyo ni dhahiri kwamba Tanzania, Serikali inakusudia kuifanya kuwa dampo la kufikishia mitambo chakavu. Tuelewe kwamba kuitisha Sheria ambayo ina malengo ya kuleta mitambo chakavu kwa ajili ya mahitaji ya umeme bado kuna lengo lilelile la kuua uchumi wa nchi na kupoteza fedha za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali iweze kukopa mabilioni ya fedha kusaidia bajeti za nchi lakini katika bajeti hiyo wasiweze kufikiria kwamba kuna haja ya kununua mitambo mipy ya kuzalisha umeme ili kuiondoa Tanzania na aibu ya kudumu ya tatizo la umeme? Bado nasema kwamba nia si njema katika kuwatumikia Watanzania, kuwatoa kwenye giza totoro la miaka yote ya uhuru hivyo tunaweza kusema kwamba Watanzania bado wako katika uhuru kandamizi dhidi ya maendeleo yao.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, *Geological Survey of Tanzania*, imekamilisha upimaji wa upatikanaji wa Madini ya Dhahabu na Almasi Wilayani Chunya mwaka 2008 katika Tarafa za Kwimba na Kipembawe hasa katika Kata za Ngwala, Lupa, Mafyeko na Kambikatoto. Upimaji huu umeonesha kuwapo kwa madini hayo kwa wingi sehemu hiso. Cha ajabu ni kuwa tayari vitalu vyote vimepewa watu na makampuni bila kuhuishwa, Vijiji, Halmashauri wala Serikali ya Wilaya. Kwa nini Kamishna wa Madini anagawa maeneo hayo bila

kuhusisha wananchi na Serikali zao? Pia maeneo ya wachimbaji wadogo yako wapi katika sehemu hizo? Kwa nini hayapo wakati Serikali ina sera ya kuwatengea maeneo wachimbaji hao?

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *PanAfrican* inayomiliki visima vya gesi huko Songsongo ina matatizo makubwa sana yafuatayo:-

- (a) Visima vilivyopo vina *corrosion*, lakini kampuni haitaki kukarabati visima.
- (b) Ina mahusiano mabaya sana na *TPDC* na Serikali.
- (c) Inakataa kushirikiana na Kampuni ya Ndovu ambayo ina kisima kiko tayari kutoa gesi kuisaldia *PanAfrican*.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanahatarisha sana upatikanaji wa gesi hapa nchini. Hata hii mitambo mipya sidhani kama itapata gesi! Serikali ina mpango gani wa kurekebisha haya? Pia Serikali ifanye haraka sana kuhakikisha kuna bomba lingine au mengine ya kusafirisha gesi kwenda Dar es Salaam. Serikali iwe na umiliki kwenye mabomba hayo na *PanAfrican* wasiruhusiwe kushiriki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Spika, nami naomba kuchangia katika hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha *RCC* Mkoa wa Dodoma, baadhi ya vijiji vifuatavyo ambavyo viro katika Wilaya ya Kondoa viro kwenye mpango wa kupatiwa umeme kuititia mradi wa *MCC*. Vijiji hivyo ni Dalai, Hamai, Mapango, Kinkima, Jangalo, Itolwa na Isusumya lakini katika kitabu cha bajeti cha Waziri ni vijiji viwili tu vya Dalai na Hamai vinavyoonyeshwa katika mpango huo wa *MCC*. Namwomba Waziri katika majibu yake anieleze na awafahamishe wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini kwa nini Vijiji vingine havikuonyeshwa na kama vimeondolewa ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa sasa imegawanyika na kuwa Wilaya mbili ya Kondoa na Chemba. Naiomba Serikali kuititia Wizara hii ya Nishati na Madini katika kutekeleza sera yake ya kupeleka umeme katika kila Makao Makuu ya Wilaya nchini izingatie Wilaya hizi pia.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha bajeti yake awatoe hofu wananchi wa vijiji vya Waida, Cheku, Sori, Kelema Balai na Paranga ambaao wana matarajio kuwa umeme utakaopelekwa Makao Makuu ya Wilaya ya Chemba utachukuliwa kutoka kijiji cha Nondo na kuititia vijiji niliyovitaja ili na wao wapate umeme huo kabla haujafika Chemba yalipo Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Chemba.

Mheshimiwa Spika, zipo tetesi zimeenea katika vijiji vya Mpendo, Kubi, Sanzana na Moto kuwa eneo hilo lina madini ya *Uranium* na wananchi hao wameingiwa na hofu kuwa wataondolewa katika maeneo yao ili kupisha uchimbaji wa madini hayo. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha haja yake anipe maeleo yatakayowafanya wananchi wa vijiji hivyo kuishi kwa amani.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie bajeti hii ya Nishati na Madini kwa kuanza na suala la bomba la gesi kutoka Mnazibay, Songsongo mpaka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa bomba la kusafirishia gesi kuja Dar es Salaam la Songsas limefikia kikomo kiasi kwamba hata mtambo wa Symbion hauzalishi kwa uwezo wake wote kwa kutopata gesi ya kutosha. Sasa kuna mpango wa kujenga bomba jipya kubwa la gesi kutoka Mnazibay kuititia Songsongo hadi Dar es Salaam ili kuwezesha mitambo mipya ya kuzalisha umeme iweze kupata gesi ya kuzalisha umeme. Mitambo mipya inayojengwa ambayo inategemea gesi kutoka bomba jipya ni ya Ubungo (Jacobsen) MW 100, Kinyerezi 240MW na Somanga Fungu 230MW.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo ni kwamba gharama za ujenzi wa bomba hili ni Dola za Kimarekani 25% ya *Equity* na 15% ya mkopo ambazo jumla yake ni Dola za Kimarekani Milioni 282. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali ilitakiwa kuchangia shilingi bilioni 131 fedha za Kitanzania ili ujenzi uanze lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, fedha hizi hazikutengwa katika bajeti ya mwaka huu na hivyo kuna uwezekano kuwa ujenzi wa bomba hili hautaanza. Ushauri wangu kwa Wizara ni kwamba, Wizara iwasilishe maombi maalum Hazina/Serikalini ili fedha hizi zipatikane na ikiwezekana Waziri aende kwa Rais ili hatua za makusudi za kupata fedha hizi zifanyike ili ujenzi wa bomba hili la gesi uanze haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa bomba hili ni kwamba, lisipojengwa basi ina maana kuwa mitambo ya kuzalisha umeme inayojengwa haitaweza kuzalisha kabisa umeme kwa sababu haitakuwa na gesi. Mitambo mipyä inayojengwa ule wa Ubungo (Jacobsen) 100MW, Kinyerezi 240MW na Somanga Fungu 230MW, havitaweza kuzalisha umeme kabisa ikiwa bomba hili jipyä la kuleta gesi kutoka Mnazibay, Songosongo hadi Dar es Salaam halijatengwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara pamoja na Serikali kuachana na mlolongo wa miradi na badala yake wajikite kwa awamu kwenye mradi mkubwa. Wakati wanaendelea na mradi huo mkubwa watafute wawekezaji wengi wawekeze na wawauzie umeme *TANESCO* hii itasaidia sana kuepukana na kukatika umeme kwa kuwa watakuwa wengi na watalipwa jinsi watakavyouza. Hili linafanya na nchi nyingi sana siyo Tanzania ndio itakuwa ya kwanza, Dubai wanafanya hivyo na nchi zingine nyingi wanafanya pia. Itasaidia kupunguza mzigo wa kutunza mitambo mingi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa Wizara kwa jinsi wanayo jitahidi kusambaza umeme vijiji na kuondoa tatizo la mgao wa umeme. Mimi ni kati ya watu ambao tumepata umeme ambapo hivi sasa unarekebishwa kutoka Old Shy – Salawe, pamoja na Sekondari ya Samuye, Itwagi, Isela na Kituli.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua kwa mwekezaji *Barrick* ambaye sasa ataanza mradi wa kuchimba na kunufaika na madini yetu katika Kata ya Mwakitalyo na tayari zoezi la tathmini limeshaanza na imekamilika. Tatizo kubwa ambalo linajitokeza ni namna ambavyo Serikali inachukua maamuzi ya kutoa leseni kwenye Makampuni makubwa kama haya bila kushirikisha Halmashauri husika pamoja wananchi ili kama kuna maombi ya wananchi wanaweza kusema na Halmashauri ikasaidia katika suala zima la tathmini ili wanaoweza au wanaopaswa kulipwa waweze kulipwa vizuri. Sasa hivi tayari kumeanza kero ya wananchi kuwa na wasiwasi wa kulipwa tathmini kidogo tofauti na matarajio yao.

Mheshimiwa Spika, kero nyingine ni Kampuni moja ya Kichina ambayo hivi sasa Kampuni hii wameanza zoezi la *exploration* katika Kata ya Mwakitalyo na baadhi ya vijiji ya Kata ya Salowe. Wanapokuwa katika zoezi la utafiti wanaingia kwenye nyumba za wananchi bila ridhaa yao na kuweza kuingia na kufanya kazi kwenye maeneo yao bila ruhusa ya wananchi, hili limesababisha kero kubwa sana. Cha ajabu walikuja hapo bila *RC*, *DC* au Mkurugenzi kuwa na taarifa ya uwekezaji wao. Naomba Wizara itueleze hao ni wawekezaji gani? Kwa nini wamekuja bila taarifa kwa *DC*, *RC* au Mkurugenzi? Naomba sana suala hili lifuatiliwe vizuri. Nashauri sasa kwanza Halmashauri ishirikishwe vizuri kwenye uwekezaji wowote kama huu ili kama kuna tatizo tuweze kutatua vizuri kwa pamoja na kwa ridhaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la mgao wa umeme, ni mkubwa sana, ni muhimu sasa Serikali ikachukua hatua za dharura za kutatua tatizo hili. Naamini kabisa Serikali inafuatilia vizuri. Hakuna mwekezaji ambaye atawenza kuwekeza kama hakuna umeme, hivyo ni muhimu sana hata kwenda kuomba msaada nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, naamini niliyoyasema yatafanyiwa kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

MHE. RAMADHAN HAJI SALEH: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujalia kuwa hai na salama hadi hivi sasa. Pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake mahiri yenye mwelekeo wa maendeleo ya ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme ndio chanzo kikubwa cha maendeleo ya nchi yetu, bila ya kupatikana umeme maendeleo yatabakia kuwa ni ndoto. Nashauri hebu Mheshimiwa Waziri awatupie jicho Watendaji wake ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara ili tuweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na uagizaji wa mitambo midogomidogo kiholela ambayo inapoteza hela nyngi kiasi ambacho utendaji wa mitambo hiyo hauonekani. Sasa napenda kushauri kuwa tungejaribu kununua mitambo mikubwa yenye *megawatt* nyngi hata kama itakuwa bei yake ni kubwa, kuliko kununua mitambo midogomidogo, ni hasara.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee katika sekta ya Madini. Madini yetu yanapotea kwa kasi, Tanzania haifaidiki na sekta hiyo ya madini, wageni wanachukua madini na kutuachia mashimo. Napendekeza Serikali ipitie upya mikataba ya madini ili nchi yetu ifalidike pamoja na wananchi ambao wamezungukwa na migodi hiyo. Wananchi ambao wamezungukwa na madini, wako katika hali mbaya kiasi kwamba maisha yao yamekuwa ni duni lakini kama mikataba itapitiwa upya basi wananchi hao watafaidika vizuri.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Wachimbaji Wadogowadogo, naomba ipitishwe ili Serikali yetu itokane na lawama kwa wananchi wao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MUSSA HASSAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja ilio mbele yetu asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kutokana na umahiri wao na uvumilivu wao katika kuendeleza Wizara nyeti na yenye kubeba ustawi wa nchi yetu, nawaomba waendelee kuwa na moyo wa subira.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukosefu wa umeme limekuwa ni la muda mrefu sasa na limeelekea kuwa janga la Taifa. Wizara haioni kuwa ni vyema ikakaa kwa dharura ikafanya mambo mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuwa na mpango mkakati, kwa kuelewa kwamba kuna vianzio tofauti vya umeme kama vile Mkaa, maji, upepo na kadhalika. Aidha kunahitajika utaalamu wa hali ya juu kufanikisha na kuendeleza (*sustainability*), aidha, fedha nyngi zinahitajika katika kutekeleza suala hili.

Mheshimiwa Spika, nashauri, kwa vile suala hili ni muhimu sana kitaifa ingelikuwa ni busara likapewe kipaumbele na Serikali Kuu ili maamuzi yatakayotolewa basi iwe ni suala linalojulikana kitaifa na usiwe mzigo wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ingeshauri Serikali Kuu kuangalia na kuona inatolewa elimu kwa wananchi ya kueleweshwa gharama na ufundu ni sehemu moja lakini pia matumizi ambayo yako nje ya uwezo wa kibinadamu ni mionganoni mwa mambo ambayo yanakwaza ufanisi au utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, la mwisho si kwa umuhimu, naiomba sana Wizara kuangalia kwa kina umuhimu wa uhusiano wa Serikali mbili, Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kuelewa kwamba suala la umeme ni mionganoni mwa kero zinazoashiria udhaifu wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, narejea kuunga mkono hoja na kwa heshima naombaa kuwasilisha.

MHE. EUGEN E. MWAPOSA: Mheshimiwa Spika, naombaa kuchangia bajeti ya Wizara iliyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri, Watumishi na Serikali kwa ujumla kwa kuandaa bajeti iliyowasilishwa pamoja na changamoto zilizopo katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa tangu Wizara hii ikabiliwe na changamoto ya kutoweza kuzalisha umeme wa kutosha jambo lilichangia sana katika kudorora kwa uchumi na kushusha kipato cha Serikali, wajasiriamali na Watanzania kwa ujumla wao. Katika kupambana na changamoto hii, Wizara imeainisha miradi mingi inayotarajiwa kuanzishwa na kumaliza ile ambayo ilishaanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri Wizara hii kuachana na huu mpango wa kuwa na miradi mingi ambayo kwanza ni gharama kusimamia kwa sababu ipo mbalimbali na badala yake kuchagua mradi mmoja utakaozalisha umeme utakaokidhi mahitaji ya umeme unaohitajika kwa sasa. Hii itasaidia Wizara kuweza kusimamia kwa karibu na kuelekeza nguvu na mipango yake yote katika mradi huu ili kuweza kuhakikisha mradi huo unafanikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naombaa sasa nijielekeze katika mpango mzima wa Wizara katika kusambaza umeme kwa mwaka 2011/2012. Katika mpango wa Waziri, nasikitika kuwa pamoja na JIMBO langu la Ukonga, Dar es Salaam kuwa pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam na ni Jimbo linakua na kuamiwa na wananchi wengi na hata Serikali inaangalia Jimbo hili katika kuhamishia wananchi wake kama ilivyofanya kwa wananchi kutoka Jimbo la Segerea, Kata za Kipawa na Kiwalani, hakuna mpango wowote wa kuleta umeme katika baadhi ya Kata na vijiji ambavyo havina kabisa umeme.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ukonga kutoka Ikulu kuna kilometra ambazo hazizidi 18 lakini cha kusikitisha sehemu kubwa hakuna umeme. Ni aibu kwa Serikali na Wizara pia. Jimbo hili liko katika Wilaya ilipo Ikulu ambayo kwa maana au maneno mengine ndiyo Tanzania, kukosa umeme na Wizara kutoweza hata kutambua hili na kuweka mpango wa kusambaza umeme kwa baadhi ya sehemu katika mwaka mzima wa fedha, ni kutokuwa makini na kutonitendea haki mimi na wananchi wa Jimbo langu la Ukonga.

Mheshimiwa Spika, namwombaa sana Waziri ahakikishe kuwa sehemu za Jimbo ambazo hazina umeme zinaingizwa katika mpango wa kupewa umeme katika mwaka huu wa fedha. Sehemu hizo ni pamoja na Kata nzima ya Msongola, Ulongoni, Kimwani, Viwege, Kinyamwezi, Ngobedi, Nzasa, Nyanunu na Bombambilii. Nahitaji majibu ya jambo hili wakati wa majumuisho ili niweze kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kusimamia ukamilishaji wa ujenzi wa njia ya umeme kati ya Mtwara hadi Tandahimba. Hata hivyo, napenda kupata maelezo ni kwa nini hakuna mradi wowote wa kuunganisha umeme kwenye Viji ya Mkoa wa Mtwara hasa kati ya Mtwara – Tandahimba – Newala ambako *line* ya umeme inapita tena sehemu zingine kama vile Kitama kupita juu ya majengo ya Sekondari huku Sekondari hiyo ikihitaji sana umeme. Aidha, kama wanasiasa tumeunadi sana mpango wa kuunganisha umeme kwa wananchi kwa bei nafuu (ya chini ya shilingi laki moja) lakini kukiwa hakuna kinachoendelea, nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, ni lini *TANESCO* Mtwara itapewa uwezo ili iweze kuunganisha/kufunga umeme kwenye nyumba mbalimbali kufuatilia maombi mengi ya wananchi lakini pia gharama zikiwa zimepunguzwa?

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Waziri, ukurasa wa 66, anataja Mikoa 16 ambayo Wakala wa Nishati Vijiji na itaratibu na kutekeleza mradi kabambe wa kusambaza umeme vijiji na kuacha Mkoa wa Mtwara wenye uhakika wa umeme wa Gesi asilia ya Mnazibay. Napenda kupata maelezo ya kina kwa nini Mtwara imeachwa?

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake, Mheshimiwa Waziri amenukuu maelekezo ya Mpango wa Maendeleo wa 2011/2012 – 2015/2016 ambako Serikali imepanga kuongeza umeme kufikia MW 2,780 na kuboresha njia za usafirishaji na usambazaji. Mpango huu ni mzuri, hofu yangu hatujawa na mkakati madhubuti wa kufanikisha nia hiyo ya Serikali. *What we have most of the time is a wishful thinking.* Hali hii haiwezi kutusaidia, lazima tuwe na mkakati wa kueleweka. Haiwezekani tukawa na mipango mingi lakini mwisho wa siku hakuna mafanikio tunayoyaona.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010/2011, ilipanga kujenga mitambo ya kufua umeme wa MW 100 Ubungo na MW 60 Nyakato, utekelezaji wa miradi hiyo hakuna. Pengine Serikali ingejipangia mradi mmoja ingeweza kufanikiwa. Hivyo ushauri wangu naomba tuwe na mradi mmoja badala ya miradi mingi ambayo hatuwezi kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la umeme ni kubwa na sasa linakaribia kuwa janga la Taifa, naomba Serikali yetu ifanye uchunguzi wa kina hasa ishirikishe vyombo vyake vya ulinzi na usalama ili kubaini sababu halisi ambazo zimepelekea bwawa la Mtera kutokujaa maji. Kwa kweli inashangaza kuona kipindi hiki cha Julai, bwawa halina maji. Mimi naamini huenda shughuli za kilimo katika mashamba ya chai ndiyo chanzo cha bwawa kutokujaa maji. Naiomba Serikali ichunguze kwa makini sababu ambazo zimefanya bwawa la Mtera kutokuwa na maji ya kutosha hata nchi yetu kuwa katika giza.

Mheshimiwa Spika, napenda nishauri kwamba kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yamesababisha mabadiliko katika hali ya hewa, naomba Serikali ione umuhimu wa kuzalisha umeme unaotokana na makaa ya mawe. Ziko nchi zilizofanikiwa sana katika umeme wa makaa ya mawe kama China. Nashauri tuziombe zitusaidie. Hata hivyo nashauri tuwe makini katika mikataba ili nchi yetu inufaikie na rasilimali hii ya makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa gesi, naomba Serikali ishirikiane na nchi rafiki kama Urusi katika kuzalisha gesi ambayo itachangia uzalishaji wa umeme. Pia nashauri wataalam wetu wawe makini kwenye eneo la mikataba.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, iwapo nchi yetu itaingizwa kwenye mikataba isiyokuwa na maslahi, wahusika wachukuliwe hatua za kisheria na ikithibitika kwamba wameilingiza nchi kwenye mikataba isiyo na manufaa kwa maslahi yao, naomba wafilisiwe na wafungwe maisha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini, nashauri Serikali ihakikishe inatekeleza azma yake ya kuipitia mikataba yote iliyoingia Serikali na Makampuni mbalimbali. Baada ya mapitio hayo, Serikali iwaambie Watanzania hali halisi ya mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba watu wamwogope Mungu. Binadamu akiishi ni miaka 70 au 80 ambayo ni ya shida na tabu. Pia tukumbuke kwamba binadamu akipata utajiri wote wa dunia hii, lakini baada ya kufa roho yake ikaenda motoni atafaidika na kitu gani? Watanzania tunaponung'unika maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu atatoa adhabu kwa wanaonung'unikiwa. Nashauri tuwe waadilifu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ihakikishe madini yetu yanaibadili Tanzania kutoka nchi maskini hadi kuwa nchi tajiri. Madini ya Tanzania ni stahiki ya Watanzania na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa kuwa nchi iko katika harakati za kutekeleza mpango wake wa 2011/2012 – 2015/2016, naomba Sekta ya Nishati na Madini iwe ndio nguzo ya kufanikisha azma hii. Sekta zote zinategemea Wizara hii. Hatuwezi kulima, hatuwezi kuwa na biashara, viwanda, utalii, huduma nzuri za afya, elimu na kadhalika bila utegemezi kwenye Wizara hii. Naomba nguvu zote zielekezwe katika kuisaidia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Watendaji wanapozembea, nashauri wawajibishwe. Bila ya kuwajibishana, hatuwezi kutekeleza mpango wetu wa maendeleo wala Dira ya Taifa ya 2025.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote waliohusika katika maandalizi ya bajeti hii. Najua kuna changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hii hasa kukatikatika kwa umeme. Hata hivyo, nataka niamini kwamba changamoto hii pamoja na nyingine zitatuliwe mapema inavyowezekana ili shughuli za uchumi zisiendelee kuathirika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda nichangie katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kupanda bei mafuta ya taa. Hivi karibuni, Serikali ilipandisha bei ya mafuta ya taa kutoka wastani wa Shs.1,500/= hadi wastani wa Shs.2,080/= karibu sawa na bei ya mafuta ya *diesel*. Sababu zilitolewa na Serikali ni kwamba inataka kukabiliana na uchakachuaji. Naamini sababu zinazotolewa na Serikali zinaonyesha udhaifu wa Serikali yenewe katika kudhibiti uchakachuaji mafuta. Udhaifu wa Serikali unasababisha wananchi maskini wa Tanzania kupandishiwa bei ya mafuta ya taa kwa kiwango kikubwa kiasi hicho. Nashauri Wizara hii iendelee kuona kwamba waliopewa adhabu ni wananchi maskini, hivyo uamuzi huo wa Serikali uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, pili, Makaa ya Mawe Magamba – Mbozi. Utafiti wa makaa ya mawe Magamba – Mbozi umeanza zaidi ya miaka sita iliyopita. Katika kipindi hicho, tani (*tones*) nyingi sana za makaa hayo zimekuwa zikisafirishwa nje ya nchi kwa kile kinachoitwa kufanya utafiti makaa hayo. Wananchi wanaauliza, utafiti huo utaisha lini? Je, Serikali yetu inafaidikaje na makaa hayo? Je, kwa nini kampuni husika isihusike katika matengenezo ya barabara za Vijiiji na Wilaya ambazo hutumika kusafirisha makaa hayo? Uzingatia kwamba magari yanayotumika ni makubwa sana kiasi kwamba hufanya uharibifu mkubwa sana kwa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wilaya ya Mbozi kuunganishwa na umeme wa Zambia. Wilaya Mbozi huko nyuma ilikuwa inatumia umeme kutoka Zambia. Baada ya kuunganishwa kwenye Grid ya umeme ya Taifa, hatukuendelea kutumia umeme wa Zambia.

Mheshimiwa Spika, kwa kizingatia tatizo kubwa la umeme lilipo nchini sasa, nashauri Wilaya ya Mbozi iunganishwe tena na umeme kutoka Zambia. Miundombinu yake bado ipo, suala ni kwa Serikali ya Tanzania kuzungumza na Serikali ya Zambia ili kuingia mkataba mpya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono, nawasilisha.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru Wizara hii kwa kuandaa bajeti na mwelekeo wa utekelezaji wa miradi mbalimbali katika kipindi cha 2011/2012. Pia nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya kwa kuwatafuta wawekezaji ambao wameweza kuchimba gesi Mkoani Mtwara na kutuwezesha kupata umeme wa uhakika katika Mkoa wetu wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kazi iliyofanyika ni kubwa sana, kazi ambayo wananchi wamekuwa na matumaini makubwa sana ya kupata wawekezaji watakaoweza kujenga viwanda mbalimbali na vijana wetu kuweza kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile wananchi, wafanyabiashara na wajasiriamali wataweza kutumia umeme huu katika uzalishaji mali, hivyo kupunguza umaskini na kuweza kumudu kuendesha maisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi za kuleta umeme katika Wilaya ya Masasi hasa Jimbo langu la Masasi, umeme huu umekuwa ukikatikatika kila mara, lakini pia njia ya umeme kutoka Nanganga, Nangoo, Ndanda, Mwena, Chigugu, Chikukwe nguzo za umeme zimekuwa zikianguka kila wakati, hivyo kupelekea kukosa umeme katika vipindi mbalimbali kutokana na uchakavu wa nguzo hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu pamoja na kuwa Mtwara ina umeme wa uhakika katika bajeti hii haijonyesha mpango wowote wa kusambaza umeme vijiji, lakini Wizara imetenga fedha ya kusambaza umeme katika Wilaya ambazo hazina umeme wa uhakika, Serikali haioni kwamba mpango huu walioouweka ni mpango ambao hautazaa matunda kwani huko walikoelekeza nguvu umeme haupo?

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu huu ningeomba sana Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake anipatie majibu yafuatayo:-

- (a) Kwa nini Mkoa wa Mtwara hasa Masasi haikupangiwa bajeti ya kusambaza umeme vijiji?
- (b) Lini Serikali itafanya marekebisho ya nguzo za umeme toka Mtwara, Masasi ili tuendelee kupata umeme bila tatizo?
- (c) Marekebisho ya bei za kuweka umeme majumbani itapunguzwa lini na kwa kiwango gani?

MHE. DK. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Spika, katika mipango ya kuzalisha umeme wa kutosheleza mahitaji ya Kitaifa vyanzo mbalimbali vimetajwa na Serikali. Hata hivyo, vyanzo hivi ambavyo viko katika hatua mbalimbali havihitaji chanzo cha joto ardhi. Chanzo hiki ni kizuri na utafiti unaonesha kwamba tunayo maeneo sita nchini ambayo yanaweza kuzalisha hadi *Megawatt* 2000 au zaidi. Jirani zetu Kenya hadi sasa wanazalisha *Megawatt* 145 na bajeti yao ya mwaka huu wanatarajia kuzalisha *Megawatt* 105 za ziada. Naishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuwekeza zaidi katika chanzo hiki kwani ni cha kudumu na hakina athari kubwa kimazingira. Uzoefu wa Orikalia huko Naivasha, Kenya unaonesha kwamba umeme huo ni rahisi sana kwani shimo moja linalogharimu *USD* 5,000,000 hadi 7,500,000 linazalisha hadi *Megawatt* 10 tofauti na vyanzo vingine ambavyo ni ghali sana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ichukue hatua za dharura na makusudi ili kuanza utafiti wa urefu wa mashimo, aina ya mitambo ya kutumia aina ya gesi mbalimbali hatarishi zilizomo katika maji mvuke (*vapour*) itakayotumika katika mashimo hayo. Ikumbukwe kwamba nchi zilizoendelea karibia zote ambazo zimekuwa na uwezekano wa kutumia joto ardhi zimefanya hivyo (Marekani, Japan na kadhalika).

Mheshimiwa Spika, napendekeza utafiti uanze mara moja katika maeneo haya sita na tathmini za athari za mazingira na jamii zianze kufanyika mara moja. (*Environmental and Social impact Assessment*).

Mheshimiwa Spika, mwisho, mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vya Jimbo la Buchosa wa *MCC* hautagusa vijiji katika Kata tatu za Lugata, Nyakasasa na Kata ya Maisome. Waziri wa Nishati na Madini aliwaahidi wananchi wa Buchosa katika mikutano ya hadhara kwamba umeme utavushwa kuingia Kisiwani Kome katika miradi ya umeme ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nataka kupata uthibitisho wa Serikali kwamba ahadi hiyo ya Serikali bado iko palepale na kwamba sasa utekelezaji utaanza katika mwaka huu wa fedha 2011/2012.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Ngorongoro ndiyo kwanza inapata umeme wa jenereta tangu uhuru wa nchi hii mwaka 1961, ni wajibu wangu kuipongeza Serikali kwa hatua hii licha ya kwamba kuna tatizo kubwa la nishati ya umeme nchini katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro Loliondo na Mji Mdogo wa biashara Warso wataanza kunufaika na umeme wa jenereta nne kubwa na kuzalisha *Megawatt* tano kwa pamoja ambao ni umeme mwingi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kazi kubwa inayoendelea sasa ni ya ujenzi wa miundombinu, uwekaji wa nguzo, usambazaji au ufungaji wa nyaya za umeme na umeme kuwashwa Septemba 2011. Namwomba Mheshimiwa Waziri Ngeleja awe mgeni rasmi siku ya uzinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia maji ya mto Pinyinyi yafanyiwe upembuzi ili kupata chanzo kingine cha nishati ya umeme kwa ajili ya vijiji vya eneo la *Lake Natron*.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iangalie uwezekano wa kupunguza gharama kwa wananchi, kuvuta umeme katika nyumba zao na taasisi za umma kama shule, hospitali, polisi, magereza na kadhalika kufanya hivyo, itawavutia wateja wengi zaidi, (hata wale wenye uwezo mdogo) na ndio hasa lengo la Serikali, wananchi wengi waweze kutumia umeme hususan wanaopata umeme kwa mara ya kwanza baada ya miaka 50 ya Uhuru.

MHE. SELEMAN S. JAFO: Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke utaratibu wa kuwawezesha wananchi wa vijiji kuwaunganishia umeme kwa unafuu ikiwezekana waunganishiwe umeme halafu gharama za uunganishaji zingizwe katika malipo ya bili zao za mwezi ili watu hawa wapate fursa ya kupata nishati hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iharakishe uwekaji wa nguzo na nyaya kwa umeme unaolekea Kisarawe vijiji. Kwa kweli naipongeza sana Serikali kwa kuanza kupeleka nguzo mpaka Maneromango hadi Msanga. Kwa kweli naipongeza sana Serikali kwa jambo hilo. Sasa naiomba longeze *speed* ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye maamuzi ya kurekebisha kanuni ili iweze kununua mitambo iliyotumika kwa ajili ya kutatua tatizo la umeme nchini mwetu.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, ombi maalum kupatiwa umeme wa mwanga wa juu katika sekondari 21, Wilayani Serengeti kwa dharura. Hii ni kutokana na msaada mkubwa wa kompyuta 165 tulizopata msaada kutoka Uhlanzi miaka miwili iliyopita (2009). Kompyuta hizo (165) ziko hatarini kuharibika ama kuibiwa. Huo ni msaada mkubwa katika Wilaya hasa kuendeleza TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kwa vile umeme wa nguvu kubwa (*high tension*) umefikia Nyamongo, ni vema usambazwe kwenda Wilaya ya Serengeti kuititia Mara-Samoche – Nyansurura hadi Rung'abure ambapo utaunga umeme unatokea Mjini Mugumu kukamilisha mzunguko, pia umeme huo utakamilisha mzunguko Kiwilaya kuweka njia mbili kutoka Nyansurura kuititia Kata ya Kisaka, Busawe, Majimoto, Kenyamonta hadi Sirari- Simba ili kuelekea Musoma vijiji. Sehemu nyingine umeme huo utatokea Rung'abuke, Kata ya Kibandabanda, Kata ya Ring'wani, Magange na kuelekea Kata nyingine jirani zikiwemo Nyambureti, Nyamatare, Massongo hadi Rigicha ambayo hazina umeme. Utaratibu huo utasaidia kufanya *looping*.

Mheshimiwa Spika, kuna vyanzo vingi vinavyoweza kuzalisha umeme Mkoani Mara na vingine uko Wilaya ya Serengeti – Majimoto penye chemichemi ya maji ya moto (*Hot spring*) ambapo panaweza kutoa *Geothermal* na gesi pia inapatikana hapo Majimoto kwa utafiti ambao *Tanzania Oxygen (TOL)* walifanya miaka ya 1990 na hata kuchukua hati miliki ya kuchimba gesi eneo hilo ambapo wananchi wamezuiwa kuendeleza maeneo yao baada ya kulipwa fidia. Lakini hadi leo ni karibu miaka 20 hakuna kinachoendelea. Pia kuna maporomoko ya maji eneo la Baragonya na Borenga. Ni vyema maeneo hayo yaendelezwe ili kusaidia upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuna utafiti bubu uliozuka na kuwalipa ujira mdogo sana vijana wanaosaidiana na watafiti bubu hao wa Kichina na wanajificha katika nyumba ya wageni ya Zebra iliyoko Mjini Mugumu – Wilaya ya Serengeti. Naomba nipatiwe jibu wananchi wa Serengeti na Taifa kwa jumla ieleweke nini kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja kwa sababu hakuna mradi wowote wa umeme umepangwa Wilaya ya Serengeti. Niambiwe kuna mpango gani juu ya kusambaza umeme Wilayani.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa nishati ya umeme kwa sasa wananchi wengi wanajihusisha kwenye kuuza makaa kwa matumizi mijini kitendo ambacho kinaathiri misitu yetu na pia kuchangia matumizi mabaya ya miti ambayo inatoa mbao za thamani kubwa kama vile mipingo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kufanya mikakati thabiti ya kutumia *gas* ambayo tayari inapatikana vya kutosha iwe ndiyo nishati ya kipaumbele kwa matumizi ya kupikia. Yapatikane majiko ya gesi na wananchi warahisishiwe kupatikana kwake.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tanga imeamuliwa kuwa Wilaya ya Viwanda na sehemu za kufanya hivyo imekwihatengwa na wananchi hata wanaoishi kando kando ya Jiji la Tanga wamejitayarisha hivyo. Vijiji hivi haviwezi kuchangia kuibadilisha Tanga iwe Wilaya ya viwanda kama jitlhada za makusudi hazitafanywa kuvipatia vijiji hivyo umeme kama tulivyoahidi kwenye llani ya 2010. Naviorodhesha vijiji hivyo kama ifuatavyo:-

- (1) Kata ya Pongwe: Vijiini Kisimatui, Kakindu, Jitengeni.
- (2) Kata ya Marungu: Kijiji ni Geza.
- (3) Kata ya Tongoni: Vijiini Mundura, Mwarongo, Tongoni, Sadani, Kiwatu, Maere, Kivindani, Migombani na Mgawisha.
- (4) Kata ya Tangasisi: Vijiini ni Kivumbitifu, Masiwani Shamba, Machui A, Machui B, na Neema.
- (5) Kata ya Kirare: Kijiji ni Mapojoni.
- (6) Kata ya Duga: Kijiji cha Songa.
- (7) Kata ya Mabokweni: Vijiini Kibafuta na Kiruku.
- (8) Kata ya Mzizima: Vijiini ni Mleni, Kongwa, Mtakuja, Kihongwe, Masagara, Kona Z, Majimoto, Mtambwe, Mabayani, Marembwe, Mpirani, Mavumbi, Pande B, Ndumi, Lwande, Mowe, Kivuleni na Msumbiji Mbogo.
- (9) Kata ya Chongoleani: Vijiini ni Chongoleani, Ndaoya Putini na Bwagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Vijiini vyote hivi vina uwezo kujieendezea kwa viwanda vidogo vidogo vikiwemo vya kutengeneza chumvi na chokaa, kutengeneza vyombo vya kauri, kusindika mazao na kadhalika bali juhudhi hizi zinakwamishwa kwa kukosekana umeme hata pale ambapo nguzo za umeme zinapita vijiji hapo.

Mheshimiwa Spika, Tanga kwa jumla kufuatia kuibuka viwanda vipyka kama vile vya Saruji na pia kufufua viwanda vingi ambavyo kwa sasa vimedorora kama vile (*Sikh Saw Mills, FOMA, Steel Rolling Mills, Fertilizer Company* na kadhalika). Tanga inahitaji umeme wa uhakika zaidi ya ilivyo sasa. Ni vema kampuni za watu binafsi zikaruhusiwa kutoa huduma hii sambamba na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Tanga kuna madini nyingi za vito vya thamani na wachimbaji wadogo wadogo wengi wanajihusisha kwenye shughuli hiyo. Wachimbaji hawa wanahitaji msaada ambaao ni pamoja na kuanzhishwa kituo cha kuvitayarisha vito hivyo ili thamani yao iongezeke

kabla ya kuuzwa nje. Wachimbaji hao warahisishiwe upatikanaji wa leseni na zana za kufanya kazi. Niombe pia kuwe na ofisi hususan ya kuwashughulikia hao Tanga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la umeme limekuwa ni janga la Taifa, Serikali haionti kuwa sasa wakati umefika wa kuwekeza kwenye umeme utokanao na mafuta ya mimea mbalimbali tunayolima? Natoa wazo hili kwa sababu nchi kama India imeweza kuongeza uzalishaji wa umeme ambao unaweza kukidhi mahitaji madogo madogo hasa kwa wananchi walioko vijijini. Serikali yetu imejikita kutafuta umeme kwa kutumia njia ya kawaida ya upatikanaji wa umeme wakati kuna njia zingine kama *Hydropower* itokanayo na *clean, renewable power.*"

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa imefikia ukomo wa kuendelea kujiridhisha na mtandao mkubwa wa miradi ya umeme ambayo haitoi tija yoyote katika kutatua tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali sasa ijikite pia kwenye miradi midogo midogo kama *Biomass gasification system* ambapo wakulima watatumia mabaki ya mazao yao kwa kukusanya angalau kilowati mia moja. Endapo wakazi wa vijijini watahamasishwa katika hii teknolojia hakika vijiji vingi vitatoa mchango mkubwa katika sekta ya nishati na wataweza kujitosheleza katika mahitaji ya nishati.

MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nishati na umeme ni chanzo muhimu katika uchocheaji wa maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Kata ya Ipililo, Ngulinguli, Senani, Mpindo na kwa Vijiji vya Mwakidiga, Isaghenke na Mbaragane, Mandang'ombe ili viweze kuibua maendeleo kuititia nishati ya umeme?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni Wizara ama sekta muhimu katika Taifa letu, lakini ajabu ni kwamba inazidi kudidimia katika *implementation* zake *day by day*.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika suala la madini, madini ni nyenzo muhimu katika Taifa hili, nchi yetu ni tajiri sana kwa madini na tungeyatumbia vizuri kupitia madini haya, nchi ingekuwa tajiri sana. Mikataba na wawekezaji katika migodi ni mibovu sana, inabidi iwe *reviewed/revised* kwa sababu inatakiwa iwe *win-win situation*, lakini ajabu nchi yenyе rasilimali hizi ndio inapoteza wawekezaji, hawa ndio wanaonufaika. Mfano, katika suala la ulipaji kodi, kwanza wanakuwa *exempted*, hatuelewi ni kwa nini, pili, kila baada ya *certain period* (i.e. miaka mitano) wanabadilishana *ownership*, kwa nini?

Mheshimiwa Spika, haya yote ni katika ujanja wa kukwepa kodi. Nchi yetu inategemea sana hawa wawekezaji. Pia kama njia mojawapo ya kukuza uhusiano, kukuza uchumi wa ndani ya nchi yetu na maendeleo, lakini ajabu wawekezaji hawa wa sekta ya madini imekuwa ni kinyume. Wananyonya uchumi wa nchi yetu kama vile wanasafrisha dhahabu nje ya nchi, pesa *zina-circulate* huko huko hazirudi nchini na *rate* ya *USD* inapanda na hivyo bei ya dhahabu inatakiwa kupanda, lakini ajabu nchi yetu bado bei ya dhahabu iko pale pale. Hawa wawekezaji wa kigeni wanaingia mikataba juu ya kusaidia *community* kwa maeneo husika lakini ajabu misaada wanayotoa, haiendani na makubaliano, pia haiendani na *income* wanayopata wao, huko ni kulaghai nchi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini, Mikataba ya Madini vyote vipitiwe upya na kurekebishwa. Ikiwezekana, pamoja na kwamba kulikuwa na Tume ya Jaji Mark Boman, maoni ya Tume ile yametekelvezwaje?

Mheshimiwa Spika, nchi na kodi kwanza. Kuwavutia wawekezaji sio kwa maana kwamba waogopwe na wanyonye nchi. Nchi ni kweli ivutie hawa wawekezaji wa nje kwenye masuala ya kuwaondolea ukiritimba tu, basi. Mgodi wa North Mara, tupatiwe majibu ya uhakika, kama wale waathirika wa Mto Tigithe wameshalipwa fidia yao wote. Ule mgodi unatakiwa usimamishwe kwa muda kwa sababu ya migogoro iliyokithiri mahali pale. Hii itaongeza nidhamu na *integrity* kwa nchi yetu. Kwa madini peke yake nchi imepoteza kodi zaidi ya bilioni 48 (CAG report 2009/2010).

Mheshimiwa Spika, suala la nishati, hususan umeme, limekuwa ni tatizo sugu sasa, kumekuwa na mgao wa umeme. Serikali sasa (ya Chama tawala) imekuwa ikipoteza *popularity* na imani toka kwa wananchi karibu wote juu ya hili tatizo! Uchumi umeshuka kwa kiwango kikubwa sana, *hence* hakuna ajira, wawekezaji pia kuja kuwekeza nchi isiyo na umeme ni ndoto. Tunahitaji tupatiwe ufumbuzi juu ya tatizo sugu hili kama vile Kampuni ya *Alex Stewart* na Kampuni nyinginezo zinazolipwa mabilioni bila *proper responsibilities*. Hizo pesa zinunue majenereta.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Kiwira *Coal Mine* lini kinafufuliwa, kwa sababu pia kitarejesha ajira, kitasaidia umeme kuwepo katika baadhi ya maeneo jirani licha ya umeme wa MCC.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi juu ya umeme Tanzania nzima hadi sasa, malalamiko haya yamekuwa ni mazoea, ni vema sasa Serikali ichukue hatua za ukweli kumaliza tatizo hilo, badala ya kuhesabu miradi kila siku tutafanya hivi, tutafanya vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Liwale limeahidiwa *generators* mbili zenyenye jumla ya *KW* 800 kutoka Ikwiriri kwa muda mrefu sasa na matokeo yake *generators* hizi mbili hazijakamilishwa hadi sasa na badala yake tumeletewa *generator* moja yenye *KW* 400 kutoka Songea na ambayo haijawa *Installed* hadi leo. Zile *generators* tulizoahidiwa mbili kutoka Ikwiriri ziko wapi? Mbona angalau hailetwi *generator* hata moja kutoka Ikwiriri ikaongezewa hii iliyotoka Songea ili zile *KW* 800 zitimie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tena tatizo la umeme Mjini Liwale, naendelea kuiomba Wizara ya Nishati na Madini, kuongeza bidii ili *generators* zile mbili ambazo tuliahidiwa kwa muda mrefu zingepelekwa Wilayani humo ili kuweza kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zoezi hili haliwezekani tena, ni vema basi Serikali ifikirie upya kuiunganisha Wilaya hii kwenye mradi wa umeme wa gesi wa Mnazi Bay kutokea Ruangwa au Nachingwea. Kwa kufanya hivyo, tatizo hili la umeme Wilayani Liwale litakuwa limekwisha. Ni vema sasa Serikali ichukue hatua za dhati ili kutatua tatizo hilo la umeme ndani ya Wilaya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. STEPHEN N. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, kufuatia tatizo la umeme kuwa kubwa, basi Serikali itamke kuwa janga la Kitaifa ili wananchi wajue na waache kuhoji. Inasikitisha sana nchi kubwa kama Tanzania yenye vyanzo vingi vya maji inakosa umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema Kihansi vyura wengi, Mtera Bwawa linapungua maji na kujaa tope, je, Mto Ruvu ni lini umepungua maji na ukizingatia una sehemu mbili ya kutoa umeme Hale na Chemka. Kwenye maporomoko ya Mto Pangani kwa nini isiboreshe mitambo yake ya nguvu ya umeme. Ya Hale leo hii toka mwezi wa pili tarehe 23.2.2011 mashine za Hale hazifanyi kazi, hii ni lawama ya nani? Kama mashine hizo ambazo zilikuwa zinafanya kazi mgao wa umeme ungepungua kiasi fulani. Shida ya umeme imekuwa kikwazo kwa maendeleo kwa kuwa Serikali ina upungufu huu katika *Grid* ya Taifa, umeme unaotoka Hale kwenye Kampuni ya Katani *Limited* ni mapambo au ni maonyesho kama kweli upo kwa nini Serikali haitumii umeme huo na kama hauna kazi, basi usioneshwe kwenye vyombo vya habari na kuwadanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawaangaliaje wananchi wa Jimbo langu ambao wamepitija na nguzo za umeme na vijiji hivi vinalinda nguzo hizo ikiwa hawapati umeme? Vijiji hivi vimepitija na umeme lakini havina umeme. Naomba Serikali ifahamu vijiji vifuatavyo: Shambakapoli, Kwamzindawa, Mkwakwani, Gereza, Mng'aza, Kerenge, Kibaoni, Lusanga, Kwemazandu, Matalawanda, Bombo, Majimoto, Kizara, Dindira, Mgwashishi, Mali, Mpale na Vugiri. Huwezi kuamini toka uhuru hadi leo vijiji hivi havina umeme na nguzo zimekwenda kwenye mashamba ya chai na mkonge na baadhi ya vijiji ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie umeme umefika Pemba, vijiji vinavyotoka umeme havina umeme. Huu ni uungwana kila Mbunge anayetoka kwenye Jimbo langu walionitangulia waliahidiwa na Serikali lakini hakuna msaada wowote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji madini wa Jimboni kwangu, ni lini wachimbaji wadogo wadogo wataacha kusumbuliwa na matajiri? Kwa mfano, kwenye machimbo ya Kalalani na Kigwasi, wachimbaji wananyanyaswa na kutishwa na kusumbuliwa na wenyewe pesa na kupokonywa sehemu zao, naomba Serikali iwagawie wachimbaji wadogo, wana haki na machimbo yao wamiliki kwenye sehemu za madini ili wasisumbuliwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu, nilipochangia katika hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nililiza kuhusu uagizaji wa mafuta kwa mpigo, nilitahadharisha Serikali yetu kuhusu nchi kuweza kukosa mafuta kama Maharamia watalazimika kuteka hiyo meli yenyenye kiwango kikubwa kama walivyoteka meli ya Saudi Arabia, je, hamlioni hilo? Pia kama hata huyo akifanya njama na watekaji akapakia maji badala ya mafuta na hilo hamlioni? Maana kuna hatari ya kuiweka nchi yetu katika janga kubwa la kiuchumi, pia nililizia kuhusu uwekaji wa rangi *mark* ya kutoza kila *US* 6.80 wakati bei ya mafuta ya taa na dizeli zinalingana. Hakuna kuchakachua tena.

Mheshimiwa Spika, pia bila kudhibiti mafuta ya ndege ambayo bei yake bado iko chini. Baadhi ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu hawa wanatumia mafuta hayo kuchanganya na mafuta ya dizeli. Naishauri Serikali kuagiza idadi maalum hayo mafuta ya ndege maana wataagiza mengi ili kuchakachua badala ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, hilo ni angalizo mara mia moja, bila hivyo Serikali itapoteza ushuru na kuendelea kuharibu magari na mitambo inayotumia dizeli.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake yenyenye kuleta matumaini kwa wananchi pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lulindi, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia vyema mradi wa upatikanaji wa gesi Mnazi Bay Mtwara ambao umewezesha wananchi wa Mkoa wa Mtwara na Lindi kupata umeme wa kujitegemea nje ya *Grid* ya Taifa. Kilichobaki ambacho tunaomba ni kusambaza umeme huo kwa wananchi kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amewaaahidi wananchi wa Vijiji vya Chiwata, Chidya, Nanjota, Mbuyuni, Luatala, Mkwangaula, Mchauru na Mnaura kupatiwa umeme katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 na pia alihakikisha tathmini ya gharama ingepatikana katika kipindi cha miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali kufuatia ahadi hiyo ili wananchi wapatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini. Naiomba Serikali kusitisha uchimbaji wa madini kwa wawekezaji wakubwa kwa maeneo mapya hadi hapo Serikali itakapokuwa na uwezo wa kuchimba kwa manufaa ya wananchi. Kwa sasa Serikali haipati faida kubwa kutokana na kubanwa na wawekezaji ambao ni *majority shareholder*.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Spika, ajali nyingi za watu zimetokea kutokana na umeme, *poor planning* yenu inatupeleka pabaya.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa ulinzi wa hali ya juu anaonipa hadi kufikia kutoa mchango wangu katika nchi yangu kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kujielekeza katika madini, inasikitisha hadi sasa mbali na kuwa na madini mengi ya aina tofauti yenye thamani kabisa hadi sasa nchi yetu haijafaidika vilivyo kutokana na madini hayo.

Mheshimiwa Spika, madini sio mimea kuwa yakiisha tutapanda mengine. Kama hatujawa tayari kujinufaisha na rasilimali hii basi ni bora kusimamisha uchimbaji wa dhahabu ambaao badala ya kuleta neema umegeuka kero kwa Watanzania wa hali ya chini hasa wanaozunguka mgodi.

Mheshimiwa Spika, bado Wizara hii haijawa na uelewano mzuri na wananchi wake hasa katika sekta zote inazosimamia. Malalamiko kwa wananchi dhidi ya Serikali mengi yanatokana na Wizara hii ambayo imeshika sehemu nyeti za kila sekta ambazo zaweza kupandisha au kushusha uchumi wa Tanzania. Huu sasa ni muda muafaka wa Wizara kuhakikisha sekta inayosimamia haziwi kama zilivyo.

Mheshimiwa Spika, narudi kujieleza tena kwenye umeme. Sasa ni muda muafaka tena kwa kutowaingilia *TANESCO* na wataalam wake kufanya kazi zao bila kutegemea Serikali, ni vizuri sasa Shirika hili likapanga mipango yake ya muda mrefu na kupanga gharama zake ili ziendane na hali halisi.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia watumiaji wa umeme wengi ni wenye viwanda, ukilinganisha na matumizi ya nyumbani. Ipo haja ya kupanga upya bei ya umeme katika migodi na viwanda kwani tafiti zinaonyesha bei ya umeme viwandani na migodini bado ni ndogo ukilinganisha na gharama za uzalishaji na usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, ni bora kuwa na umeme wa bei ghali kuliko kukosa kabisa umeme. Ni bora sasa *TANESCO* kuwezeshwa na ijitegemee kuliko ilivyo sasa. Ughali wa umeme ni bora kuliko ukosaji wa nishati hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, sasa tupo kwenye utafiti wa mafuta na kwa uwezo wa Mungu najua kwa rehema alizojalia Tanzania basi uhakika wa kupata mafuta upo. Yawezekana kabisa hata mafuta haya yakipatikana bado hali ya bei na manufaa ya uchimbaji huu wa mafuta hautainufaisha Tanzania kwa kuwa hatujaweka tayari vijana na pia hata hali ya usafishaji wa mafuta bado ni wasiwasi hata kama mafuta yakipatikana na bado tukaenda kusafisha nje ya nchi, hakika bei haitashuka na pengine itapelekea kuibiwa au kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mitambo ya kusafisha mafuta (*TIPER*) pale Kigamboni, Dar es Salaam. Lakini kwa sababu zisioeleweka kwa Watanzania wengi hatujui kwa nini Serikali iliachia shea (*share*) zake nusu na tukaamua kununua mafuta yaliyosafishwa toka nje.

Mheshimiwa Spika, napenda *specific* katika majibu ya majumuisho ya Waziri, basi aeleze kwa kina kuhusu mitambo hii na mikakati ya usafishaji wa mafuta mara yatakapopatikana ili isije ikatokea tena hatua za dharura kama ilivyo sasa katika umeme.

Mheshimiwa Spika, mitambo ya kusafisha mafuta hasa mitambo ya kisasa ni muhimu sasa na ingekuwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano sambamba na kuanza kujenga mabomba ya usambazaji wa nishati hiyo muhimu kuliko kutegemea barabara na reli ili yakipatikana bei ziweze kufanana au basi kutofautiana kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la Wizara hii, ni kuwa na mipango ya muda mfupi badala ya kuwa na mipango ya muda mrefu.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo la umeme nchini ni kubwa na la muda mrefu na kwamba umeme ni kichocheo kikubwa cha maendeleo. Ombi langu kwa Serikali, ni kuongeza bajeti ya Wizara hii mara mbili zaidi ili kuipa uwezo mkubwa wa kifedha iweze kutatua tatizo hilo siyo kutoa lawama tu kwa watendaji wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Jimbo la Mtera lina sehemu kubwa ya Bwawa la Mtera linalozalisha sehemu kubwa ya nishati hiyo, Jimbo langu lina Kata 19 na Vijiji 62 katи ya Vijiji vyote hivyo vyenye umeme ni viwili au tena kwa mchango wa Kanisa. Naomba Wizara yako iwaonee huruma na iwatendee haki wananchi wa Jimbo la Mtera kwa kuwapatia umeme katika mipango yake ya kila mwaka na kuahidi ushirikiano wangu wa dhati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Sitarajii kushika shilingi wala mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

MHE. MWIGULU L.N. MADELU: Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme ni janga la Taifa, limesababisha wananchi wengi wanalala na njaa kama kazi zao zinategemea umeme, wanaofanya kazi *saloon* za kike na kiume, mafundi wa kuchomelea vyuma, mashine za kusaga unga, pia maji yanakosekana, viwanda vinafungwa, watu wanakosa ajira, uzalishaji unashuka na mapato ya *TRA* yanashuka.

Mheshimiwa Spika, ni lazima jambo hili litatuliwe kwa hatua za dharura kwa kupata mitambo ya dharura hata ambayo imetumika. Natambua kuwa kuna kanuni ya manunuzi inayouzia ununuzi wa vifaa viliviyotumika, ni vema kwa udharura huu Serikali itengue kanuni yake hiyo na kuagiza mitambo ya haraka iliyothibitishwa kuwa bado ina ubora na iwe na uwezo wa kumaliza kabisa tatizo hilo, wakati inatafuta suluhisho la kudumu la kupunguza utegemezi wa umeme wa vyanzo vyta maji.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, kwenye upande wa migodi Serikali itatue ugomvi unaojitokeza kati ya wachimbaji wadogo na wawekezaji. Hili imekuwa tishio sana kwenye maeneo ambayo yana migodi na kusababisha uvunjifu wa amani. Pia mikataba isiyo na manufaa kwa wananchi sisainiwe tena na mapato yatokanayo na madini yarudishwe nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya mafuta ya taa, pesa inayotokana na ongezeko la tozo iende kwenye kusaidia umeme vijijini ili kutoa nishati na kuchochea maendeleo. Naipongeza Serikali kuititia Wizara yake kwa juhudhi ambazo tayari imeshazifanya katika kuhakikisha inamaliza tatizo la umeme nchini na katika kukuza uwekezaji katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE: Mheshimiwa Spika, awali naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, umeme ni tatizo sugu kwa Taifa letu, tunaweza kusema kuwa ni janga la Taifa, Watanzania wengi tegemeo lao kubwa ni umeme katika maisha yao ya kila siku, iko haja ya Wizara kuititia Serikali kwa kufanya juu chini ili kuondosha tatizo kwa kutafuta *generator* za dharura kukabiliana na hali hii kwa vile Serikali ikaamua kununua *generator* mpya, hivi sasa itachukua muda mrefu kupatikana, sasa hii itafanya kuchelewesha kupatikana huduma hii.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Bunge litengue kanuni za manunuzi ili tupate kununua mitambo iliyotumika ambayo ina dhamana ya muda mrefu tupate kujilinda katika manunuzi hayo, litakapotokea tatizo. Nafikiri hili peke yake ndio litakuwa suluhisho kwa mara moja kwa ukosefu wa umeme katika nchi yetu na litakuwa jawabu zuri kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, nchi yetu imebarikiwa kuwa na madini mengi sana, lakini kilio cha Watanzania mali yetu inaliwa bila ya sisi kunufaika, iko haja sasa kuipitia mikataba yote ya madini ili kuwatoa hofu Watanzania, pia Serikali kuititia Wizara ya Nishati na ifikirie kutenga maeneo maalum kwa wachimbaji wadogo, ambazo mali zinazopatikana kwa wachimbaji

wadogo, napendelea Benki Kuu inunue mali hizo na ifanye mpango wa kuzidishia thamani fedha yetu kwa kuwa na akiba ya dhahabu katika Benki yetu Kuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE: Mheshimiwa Spika, Nawapongezeni sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri. Pamoja na mazingira magumu mnayofanya kazi katika Wizara yenu ya Nishati na Madini, napenda niwapongeze na kuwasifu sana kwa umahiri mnaoonyesha katika utekelezaji wa majukumu yaliyo chini ya Wizara. Jambo kubwa ninaloliona kuwaweka katika mazingira hayo magumu ni pamoja na ufinyu wa bajeti na nyenzo za kutosha wananchi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo, naiunga mkono hoja na nawatachia kila la kheri katika kukabiliana na changamoto nydingi katika utekelezaji wa mipango mliyoainisha katika hotuba ya makadirio ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, bado nina imani kubwa ya kwamba iwapo mazingira magumu yanayowazunguka hivi sasa yataboreshwa kwa hakika mnao uwezo mkubwa wa utekelezaji wa kazi zenu zote.

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushe ahadi ambayo Serikali ilikwishatoa kwa wananchi wangu wa Kijiji cha Msanga ambacho kiko kilomita nne tu kutoka Chamwino, Ikulu) kwenye eneo la umeme ya kwamba watapelekewa umeme kupitia REA na Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima alikwishafika Msanga kuwathibitishia kuwapelekea umeme kupitia REA,

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni tamko la Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kuwahakikishia wananchi wa Kijiji cha Msanga kuwa watapatiwa umeme kupitia REA.

Mheshimiwa Spika, katika usimamizi wa TANESCO Wilaya ya Kiteto, Mkoani Manyara inasimamiwa na Meneja wa TANESCO, Mkoa wa Dodoma. Maeneo yaliyoko Wilayani Kiteto ambayo kwa sasa yamepatiwa umeme yako karibu sana na Vijihi vya Tarafa ya Itiso kwenye Jimbo langu la Chilonwa ambako ni rahisi kuwafikishia umeme kutokea Kiteto.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuiomba TANESCO iangalie uwezekano wa kuvipelekea umeme Vijihi vya Zajilwa, Izava, Segala na Itiso kutokea maeneo ya Matui, Wilayani Kiteto na Soya, Wilayani Kondoa. Wananchi wangu wa maeneo hayo wanasubiri kauli ya Serikali kuhusu ombi hili.

MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ngeleja na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza nawapa pole kwa kazi kubwa sana katika Wizara yenu yenye changamoto nydingi sana lakini Mungu atawavusha. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba sana Wilaya ya Kilombero ambako kuna manung'uniko mengi juu ya kukosa umeme.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero ina vyanzo vya umeme viwili; Kihansi na Kidatu, lakini Kata zetu nydingi ziko gizani, Kata kama Idete, Mbingu, Mchombe, Mngeta na vijihi vingi tu viko gizani hata kama wao ni walinzi wakuu wa vyanzo vya maji na nguzo za umeme!

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara inihakikishie kama Kata hizo zitapatiwa umeme katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, wachimbaji wadogo ni kundi kubwa sana. Wako *disorganized* na wabishi. Naishauri Serikali iwavumilie, iwaelimishe, iwasaidie kupata mikopo

midogo midogo ili waone kuwa tunawajali maana wana uchungu sana na wawekezaji. Hii itapunguza fujo na ugomvi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MESHACK J. OPULKWA: Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza bei za umeme vijiji ili kutekeleza azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi umeme angalau kwa asilimia thelathini ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna mwananchi yejote wa Kijiji mwenye uwezo wa kulipia *connection fee* ambayo ni kubwa sana, ukilinganisha na Watanzania wengi wanaoishi *below poverty line*.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, hakuna nchi yoyote iliyoendelea bila nishati ya umeme. Umeme hutumika viwandani na viwanda ndio vilivyoleta mapinduzi ya maendeleo kiuchumi. ni jambo la kushangaza kuona Tanzania pamoja na rasilimali nyingi zinazozalisha umeme kama vile maji (mito mikubwa), gesi na makaa ya mawe bado nchi imeendelea kuwa gizani na hivyo kutishia uchumi wa nchi na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tungependa Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu ni nini hasa chanzo cha tatizo la umeme na ni nini mkakati wa kulitatu? Inashangaza wakati tunapoahimisha miaka 50 ya uhuru ni Watanzania asilimia kumi tu wenye umeme! Hali hii ni mbaya sana kwa maendeleo ya nchi. Lakini hata asilimia hiyo, bado umeme umekuwa wa kusuasua na hivyo kutopata umeme kila wanapouhitaji.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya kutokuwa na umeme wa uhakika umepelekea wananchi kukata miti hovyo kwa ajili ya kuni za kupikia na mikaa (*charcoal*). Hali hii inahatarisha jangwa na upungufu mkubwa wa chakula kutokana na ukame. Athari hii ni kubwa sana kama Serikali haitahakikisha inawapatia umeme wa uhakika wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna tetesi kuwa nchi yetu inataka kuanza kuchimba na kuuza madini ya *uranium*. Wote tunajua *uranium* ni madini yenye hatari na athari kubwa kwa afya za binadamu. Pamoja na umuhimu wa madini haya, kwanza yana gharama kubwa sana katika kuyatayarisha hadi kufikia hatua ya kuzalisha umeme au nyuklia. Lakini cha kushangaza tuna vyanzo vingi ambavyo havijatumika vya kutosha mfano, makaa ya mawe na gesi asilia. Ni vema vyanzo hivi vitumike kwanza kabla hatujakwenda kwingine.

Mheshimiwa Spika, *uranium* ni madini ambayo yanapigwa vita sana ulimwenguni hasa kutokana na matumizi mabaya ya nyuklia *power* ambayo inaweza kupelekea vita vya tatu na vya mwisho vya dunia.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama nchi inayopenda amani itakuwa ni jambo baya na hatutaeleweka kama ndio tutakuwa tunauza *uranium* ambayo ndiyo nishati ya kutengeneza nyuklia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningetaka Serikali ipunguze bei za kuunganisha umeme ili wananchi wengi zaidi waweze kupata. Gharama za kuunganisha ni ghali sana mfano, nguzo moja hadi Sh.1,500,000/=, hii ikimaanisha kama uko umbali wa kuweka nguzo tatu ni Sh. 4,500,000/=. Jambo ambalo ni gumu sana.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, kwanza naiunga mkono hoja, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri kuyazingatia mambo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mradi wa Kufufua Umeme wa Somanga, Fungu MV 230. Mwaka 2005 tuliahidiwa kuwa mradi huu utakamilika ili wananchi wa Mkoa wa Lindi wapate

umeme wa uhakika. Nataka kujua mpango huu utaanza lini? Katika bajeti hii ni kiasi gani kimetengwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bei ya mafuta ya taa imepanda sana, je, ni kwa namna gani fedha ya mafuta ya taa inavyoweza kuisaidia *REA* ili iweze kusambaza umeme vijiji.

Mheshimiwa Spika, nashauri sasa Fungu la *REA* lionezwe ili kukabiliana na changamoto ya umeme vijiji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme katika Viji na Miji vya Kilangala, Mnimbila, Kitomanga na Mkwajuni. Umeme upo Mchinga II, tunaiomba Serikali kupeleka umeme Kijiji cha Kitomanga kilomita 15 kutoka Mchinga II, kandokando ya barabara kuu kwa sababu umeme ni huduma muhimu kwa matumizi ya hospitali na tayari tumeekubaliana kuwa hospitali ya Wilaya ya Lindi Viji, itajengwa Kijiji cha Kitomanga na tayari kazi hiyo imeanza. Hivyo viji vilivyopo kati ya Mchinga II na Kitomanga vitanufaika na kupita umeme katika maeneo hayo, Viji hivyo ni Kilangala, Mnimbila, Kitomanga yenyewe na Mkwajuni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naanza kwa kuunga mkono hoja japokuwa nina machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme ni suala mtambuka katika mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu. Hivi sasa tunashuhudia mgao wa umeme unavyoathiri uchumi wa Taifa hili. Katika uendeshaji wa viwanda na taasisi mbalimbali tunashuhudia jinsi gani wamiliki wa viwanda au taasisi hizo wanavyolazimika kutumia jenereta ili waweze kuendesha miradi yao. Hii inapelekea wao kuongeza bei katika mali wanazozalisha hatimaye mwananchi ndiye anayeumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile haitoshi wananchi ambao wamejajiri wenye nao wanaathirika kwenye uzalishaji na kupelekea kudorora kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi maendeleo yatakuja kama hakuna umeme na hivyo kupelekea kutokuwa na mawasiliano kwa wakati muafaka. Wananchi watahabarishwa vipi kwa kutokuwa na umeme kwani sote tunajua maeneo mengi wanategemea ama kusikiliza *radio* au kuangalia runinga (7V) kwani magazeti yanachelewa kuwafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipatiwe majibu ni lini tatizo hili la umeme litatoweka au japo kupungua ili tuendeleze nchi yetu hasa kwa sasa ambapo tuko katika kuadhimisha miaka 50 ya uhuru wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kuunganisha umeme ni kubwa sana, ni lini au Serikali ina mkakati gani wa kupunguza gharama hizo ili wananchi waweze kuweka umeme kwenye makazi yao na wao waweze kusonga mbele kimaisha hasa kwa wananchi wa viji vilivyopo Mkoa wa Pwani katika Wilaya zake ambazo ni Kibaha, Mafia Bagamoyo, Mkuranga, Rufiji na Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mkakati gani wa kupunguza miradi yake ya uzalishaji umeme ili iwe michache na kuiwezesha (Serikali) kuwa karibu na usimamizi mzuri na hata gharama zitapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo iko zaidi ya thelathini, naomba unipatie majibu. Inawezekana uwezo wa kifedha ni mdogo hatimaye miradi huzorota na umeme unakuwa tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya umeme viko vingi sana nchini, hatuna sababu ya kuwa na mgao, juhudzi za makusudi zifanywe ili kuongeza ufuaji wa umeme na ushawishi wa kuwapata wawekezaji binafsi au mashirika ya umma yenyewe uwezo ufanywe kwa haraka ili tusaidie kututua tatizo hilo na kuweza kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali inipatie majibu kwa maswali yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR: Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa umeme ni tatizo kwa jamii unapokosekana na hivi sasa suala la umeme katika makazi ya wananchi limekuwa suala sugu na hasa tukiangalia Jimbo la Temeke na katika Mtaa wa Azizi Ali kwenda Temeke, Mtaa wa Bustanini, Aziz Ali unakatika masaa 24 au masaa 12. Ukweli tatizo la umeme kwa mtaa huu ni tatizo kubwa, hata naweza kusema kwamba ni janga la Taifa kukosekana kwa umeme, maana jamii yote inaathirika. Suala hilo linahitaji ufumbuzi na Wizara yako ndio msimamizi wa janga hili.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanakuangalia wewe ndio muokozi wa janga hilo na Mungu atakusaidia upate uwezo na kukamilisha kwa yote uliyoyapata ili kuwasaidia wananchi na nchi hii.

Mheshimiwa Spika, suala la ulipaji wa umeme baada ya matumizi ya jamii. wakati wananchi wanapokwenda kulipia umeme au kununua wanakutana na changamoto zisizo za msingi kutokana na wahusika ambaa wauzaji au wanaopokea fedha za mauzo. Ikiwa mlipaji mzuri kama unaletewa deni huna tatizo unalipa, basi utaletewa deni kubwa na ukisema sitaki tatizo nitalipa, basi ndio umetangaza matatizo kila baada ya miezi mitatu unaletewa bili kubwa kuliko ile uliyolipa. Hata kama kila mwezi unalipa na kuonesha risiti bado unatakiwa ulipe au unakatiwa umeme, kwao ndio mavuno kutoka katika jasho lako. Sana ukifuatilia utaishia kugombana na kujenga chuki na kuongeza maadui.

Mheshimiwa Spika, ningeliomba kujua suala hilo ni la Shirika, *TANESCO* au ni katika vituo vya mauzo, naona kwamba *TANESCO* ndio inawatuma ili kupata fedha za ziada kulipia madeni yao, lakini isiwe kujipatia fedha za wananchi kinyume cha utaratibu. Hii ni kuliangamiza Shirika kuonekana linapata fedha kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme Zanzibar. Umeme kwa upande wa Zanzibar ni tatizo, katika usambazaji wa mitaani Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ina ratiba nzuri na unapatikana vizuri tu. Lakini ugumu ulipo unatokana na huku Tanzania Bara kuufanya umeme bei juu kuliko Tanzania Bara. Mnaifanya Zanzibar mtu wa kijijini kuridhika kuwa hana umeme kutokana na bei juu inayotokana na kupandisha *tariff*, kuwa juu kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba SMT ikishirikiana na Wizara yako kuliangalia suala la bei ya umeme kwa Zanzibar kwani nchi hizi mbili ni za Tanzania, matumizi ya umeme Zanzibar ni madogo ukilinganisha na Tanzania Bara, basi tunaomba uwiano wa bei za umeme baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Hakuna mmiliki wa Tanzania, sote tupo katika nchi moja ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ningependa kuona kwamba suala hilo linapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Spika, usambazaji umeme wa *TANESCO* na *REA*. Kwa kuwa shule ya sekondari ya llembula nguzo zimefika karibu ya nusu kilomita kwa takribani zaidi ya miaka kumi. Je, lini Serikali itakamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa *TANESCO* ilivuta umeme zaidi ya kilometra nane toka Wanging'ombe mpaka Kijiji cha Wangutwa yaliyopo makazi ya aliyekuwa Mbunge Ndugu Thomas Nyimbo na kuweka transfoma inayohudumia nyumba moja tu kwa zaidi ya miaka 15. Je, Serikali ya CCM haioni iko haja kusahihisha kasma hii kwa kusambaza umeme kwenda zahanati ya Kijiji cha Wangutwa na shule ya sekondari ya Kata ya Uhambule inayoitwa Thomas Nyimbo?

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Mhaji Igiwe na Mdandu *TANESCO* wameanza kuweka transfoma na kuunganisha umeme kwa wananchi. Je, *TANESCO* kwa nini imewaacha kuwapa umeme wale waliolipa *deposit* zaidi ya miaka mitatu iliopita na badala yake wanawapa

kipaumbele waombaji wapya? Naomba *TANESCO* wapeleke umeme shule za sekondari za Igima na Wanike.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa Kampeni ya Uchaguzi 2010, Rais aliahidi vijiji vya Dulamu, Palangiwani, Kuvinto, Mambegu, Ludinga na kadhalika vitapatiwa umeme. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii ili wananchi wajandae kupokea ahadi hii nzuri ya Rais. Kijiji cha Dulamu ndipo makazi ya Mbunge wa Jimbo la Njombe Magharibi na Makao Mkuu ya Ofisi ya Mbunge yanajengwa Igwachanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mpango huu na ambao umo ndani ya llani naomba shule ya sekondari ya Luduga ipatiwe umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Imlinyi na hasa Kata za Kipengele, Igosi, Ulembwe, Wangama yote ya Njombe, Makete inaongoza kwa kuwa na nyumba bora na za mfano katika vijiji vya Tanzania. Lakini hawana umeme. Nina uhakika umeme ukipelekwa huko karibu nyumba zote wanahitaji umeme. Je, Serikali iniambie ni lini Shirika la *REA* litapeleka umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* wamejenga *line* toka Igwachanya na kuunganisha Viji vya Chalowe, Mtapa na Kidungala lakini transfoma iliyowekwa ni ndogo. Naomba wapatiwe transfoma kubwa inayolingana na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* wamejenga *line* toka Wanging'ombe mpaka Utiga. Naomba umeme huo upelekwe kwenda Kijimbe Sekondari na Viji vya Ifuala, Ikingula na Katange.

Mheshimiwa Naibu Spika, *REA* tayari wamefanya mapitio ya awali katika Kijiji cha Wangama, naomba *REA* wakamilishe mipango ya vyanzo vya umeme ili umeme upelekwe Wangama na Shule ya Sekondari ya Maria Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umeme usambazwe zaidi katika maeneo yanayozunguka hospitali ya Illembula. sasa hivi Kijiji cha Illembula imekuwa ni mji mdogo na maeneo mengi hayana umeme, yapo maeneo *TANESCO* walisambaza nguzo kwa zaidi ya miaka 15 sasa, lakini hawajaendeleza mradi huo. Je, Serikali lini iniambie kazi hiyo na kuongeza maeneo mengine yatafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei ya nguzo za umeme. Bei ya nguzo moja kwa maeneo ya Njombe haizidi Sh.30,000/=. Je, kwa nini *TANESCO* inataka mwananchi wa Njombe alipie nguzo moja zaidi ya Sh.1,200,000/=. Je, kuna mantiki kweli? Je, Serikali haioni tukiachia hali hii iendelee, tutakatisha tamaa wananchi wa kawaida?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la *REA*. Kwenye hotuba yako kuhusu utekelezaji wa miradi ya *REA* naona *REA* itajikita kwenye mikoa 16 tu katika ya 21. Je, ni lini shirika hili litakuja Mkoa mpya wa Njombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa juhudi zao katika kutumikia wananchi kuititia Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kuona kuwa Wilaya ya Hanang ambayo ndiyo Jimbo langu haikupewa mradi hata mmoja wa umeme vijiji. Naona kuwa pengine ni kwa bahati mbaya, kwani wakati wa Kampeni, Rais alitoa ahadi kwa vijiji kumi, hivyo sijaelewa kwa nini Wilaya na Jimbo langu haikuorodheshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara. Naomba Waziri atoe maelezo kwa sababu mimi nalaumiwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Gendosi na Balong'odo kuna maziwa ya chumvi moja katika kila Kata. Inaonekana kama kuna utata katika umiliki wa rasilimali hizi. Naomba Wizara isaidie kuondoa utata huo ili tuje kuwa ni Kijiji au Kata au Halmashauri ndiyo ipewe umiliki ili matumizi ya chumvi yasilet migogoro kati ya mamlaka hizo tatu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono taratibu za kupata mitambo ya dharura lakini kuwe na uwazi wa kutosha ili tuongeze kwa haraka umeme kwenye gridi ya Taifa. Hatua hii pengine itasaidia vijiji vingi kupata umeme ikiwemo Jimbo langu. Hata hivyo, nataka kujua kwa nini na ni vigezo gani vilitumika kuacha Jimbo langu kuorodheshwa katika Mkoa wa Manyara. Je, ni hila au ni *omission*.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Spika, Namshukuru Mungu kwa afya nzuri na alivyotuwezesha kuwepo Bungeni tena leo. Namwomba atujalie kuyatekeleza na kuyajadili tena yale tuliyotumwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na timu yake kwa kuiongoza Wizara hii nyeti, kwa utekelezaji na kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo na matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri wanayoifanya kuishauri Wizara katika mipango yake na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, umeme ni janga la Kitaifa, uchumi wa nchi kuwa uchumi mkubwa na mdogo unategemea umeme.

Mheshimiwa Spika, viwanda vikubwa na vidogo vyote vinategemea umeme. Lakini hata wafanyabiashara wadogo wadogo kama vile mama nitilie na wauza *ice cream* wanategemea umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini hospitali zote za Rufaa, Kitaifa za Mkoa, Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati zinategemea umeme katika shughuli mbalimbali kama vile upasuaji, usuuzaji (*sterilization*), kufua nguo na mashuka ya wagonjwa, kupikia chakula cha wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, umeme ndio suluhu ya uharibifu wa mazingira (*deforestation*) kwa kukata miti hovyo kwa ajili ya kuni na mkaa na umeme ndo maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa umesahaulika muda mrefu, Mkoa mkubwa kama Rukwa kutegemea umeme wa *generator* na kuufanya Mkoa kuendelea kuwa maskini wakati ungeweza kusindika unga, mafuta ya alizeti, mafuta ya karanga, maharage, samaki wa Ziwa Rukwa na Tanganyika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, muda umefika wa kuwapatia umeme wa *Grid* ya Taifa ili waweze kuinua uchumi na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Serikali ikaleta mageuzi ya umeme nchi hii ili kuikomboa Tanzania kutoka lindi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini. nchi yetu hivi sasa imekua ikipiga kelele kutoka kila eneo lenye machimbo ya dhahabu, pamoja na madini mengine kutokana na ardhi inayomilikiwa na wananchi kupewa wawekezaji ambao huendesha kazi hiyo ya uchimbaji na kwamba inakubaliana juu ya suala la maslahi hayazingatii suala la yule mwananchi ambaye ni mmiliki wa eneo hilo la ardhi ambalo madini yamegunduliwa na pia hata Serikali ya kijiji husika nayo maslahi yanakuwa madogo mno.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kutosimamia vizuri na ikaandaa mazingira mazuri ya kumsimamia au kumlinda mwananchi anayemiliki ardhi yenye madini aliopewa Mwekezaji, hii ni kumdhailisha mwananchi wetu, kwa kuwa yeye hana nafasi ya kufanya majadiliano na Mwekezaji. Hivyo basi, naishauri Serikali kama mlinzi wa haki za raia wake itengeneze utaratibu wa kumlinda mtumiaji wa asili wa ardhi yenye madini kwamba Mwekezaji apewe sharti la kumpa mwenye ardhi hiyo kiasi fulani cha mapato ya madini yatakayopatikana toka eneo hilo la ardhi.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba wazalendo katika maeneo yao dhahabu inachimbwa na inaondoka ilhali Mtanzania ambaye ni mmiliki wa ardhi hana anachoambulia zaidi ya mashimo ambayo yanaachwa baada ya uchimbaji jambo ambalo linabaki kuwa hatari kwa wananchi wetu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mgao wa umeme. Mimi binafsi juu ya tatizo hili la ukosefu wa umeme ingawa Serikali kupitia wasemaji wa jambo hili mara nyingi wamekuwa wakitwambia kwamba tatizo hili husababishwa na uhaba au kina kidogo cha maji, lakini naomba niamini kwamba hilo sio tatizo la msingi, ila tatizo letu ni uchakavu wa mitambo na jambo hili, Serikali inaona ni aibu kulikubali.

Mheshimiwa Spika, ni afadhali Serikali ubebe lawama kwa kukubali ukweli huu, kuliko kupata lawama kila siku kwa kuliacha Taifa likiwa katika tatizo hili lisilokwisha.

Mheshimiwa Spika, ni rahisi sana kumdanganya mtu mmoja kwa kuwa anawezekana akawa si anaelewa juu ya jambo hilo, lakini Watanzania hivi sasa wako zaidi ya milioni 40, yawezekana kabisa kati yao ni wataalam kabisa juu ya jambo hilo, hivyo basi, tupo ambao tunajuliza kama tatizo, sio uchakavu wa mitambo na ikiwa tatizo ni kina cha maji, mbona hata vipindi nya mvua za mafuriko bado tunakuwa na tatizo la mgao na kwamba wengine wanapata mgao wa umeme na wengine wanapata mgao wa kiza totoro.

Mheshimiwa Spika, sasa tuache kuwageresha wananchi na Serikali ijione tu kwamba imo kwenye aibu kubwa ya kuendelea na tatizo hili la muda mrefu na huku ikielewa kwamba, hili ni jambo linalohatarisha maisha ya wagonjwa hospitalini, lakini pia linainyima Serikali mapato makubwa kila umeme unapokosekana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ahsante.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TPDC* ni Shirika muhimu katika utafutaji wa gesi na mafuta hapa Tanzania na kwa kuwa Shirika hili ni mali ya Serikali na kwamba inaipatia Serikali fedha (mapato) mengi yatokanayo na shughuli wanazozifanya, naiomba Serikali ilipe nguvu (meno) Shirika hili kwa kuwapatia mgao wa fedha za kutosha ili iweze kuendesha kazi zake vizuri. Ni vema Serikali ilipe kipaumbele Shirika hili la *TPDC* ili iweze kuongeza pato la Taifa zaidi.

Mheshimiwa Spika, utumiaji wa gesi asilia. Naiomba Serikali kupitia Shirika lake la *TPDC* iweze kuelimisha wananchi juu ya matumizi ya gesi kwa vyombo vya usafiri hapa nchini ili gari na vyombo vinavyofanana badala ya kutumia *diesel* na *petrol* toka nje ya nchi iweze kutumia gesi ili Serikali ifaidike kwa kuuza gesi yake hapa ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati ya umeme. Umeme umekuwa ni gumzo kubwa hapa Tanzania kitu ambacho kinatoa picha mbaya kwa Serikali yetu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali katika mipango yake iliyojipanga, iharakishe utekelezaji wake ili Taifa lipate umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, na kwamba ipunguze au iondoshe malalamiko ya wananchi juu ya uongozi uliopo madarakani. Serikali inatakiwa ibuni njia mbadala ya uzalishaji umeme na si kwamba kutegemea maji peke yake.

MHE. AGGREY D.J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi naomba pia nitambue kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Adam K. Malima, Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini. Ni ukweli usiopingika kwamba Mheshimiwa Malima amekuwa na msaada mkubwa katika Wizara jambo ambalo kwa ushirikiano na mshikamano mkubwa na Waziri wake wameweza kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara. Hongereni sana Waheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza ndugu zenu wote wanaofanya kazi chini ya Wizara hii pamoja na taasisi zote zilizopo na zinazofanya kazi sambamba na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya kipekee niwapongeze wafuatao: Bwana David Kitundu Jairo, Katibu Mkuu, Ndugu Mhando, *C.E.O TANESCO*, Dokta Mwakayesia, Mkurugenzi Mkuu *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia kazi nzuri inayofanyika Wilayani Siha ya kujenga njia za kusambaza umeme ili wananchi wengi waweze kupata huduma hii muhimu. Naomba kukumbushia yale maeneo ambayo yalisahaulika katika michoro na ambayo baada ya kuwasiliana na uongozi wa *REA*, wameniahidi maeneo hayo yanashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo hayo ni Kata ya Olkolili katika Kitongoji cha Sinai, Kijiji cha Olmelilli, Kijiji cha Embokoi, Kijiji cha Naibilie, Kijiji cha Lekrimuni, Kitongoji cha Lekrimuni, Kijiji cha Kandashi, vitongoji vya Soitolom na kile cha Karikacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nikumbushie mradi wa umeme unaotoka Kijiji cha Lawate kwenda Tarafa ya Siha Magharibi, Kata ya Ngare-Nairobi ambao upo chini ya *TANESCO*. Naomba sana nguzo ambazo zimekwisha kusimikwa katika mradi huo zisije zikaachwa zikaoza. Kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu la kuitazama upya sheria ya manunuzi ili ikidhi mahitaji yetu ya sasa naiunga mkono na nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kwa Wilaya ya Masasi kuwa kila mwaka mmoja kabla ya uchaguzi mkuu, huwa kunaanzishwa mradi ambao baada ya kupita uchaguzi mradi huo huwa unakomea hapo. Mwaka 2009 ulianzishwa mradi wa umeme ziliwekwa nguzo na nyaya na ahadi iliyokidai ya kwamba kabla ya mwezi kuanzia Juni, 2009 hadi Agosti umeme ungekuwa tayari. Lakini hadi leo kipande cha kutoka Nyangao Wilaya ya Lindi Vijijini na Nanganga hadi Ndanda Wilaya ya Masasi kipande ambacho kuna umbali wa karibu kilomita 32 tu. Sasa inaonekana hili kufanyika kama ni katika kampeni ya uchaguzi kama maandalizi.

Mheshimiwa Spika, si mradi huo tu ambao umefanya hivyo. Mwaka huo huo palikuwa na mradi wa maji ambao wataalam walipitia kupima na kuweka alama mpaka kwenye miti wakidai mtaro utapita humo. Lakini mwisho wa yote hakuna kilichoendelea.

Mheshimiwa Spika, hali kama hii inaleta usumbufu kwa kupewa matumaini na badala yake ni kukatishwa tamaa. Hivyo, Serikali iache kuwahadaa wananchi wa maeneo haya kwani huo umeme unahitajika sana.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, Kati ya Julai, 2008 hadi 17 Disemba, 2009 katika Kisiwa cha Songosongo, Wilayani Kilwa ambako mradi wa uzalishaji gesi unaendelea, ng'ombe wapatao 68 na mbuzi 17 walikufa baada ya kunywa maji yenye kemikali katika eneo linalodaiwa kufukiwa mabaki ya kemikali iliyotokana na uzalishaji wa gesi.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba wataalam kutoka Wizara ya Nishati na Madini, Afya pamoja na uongozi kutoka Wilayani iklongozwa na *OCD* walifika Kisiwani hapo kufuatilia tukio hilo.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu umepita tangu wataalam hao na uongozi huo ufile na kuondoa kwa maelezo ya kwenda kufanya uchunguzi bila kurejesha matokeo ya uchunguzi na hatima ya wananchi walipoteza mifugo yao:-

- (a) Naomba maelezo ya uchunguzi huo.
- (b) Iwapo uchunguzi umechukua muda mrefu kiasi hicho kuna mategemeo ya wananchi hao kulipwa fidia ya mifugo yao.
- (c) Tutahakikisha vipi kwamba madhara yaliyotokea hayataendelea kutokea tena kwa mifugo au kwa binadamu? Tafadhali naomba maelezo japokuwa kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, rasilimali za nchi ikiwemo gesi ya Songsongo ni moja ya misingi mikuu ya Serikali katika jitihada zake za kukuza uchumi na kuinua kiwango cha utoaji wa huduma bora za jamii.

Mheshimiwa Spika, kila sehemu inayochimbwa madini, wananchi wa Wilaya hiyo wanapata manufaa ya kupewa misaada ya ujirani mwema pamoja na mrahaba ambao Halmashauri zao hupewa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilwa kuna mradi wa gesi ya Songsongo pia tunaelezwa kwamba, katika gesi hakuna mrahaba:-

- (a) Je, Halmashauri ya Kilwa katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na rasilimali zake ndani ya Wilaya yake, inapata nini kutoka katika mradi huu wa gesi ya Songsongo.
- (b) Pamoja na misaada waipatayo wananchi wa Kisiwa cha Songsongo ya ujirani mwema. Je, wananchi wengine wa Wilaya ya Kilwa ambayo mradi huu unatekelezwa kupitia Halmashauri yao ya Kilwa wananaufaika vipi na mradi huu wakati naambiwa gesi haina mrahaba.

Mheshimiwa Spika, tafadhali naomba maelezo.

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza sana taarifa ya Waziri Mkuu ya ununuzi wa mitambo ya dharura lakini naomba utekelezaji huo uchukuliwe juhudui za hali ya juu ili ahadi yake itekelezeke mapema.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ikubaliane na Wawekezaji wengi ambao wanawenza kuleta huduma hii ya umeme ili suala hili la ukosefu wa umeme pia lipungue na litokomee kabisa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ifute kabisa kauli yake ya kujenga jengo la Ofisi kwa kutumia pesa nyngi na badala yake pesa hizo watafute njia mbadala ya kuleta umeme.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie kwa kina milima yetu ya Oldonyolengai iliyopo Mkoani Arusha kutafuta wataalam na kuifanya uchunguzi na baada ikiwezekana tupate umeme badala ya kuiachia milima hiyo kulipuka kila mara.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ifanye ziara nchi ya jirani yetu Kenya (*Ken Gen*) iliyoko Naivasha kwenda kuangalia wanavyofuata milima kutoa umeme badala ya kuachia milipuko ya bure.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mambo muhimu ya mchangano wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhaba wa umeme. Katika historia ya nchi yetu kuhusu upatikanaji wa umeme hajjawahi kutokea kipindi kigumu cha mgao wa umeme kama ilivyotoka sasa. Ushauri wangu ni kwamba Serikali ichukue hatua za kidharura kama vile nchi imevamiwa na adui giza. Tusiwe na woga wa kuvunja kanuni za kawaida na kuweka kanuni za dharura. Sheria ya Manunuzi itazamwe kwa dharura ili maamuzi yatekelezwe kwa haraka bila woga wala ubabaishaji. *Generator* au vifaa vya umeme vinunuliwe kupunguza uhaba wa umeme bila woga.

Mheshimiwa Spika, ombi la umeme, Jimbo la Lushoto. Wakati wa kampeni ya uchaguzi Mkuu wa 2010, Rais aliahidi wananchi wa Tarafa ya Mlola, Jimboni Lushoto kwamba watapatiwa umeme. Naomba Serikali ichukue hatua ya utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais. Tarafa hiyo ya Mlola inazo Kata Sita, za Malibwi, Kwekanga, Kilole, Mlola na Makanya. Kata jirani na maeneo hayo zina umeme, hivyo kufanya malalamiko ya wananchi wa kata zisizo na umeme kuwa ya msingi. Naomba *REA* na *TANESCO* washirikiane kutekeleza ahadi ya Rais mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishaji wa mashirika na taasisi zilizopo ndani ya Wizara. Wizara ina taasisi na mashirika nyeti sana kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Nashauri uimarishaji wa mashirika na taasisi zilizopo. Pia ni muhimu kuhuisha majukumu ya mashirika hayo hatimaye kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi. *TANESCO* irekebishwe muundo wake ili kuongeza ufanisi na iongezewe mtaji na kuimarisha uongozi katika ngazi za kati na chini. *TPDC* liimarishwe na mpango wa kuagiza mafuta kwa wingi utekelezwe bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *EWURA*. Ipewe uwezo wa kusimamia kanuni na sheria. Ni aibu mdhibiti anatoa maelekezo na utekelezaji haufanyiki lazima mamlaka ipatiwe ushirikiano na kanuni zenye uzito stahili. Wizara kama msimamizi wa sekta ya nishati na madini, lazima iratibu shughuli za taasisi nyingine kusaidia *EWURA* suala la kupunguza bei ya mafuta ni mtihani kwa Wizara na Serikali kwa ujumla. Suala la kupunguza bei ya mafuta kama ilivyoahidiwa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *REA*. Shabaha ya kuundwa *REA* ni kuleta msukumo na mapinduzi ya kupeleka umeme vijijini. Shabaha na malengo kusudiwa yasipofikiwa ni changamoto. Nashauri uandaliwe mpango kamambe wa muda mfupi, wakati na wa muda mrefu. Maeneo yatakayopewa umeme yatambuliwe kwa kuorodheshwa. Kwa kufanya hivyo, tutajenga matumaini kwa wananchi. *REA* waongezwe mtaji wasitegemee tu Mfuko wa uendelezaji umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Mheshimiwa Spika, ununuzi wa *second hand generators*. Hali ya umeme inatisha sana. Uchumi wa nchi unadidimia. Watu hawana kazi na mashirika na miradi midogo midogo ya watu binafsi inaendelea kufungwa.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa, hatua za dharura zichukuliwe ili ziwezeshe kununua majenereta ya *second hand* na kupunguza mgao wa umeme. Langaliwe kuwa majenereta hayo yawe katika hali nzuri na yawe yametumika kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa kujenga Afisi Kuu ya Wizara. Katika mwaka 2011/12 Wizara imetenga zaidi ya Sh. 3,000,000,000/= kwa ajili ya kujenga Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara isimamishe mara moja azma ya ujenzi huu badala yake fedha hizo zitumike kununulia majenereta ya *second hand* niliyoyaeleza hapo juu. Wananchi hawatafahamu kwamba wao hawapati maji, miradi imefungwa na matatizo mengine mengi kutokana na kukosekana kwa umeme.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kupongeza hotuba ya Waziri ilioandaliwa vizuri na kama yaliyoelezwa katika hotuba yatakelezwa kwa ufanisi mkubwa tutakuwa tumeondokana na tatizo la uhaba wa umeme katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, haja yangu upatikanaji umeme katika mji mdogo wa Laela na ahadi ya Mheshimiwa Rais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Laela ndio mji mdogo katika Wilaya ya Sumbawanga Vijiji na ni Mji ambaa ndiyo Makao Makuu ya Wilaya yanapoandalishi. Hivyo, shughuli nyingi za Serikali zinazohitaji umeme. Zitatakiwa kufanyika pia ni mji unaozungukwa na wakulima wengi wanaolima mazao ya karanga, alizeti na kadhalika ambayo yanahitaji kuwa na viwanda vidogo. Tunazo shule za sekondari nyingi zaidi ya kumi ambazo zinahitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme vijiji (*REA*) katika Mto Nzovwe. Jimbo la Kwela limezaliwa kuwa na mito mingi yenye sifa za kuweza kuzalisha umeme. Lakini kwa leo, naomba Serikali inipe majibu namna ambavyo imejipanga. Katika kuutumia Mto Nzovwe uliopo katika Jimbo la Kwela, Tarafa ya Mtowisa Kata ya Milepa, Kijiji cha Msia.

Mheshimiwa Spika, Mto huo ulishafanyiwa *Research* na kuona kuwa tunaweza kupata umeme kiasi cha *Megawatt* tano. Umeme ambaa unatosha kabisa kuenezwa katika Wilaya au Jimbo la Kwela na inasemekana kuwa zipo Kampuni zilizoomba kufanya kazi ya kutengeneza umeme huo kupitia *REA*, naomba kujua ni nini kinaendelea hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, umeme wa nguvu ya juu (*solar*). Naishukuru Serikali kwa kufunga *solar* katika baadhi ya Kata zangu katika huduma muhimu kama vile Zahanati, Vituo vya Afya, sekondari. Naomba kazi hiyo nzuri iendelee katika kata za Milepa, Illemba, Kaoze, Miambalua, Kalambanzite, Kaengesa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kupata ufanuzi huu, nitaunga mkono hoja.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi ngumu na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa nchi yetu ina matatizo sana na umeme wafanyabiashara wote wadogo na wakubwa wanapata shida sana, kwani bidhaa zao zinaharibika na biashara zao zinadorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii, inawapatia shida na matatizo na kuendeleza umaskini badala ya kupunguza umaskini!

Mheshimiwa Spika, akinamama na vijana ambaa wangeweza kuijendeleza kupitia viwanda vidogo vidogo, ukweli kabisa hawawezi kuendelea bila ya uhakika wa umeme. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuwa Serikali ichukue hatua za haraka na kushughulikia tatizo hili. Serikali iliangalie kwa makini kwa kununua *generators* za kunusuru tatizo hili. Kwa sasa tunapata mgao wa umeme, mgao ni mkali, lakini kumbuka kuwa kiangazi ndio kinapamba moto, maji Mtera yanazidi kushuka kina, maana yake, tatizo litazidi zaidi hivi karibuni. Tafadhalii sana Serikali yetu chukueni hatua za haraka.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Morogoro Vijiji, Mvomero, Kilombero, Kilosa, Gairo na Ulanga, naomba vipatiwe umeme kupitia *REA* au umeme wa *grid*. Akinamama wa Morogoro waweze kuendeleza miradi yao, hasa ya usindikaji wa matunda na mbogamboga. Naomba ombi langu lipokelewe.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Nyakayanja, Nyaishozi, Ihembe, Nyakasimba, Kyanyamisa, Chamugisha, Kamuli Wilayani Karagwe, naomba vipatiwe umeme. Nashukuru Serikali mpango umeanza, lakini ombi langu umeme huu uharakishwe ili wananchi wapate maendeleo. Tangu enzi ya wakoloni vijiji hivi, hawaajaona umeme wanatumia koroboi ndogo na taa za karabai.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iharakishe kuleta umeme Ruvuma ambaa hawana umeme wa *grid*. Shukrani mpango ulioanza, lakini kukamilika mwaka 2014 ni mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kuleta na kuweka *generators* Namtumbo na Songea Mjini, wananchi wanausubiri sana, naomba Wizara wafanye haraka sana ili wananchi wapate uhakika wa umeme na kuendelea na miradi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iijitahidi sana, hasa kwa umeme wa juu (*Solar power*) kwani ni rahisi sana kwa kutoa umeme na kusaidia, hasa kwenye taasisi mbalimbali kama shule na hospitali. Bila ya umeme wa uhakika elimu ya wanafunzi wetu, haitawenza kuendelea vizuri. Kwani tukiwa kwenye giza, wanafunzi watafanyaje *studies* zao, yaani kujisomea!

Mheshimiwa Naibu Spika, bila umeme wa uhakika, wagonjwa hospitalini kwetu au nchini watapata shida, hasa kwenye vitengo vya upasuaji na mionzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, gesi ya Songsongo na Mnazibay, usimamiwe kusudi mikoa mingi ya jirani ipate umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, gesi ya Mkuranga imeishia wapi? Tunayo gesi ya kutosha nchini ambayo ikifuatiliwa na kusimamiwa itapunguza tatizo la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa upepo tayari upo Mkoa wa Singida. Tatizo ni mimi, teknolojia hii isienezwe mahali popote ambapo kuna uhakika wa upepo mkali hapa nchini? Tukijitahidi kutumia njia zozote zile za vyanzo vya umeme tutafanikiwa kupunguza tatizo hili nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *PPP* wafanyabiashara binafsi wakaribishwe kwa wingi katika kuzalisha umeme hapa nchini. Wananchi wapate umeme kuititia njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Makaa ya mawe ombi na ushauri ni kuwa miradi hii isimamiwe na kufuatiliwa kikamilifu, uzalisho umeme, wananchi wanufaikie kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *EWURA*. Serikali imepunguza mafuta ya *diesel* na *petrol*. Lakini cha kushangaza, badala ya bei kushuka, imepanda. Ushauri bei hizi ziangaliwe kwa undani, kwani watu hawaoni unafuu au mantiki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* iimarishwe, kusudi ifanye kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu yeypote aliyepata madaraka Namtumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuona tatizo la umeme nchini na kuja na mipango ya kuanza kutafuta suluhisho la kudumu. Japo suluhisho hilo haliwezi kutekelezwa kwa sasa lakini mipango mizuri iliyoonekana kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano ukisimamiwa utekelezaji wake tunaweza kuja na suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme kwa sasa unaathiri uchumi wa nchi na pengine kuteremsha heshima ya Serikali katika kusimamia uchumi wa nchi na mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la umeme nchini limesababishwa na mipango isiyonna mbali. Nashauri kutafuta wataalam washauri, watusaidie katika kuanza kuwekeza kidogo kidogo. Kuelekea kutafuta utatuzi endelevu wa tatizo hili, ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Rais akiambatana na Waziri wa Nishati katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Nkasi hazitekelezwi na hii inamwangusha Rais wetu Mpewda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nkasi ni mionganini mwa Wilaya chache sana nchini ambazo wananchi wake wameanza kupoteza imani kwa Serikali na pengine kufikiria kuwa labda wawakilishi wao ni butu. Pamoja na ahadi za mara kwa mara lakini bado wananchi hawajapata huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, dalili zinazoendelea kwa sasa zinaweza kurudisha imani iliyopotea endapo tutaendelea na spidi hii hadi kupata umeme ifikapo Disemba, 2011 kama anayoahidi Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushauri katika masuala ya umeme nchini. Nchi ijikite katika kutafuta suluhisho la umeme kwa misingi ya kutumia rasilimali asilia za nchi kama gesi, upopo, makaa ya mawe na maporomoko yanayoonekana hayajawahi kuathirika katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu, kwa vile umeme unapita Namanyere kutokea Sumbawanga. Nashauri vijiji vilivyoko njiani kama vifuatavyo, vifungiwe umeme hata kabla ya umeme kufika Namanyere. Vijihi vina Shule za Sekondari, Zahanati na Shule za Msingi nazo ni: Nkundi, Kipande, Kantawa, Mikundikwa, Kasu, Chala, Kacheche, Londokazi, Ntalukubila na Kanazi. Naomba vile vile pawepo utaratibu wa kusogea umeme Ziwa Tanganyika ili kuvutia wawekezaji wa minofu ya samaki wa ziwa hilo. Umeme utasaidia ajira kwa vijana wengi na kupungua kwa kiasi tatizo la ajira katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia mbalimbali zitawezeshwa kutumika katika shughuli za huduma na uchumi (TEHAMA).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini. Mikataba ya migodi hii iangaliwe upya haraka iwezekanavyo hata sheria iliyobadilishwa karibuni inaweza kuwa na dosari nyngi, tunaomba Muswada mpya uje tuweze kushughulikia katika Bunge hilli la kumi ili tuzingatie mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauaji makubwa ya mara kwa mara na vurugu zinazotokea maeneo ya wawekezaji lazima zikomeshe na wahusika wawajibishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yanayolalamikiwa kuwa yanaathiri maisha ya watu kwa madawa yanayotumiwa kusafisha madini yetu ufumbuzi utafutwe haraka, lazima Serikali kuthamini raia wake, iwe na masikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti zaidi unahitajika katika kuendelea kubaini maeneo yenye madini zaidi na mafuta hasa katika Mkoa wa Rukwa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vema hotuba yake nampongeza Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Maofisi wote kwa kumsaidia Waziri kuandaa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Namtumbo haina umeme toka tupate uhuru. Nimekuwa nikiahidiwa toka 2006 kuititia Bunge lako Tukufu na Serikali, mimi na wananchi wa Namtumbo tuliendelea kupata matumaini na hasa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alipotamka Bungeni kwa vipindi viwili tofauti Bunge la Tisa na Bunge la Kumi.

Mheshimiwa Spika, matumaini makubwa yalijitokeza alipofika Namtumbo, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Adam Malima na kuwaeleza wananchi kuwa, sasa wakati wa Namtumbo kuititia umeme umefika na jenereta ya *Megawatt* 1.25 litafungwa Namtumbo Mjini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri alituhakikishia na baada ya muda walifika wataalam kutoka *TANESCO*, Makao Makuu na walituomba eneo tukawapa maeneo mawili moja la kuweka mtambo wa kuzalisha umeme na moja la kuweka Ofisi ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matumaini makubwa yote hayo Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini wakati anawasilisha kauli ya Serikali Bungeni alisema mpaka Disemba, 2011 umeme utawaka Namtumbo na leo tarehe 15 Julai, 2011 katika hotuba ya Waziri, aya 132 amesema: "Uungaji wa jenereta tisa zenye uwezo wa kufua umeme *megawatt* 1.25 kila moja kwa ajili ya Makao Makuu ya Wilaya ya Namtumbo, Sumbawanga, Nkasi na Ngorongoro unaendelea kufanywa na Mkandarasi Zwart Techniek ya Uhlanzi.

Mheshimiwa Spika, katika aya hiyo ya hotuba ya Waziri imeeleza Jenereta nne zenye *megawatt* tano zimefungwa Ngorongoro na nne zenye uwezo wa *megawatt* tano zimefungwa Sumbawanga na hii moja iliyobakia inatarajiwa kufungwa Namtumbo. Sasa kinachonishangaza

mie kwa nini Namtumbo ifungwe yenyе uwezo wa kufua *megawatt* 0.4 wakati inatakiwa ifungwe ya *megawatt* 1.25 kama zilizofungwa katika Wilaya zingine na maelezo yanasema zimenunuliwa jenereta tisa kila moja yenyе uwezo wa *megawatt* 1.25 iweje mje mtufungie 0.4 inatoka wapi hiyo? Kwa nini mfunge yenyе uwezo mdogo, mnataka nije tena kila mara kulalamika umeme hautoshi?

Mheshimiwa Spika, sisi tuna taasisi, majengo ya taasisi nyingi, watu binafsi tunategemea kuwa na viwanda vidogo vya *ku-process* mazao yetu mbalimbali, mafuta na chakula ambavyo vipo ili uwezo wake mdogo sababu ya kukosa umeme. Hospitali ya Wilaya, Ofisi za Halmashauri, Ofisi ya DC na pia kuna mradi wa Urani ambao tunategemea watakuwa na kiwanda chao kidogo cha *Refabrication* ambacho kitahitaji umeme wa kutosha ambacho tunategemea kitatoa ajira nyingi.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo mazuri na mtufanyie mtambo wa *megawatt* 1.25 kama maelezo ya awali yanavyosema.

Mheshimiwa Spika, hakuna dalili zozote zinazoendelea katika maeneo tuliyowapa kuweka jenereta hadi leo. Je, kweli umeme utawaka Namtumbo Disemba, 2011.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia taarifa hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Katibu Mkuu Ndugu David Jairo, watendaji wote wa Wizara walioshiriki kuandaa bajeti hii muhimu sana Watanzania kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo mkunjufu naomba Mwenyezi awape upendo, moyo wa uwajibikaji, mshikamano na afya njema ili waweze kutekeleza azma yao vema. Hivyo basi, kabla ya kuanza kutoa mchango wangu ambao nategemea kupewa majibu na Waziri na Naibu Waziri wakati wakijibu hoja za Wabunge nitamke rasmi kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la mgao wa umeme. Napenda kuipongeza sana Kamati ya Nishati na Madini chini ya uongozi wa Mheshimiwa January Yusuph Makamba, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini na mimi Makamu Mwenyekiti wake pamoja na wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri na nzito ya kujadili bajeti ya Nishati na Madini kuhusu matumizi na mapato kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa kazi ilikuwa kubwa na ngumu kulingana na ukubwa wa Wizara hii na unyeti wa umeme, kupitia vyanzo mbalimbali na madini kwa ajili ya kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo ya upatikanaji wa umeme kwa hatua ya haraka, hatua ya Kati na hatua ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati yalifkia karibu thelathini lakini Serikali imekuwa na utekelezaji wa polepole sana wakati nchi inaingia gizani, viwanda uzalishaji umeshuka sana hata wajasiriamali wakiwemo wanawake unatishia amani na familia nyingi kuyumba kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naiomba sasa Serikali kuchukua hatua za haraka za kutatua suala la uzalishaji wa umeme. Natambua kinachokwamisha ni gharama kubwa za uzalishaji na kuogopa bei kubwa ya kuwaanzia watumiaji wa umeme, Serikali lazima iangalie namna ya kubeba mzigo wa kufidia gharama kubwa ya umeme ili wananchi washindwe kulipia umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme Mkoani Singida kupitia REA. Napenda kuikumbusha Serikali juu ya miradi yake ya umeme kupitia mradi wa umeme vijijini kupeleka Chikuyu, Kilimatinde, Chibumagwa na Kintiku, kweli ni wa polepole sana naiomba Serikali longeze kasi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wilaya ya Manyoni, Jimbo la Manyoni Mashariki halina umeme zaidi ya Manyoni Mjini. Naishauri Serikali kulitazama Jimbo hili kwa jicho la huruma sana kwani Watanzania wote ni sawa.

Mheshimiwa Spika, vile vile naikumbusha Serikai ahadi yake ya kupeleka umeme Kituo cha Afya Mgongo, Tarafa ya Shelui ambayo imekuwa ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa upepo Singida. Naipongeza Serikali kwa kugundua kwa upepo uliopo Singida Mjini unaweza kuzalisha umeme wenye *megawatt* mia moja. Kwa taarifa za Mheshimiwa Dokta Parseko Kone, Mkuu wa Mkoo wa Singida ni kwamba wakandarasi waliojitekeza ni wawili lakini hadi sasa amefika mmoja tu. Napenda kupata majibu ya Serikali, mwingine yuko wapi kwani kwa mwendo wa polepole mradi huu hautatekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa wakazi wa eneo la kujenga mitambo ya kuzalisha umeme wa upepo. Napenda kuitaarifu Serikali kuwa kunasababisha migogoro kila mara kwa wananchi sio jambo jema, hivyo ni vema tathmini ifanyike ya mali za wakazi ambao wanatakiwa kuhama kabla ya ujenzi wa mitambo kuanza.

Mheshimiwa Spika, hivyo napenda kujua wananchi wa Kitilimo na vijiji jirani eneo ambalo mitambo ya kuzalisha umeme wa upepo itajengwa ni lini watafidhiwa ili ujenzi uanze bila migogoro.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogo wadogo. Naipongeza Serikali kutenga fedha kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo wa madini. Hivyo, ni matumaini yangu wachimbaji wadogo wadogo walioko Mkoani Singida, Vijiji nya Sambaru, Mang'onyi, Londoni na Mwani (Singida Vijijini), Sekenke, Misigiri, Mpambala na Maruga watanufaika na fedha hizi hususan wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kuwa wachimbaji wadogo wadogo wanashindwa kunufaika na madini haya pamoja na kuwa waanzilishi wa uchimbaji kwa sababu ya kukosa miundombinu ya kisasa. Ni vema Serikali iwawezeshe wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwakopesha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Chumvi, Chinangali, Manyoni na Nkonkilangi, Iramba nina matumaini yangu, Serikali inawatambua wanawake wanaotengeneza chumvi huko Manyoni (Chinangali) na Iramba Nkonkilangi. Pamoja na mradi huu mzuri bado kuna tatizo la chumvi kutokuwa na madinijoto, naiomba Serikali itamke namna ya kusaidia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchakachuaji wa mafuta. Naipongeza sana Serikali kwa ufumbuzi wake wa kuondoa tatizo la uchakachuaji kwa kuondoa msamaha wa kodi ya mafuta ya taa na kufanya bei ya mafuta ya taa, dizeli, petroli na mafuta ya jeti kuwa moja. Hii itasaidia sana kuondoa uchakachuaji wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, naiomba *EWURA* kuweka uwakilishi kila Mkoo pamoja na kuhakikisha vinasaba vinatumika kwenye vituo vya mafuta, vyote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kushuka kwa bei ya mafuta. Pamoja na Serikali kutangaza kushuka kwa bei ya mafuta lakini hadi sasa bei bado juu. Naomba maelezo, bei itashuka lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu ujenzi wa Makao Makuu ya Nishati na Madini, Dar es Salaam. Naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga Makao Makuu ya Wizara hii ili kuachia jengo la *TANESCO* ambalo ndilo wanalitumia kama Makao Makuu hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri, kwa kuwa Waziri Mkuu alipokuwa anahitimisha bajeti yake alitamka rasmi kuwa Makao Makuu ya Wizara zote yatajengwa Dodoma ambako ndio Makao Makuu ya nchi yetu. Pia na kwa kuwa hata gharama za ujenzi hadi kumalizika bado hajulikani, napenda kushauri Serikali, fedha zilizotengwa bilioni tatu zihamishiwe Mfuko wa *REA* na zitumike kupeleka umeme Kata mpya ya Mgongo, Tarafa ya Shelui, Wilayani Iramba ambayo ni ahadi ya Serikali ya zaidi ya miaka minne sasa. Nahitaji ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme tokwa Singida Mjini kwenda Sepuka. Napenda kuikumbusha Serikali ahadi yake ya kupeleka umeme Sepuka, ahadi ambayo imekuwa ya muda mrefu zaidi ya miaka minne. Nimefuatilia bajeti yote, sijaona fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ambao wananchi wamechoshwa sana na ahadi ya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wakati wakijibu hoja anipatie majibu yenyewe kuwatia moyo wananchi wa Sepuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliohusika katika uandaaji wa hotuba hii. Hotuba ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mradi mzuri unaolenga Watanzania wengi, mradi wa usambazaji wa umeme vijiji katika Mikoa 16, Mkoa wa Kagera, ukiwemo huu ni mradi mzuri lakini tunaomba kasi ya utekelezaji iongezeke kusudi watu wengi na vijiji vingi zaidi viguswe.

Mheshimiwa Spika, nilipeleka maombi ya umeme kuitia mpango wa usambazaji umeme vijiji kwa Kata ya Katoma, Bukoba Vijiji, Vijiji vya Lukindo, kuelekea kwenye shule ya msingi ya Askofu Kilaini, kinachohitajika hapa ni *sub station* na nguzo na nyaya. Ombi nilileta tangu mwaka 2009. Niliahidiwa kuwa umeme ungepatikana, lakini hadi leo hakuna, naomba maeneo hayo ya Katoma, Lukindo, Bushasha, Mahuguru hadi Kabale wapatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, bila umeme hakuna maendeleo, hakuna elimu bora, huduma za mahoteli zinaathirika, huduma za hospitali, ujasiriamali (usindikaji wa juisi, utekelezaji wa mbao, uchomaji vyuma, ufundi vyerehani) vinaathirika, watu wanashindwa kuzalisha, wanapata hasara. Watu wanachotaka ni umeme. ni lini Serikali itanunua mitambo kwa haraka kunusuru nchi kuokoa wajasiriamali na watu wote walioathirka na ukosefu wa umeme, ili umeme upatikane sasa na Serikali iweze kuitia *TRA*? Bila umeme maisha yatakuwa magumu sana.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta ya taa inaendelea kupanda, kiasi kuwa huko vijiji watu wanateseka. Ni lini Serikali itadhibiti upandaji kiholela wa bei hizi?

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua kuwa sekta ya umeme ni kichocheo cha maendeleo ya viwanda, kilimo cha umwagiliaji, mawasiliano na kwa kiasi kikubwa huduma za jamii bora, zinategemea upatikanaji wa umeme, napendekeza:-

Kwanza, Serikali iongeze bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Pili, Wizara iwekeze katika kununua miradi au mitambo mikubwa, ili umeme upatikane katika mwezi mmoja hadi miwili ili kunusuru Taifa letu.

Tatu, kwa kuwa sasa, umeme ni janga la Taifa Serikali itafute fedha kokote kunakowezekana, tuwe na *Rescue package* tufufue sekta ya umeme.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA: Mheshimiwa Spika, utekekelezaji wa ahadi ya Rais wakati wa kampeni 2000. Kwanza nikupongeze Waziri, Naibu Waziri na Makatibu wakuu wote na Wakurugenzi wa vitengo vyote.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri arejee barua niliyomwandikia kuhusu hili ninalotaka kuchangia.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ruangwa, Wilaya ya Ruangwa ni eneo lililounganishwa na mtandao wa umeme kutoka Masasi kuitia Nachingwea. Tunashukuru kwa kuunganishwa.

Mheshimiwa Spika, Jimbo hili pamoja na umeme uliopo bado kuna mapungufu yaliyopo hasa Shirika la TANESCO halijamudu kusambaza kwa wananchi angalau Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wakati wa kamjeni ya uchaguzi mwaka 2000, Rais wa Awamu ya Tatu, Rais Mstaafu Benjamin Mkapa aliahidi kuvipatia umeme Vijiji vya Mnacho, Malolo na Nanganga ambavyo viro kando kando ya barabara iendayo Lindi na upande wa pili wa Mbekenyera. Kazi hiyo ilishaanza kufanya upimaji urefu wa njia zote pia kujua idadi ya walaji ambayo ilitosha mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kuleta nguzo zilizotakiwa ziunganishe mtandao wote kutoka Mkoa ambako umeme wa sasa umefikia.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kukujulisha tena kuwa mpango huo ulisitishwa huku kukiwa kuna mahitaji makubwa. Nguzo zilizoletwa mwaka 2003 ziliunganishwa mwaka 2006 bila ya kusambaza umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazofanya pamoja na changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hii. vile vile nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii, yeye binafsi na watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe shukrani zangu kwa Serikali kwa kuonyesha nia ya dhati ya kupeleka umeme katika vijiji vya Bisheshe, Nyakayanja, Nyashozi na Ihembe. Naishukuru Serikali kwa uamuzi huu thabiti wananchi wa vijiji hivi walipokea kwa furaha taarifa ya Mheshimiwa Waziri aliposema kuwa Mkandarasi atakabidhi umeme huu ifikapo Desemba, 2011. Tayari wananchi wameanza kununua vifaa vya kutumia umeme kwa matumizi kuwa watakula sikukuu ya X-Mas na mwaka mpya kwa kuzindua vifaa vyao vya umeme. Tumeomba Serikali isimamie kauli yake mkandarasi atimiza wajibu wake wa kuwasha umeme ifikapo Desemba, 2011. Ikumbukwe hii ni ahadi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia aliyekuwa Naibu wa Waziri wa Nishati na Madini, Lawrence Masha mnamo mwaka 2006 iliahidi kupeleka umeme katika Vijiji vya Ihanda, Rukole, Kamagambo, Nyakagoyagoye hadi Nyakaiga. Ahadi hii imeendelea kuelezwu kila mwaka kuanzia 2007, 2008, 2009, 2010 na katika kamjeni za uchaguzi, Mheshimiwa Rais akiwa Kijiji cha Nyakaiga, Jimboni Karagwe aliahidi kuwa umeme utawaka mwaka 2011. Ahadi hii ilishuhudiwa na Mheshimiwa Waziri aliyeambatana na Rais. Ajabu, leo hii sioni chochote katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Maana yake ni kwamba Serikali haina mpango wowote wa kupeleka umeme huu katika vijiji hivi. Ni kwa nini ahadi ya Mheshimiwa Rais haianzi kufanyiwa kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nguzo za umeme zilizopelekwa Vijiji vya Ndama, Rukaka, Nyabwegira, Kakilo, Runyaga imekuwa ni kero kwa wananchi kwani ziko pale takriban miaka mitano zingine zimesimikwa na nyininge zimelazwa chini. tunaomba umeme siyo nguzo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karagwe inayo maporomoko ya maji yanayoweza kutoa umeme wa kutosha Wilaya ya Karagwe na Kyerwa. Maporomoko hayo yako Murongo (Murongo water falls) na mengine yako Kijiji cha Kibogoizi, Kata ya Ihembe Wilayani Karagwe. Pia yapo maporomoko ya Karagwe Kitongoji cha Kashambi. Najua Serikali haina habari yoyote na maporomoko haya.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Tanzania tunayo gesi ya kutosha kwa matumizi ya nyumbani, kuzalisha umeme na matumizi ya kuendesha magari. Shirika la Maendeleo ya *Petrol* la Taifa (TPDC) wameshaanzisha program ya kutumia gesi kwenye magari. Hili ni jambo jema kwa Taifa letu. Maoni yangu ni kwamba naomba magari yote ya Serikali yanayoagizwa yawe tayari yamefungwa vifaa vya kutumia gesi na siyo *petrol*, pia magari yote ya umma kwa maana ya

Mashirika ya Umma, TAMISEMI, Serikali Kuu na viongozi wote wa Serikali sharti magari yao yawe ni yale yanayotumia gesi na si *petrol*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya umeme Serikali ifanye kila linalowezekana, bei ya umeme isipande mara kwa mara kwani Watanzania walio wengi hawawezi kumudu gharama za umeme kwa sasa. Umeme vijijiini uwekewe utaratibu wa kuwawezesha wananchi wa kipato kidogo kuingiza umeme majumbani kwao kwa bei ya chini na kulipia gharama ndogo za matumizi yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nguzo za umeme. Ni kwa nini TANESCO inaendelea kuagiza nguzo za umeme kutoka nje ya nchi kwani gharama za nguzo za umeme ziko juu kutokana na nguzo hizo kutopatikana hapa nchini. Nchi yetu inayo miti mingi ya nguzo za umeme kama vile mikaratusi ya Kagera na sehemu nyinginezo, pia miti mizuri ya *pine* ya Iringa, Moshi, Mbeya, Kagera na kadhalika. Nashauri Serikali iliangalie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya taa yamepanda bei. Hii si habari njema kwa wananchi wengi waishio vijijiini. Nia na madhumuni ya mpango huu ni nzuri sana kwani inalenga kuondoa uchakachuaji wa mafuta ya taa na dizeli. Ombi langu kwa Serikali ongezeko la ushuru wa mafuta ya taa toka shilingi hamsini na mbili (52/=) hadi shilingi (400/=) zipelekwe Wakala wa Umeme Vijijiini (*REA*) ili zisaidie kupeleka umeme kwenye vijiji vingi kama siyo vyote nchini.

Mheshimiwa Spika, nazidi kuwatia moyo na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini chini ya uongozi mahiri wa Waziri William Mganga Ngeleja, Naibu Waziri, Adamu Kighoma Malima, Katibu Mkuu Ndugu Jairo na timu yake yote.

Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto zinazokabili Wizara hii tutaendelea kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha kuwa madini ya Tanzania yanawanufaisha Watanzania wote na nishati ya umeme inafika vijiji vyote nchini. Hata hivyo, lazima tukiri kuwa Wizara hii bado ina kazi nzito ya kudhibiti madini ili yawanufaishe Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini. Tanzania ina madini mengi yaliyosambaa katika mikoa mbalimbali. Upo ushahidi kuwa madini ya dhahabu yanaabiwa na wachimbaji wakubwa. Taarifa zinazotolewa kwa dhahabu inayosafirishwa nje ya nchi sio sahihi hivyo kulinyima Taifa mapato makubwa. Serikali haina budi kujenga viwanda vya kusafisha madini hapa hapa nchini ili tusafirishe dhahabu safi inayojulikana uzito wake.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo, bado hawajapewa msaada wa kutosha kuwawezesha kwa mikopo ya kuchimba madini. Tukumbuke hawa ndio wenye haki zaidi ya kufaidi rasilimali ya nchi hii. Kwa ujumla mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa ni mdogo mno na kwa kweli inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya umeme. Kama tujuavyo umeme hivi sasa ni janga la Taifa. Kukosekana kwa umeme wa kutosha kunaathiri uchumi wa nchi na maisha ya Watanzania mmoja mmoja. Hivyo, Serikali ni budi ichukue hatua ndani ya muda mfupi ili mgao wa umeme ukome.

Mheshimiwa Spika, bei ya umeme bado ni kubwa kwa Watanzania wa kipato cha chini kuweza kumudu. Hata hivyo, bado kuna urasimu mkubwa wa utoaji huduma za umeme kwa wateja. Bado kuna upungufu wa vifaa muhimu hasa hapa Dodoma, kwa mfano, Mita za Luku na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta ya taa, *diesel/na petrol*. Bei ya nishati hii ni ya juu sana. Hata kama bei ya mafuta katika soko la dunia imepanda, lakini Serikali katika kuitisha hotuba ya bajeti iliahidi kupunguza tozo mbalimbali zipatazo 21 ili kushusha bei ya mafuta. Inasikitisha kuwa hadi leo bei ya mafuta hazijashuka. Lakini cha kusikitisha zaidi ni kuwa bei ya mafuta ya taa ambayo ndio kimbilio la Watanzania wengi wa vijiji imepanda. Bei ya nishati ya mafuta ikipanda bidhaa na huduma nyingi zinapanda bei na hivyo kuyafanya maisha ya Mtanzania kuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, suala la uchakachuaji wa mafuta ni kubwa na linahatarisha sio tu kuikosesa mapato Serikali, lakini pia kuharibu *engine* za magari ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina budi kudhibiti uchakachuaji wa mafuta kwa hali yoyote.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ya Nishati na Madini itekeleze mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara ihakikishe bei ya *petrol* na diezeli inapunguzwa ili kutekeleza ahadi ya Serikali ya kupunguza bei ya bidhaa hizo kwa lengo la kupunguza hali ngumu ya maisha ya wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara ihakikishe azma ya Serikali za muda mrefu kuanza kwa mfumo wa uagizaji wa mafuta ya pamoja ili kupunguza gharama inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali itenye fedha za kutosha kwa Wakala wa Nishati Vijiji (REA) ili kuhamasisha, kuwezesha uendelezaji wa miradi ya nishati bora vijiji. Mwaka 2010/2011, zilipitishwa shilingi bilioni 58.9 lakini hadi Mei, 2011 zilitolewa shilingi bilioni 13.6.

Mheshimiwa Spika, nne, gharama za kusambaza na kuunganisha umeme majumbani kwa wananchi ni kubwa mno. Serikali iingilie kati ili wananchi wengi wa vijiji waweze kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali ielegeze dhamira yake ya kuidhamini TPDC ili iweze kupata mikopo itakayowezesha utekelezaji wa miradi yake, hasa mradi wa kusambaza gesi majumbani, kwenye magari na viwandani.

Mheshimiwa Spika, sita, Jedwali Namba tatu, miradi katika mpango kabambe wa kusambaza umeme wa gridi vijiji katika mikoa 16. Kwa upande wa Mkoa wa Kilimanjaro sioni usambazaji wa umeme kwa vijiji vya Jimbo la Vunjo.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingi vya Jimbo la Vunjo havijafikiwa na umeme huo na ningependa Waziri wa Nishati na Madini atoe maelezo, atatusaidiaje?

MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme Vijiji Jimbo la Igalula kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 30/9/2010 Ilolansimba, Wilaya ya Uyui. Kwa niaba ya wanajimbo la Igalula nakumbushia utekekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete aliyoitao Ilolansimba Uyui, tarehe 30/09/2010 kuwa vijiji vifuatavyo vitapata umeme awamu hii kutoka Tabora Manispaa kuititia Ndevelwa mpaka vijiji vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, (1) Goweko, (2) Imalakaseko (3) Igalula (4) Kigwa – A, (5) Kigwa – B.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi Mheshimiwa Waziri Ngeleja ulivitaja pia katika majibu yako Bungeni katika Bunge la tisa mwezi Juni au Julai, 2010. Nakushukuru kwa kumbukumbu nzuri, wana Igalula wanaamini mwaka huu umeme unakuja Jimboni Igalula.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, nimelalamika muda mrefu, miaka mingi kuhusu Tarafa ya Ndagalu, Jimbo la Magu kutokuwa na umeme hata bulbu moja, miaka 50 baada ya uhuru. Naomba nipatiwe majibu ya uhakika kwamba mwaka ujao wa fedha mradi wa umeme wa Talbo-Nyashana-Maligisu-Kabila Centre utatekelezwa. Mimi na Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, tumeleta suala hili hapa Bungeni, tumekuwa tukipewa matumaini bila utekelezaji. Iliyobaki sasa ni kuomba huruma yenu ili wananchi wa Tarafa hii nao waone mwanga wa uhuru.

Mheshimiwa Spika, nataka kupata majibu iwapo lalamiko langu nililoliwasilisha kwa Mkurugenzi Mkuu TANESCO Bwana Mhando, kuhusiana na uhamishwaji wa nguzo za umeme zilizosimikwa ndani ya kiwanja changu huko Gongo la Mboto bila ridhaa yangu. Iwapo halijatekelezwa niandae utaratibu wa kuenda Mahakamani maana limekuwa suala la muda mrefu sasa. Nimekuwa nkipewa ahadi kila mara pasipo utekelezaji. Nimekwenda Ofisini kwa Bwana Mhando mara nyingi bila utekelezaji. Napenda nipate majibu kabla ya Jumatatu ili niamue kama nisimame kwenye vifungu siku ya Jumatatu tarehe 18/07/2011 au la.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ina taarifa ya uwepo wa wawekezaji wa nje uchwara, matapeli wanaodhulumu Watanzania, na kuwatolea matusi, wanakiuka sheria na taratibu za nchi kuhusiana na uchimbaji, uuzaaji wa madini, hasa dhahabu ikiwemo eneo la Nyarugusu? Inasemekana wageni hawa wanajivunia kulindwa kwao na vigogo wa Wizara. Nina ushahidi na nimeshazungumza na Kamishna wa Madini lakini utekelezaji bado. Naandika hili kwa taarifa (sitaki majibu) lakini najipanga namna gani nitachukua hatua za Kibunge kushughulika upuuzi huu ambao hauwezi kuvumiiliwa. Miaka 50 baada ya uhuru wa Watanzania kunyanyaswa na kutukanwa matusi ya nguoni na Mzungu kibaka au tapeli.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini naomba kero zangu *paragraph* ya pili na tatu, nipatiwe majibu.

MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nianze kutoa mchango wangu katika Wizara ya Nishati na Madini, kwa kuiomba Wizara itoe maelezo juu ya kuwa na bajeti finyu ya Wizara wakati kuna matatizo makubwa katika *sector* hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa wakati huu, ni lazima Wizara iwe na mipango ya dharura ya kupata nishati ya umeme ambayo itawasaidia wananchi wa Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naomba Wizara iliangalie kwa kina ni kusukuma mipango ya kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vlijijini (REA).

Mheshimiwa Spika, maendeleo yoyote yale hayawezi kupatikana bila kupeleka nishati ya umeme vijijini kwani wananchi wengi wanaishi vijijini ambako ndiko kuna shughuli za kiuchumi na hasa za kilimo. Wananchi hawa wakiwezesha watakuwa na uwezo mkubwa wa kusindika mazao yao kama matunda, mboga mboga na kuongeza thamani ya mazao kama vile mahindi kwa kuyasaga unga kwenye viwanda vya kusindika mazao hayo. Pia kukiwa na umeme wakulima wanaozalisha zao la mpunga wangeweza kusindika au kutumia mitambo ya kisasa itakayoendeshwa kwa nishati ya umeme hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Wizara itupatie umeme vijijini hasa katika Jimbo la Mpanda Vlijijini katika maeneo ya vijiji vifuatavyo:

Kwanza, Kabungu, Mchaka Mchaka, Ifukutwa na Kijiji cha Majalila. Vlijiji hivi ni rahisi sana kupeleka umeme katika maeneo haya kwani umeme kutoka Kijiji cha Milala kwenda Kabungu shule ya sekondari ni rahisi na karibu sana.

Pili, Mradi wa kupeleka umeme katika maeneo ya Tarafa ya Karema utawasaidia sana wananchi wa eneo la Ziwa Tanganyika ambao wengi wao wanajishughulisha na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, eneo hili likipewa au kushughulikiwa ipasavyo tutaongeza pato la wananchi na pato la Taifa kwani katika eneo hili kuna wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwa kutaka kujenga Kiwanda cha Kusindika Minofu ya Samaki katika Ziwa Tanganyika katika eneo la Ikola.

Mheshimiwa Spika, mbali na vyanzo vingine vya umeme, Mpanda kuna maeneo yanayoweza kutoa nishati ya umeme katika Mto Mnyamansi na Mto Lugonesi katika Tarafa ya Mwese maeneo haya yakifanyiwa utafiti, kuna uwezekano mkubwa wa kupata nishati ya umeme ambao unaweza kusaidia katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Shirika la *TANESCO* liache urasimu usiokuwa na manufaa hasa pale wanapofanya uzembe wa kupeleka nguzo za umeme kwa wateja kwa wakati muafaka kwa kutaka kitu kidogo kwa wateja. Tabia hii sio nzuri kwa shirika hili.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni uzembe wa kuwaachia wateja *kuijingizia* umeme bila kuilipia tatizo hili ni kubwa sana hasa kwa wateja wakubwa ambao hawalipi umeme kwa stahili yake.

Mheshimiwa Spika, endapo mawazo yangu yatakekekezwa, nitaunga mkono hoja.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii nami kuchangia bajeti hii ya Wizara na Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuzungumzia upatikanaji wa nishati ya umeme yenye uhakika. Hivi sasa kumekuwa na mgao wa umeme, ambao umechukua muda mrefu sana. Limekuwa ni janga la Kitaifa ambalo limepelekeea athari mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Ningependa kupata tamko la Serikali ambalo litalezeza ni hatua gani za haraka na za sahihi, zitachukuliwa ili kukabiliana na tatizo hili kubwa la mgao wa umeme linalolikabili Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia Serikali ikatafuta au ikatumia vyanzo vingine mbadala kama vile gesi asilia, upopo na makaa ya mawe ili vyanzo hivi viweze kuzalisha megawati zisizopungua 445 wakati hivi sasa kiasi kinachopatikana ni megawati 290 tu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, umeme unaozalishwa wa asilimia 67 tu katika *Grid* ya Taifa, ya mahitaji yote. Hali hii haikubaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia haina budi kuchukua hatua za makusudi na kuchukua mikopo ya muda mrefu ambayo ina riba nafuu, itakayosaidia kuwekeza katika sekta hii hususan, majenereta makubwa, pamoja na kuharakisha utekelezaji wa mradi wa *Stigler's Gorge*.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa na ushahidi mbalimbali unaodhihirisha na kuthibitisha jinsi watu mbalimbali wanavyofaidika na mkataba wa *IPTL* na *Dowans*. Inaeleweka pia, jinsi maafisa waandamizi wa *RITA* na wakubwa wengine wanavyonufaika. Ni sababu gani zinazopelekeea *RITA* kuendelea kuwa mfilisi wa *PLT*? Mchakato wa ufilisi wa *IPTL* utakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, je, endapo kampuni hii itafilisiwa rasmi, nini hatma ya mkataba baina ya *IPTL* na Serikali (*TANESCO*)? Je, Mkataba ulieleza nini au hatua gani itachukuliwa katika utekelezaji wa Mkataba endapo, *IPTL* itafilisika? Hapa kuna lindi la rushwa na ujisadi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ametujalia neema kubwa ya vyanzo vingi vya kupata umeme, kama gesi, makaa ya mawe, upopo na mvua, sasa kwa nini kusiwe na mpango wa dharura ili kuzalisha umeme? Tatizo hili limedumu kwa muda mrefu na sasa limekuwa janga la Kitaifa. Wananchi wanapata adha kubwa, athari kwa uchumi. Bei za

bidhaa zimepanda, matatizo chungu nzima yamewakumba wananchi. Tatizo la umeme litatuliwe.

Mheshimiwa Spika, uchakachuaji wa mafuta bado ni tatizo, nasema hayo kwa kuwa yamenikuta wiki tatu zilizopita, niliweka mafuta yaliyochanganywa na maji na ilikuwa njia ya Tanga, bahati mbaya sina uhakika ni kituo kipi kwa kuwa niliweka vituo tofauti tofauti. Adhabu kali zitolewe kwa wote wanaojihusisha na uchakachuaji wa mafuta ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni na iwe *issue* ambayo ni *serious*, anayekamatwa aadhibiwe. Naomba watangazwe hadharani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, naomba kujua mradi wa upelekaji umeme Mgeta, mpango wa Serikali kukamilisha mradi huu upo vile vile utakamilika Novemba 2012? Je, malipo ya fidia yamekamilika?

Mheshimiwa Spika, naomba pia kujua Serikali ina mpango gani kupeleka umeme Kata za Doma, Melela, Kaga, Kibati na Pemba? Kata za Doma na Pemba ni Kata zilizopo barabarani na ni kilomita 36, toka ulipo umeme, miji inakuwa vituo vy aya na zitaboresha vivutio, mbuga za wanyama Mikumi. Kata ya Kaga ina vijiji vitano, ndipo barabara kuu ya Magole-Turiani- Mziha, Kata za Pemba na Kibati umeme unaweza kupelekwa Kutokea Handeni na Kilindi.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ya Vijiji vy a Kidudwe, Kisala, Kunke, Makuyu na Mgudeni. Tatizo la kupatiwa umeme vijiji hivi inaelezwa ni transforma, wakati mwingine ni nguzo zisizopungua 10 au 15. Naomba sana vijiji hivi viingizwe katika mpango wa kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo ya hoja nilizoviwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara na *REA* kwa hatua nzuri ilizochukua za kuanza kusambaza umeme kutoka Itigi kwenda Kata ya Kitasaka (Dorato), Kata ya Mgandu na Kata ya Mitundu, kwa hatua hiyo, vijiji vifuatavyo vitanufaika na mradi huu muhimu wa nishati: Mlonghojii, Doroto, Lulanga, Itagata, Kayui, Mtakuja, Makale, Mitundu na vitongoji vy Uswesamoni Mwamatiga na Ipalalyu.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yote yana uchumi mkubwa kutokana na kilimo cha tumbaku, kurina asali, nta, mbao na ufugaji na sasa kilimo cha alizeti na maharage aina ya soya. Kupatikana kwa nishati ya umeme kutawainua wananchi wa maeneo haya zaidi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru kipekee Mheshimiwa Waziri na pia Naibu Waziri na Mkurugenzi wa *REA* kwa kunisaidia sana Mbunge na kuona mradi huu unaanza.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa, mkakati uanze wa kuendeleza mradi huu kutoka Mitundu kwenda vijiji vy Kalangali, Kata ya Mitunda; Kijumbo na Kivumbi, Wilaya ya Sikonge; Mwamagemebe, Kata mpya ya Mwamagemebe, Wilaya ya Manyoni; Kintanula, Kata mpya ya Mwamagemebe, Wilaya ya Manyoni) na Rungwa, Kata ya Rungwa.

Mheshimiwa Spika, mikakati ianze sasa kwa sababu ni mstari mmoja wa eneo kuishia Mitundu pekee hakutoshi. Nitaomba kupata ufanuzi au maelezo ya ziada wakati wa majumuisho kama kuna mipango yoyote au mikakati yoyote inayoandaliwa hivi sasa kuelekeza nguvu ya usambazaji umeme katika maeneo hayo mapya.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. JAJI FREDERICK M. WEREMA: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya kuwasilisha makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2011/2012. Hata hivyo, maoni yangu na ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ufuaji wa umeme usitegemee sana matumizi ya maji. Ama ni vema kuanza miradi ya malambo ya kuhifadhi maji illi wakati wa mvua, maji haya yahifadhiwe badala ya kufunguliwa maji kwenye mabwawa ya ufuaji umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna hatari hivi sasa ya mabwawa ya ufuaji umeme kukauka, naunga mkono kwamba, sheria na kanuni zilizotungwa kutekeleza sheria ya manunuzi ya umma zibadilishwe ili kuruhusu mitambo iliyotumika kununuliwa. Masharti yawekwe kwamba mitambo hiyo iwe *certified* na kwamba utaratibu wa kuitisha ununuzi huo wakati wote uwekewe masharti magumu kuzuia matumizi mabaya ya ruhusa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inahitaji kuhakikisha kwamba wawekezaji katika sekta ya nishati hawawezi *cartels* ambazo zinaathiri maslahi ya umma. Kwa mfano, Wizara inahitaji kuhakikisha kwamba taasisi zinazohusika kwa mfano, *TPDC, EWURA, TANESCO* na Wizara zinabadilishana taarifa muhimu badala ya kutegemea *Songas* au kampuni ya *Pan African*.

Mheshimiwa Spika, Wizara isimamie upatikanaji wa wataalam Watanzania kwa kuhakikisha kwamba tunawaandaa wataalam katika sekta ya nishati na madini. Taasisi za *TPDC, TANESCO* waanzishe Mfuko kwa ajili hiyo. Maeneo haya ni maeneo mtambuka ambayo yanahitaji elimu ya uchumi, sheria, kodi, ufundi (*engineering*), ni vema wataalam hao waandaliwe kwa kuzingatia maeneo hayo,

Mheshimiwa Spika, Mikataba ya madini inaleta hisia kwamba Serikali haikuwa makini wakati wa kuandika mikataba hiyo. Nashauri kwamba, suala hili sasa lishughulikiwe kwa kuititia mikataba hiyo ili kama itaonekana kama haina maslahi kwa umma basi ihuishwe na kuanza mazungumzo na wawekezaji bila kutumia nguvu ya dola. Ili kufanya hivyo, iundwe Kamati ndani ya Serikali kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa madini na vifo. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kwamba, kila panapopatikana au kugunduliu kwa madini kunakuwa na *rush* ya watu kwenda maeneo hayo kwa wale tunaowaita wachimbaji wadogo wadogo. Nashauri kwamba eneo hili lisimamiwe vizuri kwani ni chanzo cha magendo ya madini na kuvushwa kwa madini hayo kwenda nchi jirani. Madini hayo ni dhahabu na *Tanzanite*. Moja ya nchi jirani ingawa haina mgodi wowote wa dhahabu au *tanzanite* inaongoza katika kuuza madini hayo nchi za nje. Madini ni rasilimali ya Taifa. Taifa linapaswa kusimamia na kuzuia nchi nzima kuzungukwa na wachimbaji wadogo wadogo ambaeo matokeo ya uchimbaji wake huonekana.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, viongozi wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Nilidhani kwamba kutakuwa na msukumo wa kusambaza umeme katika Wilaya ya Musoma Vijiji kutokana na chanzo cha Mgodi wa Nyamongo. Nashauri kwamba Vijiji vya Magatini (Serengeti), Wegero, Kongoto, Buswahili, Kiagata, Masurura na Ryamisanga vihusishwe katika mradi huo ili kusaidia kusukuma maji katika maeneo hayo, matumizi ya umeme katika viwanda vya maziwa na katika shule zote katika maeneo hayo. Upatikanaji wa umeme katika maeneo hayo utafungua fursa za maendeleo kama vile usindikaji wa maziwa na nyama ya ng'ombe na mbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, naunga mkono hoja.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usumbufo mkubwa wanaopata wateja wanaohitaji mita za Luku, urasimu ni mkubwa na ni vema nipate ufanuzi wa:-

Kwanza, bei halisi mita ya Luku. Kwa kubadilisha toka mita za kawaida na mita ya Luku kwa nyumba mpya iliyojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya gharama ya umeme kwa wateja ni kubwa, ni vema Serikali ikaliangalia upya tatizo hili la nishati hii muhimu ambayo kupanda kwake kunakwenda sambamba na kupanda gharama za maisha ya Mtanzania, hali iliyochangia kukua kwa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgao wa umeme umeathiri sana uzalishaji viwandani na wajasiriamali wadogo wadogo ambao tegemeo lao la kujikwamua kiuchumi linaendelea kufifia. Nchi iko katika jinamizi la giza katika nchi huku Serikali ikiendelea na mikakati na michakato ambayo hadi sasa hakuna ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kuchakachua mafuta bado halijapatiwa ufumbuzi wa kukomesha tatizo hilo hali ambayo inapelekea kuharibika kwa magari na kuingiza hasara kwa wenyewe mali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikubali umeme unaitikisa nchi, kiuchumi, kisiasa na kijamii, naomba Serikali itoe maelezo, ina mkakati gani wa dhamira wa kuondokana na mgao wa umeme usio na ratiba?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kufufua umeme ya gesi asilia ya Kinyerezi (megawati 240 Gesi asilia) Somanga Fungu (megawati 2490 Gesi asilia) Mnazi Bay (megawati 300 Gesi asilia) Kiwira (megawati 200 Makaa ya Mawe), bado hayajaonekana kuwa kuna dhamira ya kweli ya kupatikana haraka kwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Julai, 2010 Serikali ilitoa kauli Bungeni kuhusu utekelezaji wa miradi mipy ya kupeleka umeme vijijiini, kuitia Wakala wa Nishati Vijijiini (*REA*) kuitia *Millenium Challenge Cooperation (MCC)* katika Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga kwa Vijiji vya Msaza, Magamba lakini hadi leo hakuna umeme na Serikali iliahidi ndani ya miezi 12 kazi itakamilika lakini ni tofauti kabisa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Kijiji cha Nzeri, Kata ya Misima, ambapo kuna ranchi ya ng'ombe, ambapo huduma hiyo ikafika watasindika maziwa na kuongeza kipato katika dhana nzima ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SAID MUSSA ZUBEIR: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uzima.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu kwa kutambua kuwa suala la umeme ni janga la Taifa na kutoa maelekezo mazuri ya jinsi ya kulikabili.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waziri na Naibu wake kwa jitihada zao kubwa za kutaka kuepukana na tatizo hili, kufuatana na ukubwa wa tatizo, Serikali inatakiwa iwe na mipango madhubuti ya dharura na itoe kipaumbele kwenye sekta hii ambayo ni uti wa mgongo kwa ukuaji wa uchumi na sio kama walivyofanya kwenye bajeti hii kwa kuwa Watanzania wanachotaka kuona ni umeme tu, basi kuwa haja ya kupigana kwa hali yoyote ile ili umeme upatikane.

Mheshimiwa Spika, vile vile tuharakishe upatikanaji wa gesi asilia pamoja na miradi ya Liganga na Mchuchuma ili tuweze kuzalisha umeme wa kutosha kwa siku za baadaye ili tatizo hili liwe historia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la madini, ukweli inasikitisha sana kuona madini yanamalizwa na nchi ingali katika umaskini mkubwa nahisi imefikia wakati sasa wa kusitisha uwekezaji huu ili tujipange upya kwa maslahi ya Watanzania ikibidi hata kama tuache kama hatuna utaalam wa kutosha ili vizazi vyetu vije kurithi wakati huo pengine wao watakuwa na utaalam na kuchimba madini hayo kwa maslahi ya nchi yao na kujiondoa katika umaskini huu kinyume chake tutamaliza rasilimali za nchi na kuacha mashimo ya kufugia nyoka tu.

Mheshimiwa Spika, bado hatujachelewa sana tuna nafasi ya kuipitia mikataba na kufanyiwa marekebisho au kuivunja kabisa, huu si wakati wa kuendelea kukaa na kutazama jinsi watu wanavyopora rasilimali tulizonazo na kutuachia umaskini kwa kisingizio cha uwekezaji na

uhisani. Naiomba sana Serikali itafakari hili na kulifanyia kazi kwa umakini mkubwa na hakika kwa ujasiri wa Serikali yetu na umahiri ilionao tutafanikiwa na kujkwamua kiuchumi kwa kutumia rasilimali zetu tulizonazo na sio kwa kutegemea wahisani.

MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Malima kwa umahiri wao wa kuliongoza Wizara hii yenye wadau wengi lakini wanakabiliana na changamoto zote kwa kufanya kazi usiku na mchana. Hongereni sana na msikate tamaa "mchumia juani hulia kivulini". Iko siku mambo yatawanyookea na nchi yetu itakuwa nuruni *full time!*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na madini ambayo, kamwe tusingekuwa mionganoni mwa nchi maskini sana duniani. Huenda tumechelewa kwa kuwa sehemu kubwa ya madini yetu yametumika vibaya kutokana na mikataba mibovu ya awali. Naiomba Serikali isafishe, kwa namna yoyote ile, hata kwa maamuzi magumu, ubadhirifu wa aina yoyote kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipunguze (*i-subsidize*) gharama za kuunganisha umeme ili wananchi wa vijiji waweze kumudu gharama hizo.

Mheshimiwa Spika, ujasiriamali unaohamasishwa nchini ili watu waondokane na umaskini, ni lazima uende sambamba na umaskini, ni lazima uende sambamba na uanzishwaji wa mabenki vijiji ili wajasiriamali hao waweke fedha zao benki. Bila umeme, kazi ya benki itakuwa ngumu. Naomba Serikali ione changamoto hili na kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu iwe inachukua kwa uzito unaostahili malalamiko ya muda mrefu ya wananchi, kama ilivyo kwenye sekta ya nishati na madini imeweka historia mbaya ya kupelekeea viongozi kujiuZulu, Tume mbalimbali kuundwa na kadhalika, lakini bado malalamiko yapo au yamezidi na ufumbuzi haupo au haujulikani. Tunaomba Serikali itoe tamko kuhusu tatizo hili lisilo na ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali ilipotoa amri ya kupandishwa kwa bei ya mafuta ya taa ili kudhibiti uchakachuaji, bei ya *petrol* na *diesel* zimebakia pale pale, au kupanda kwa maeneo mengine. Hii ni dhahiri hakuna *seriousness* katika maamuzi tunayofanya.

Mheshimiwa Spika, ifike mahali, kwa suala la umeme na madini ya nchi yetu, tuseme *enough is enough*, tutafute ufumbuzi ikibidi tuachilie mbali maeneo mengine ya kipaumbele, tujizatiti katika hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, natoa masikitiko yangu kuona hakuna hata kijiji kimoja cha Wilaya ya Babati Vijiini na Wilaya nzima ya Hanang.

Mheshimiwa Spika, Hapatatosha!! Kwa hili, siungi mkono hoja.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu wake kwa kuongoza Wizara inayolalamikiwa kila kukicha. Watanzania wamekata tamaa ya kuwa na umeme wakati wote na kutumia umeme kwa shughuli za uzalishaji. Watanzania wamechoka kusikia mipango mingi ya Wizara hii kuhusu utatuzi wa mgao wa umeme usio na utekelezaji au suluhisho la kudumu, tumechoshwa na mgao wa giza badala ya umeme. Uchumi wa nchi hauwezi kukua katika hali hii ya mgao wa umeme. Nilidhani baada ya sakata la *Richmond* Wizara ingepata fundisho na kujivekeea mikakati ya kudumu ili utokeapo ukame nchi isiingie kwenye giza tena nilitegemea *TANESCO* kuachana na mitambo ya kukodi ya *IPTL Symbioni, Agreko International* na kadhalika bali ingejiwekeea mikakati ya kuwa na mitambo yake ya dharura utokeapo shida ya umeme. Mitambo hii ya kukodi hubebesha Watanzania mzigo mkubwa wa kulipa *Capacity charges* na kadhalika ifike wakati Wizara ya Nishati na Madini ifikirie jinsi ya kununua mitambo ya kufua umeme.

Mheshimiwa Spika, kutohana na tabia nchi kubadilika na ukame kuwa mkubwa tuache kutegemea maji tu kuzalisha umeme na mitambo ya kuwanyonya Watanzania siyo suluhisho.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kufua umeme kwa makaa ya mawe ya Kiwira wa megawati 200 umesimama kutohana na Kampuni ya *Tan Power Resources* kushindwa kuutekeleza. *NSSF* waliomba Serikali kuwapa mradi huo kama walivyojieleza kwenye Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma mwezi Aprili, 2011. Ningependa kujua hatua iliyofikiwa kati ya Serikali na *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, tunayo makaa ya mawe Mchuchuma ambapo Kampuni ya Kichina ya *Sunchan H. Corp* wako tayari kuingia ubia na *NDC* na kuanza kufua umeme wa megawati takribani 600. Watanzania wanaoteseka kwa kukosa umeme waelezwe mradi huu utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha uliopita tulielezwa juu ya uzalishaji umeme kwa kutumia rasilimali ya upepo. Hatua iliyoelezwa na Wizara hairidhishi na siyo kwa mradi huu tu bali kwa miradi mingi iliyoelezwa kwenye hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya *biogas* hajatiliwa mkazo na Halmashauri zetu na hakuna jitihada zozote za Serikali kutoa elimu ya matumizi ya *biogas* kwa wananchi wake. Matumizi ya *biogas* ingewasaidia sana wananchi walioko vijijini katika suala zima la utunzaji mazingira na kutokusubiri umeme wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijawatendea haki Watanzania wanaotumia mafuta ya taa kwa matumizi mbalimbali kwa kupandisha bei ya mafuta ya taa maradufu. Kwani watumiaji wa mafuta ya taa ndio wachakachuaji? Serikali inawajua wachakachuaji bila ya kuwachukulia hatua za kuwafungia biashara zao. Serikali ipambane na wachakachuaji isiwaadhibu watumiaji. Kuwaadhibu watumiaji kwa kupandisha bei ya mafuta ya taa ni sawa na kuwaogopa wafanyabiashara wanaochakachua mafuta.

Mheshimiwa Spika, huduma ya kuunganisha umeme katika nyumba za wananchi ni ghali sana na wananchi wengi wanalamika Serikali iangalie namna ya kupunguza bei.

Mheshimiwa Spika, maendeleo katika Wilaya zenyenye migodi ziwe tofauti na Wilaya zingine kimaendeleo. Sioni sababu ya Wilaya ya Kahama kukosa barabara ya lami pale Mjini wakati, Mgodi wa Buzwagi uko pale pale mjini, hali kadhalika Wilaya ya Geita. Huku ni kuwanyanya wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua tahadhari ilichukuliwa kwa wananchi wa Bahi kuhusu uchimbaji wa Urani. Urani ni hatari kwa maisha ya watu itakapoanza kuchimbwa na wananchi waishio Bahi eneo la mgodi hawajui lolote kuhusu maisha yao kuwa hatarini, Urani itakapoanza kuchimbwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono bajeti, naomba kusisitiza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wa Kahama wapewe eneo na wawezeshwe.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Kahama ianze kulipwa 0.3% ya *Government turnover* ya Kampuni za uchimbaji (*ABG*) za Bulyanhulu na Buzwagi kama *Cess* kwa Halmashauri kama Sheria ya Madini ya 2010 inavyosema. Si haki kwa Halmashauri hii kulipwa \$ 200,000 pekee.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo eneo la Mwazimba (Jomu) wa Kagomlo wasiondolewe eneo hilo kwani Wizara inajua historia yao kuwepo hapo kwa kuzingatia barua zangu nyingi kwa Waziri kuhusu jambo hili. Muafaka unaofaa ni kuingia ubia na Mwekezaji mkubwa ambaye Wizara inamtaka.

Mheshimiwa Spika, naomba mradi wa umeme Bukombe (unaopitia Vijiji vya Illogi, Lungunya, Shilela, Ikinda na Segese Jimboni Msalala) utekelezwe mapema. Mheshimiwa Rais aliahidi mwezi Novemba, 2010, hadi sasa haujaanza!

Mheshimiwa Spika, naomba *REA* iongezewe bajeti ili iweze kugharamia miradi ya umeme vijiji ini ikiwemo miradi ya Jimbo la Msalala.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote haya kwanza, naunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati. katika jedwali namba moja. Manispaa ya Tabora haimo kabisa, sielewi kwa nini Tabora imesahauliwa. Ni aibu katika Manispaa ya Tabora Kata zifuatazo hazina umeme na hatujui tutapata lini. Naomba Waziri utakapokuwa unajibu hoja yangu, Kata zifuatazo nazo uzikumbuke.

Mheshimiwa Spika, Kata zisizo na umerme ni Mtalikwa, Ifuha, Uyui, Misha, Kabilia, Kakola, Ikomwa, Mdevelwa na Kalunde. Hizi ni Kata tisa, sio tatizo dogo umeme wa Tabora Manispaa kwa siku moja, tunatumia *units* kati ya 60,000 au 80,000/=. Hivi kweli hata sisi mnatuweka kwenye mgao sawa na Dar es Salaam au Arusha amba wanatumia *units* nydingi sana.

Mheshimiwa Spika, maana yangu hapa Tabora hatuna viwanda, kwa hiyo, mtapotuwaka katika mgao tunaonewa tu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya *TANESCO*. Magari wanayotumia yamechoka sana, naomba wapatiwe magari mengine kwani haya hasa yamechoka sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kambi ya Jeshi, Milambo. Nguzo zilizowekwa katika maeneo ya Jeshi ambako familia za wanajeshi, wanatifua ardhi kwa maana ya kulima hata pale nguzo zinapopita, matokeo yake mvua zikinyesha nguzo hizi zinaanguka na kusababisha adha kubwa ya umeme katika Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mwaka huu Manispaa yangu ya Tabora imesahauliwa sana, hata hivyo, naunga mkono hoja ya Waziri.

MHE. ABIA M. NYABAKARI: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini, Mtanzania anaamini kuwa chombo hiki kikisimamiwa vizuri ndicho kinawenza kuwa mkombozi pekee wa Mtanzania, kingeinua hali ya uchumi nchini, lakini kwa bahati mbaya hali mbaya inaendelea kuzorota kila siku.

Mheshimiwa Spika, Mtanzania wa kawaida amekata tamaa na Serikali yake ni hivyo kutokuwa na imani na Serikali yake kabisa.

Mheshimiwa Spika, licha ya kusemwa sana, Wizara hii kwa maovu yake, lakini pia Wizara hii ikae na kujisahihisha ione kwa undani chanzo cha uovu huu uko wapi, ngazi za juu, hasa watendaji wa Serikali au siasa na utendaji viko pamoja katika utekelezaji huu mbovu au usimamizi haufai?

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu ametupa neema tele, wasomi tele, lakini wasomi wengi wao wamekuwa kitanzi kwa Serikali na CCM yao na pia kwa wanyonge.

Mheshimiwa Spika, sikio la kufa halisikii dawa. Wahenga pia walisema Mnyonge Mnyongeni lakini haki yake mpeni. Utendaji uliopo haulingani na Wizara hii nono unaowenza kufanya watoto wake wafe njaa. Ni aibu kwa Wizara na Serikali yake kumpa Waziri taarifa za uongo kwa mfano, kusema Namanyere, Nkasi tayari nguzo zimeanza kuwekwa huku ndiko kujidhalilisha dhahiri kama utendaji wa Wizara hii ni dhaifu.

Mheshimiwa Spika, naomba aliyetoa taarifa hizi kwa Waziri ni dhahiri kabisa anastahili kupisha nafasi hii kwa sababu amefanya Waziri wa Nishati na Madini na Wizara yake kuonekana katika utendaji wake kuna hila.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka usemi huu utakaporekebishwa kweupe.

MHE. JUMA SURURU JUMA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri. Serikali ilichukulie hatua suala la ukosefu wa umeme nchini, ikiwa kwa njia ya dharura au wa muda mrefu kwa vyovyote vile, Serikali iipatie umeme nchi. Pia nashauri kama kuna mtendaji anafanya vitendo vya ubadhirifu dhidi ya huduma ya umeme nchini, basi asitazamwe usoni, awekwe upande, ili huduma ipatikane kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ahadi ya Serikali ya kuwalipa fidia wananchi wa Songosongo ni vema ahadi hiyo ikatekelezwa haraka sana kwani ahadi ni deni na ni vema Serikali ikatimiza wajibu wake hasa kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migodi, kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi kuhusu kunyimwa haki yao ya msingi ya kuitumia migodi ilio katika sehemu kwa kuchimbwa na wananchi wadogo wadogo. Serikali ilisimamie suala hilo kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke *special generator* katika sehemu muhimu kama hospitali, Ofisi za Serikali, Bunge, Mahakama, Vyuoni na kadhalika.

MHE. AMINA ABDULLA AMOUR: Mheshimiwa Spika, nitazungumzia suala la umeme, hali ya nchi ni mbaya sana, giza limetawala nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naungana na mtoa hoja ambaye amesema suala la umeme ni janga la Taifa na kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwa urefu tatizo la umeme, mambo mengi yanaharibika, wafanyabiashara wanashindwa kufanya biashara zao na maji pia huwa hayapatikani kwani maji huwa yanavutwa kwa *pump*.

Mheshimiwa Spika, hali ya umaskini inazidi katika nchi kutokana na ukosefu wa umeme, mazao ya mahindi ambayo ni zao ambalo linawasaidia maskini wengi lakini wanapotaka kusaga hayo mahindi na kuza unga inashindikana kutokana na ukosefu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, zamani katika mgao wa umeme huwa kwa masaa lakini siku hizi hata Jiji kubwa la Dar es Salaam linakosa umeme hadi siku mbili na juzi tu Jumapili iliyopita, umeme ulikosekana kwa muda wa siku mbili usikatike, hili nataka Mheshimiwa Waziri anipatie jawabu kwani wananchi wengi wana wasiwasi juu ya kukatika kwa umeme siku ya Jumapili.

Mheshimiwa Spika, tumechoka kusoma haya makaratasi yanayoeleza medawart KV na mambo ya ajabu ambayo sisi hatutaki kuyajua sisi tunataka umeme tena kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, ninacho kiona ni kwa Serikali ya CCM, imeshindwa kabisa kuleta umeme na namshauri kwa heshima na taadhima Waziri wa Nishati na Madini ajuzulu ili kulinda heshima yako na pia kukipa hadhi chama chako.

Mheshimiwa Spika, ni bora Mheshimiwa Waziri ukubali kuwa umeshindwa ili umpshe mwingine ashike nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho unasema tunataka mitambo mipyä, hatutaki mitambo ya umeme chakavu, tuko tayari tukae muda zaidi kusubiri umeme, tumeshasoma ya *Dowans*, hatutaki tena.

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, Sekta ya Nishati. Hali ya nishati ya umeme nchini inatisha sana. Kukosekana kwa nishati ya umeme kumefanya wananchi maisha yao yazidi kudidimia.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wakubwa, wadogo wadogo na wajasiriamali wengi wamesitisha miradi yao na mingine miradi yao mingi imekufa. Hivyo, hata kula yao na watoto sasa ni tabu.

Mheshimiwa Spika, ahadi nyingi zinazotolewa na Wizara hii na ambazo hazitekelezwi zinaashiria mipango na mikakati mibovu inayowekwa, aidha, kwa makusudi au kwa nia ya kuwaangusha viongozi wa juu.

Mheshimiwa Spika, inaelekea watendaji wakuu hawako *serious* na kazi zao na Serikali nayo hajatoa kipaumbele katika kuipatia fedha za kutosha Wizara hii kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ule mradi ambaao ungeliondoshea shida ya umeme (*Stigler's Gorge*) – ambaao ulibuniwa muda mrefu na kuelezwu ungetekelezwa umeishia wapi?) Lini utaanza?

Mheshimiwa Spika, Uganda imetumia Lake Victoria maji kwa ajili ya kupata umeme, kwa nini nasi Tanzania tusifanye hivyo kwa vile ziwa ni letu sote?

Mheshimiwa Spika, pili, gesi na mafuta. Kambi za utafutaji mafuta zimesikika kwa muda mrefu. Je, utafutaji huo hauna muda maalum? Je, ziko dalili ya kuweko na mafuta nchini Tanzania (na Zanzibar?)

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia toka Mnazi Bay na Songosongo hadi Dar es Salaam na Tanga ni habari njema, lakini ni kweli au mipango katika karatas?

Mheshimiwa Spika, ni kwa *TIPPER* isikabidhiwe wawekezaji binafsi waendeshe.

Mheshimiwa Spika, naiombea nchi yangu ipate gesi ya kutosha na mafuta ya kutosha ili adha hii tunayoipata wananchi iishe milele.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za Wizara katika kutafuta mafuta maeneo mbalimbali nchini lazima zipongezwe. Je, maeneo tunayopakana na Uganda ambayo wamepata mafuta, upande wa Tanzania hakuna? Ama hajatokea mwekezaji wa kutafuta mafuta?

Mheshimiwa Spika, je, tunasemaje umeme wa jua? Mola ametupa jua na siku 365 kwa mwaka mbona hatutoi *priority* angalau kwenye maeneo vijijini katika uzalishaji huo mdogo mdogo.

Mheshimiwa Spika, tatu, madini na vito, bado yanamsaidia mwekezaji zaidi kuliko nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini vitalu vya madini na tusifanye kwa makusudi kuwa nafasi wananchi wetu wamiliki na Serikali iwasaidie kupata wafadhili wawekezaji ili waingie ubia.

Mheshimiwa Spika, tatizo la madawa ya usafishaji madini yaliyoathiri wananchi na wachimbaji wadogo, ardhi, mimea na wanyama kule Nyamongo na maeneo mengine ya uchimbaji migodi hiyo ikafungwa kwa muda ili kutoa nafasi kwa wawekezaji wasafishe eneo na kurejesha mazingira katika hali yake ya awali.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo mengine ya migodi ambayo yana *airship* na ndege zinazotua na kuondoka *within a matter of few mining minutes* na hata ukipiga picha hazitoki, fanyeni uchunguzi.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Spika, je, Serikali kuititia Wizara ya Nishati na Madini inatambua kwamba Jimbo la Mpwapwa pamoja na lile Jimbo la Kibakwe, Majimbo haya kwa

pamoja yana utajiri mbalimbali wa madini ambayo yamegundulika na yanaendelea kugundulika siku hadi siku. Kufuatia ugunduzi huu ambao kwa kiasi kikubwa inatokana zaidi na juhudzi za wananchi wenyewe, wanaoendelea kugundua madini mbalimbali (yakiwemo madini ya aina ya copper, mica na kadhalika) bila ya msaada wowote wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, hali halisi inavyoendelea hivi sasa, wachimbaji wadogo wadogo wakiwemo na wawekezaji wengi wakiwemo raia kutoka mbali kama vile China wanaonekana katika maeneo mbalimbali, na kujihusisha na uchimbaji wa madini, kwa vibali wanavyopata kwa kusaidiwa na Wenyeviti wa Vijiji wa maeneo husika. Je, utaratibu huu ni sahihi. Kama siyo sahihi, Wizara itasaidiaje ili kuokoa rasilimali hii kubwa na inachukua hatua gani kudhibiti wachimbaji wadogo wadogo wanaoshirikiana, wawekezaji wanaojitokeza hivi sasa katika maeneo haya niliyoyataja (katika Majimbo ya Mpwapwa na Kibakwe (Winza).

Mheshimiwa Spika, nashauri, Wizara (kutumia wataalam wake) watembelee Majimbo haya kwa nia ya kujionea utajiri uliopo na udhibiti wake, ili Serikali na maeneo husika waweze kufaidika na rasilimali hii, hatimaye kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, REA uboreshaji na uenezaji wa umeme katika Vijiji vya Jimbo la Mpwapwa. *Mapping* ya maeneo ya umeme unaosambazwa na REA haijaenezwa kikamilifu katika maeneo au vijiji vyote katika Jimbo la Mpwapwa, hususan vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu ambayo yanahitaji umeme ambayo bado hayajaunganishwa, ni kama haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mazae. Zipo shule mbili za sekondari, moja ni shule ya wasichana ya Mazae, Bweni ambayo ujenzi wake umekaribia kumalizika na shule nydingine ni *Private Mazae* ya Wavulana, vile vile ipo zahanati au Kituo cha Afya kinachoitwa Mama Italia ambacho kimefikia hatua nzuri mwezi September, 2011 Kituo hiki kitafunguliwa si muda mrefu, je, ni lini yatapatiwa umeme maeneo haya na yaliyo jirani na kituo hiki cha afya zikiwemo shule mbili za sekondari.

Mheshimiwa Spika, nashauri wataalam wa REA pamoja na TANESCO, Wilaya ya Mpwapwa kwa pamoja waweze kuangalia uwezekano wa kuanganisha Kata ya Mazae, hususan maeneo niliyoyataja ili yaweze kuanganishwa ili umeme ufile na kusaidia kutoa huduma bora ya afya.

Mheshimiwa Spika, naomba Mratibu wa REA katika Jimbo la Mpwapwa asaidie utekelezaji wa maboresho haya.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na kutafakari hali halisi kwa kipindi cha miaka saba iliyopita 2005 – 2011 na kwa hali hiyo naona ni vema kuchangia kwa maandishi badala ya kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa utekelezaji wa miradi ifuatayo kumechangia nchi kuwepo gizani: Kwanza, Mradi wa Umeme Kiwira. Ulikuwepo mkakati mzuri wa wastani wa megawati 200 kutoka katika Umeme wa Kiwira. Utekelezaji umeingiliwa na ubia, ubinafsishaji na sera potofu na matokeo yake nchi imepoteza na wafanyakazi wanadai malipo yao toka Serikali Kuu. Nini kauli ya Serikali kutokana na kushindwa kwa mradi huo?

Mheshimiwa Spika, pili, *Stigler's Gorge* megawati 2000. Bonde la uwezeshaji wa gharama za mradi tazamio la matunda ya mradi huo ndio ulikuwa nguzo ya Taifa kwa mahitaji ya muda mrefu lakini hadi sasa haukuanza hata kutekelezwa. Nini kimekuwa kipingamizi cha kuanza utekelezaji. Je, siyo hila za kukwamisha nchi ili miradi ya ukodishaji iendelezwe? Wizara inasema nini kwa hili?

Mheshimiwa Spika, tatu, Mradi wa umeme toka gesi ya Mnazi Bay. Wawekezaji wa Mnazi Bay walipewa nguvu na matarajio makubwa ya kuzalisha na kusambaza umeme Mkoo ya Lindi na Mtwara hata kudiriki kuiondoa TANESCO katika mfumo wa usambazaji.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* imelaumiwa kwa kuchelewesha uwezekano na kupatikana fedha za mkopo kwa wawekezaji wa Mnazi Bay. Hata hivyo, matarajio ya kupata umeme wa gesi toka Mnazi Bay bado yamedumaa chini ya kiwango kilichotarajiwa Wizara inasema nini juu ya hilo.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kupata umeme kutoka katika mradi huo, ndio kunachangia kuendelea kununua umeme wa kukodisha kwa gharama kubwa kutoka *IPTL* MW 100 *Aggreko* megawati 50, *Ex-Dowans* megawati 90.

Mheshimiwa Spika, gharama kubwa za malipo kwa miradi ya *IPTL* na *Ex-Dowans*. Mikataba ya *IPTL* inataka *TANESCO* kulipia gharama za ku-service mitambo ya *IPTL* kwa kumtumia Wakala au Kampuni ya Kigeni. Mara nyingi spea mpya zimefungwa katika mashine hizo na kulipiwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya kuendesa mitambo ya *IPTL* yanalipwa na *TANESCO*. Mwanzioni walikuwa wanatumia *JCTA* na kwenda kwenye *GAPCO* kwa bei ya juu kuliko bei ya juu kuliko bei za mafuta ya aina hiyo kama yalivyokuwa yakiagizwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*). Kwa nini hili limekuwa linatokea na kuendelea chini ya Wizara ya Nishati na Madini iliyojua inasimamia pia *TPDC*?

Mheshimiwa Spika, gharama za kununua umeme wa *IPTL*. Pamoja na kulipia gharama za mafungu (a) na (b), bado bei licha ya kupatikana kwa mfumo wa tenda, ni kubwa na malipo kufanyika hata kama uzalishaji haukufanyika.

Mheshimiwa Spika, kutoridhiwa kuanzishwa kwa kampuni za *GASCO* na *KILAMCO*. Kampuni ya *GASCO* iliundwa kama kampuni tanzu ya *TPDC* ili kusimamia uuzaaji na usambazaji wa gesi toka *Songosongo* na *KILAMCO* kwa lengo la kusimamia uzalishaji wa mbolea kutokana na gesi ya Mnazi Bay.

Mheshimiwa Spika, Kampuni hizi mbili za Watanzania wazalendo zikaachwa na kufutwa na badala yake ikaletwa kampuni ya kigeni *Pan-African Energy*, ikasajiliwa Tanzania na kupewa kazi ambazo zingefanywa na *GASCO* chini ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Leo *Pan-African Energy* imehusishwa katika kutoilipa *TPDC* ipasavyo na inapeleka nje ya nchi fedha zake kwa malipo ya fedha za kigeni. Kiuchumi hii inaathiri uwiano kati ya gharama za mauzo nje ya nchi na manunuji kutoka nje ya nchi!

Mheshimiwa Spika, tangu gesi imeanza kuzalishwa Mnazi Bay, mradi wa mbolea kama *KILAMCO* iliyojua imeandaliwa haueleweki kama utaanza vipi na bila shaka kwa kuleta kampuni ya kigeni! Wizara inaeleza nini juu ya hili?

Mheshimiwa Spika, kushindwa kuanza kwa ujenzi wa bomba la mafuta toka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Dhamira ilikuwa nzuri kusafirisha mafuta kwa bomba kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Kampuni zilizokuwa na sifa za kutia hofu. *Richmond* na wengine walijitokeza kutaka kujenga mradi huo na wengine kujitokeza lakini hadi leo mradi huo umeshindikana na wenzetu wa Kenya kufanikisha ujenzi wa bomba kama hilo kutoka Mombasa hadi Nairobi hadi Kisumu na sasa Kampala Uganda.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *Richmond* ilitoa ushauri wa kununua mitambo ya kuzalisha umeme megawati 70 – 100. Je, Wizara ilifutilia Ankara zilizowasilishwa katika ripoti ya *Richmond* kuonesha kuwepo kwa mashine za aina ya zile za *IPTL*, *Dowans* na bei za wakati huo ili *TANESCO* iwezeshwe inunue na kumiliki mitambo ya kuweza kuzalisha umeme badala ya kuendelea kutegemea *IPTL Ex-Dowans*, *Aggreko*. Mitambo hiyo ilikuwa mipyga na sio iliyotumika.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuvuta umeme. Leo *TANESCO* kwa viwango vya *EWURA* inamtaka mwananchi kulipia gharama za nguzo, nyaya, (*labour*) pamoja na *Service Line Charges* ili kumwezesha kupata umeme. Hali ambayo inawezesha *TANESCO* kuweka mita na Luku na kuanza kutaka malipo kwa mteja bila kujali gharama alizolipia. Hii sio haki kwa utendaji. Je, Tanzania itaendelea hivyo mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, ushauri juu ya bei za mafuta. Ni jukumu la Mamlaka *EWURA* kushauri Serikali juu ya bei za mafuta. Wizara ya Fedha ilipotoa tamko la kupunguza viwango vya kodi za mafuta na kuainisha kwamba bei za mafuta zitashuka *EWURA* ilitakiwa kushauri Serikali kwamba. Kiwango (*Ratio*) ya ongezeko au pungufu ya bei ya mafuta katika soko la dunia na kwa mtazamo wa kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania (kwa kuzingatia kuwa bei za mafuta zinajengwa kwa mfumo wa Dola) kwa kulinganishwa na petrol na mafuta ya taa, isingekuwa sahihi kutoa viwango vya bei katika ngazi ya reja reja kama ilivyotolewa na Wizara ya Fedha. Matokeo yake ni kuwa na bei za mafuta za juu, sasa zaidi ya zile zilizotolewa kauli na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ushauri upokelewe ili kuimarisha utendaji wa Wizara kwa mahitaji ya bajeti za baadaye.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, nichangie kwa kutambua umuhimu na unyeti wa Wizara hii. Ni kwa takriban miaka sita sasa imekuwa ni mazoweya ya Serikali kutoa kauli za matumaini kwa Watanzania kuwa tatizo la umeme litafikia mwisho hivi karibuni. Semi hizo ni za kuona Watanzania hawana uwezo wa kuiwajibisha Serikali kutokana na Serikali kutumia nguvu ya dola (Polisi) mara wananchi wanapopeleka ujumbe kwa Serikali kwa njia ya maandamano. Huu si utawala bora hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa umeme mjini na vijijini, kunapelekea Watanzania wengi wa kipato cha chini na kati kuwa na maisha magumu kwa kukosa ajira na waliojajiri (wajasiriamali).

Mheshimiwa Spika, Watanzania wamechoka kusikia. Upatikanaji wa umeme kama hadithi za Alfu Lelaulela. Serikali lazima itoe ahadi zenyehu uhakika na si za kubahatisha, tumechoka. Tunawaheshimu, mwisho uvumilivu utakwisha, ni bora kama Serikali haina majibu ya uhakika ikubali kuwajibika. Huo ndio ukweli wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nchi kukosa umeme ni aibu ya Serikali na Taifa letu. Nashauri Wizara iwe na vyanzo vikubwa visivyozidi vitatu au viwili na iwekeze huko kwa umeme wa uhakika na si kutawanya nguvu kwenye miradi mingei.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini. Nchi yetu imejaaliwa kuwa na madini ya aina nyingi, lakini madini hayo hayajamfaidisha Mtanzania badala yake yamekuwa ndiyo chanzo cha unyanyasaji, mauaji kwa wananchi. Hivyo, Serikali ichukue hatua za haraka kuleta sheria Bungeni za kunufaisha nchi badala ya wageni.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, naomba kwenye tatizo la umeme *focus should be on a few viable large projects which will provide base load supply that is 24/7.*

Mheshimiwa Spika, *Stigler's Gorge* inahitaji six years down the line kama mradi utanza leo. Pia kuna issue ya hydrology risk.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji sana kwa diversify more to gas and coal. Badala ya kuwa na miradi midogo mitatu Kiwira wa megawati 200, Ngaka wa megawati 400 na Mchuchuma wa megawati 600, investors should bid for 1000 Megawatt and the one with lowest tariff and appropriate technology for emissions compliance, should come on stream first (the current project scale is too small in considering economies of scale to achieve lower unit costs of electricity).

Mheshimiwa Spika, the Mtwara Project should be up scaled from 300 megawatt to 1000 megawatt to achieve economies of scale. Tubadilishe technology kutoka kwenye open cycle to combined cycle gas turbine ili kupata higher power generation efficiencies, kwa hiyo ni miradi miwili tu.

Mheshimiwa Spika, *Gas 100 megawatt na coal 1000 megawatt* hii ndio njia pekee tu ya kutatua tatizo la umeme nchini na tutapunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, *TANESCO* watoe maelezo ya kina kwa nini wanamtumia *REX Attorney* na wamempa kesi ngapi? Ameshinda ngapi na amelipwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *crisis* ya *gas*. Kwa nini tusichukue maamuzi magumu ya kuvunja mikataba yote ya *gas* hao *Pan-Africa* na *Songas* ili kazi hii ifanywe na *TPDC* peke yake, so that the country will benefit from this resource.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini imeipa Kampuni ya *Shanta Mining Co. Ltd.* leseni ya utafutaji madini ya dhahabu katika eneo la Sambaru, Kata ya Mang'onyi katika Jimbo la Singida Mashariki. Eneo la leseni ya *Shanta Mining* limekuwa litumiwa kwa miaka mingi, wachimbaji wadogo wa dhahabu ambao wamejipatia wao na familia zao riziki na kuchangia katika uchumi wa eneo hilo la Singida Mashariki na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Serikali kutoa leseni kwa *Shanta Mining* ni kwamba wachimbaji wadogo wamefukuzwa na wanaendelea kufukuzwa katika maeneo ya Londoni, Sambaru, Taru na Kinyamberu hali ambayo imeongeza umaskini wa kipato hasa hasa kwa mwaka huu ambako kuna upungufu mkubwa wa chakula katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Singida Mashariki na Wilaya ya Singida Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa vile leseni ya utafutaji madini ya *Santa Mining* inatarajiwa kwisha muda wake tarehe 29 Oktoba, 2011 namwomba Waziri wa Nishati na Madini atoe kauli rasmi kwamba baada ya muda wa leseni ya *Shanta Mining* kwisha tarehe iliyotajwa, Kampuni hiyo itaamriwa kuachia eneo hilo ili kuwawezesha wachimbaji wadogo wa dhahabu wa Kitanzania waendelee na shughuli za uchimbaji hasa hasa katika kipindi cha njaa.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa dhahabu unaofanywa na Makampuni makubwa ya kigeni umesababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira katika maeneo ya migodi ya dhahabu ya *North Mara Wilayani Tarime, Geita, Tulawaka and Golden Pride Wilayani Nzega*. Pamoja na mambo mengine, Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kama ilivyokuwa kwa sheria ya madini ya mwaka 1998, inayolazimu Makampuni yanayochimba madini kuweka dhamana ya urekebishaji mazingira (*rehabilitation land*) kwa ajili ya kulipia gharama ya kusafisha mazingira yaliyochafuliwa na shughuli za uchimbaji madini. Namuomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kulieleza Bunge ni fedha kiasi gani zimetolewa na Makampuni gani yamelipa fedha hizo za dhamana ya urekebishaji wa mazingira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inawalazimu wachafuzi wa mazingira kulipa fidia kwa uchafuzi wa mazingira na kwa waathirika wa uchafuzi huo. Waziri atoe kauli ya Serikali ni makampuni yapi ya madini ambayo yamelipishwa fidia ya uchafuzi wa mazingira katika maeneo yanayozunguka migodi.

MHE. SAID SULEIMAN SAID: Mheshimiwa Spika, kuhusu utafutaji na upatikanaji wa mafuta katika Kiswa cha Pemba, ninavyofahamu kuwa jithlada za kutafuta mafuta ulianza zaidi ya miaka 60 iliyopita na visima vinne vilichimbwa. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuvuja kwa mafuta yanayotoka katika kisima kimojawapo kilichopo katika ufukwe wa Tundauwa? Nihavyofahamu mafuta yaliopo si ya Muungano lakini baadaye yalifanywa ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Samuel Sitta aliviyoliezea Bunge lako Tukufu hivi karibuni swali, je, huoni kuwa Mheshimiwa Sitta alilichanganya Bunge kwa sababu ugunduzi wa mafuta hasa Zanzibar ulifanywa kwenye miaka ya 1950 na Muungano ulizaliwa mwaka 1960?

Mheshimiwa Spika, kwa nini madini na gesi yasiwe mambo ya Muungano ikiwa yatapatikana katika ya bahari ya Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar kama Mheshimiwa Samuel Sitta aliviyoliezea Bunge sababu zinazopelekea mafuta kufanywa kama ni mionganini wa mambo ya Muungano, haoni uwezekano wa kupatikana madini na gesi katika bahari iliyopo bahari ya

Bara na Zanzibar upo au tena ni mkubwa. Swali, kwa nini madini na gesi yasifanywe kuwa ni mambo ya Muungano?

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENG: Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji umeme kwa njia ya maji kwa upande wa Nyanda za Juu Kusini ipo mito mikubwa inayoweza kuzalisha umeme kupitia maporomoko yake. Miti hii ni Rumakau uliopo Wilayani Makete na unapeleka maji yake Ziwa Nyasa na Ruhudji uliopo Wilayani Njombe, mito hii miwili ina maporomoko makubwa yanayoweza kuzalisha umeme mkubwa sana kama ifuatavyo:-

Rumakal	-	MW 222
Ruhudji	-	MW 350

Mheshimiwa Spika, sifa nyingine ya mito hii ni kwamba inapata mvua nyingi sana kila mwaka, mathalani Mto wa Rumakal unapata mvua miezi nane katika mwaka. Serikali imeonyesha wasiwasi wa kufua umeme kwa njia ya maji kutokana na ukame ambao umekuwa unaikumba nchi mara kwa mara. Ni vizuri ikaeleweka kwamba vyanzo vya maporomoko ya Mtera na Kihansi vipo katika maeneo ambayo yanakubwa na ukosefu wa mvua za kutosha. Napenda kufahamu ni kwa kiasi gani Serikali imejipanga ili kuona miradi ya Rumakal na Ruhudji inakamilishwa haraka sana, kwani ni miradi yenye maji ya kutosha kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Umeme Vijiji (REA). Napenda kuipongeza sana REA kwa kazi nzuri inayofanya ya kusambaza umeme vijiji. Napendekeza wakala wa umeme yaani REA waandae mpango/mkakati unaonesha namna watakavyosambaza umeme nchi nzima. Utaratibu uliopo sasa unaonesha Nyanda za Juu Kusini zina miradi kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Makete ina mito mingi yenye maporomoko madogo na makubwa. Napendekeza Serikali ifanye tathmini na ianzishe miradi hii midogo itakayowezesha wananchi/vijiji vingi kupata nishati ya umeme, mpango huu ukifanikiwa utasaidia wananchi wengi wa mikoa ya Iringa, Mbeya na Rukwa ambako kuna mito mingi kupata umeme na vilevile umeme uliobaki utaingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyopitiwa na nguzo za umeme Wilayani Makete vitapata lini umeme? Ningependa kujua mkakati wa TANESCO kuvipatia umeme vijiji vya Ujuni, Nkenja, Isapulano na Luvulunge vilivyopitiwa na nguzo za umeme unaokwenda mjini Makete. Wananchi wa vijiji hivi wanalinda nguzo za umeme muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na kuunga mkono hoja.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa taarifa kuwa nitaunga mkono hoja ya Waziri iwapo tu atajibu kwa ukamilifu hoja zangi zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Somanga Fungu ambacho kinazalisha MW 7.5. Kwa hivi sasa vijiji vitatu katika Jimbo la Kibiti vina umeme navyo ni Bungu, Kibiti na Mchukwi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vijiji hivyo kupata umeme, idadi ya watumiaji bado ni ndogo mno. Walilouanganishiwa umeme ni wale tu walio ndani ya mita 30 kutoka kwenye nguzo. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuwaunganishiwa umeme wananchi walio wengi ambao wapo nje ya mita 30 ukizingatia kuwa umeme upo mwingu na watumiaji ni wachache? Aidha, ni vizuri pia Serikali ikapunguza gharama za kuanganisha umeme kwa watumiaji kwani gharama ni kubwa mno kwa wananchi wetu ambao kwa kiasi kikubwa hawana uwezo wa kugharamia shilingi 500,000/= kwa nguzo moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kutaka kuongeza bomba lingine la gesi toka Somanga hadi Dar es Salaam, ni vizuri basi ahadi iliyotolewa na Serikali katika mpango wake wa *way leave electrification* ni kuwa vijiji vyote vinavyopitiwa na bomba la gesi ni lazima vipatiwe umeme, itekelezwe. Hivi sasa umeme huo umefika katika kijiji cha Bungu, lakini vijiji vya Upenda, Jaribu Mpakani na Mjawa hadi sasa havijapata umeme. Naishauri Serikali kabla ya

kutekeleza mpango wa pili wa kujenga bomba la gesi ni vizuri kutekeleza ahadi hiyo ya kuweka umeme katika vijiji vya Jaribu Mpakani, Mjawa na Uponda.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu upelekaji wa umeme katika Mji wa Nyamisati, mji huu una taasisi nyingi ikiwa ni pamoja na kiwanda cha kuhifadhi samaki, shule mbili kubwa za sekondari na kituo cha afya. Aidha, wakati umeme huo unapelekwa Nyamisati pia utasaidia sana kuwapatia umeme wananchi na taasisi mbalimbali za Serikali kama vile shule za sekondari za Mlanzi na Mahege pia zahanati na vituo vya afya katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nirudie kusema kuwa nitaunga mkono iwapo tu hoja ya kupatiwa umeme wananchi wa Jaribu Mpakani kuitia mpango wako wa *Way Leave Electrification* utatekelezwa.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi umeme limekuwa ni tazito kubwa ambalo linaathiri sana uchumi wa nchi yetu, viwanda vikubwa na viwanda vidogo vidogo vinashindwa kufanya kazi ya uzalishaji kwa muda uliopangwa katika shughuli za uzalishaji kutokana na kukatika kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mufindi Kusini kuna viwanda vikubwa kama vile *Uniliver Company*, Kiwanda cha Karatasi Mgololo, Kiwanda cha Chai Mufindi na viwanda vya mbao. Viwanda hivi vinategemewa sana katika uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, kukatika kwa umeme mara kwa mara kunaathiri sana uzalishaji katika viwanda.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mufindi Kusini wananchi wamejitahidi sana kujenga nyumba kwa kuezeka bati wakitegemea wanaweza kuingiza umeme. Jimbo sasa hivi kuna vijiji vichache sana ambavyo vina umeme ambavyo ni Nyololo, Igowole, Kasanga, Mtwango na Sawala tu, jimbo lina vijiji 77. Lakini vijiji ambavyo vina umeme sio zaidi ya vijiji kumi kati ya 77. Je, Serikali inafikiria nini au ina mkakati gani wa kupeleka umeme katika vijiji vya Mbalamaziwa, Malangali, Ihovanza, Maduma, Lwing'ulo, Idinda, Ikangamwani, Nyigo, Ihawaga, Ihomasa, Kihanga, Kitesangwa, Luhunga, Rugema, Makungu, Matanana, Bumilayinga na Uole.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mufindi Kusini ndilo linalozalisha nguzo za umeme katika nchi ya Tanzania. Sasa jambo la kushangaza Jimbo ambalo linazalisha nguzo za umeme halina umeme, wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini wanaomba sana Jimbo lipatiwe umeme kwa vijiji ambayo vimetajwa katika karatasi hii. Pia kuna zahanati nyingi hazina umeme, kuna kituo cha watoto yatima cha Nyololo hakina umeme, kuna sekondari hazina umeme. Naomba Serikali kwa Bajeti hii waweze kupeleka umeme katika sehemu zote muhimu katika Jimbo la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maeneo Rais aliahidi kama vile Kijiji cha Mbalamaziwa na Malangali, Rais aliahidi kuwa watapewa umeme, naomba Serikali itimize ahadi ya Rais wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, kuhusu Gridi ya Taifa, je, Serikali ina mpango wa kuunganisha Gridi ya Taifa na Mikoa ya Kusini Mtwara/Lindi kwani nishati pekee kwa sasa inayotajariwa kwa kuongeza nguvu hiyo kutoka katika gesi ya huko Kusini.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya miaka minne sasa *TANESCO* imesitisha uboreshaji wa mikoa ya Kusini ya Mtwara/Lindi katika huduma zake kwa sababu ya kufanya hivyo ni *TANESCO* kuwa katika mazungumzo na Kampuni ya *Umoja Light* ambayo ingetoa huduma hiyo badala ya *TANESCO*. Mazungumzo haya yamedumu miaka minne. Mazungumzo hayo yameishia wapi?

Mheshimiwa Spika, mikataba ya *TANESCO* na wateja wake kwa kiasi kikubwa haizingatii fidia inayotokana na kukatika umeme na unaporejeshwa umeme huo huharibu vifaa vya wateja kama redio, friji, televisheni na kadhalika. Nani ana wajibu wa kulipia gharama hizo inapotokea?

Mheshimiwa Spika, Tanzania inavyo vyanzo vingi vya nishati ya umeme katika nchi yetu. Kama makaa ya mawe, 44% ya nishati ya umeme duniani hutokana na makaa ya mawe Tanzania ni nchi ya kumi na moja duniani yenye mito miwili inayoweza kuzalisha nishati hiyo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina bahati ya kuwa na nishati ya gesi kutoka Kilwa/Mtwara kwa uwezo huo tuliokuwa nao *TANESCO* (Serikali) inakwama wapi katika kutoa tatizo hilo kubwa la umeme.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri kwa hotuba yenye ufanuzi wa kina kuhusu mipango ya Serikali katika kushughulikia sekta hii muhimu za nishati na madini. Lakini pia nimpe pole Mheshimiwa Waziri kwa changamoto nydingi zinazojiteza kuhusu sekta hizi. Mathalani, mahitaji ya umeme yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kutokana na hatua za maendeleo na uwekezaji unaofanyika nchini mwetu. Hatua hizi njema hazijaenda sambamba na upatikanaji wa nishati, husani ya umeme ambayo imeathiriwa sana na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo katika hali hio inabidi Serikali isimamie kwa haraka na uthabiti mazungunzo yanayoendelea ya mikataba pamoja na utekelezaji wa makandarasi wafanya kazi usiku na mchana.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimevutiwa na hatua zinazoendelea kutekelezwa na kusambaza umeme katika Jimbo langu la Busege. Hadi sasa nyaya zimetandazwa kati ya Lamadi na Mkula kuelekea Bariadi, *transfoma* imefungwa Mwanongi ili umeme usambazwe katika vijiji vya Mwandiga, Mamala, Badugu na Busami. Hata hivyo kwenye kitabu cha hotuba pia Waziri ameutaja mpango wa umeme vijiji kuanzia Nyashimo, Nyangili hadi Ngasamo. Kweli kwangu ni faraja kwani maeneo yaliyolengwa ni maeneo ya kibashara vikiwemo viwanda vya pamba, hospitali kubwa lakini pia kutekeleza ahadi ya Rais ambayo Mheshimiwa Waziri anaifahamu! Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nilikuwa nikiwaza binafsi kuhusu suala la Bajeti ndogo ya Wizara hii. Hivi kwa nini tusingie mkatiba wa kubadilishana madini yetu kwa kujengewa miundombinu ya nishati ili kero hii ikaisha mara moja badala ya kusubiri kukopa kwenye mabenki? Urasimu wa mikopo unatuchelewesha kumaliza tatizo hilli na hata kufanya wananchi wapoteze imani na Serikali yao. Nchi zingine zinatumia mafuta yao kujengewa miundombinu wanayoihitaji, mfano Angola, tuliflikirie hilo nasi.

Mheshimiwa Spika, kule Jimboni kwangu kuna wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu kwenye Mlima Ngasamo, sasa hivi hapo ni mahali muhimu pa kiuchumi, sambamba na Sera ya Madini ya mwaka 2010, hawa watu wanatakiwa kusaidiwa kuunda ushirika, wapewe elimu na kuwawezesha ili wafunaike na kazi hiyo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atuweke na sisi kwenye mpango wa kuwawezeshwa. Pia naomba hamasa itolewe hapo Ngasamo ili kuongeza ajira na biashara. Kuachia uchimbaji ukaendelea hivyo bila elimu utasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na bila kuwapatia manufaa ya kutosha. Naomba pia mgogoro wa leseni na viwanja utatuliwe kwa haraka na kwa haki kwani unawenza kusababisha uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Wizara itusaidie kuvutia wawekezaji wa kuchimba chokaa iliyopo kwa wingi katika Kata ya Shigala. Ningependa wawekezaji wanaojali mazingira na utu pia, ili Jimbo letu pamoja na Taifa viweze kufaidika na machimbo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme liliopo nchini ni pigo kubwa kwa uchumi wa nchi yetu. Ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa na viongozi wetu wa Wizara na Shirika la *TANESCO* na ambazo hazijatelezwa zimekuwa chachu ya hasira ya wananchi kukosa imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuishauri Serikali kutekeleza haraka mpango wake wa *Public/Private Partnership*. Matatizo yote ya umeme tunayoyapata sasa hivi yametokana na ukiritimba (*monopoly*) ya Shirika la Umeme (*TANESCO*).

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itangaze *tender* hizo na itoe vivutio (*incentives*) vizuri kama ilivyotoa kwa Makampuni ya Madini ule mwaka 1997 lakini wakati huu Serikali iwe makini na aina ya mikataba itakayoweka na wabia hawa.

Mheshimiwa Spika, vipo vyanzo vingi vya kupata nishati mfano ni *solar, bioges* na kadhalika. Nashauri Serikali ihamasithe (*ku-encourage*) wananchi wake kutumia umeme aina hii. Vifaa vya *solar* vimepunguzwa ushuru lakini pia kwa wale wenye mifugo watumie *biogas* na shule zitumie gesi ya *biolatrine*.

Mheshimiwa Spika, kwa namna hii wananchi watatumia umeme mwingine ambao hauko katika gridi na hivyo ku-serve ule umeme wa gridi ambao wananchi hawa wangeutumia.

Mheshimiwa Spika, ipo mito midogo midogo ambayo nako kunaweza kupatikana umeme. Tumeshuhudia *mission* nyingi maeneo ya Arusha, Iringa na Tanga.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia *REA* (Wakala wa Umeme Vijijini) ihamasithe wananchi au taasisi zenyenye ubunifu zitengeneze umeme kutoka mito hii na hivyo kutimiza azma ya kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, nchi kama Marekani wana madeni makubwa na bado Bunge lao wanajali kuongeza kiwango cha deni. Wataalam wa fedha (*Modgilla & Miller*) wanasema na nanukuu; "*Debit money is cheaper than equity*" (fedha ya mkopo ni nzuri kutumia kuliko fedha yako mwenyewe).

Mheshimiwa Spika, kwa suala nyeti kama umeme nashauri Serikali iwasiliane na Benki ya Dunia au *donors* wengine kuomba mkopo wa kutengeneza umeme wa kutoka nchini ili kuokoa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijitahidi sana kufanikisha uwepo wa umeme nchini kwani kutokuwa na umeme ni gharama kwa nchi kuliko kuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini iangaliwe upya jinsi ya kuwashirikisha *Local Government Authorities* hata kwa taarifa tu katika Kamati za Halmashauri na *Council Management team*.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ludewa Kata ya Mundindi na Nkomangombe kuna madini ya chuma/dhababu/*urenium* na kadhalika. Aidha, wananchi bado hawajaoneshwa mpaka ili kujua maeneo yenye madini yasiwekewe miradi endelevu mgano, josh/o/zahanati na kadhalika. Wananchi wameambiwa wanapaswa kuhama. Swali, ni lini wananchi wa Ludewa – Mundindi watalipwa fidia waliopo eneo la madini wanaopaswa kuhama? Eneo la kuhamia ni wapi na *plan* ya eneo bado hajafanyika, *who is responsible exactly* kwa ajili ya kuelekeza mandini ya Mundindi Ludewa? Je, ni lini Serikali italeta Afisa Madini wa Wilaya ya Ludewa? Wananchi wana maswali hakuna wa kujibu katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, eneo la Iwela kuna watu walienda kutafiti madini, je, kwa nini watafiti wa Madini Iwela, Ludewa wanatafiti bila mwakilishi wa Serikali kuwepo (Afisa Madini) na hivyo Serikali inajuaue mtafiti ana tafiti (*explore*) au anachimba na kuchukua (*extract*) madini kama hakuna mwakilishi wa Serikali?

Mheshimiwa Spika, je, vibali vya *PL* vya kutafiti madini kwa nini vinauzwa kutoka mmiliki mmoja kwenda mmiliki mwininge pasipo kuwashirikisha wadau wa maeneo husika ya Iwela Ludewa? Baada ya kupata majibu ya kuridhisha kuhusu Ludewa nitakuwa tayari kuunga mkono hoja.

Kwanza Ludewa iwepe Afisa Madini haraka, ushirikishwaji wa *Local Authorities* wakati wa kutafiti madini, Serikali inajua kuwa watafiti wanatafiti na sio kuchimba na kwa nini Serikali isifanye utafiti yenewe kwa *joint venture PPP* na Mashirika na kuacha 100% kampuni za nchi ambazo hutudanganya wanachimba na sio utafiti. *Answer all please.*

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini ningependa kujua mpaka sasa Serikali imechukua hatua gani kufanya *mapping* ili kujua kiwango cha madini katika maeneo mbalimbali nchini ili kuepuwa hasara ambazo tunaingia kutohana na kuruhusu makampuni kufanya tafiti yenewe hali inayoacha mashaka juu ya kiwango halisi cha madini tulioelezwa na mwekezaji. Lazima tuhakikishe *exploration* tunafanya wenyewe ili tuingie mikataba tukijua tuna kiasi gani cha madini katika eneo ambalo tumeipa kampuni ichimbe.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa majibu gani kuhusu mgodi wa chumvi Uvinza amba leo kuna taarifa za mwekezaji wa Kampuni ya *Great Lake Mining Corporation* ameng'oa mitambo na mpaka sasa *plant* iliyokuwa ikizalisha chumvi kwa kutumia umeme imekufa na kubaki shamba la mahindi, *plant* hii ilijengwa na Wataliano na kiwanda kilichotoa chumvi bora Afrika ya Mashariki na Kati.

Tafiti zinaonesha kuwamba mgodi huu wa Uvinza ulizalisha 30% ya chumvi yote inayotumika eneo la Tanzania, Congo, Rwanda, Burundi na Zambia na kwa wastani binadamu hutumia kilo nne za chumvi kwa mwaka. Ukichukua idadi ya wote wanaoishi eneo hili utaona ni kwa namna gani Taifa linapoteza mapato. Nataka majibu ya Serikali kuhusu hatma ya mgodi huu amba uliuzwa kwa bei ya kutupwa tukadhani mwekezaji ataendeleza na badala yake mwekezaji ameamua kung'oa na anauza mitambo na mali za mgodi huu. Je, huu ndio utaratibu na kusimamia na kuendeleza migodi yetu? Mwekezaji anauza na ninao ushahidi anauza mgodi/mali.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua hatima ya 15% *capital allowance* ambayo miaka yote inanyonya Taifa letu kuititia Mikataba ya Madini. Kuna taairfa zisizo rasmi kwamba migodi ilio chini ya Barrick wameamua kusamehe, kweli? Na kama Barrick wamesamehe katika migodi yao kwa nini utaratibu huo usiwe kwa migodi yote hasa ikizingatiwa kuwa kipengele hiki ni kuruhusu wizi? Naomba sana kujua suala hili.

Mheshimiwa Spika, nini mpango wa Serikali kujengea uwezo Watanzania kwa kuwapa uzoezi na elimu ya kuendesha migodi ya madini? Kwa kuwa sheria imesisitiza wawekezaji kuhakikisha wanatoa nafasi ya kutosha kwa wazawa hata kwenye *management* za juu katika uendeshaji wa haya makampuni. Naomba kujua katika Makampuni yote ya Madini Tanzania, *management* za juu zina watendaji wangapi jumla na wazawa ni wangapi na kwa nini Serikali isihakikishe wawekezaji wanafuata sheria kuhakikisha tunakuwa na wazawa katika migodi hii ili waelewe namna tunavyoibiwa?

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo ambalo tunapoteza mapato mengi ni hoja ya makampuni kutumia mitaji kutoka benki za nje ambazo nyingi ni zao. Madhara ya utaratibu huu ni kupoteza pesa nyingi za kigeni na pia Serikali kushindwa kupata taarifa nyingi kuhusu migodi hii lakini zaidi kuondoa dhana ya nafasi ya Serikali na Taifa katika umiliki wa rasilimali ya madini.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itumie pesa za Mifuko ya Hifadhi kutoa pesa *7IB* ili moja ya sharti kwa makampuni haya iwe kukopa *7IB*. Huu ni uzoefu katika baadhi ya nchi kama China katika kudhibiti faida za rasilimali ya madini kwa maslahi ya Taifa. Mifuko ya Hifadhi Tanzania inazo

pesa za kutosha. Wanaweza kuwekeza mpaka trillioni nne kwa kuanzia na hii ina faida kwao na kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, umeme na mjadala wa umeme umekuwa tatizo kubwa sana na kuna kila dalili kwamba Serikali kwa pamoja imeshindwa. Hali ya sasa ambapo Mawaziri wa Serikali moja wanatoa maoni yanayogongana mbele ya umma ni kielelezo kwamba Serikali imeshindwa. Nachouliza hapa ni kwa nini Baraza la Mawaziri lisivunjwe kupisha timu nyingine itakayoweza kuondoa tatizo hili kwani lina historia na imefika ukomo?

Mheshimiwa Spika, kuondoa tatizo hili la umeme ndani ya miezi miwili nashauri Serikali itumie utaratibu wa kuagiza nje wenyе mitambo iliyo tayari kuzalisha umeme walet na kuanza kutumia. Huu ni mfumo ambao mitambo inaletwa na kama tayari tuna gesi tutaanza kutumia mara moja kwa kuwa haitohitaji muda ya kujenga miundombinu ya *plant* hizo ambayo ingechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la mgogoro wa umeme Mkoa wa Kigoma unashauri Wizara ifikirie kufanya mazungumzo na NSSF kuweza kukopesha Serikali/TANESCO itekeleze mradi wa MW41 uliokuwa ujengwe kuititia *MCC*. Pamoja na hili napenda kuishauri Wizara kuhakikisha *REA* wanaweka msukumo zaidi kwenye mikoa ambayo haina umeme kwa maana ya Gridi ya Taifa. Inasikitisha kuona mikoa yenye Gridi ya Taifa ambayo hiyo hiyo inayofaida *REA*. Hii inasikitisha sana hasa kwa sisi Wabunge wa mikoa ya Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali/TANESCO inatumia għarama kubwa sana kulipia makampuni ya umeme ya kukodi. Kwa taarifa zilizopo ni kwamba makampuni haya yanazalisha 45% ya umeme wote lakini yananyonya 80% ya mapato yote ya TANESCO. Moja ya sababu ni mikataba mibovu hasa eneo la *capacity charges* ambazo mfumo wake ni mbovu, mimi ninafahamu makampuni ambao yangeweza kuzalisha umeme hapa na yanazalisha nchi zingine bila kutuingiza mkenge wa *capacity charge* na tena kwa *energy charges* nafuu. Naishauri Wizara ianze utaratibu kufuatilia kwa karibu kampuni hizi kuondoa hasara za namna hii.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa mchango wangu naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya CCM inayooongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuweza kukumbuka Mkoa wa Kigoma kwa kutekeleza llani ya CCM kwa kuweza kufunga mashine (*generators*) katika Wilaya ya Kigoma, Kasulu na Kibondo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa juhudzi za makusudi ziongezwe ili umeme uweze kuwaka mapema iwezekanavyo kwa sababu wananchi wana hamu ya kuona umeme unawaka katika Wilaya ya Kibondo na Kasulu.

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya kuona umeme umewaka katika Makao Makuu ya Wilaya naomba vijiji vyote vinavyozunguka Makao Makuu ya Wilaya hizo vipewe umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba Wilaya zote tatu mpya zinazoanzishwa nazo zipelekewe umeme ambazo ni Kakonko, Buhingwe na Uvinza.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuititia *REA* iweze kutupelekea umeme katika vijiji ambavyo viro mbali na Makao Makuu ya Wilaya, lakini wakati tukisubiri umeme wa *REA* Serikali itusaidie kutupatia umeme unaotokana na jua (*solar*) ili uweze kusaidia kwenye vituo vya afya ili wanawake wawze kupata huduma stahiki wakati wa kujifungua, pamoja na shule za kutwa ambazo zina hosteli nazo ziweze kupata huduma yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu, naomba kuunga hoja mkono.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, Serikali imewaaahidi wananchi wa Bukombe kuwapelekea umeme toka mwaka 2000. Ahadi hii imerudiwa katika awamu ya nne mara kadhaa (2005, 2010 na 2011). Waziri anawaambia nini wananchi wa Bukombe kuhusu utekelezwaji wa ahadi hii?

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa umeme unasababisha ukosefu wa ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji katika shule za msingi na sekondari Bukombe (na kwingineko). Je, Serikali itapeleka lini umeme wa mionzi ya jua katika shule hizi ili ufundishaji na ujifunzaji uboreke?

Mheshimiwa Spika, kadhalika tatizo la kutokuwepo umeme katika zahanati na vituo vya afya Bukombe ni kero kubwa sana. Je, Serikali itapeleka lini umeme wa mionzi ya jua katika sehemu hizo za tiba ili kuboresha huduma za tiba?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, Bukombe na Wilaya jirani (Biharamulo, Geita, Kahama) kuna kilio cha muda mrefu cha wachimbaji wadogo kunyimwa haki ya kupewa maeneo ya kuchimba madini na pia kutopewa msaada wa zana stahiki.

Mheshimiwa Spika, napendekeza yafuatayo:-

(a) Wachimbaji wadogo watengewe maeneo pemberi mwa maeneo yenyeye migodi mikubwa kuondoa tatizo la migogoro baina ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo katika maeneo hayo. Hili linawezekana katika maeneo mengi.

(b) Kuwa na mfuko maalum wa uwezeshaji kwa wachimbaji wadogo utakaochangiwa na Serikali na makampuni ya uchimbaji madini. Mfuko huu utumike kuwawezesha wachimbaji wadogo kununua zana za uchimbaji madini.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro wa siku nyingi tangu mwaka 2008 baina ya utawala wa Kampuni ya *Caspian* (Kitengo cha Uchimbaji Madini). Mgogoro huu unahu kima cha chini cha wafanyakazi nane (katika kitengo hicho) cha shilingi 150,000/= ambacho wanalipwa badala ya mshahara wa shilingi 350,000=/. Serikali inasema nini kuhusu mgogoro huu wa siku nyingi na itawasaidiaje wafanyakazi hawa?

Mheshimiwa Spika, kuna Makampuni ya Madini ya nje yaliyokuja nchini zamani na yakapata leseni za utafiti (mfano, *TANCAN, Resolute, Kabanga, Nickel*) na kufanya utafiti kwa muda mrefu. Je, makampuni haya yatachukua lini leseni ya kuchimba madini ili yaanze kazi hiyo na kuanza kulipa kodi na kuchangia maendeleo ya maeneo haya?

Mheshimiwa Spika, maswali kuhusu mipango ya Nishati Bukombe (Tazama Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini) katika ukurasa wa 115, Mradi wa Taa za Mwanga Bora Vijiijini. *Community-Based Solar Power Trading*, mradi huu unatekelezwa Chato, Biharamulo, Kahama na Bukombe. Je, unatekelezwa Bukombe yote au Kata kadhaa tu? Utaanza lini na utakamilika lini?

Katika ukurasa wa 117, aya ya 19, *Tanzania Affordable Rural Electrification Plan (TAREP)*. Mradi huu unatekelezwa Kibondo na Bukombe, utahusu kata zipi na utaanza lini na kukamilika lini?

Ukurasa 129, miradi inayofadhiliwa na AFDB (Benki ya Maendeleo ya Afrika). Maswali, mradi huu unaanza lini na utakamilika lini? Hapa hata gharama haikuoneshwa na hatua iliyofikiwa haikuonyeshwa. Kwa nini Kata nyingine muhimu zilizo katika Jimbo la Bukombe kama vile Runzewe, Namonge, Uyovu na Busonzo hazikuorodhwshwa kwenye orodha iliyoo ukurasa 129? Wananchi wamesubiri kwa muda mrefu kupata umeme, wote wapelekewe umeme bila kuwabagua.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Novemba, 2008 Serikali ya Tanzania ilitoa tamko juu ya nia yake ya kujunga na Asasi ya EITI kwa dhamira ya kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za madini, gesi asilia na mafuta na ilipatiwa usajili wa watu tarehe 14 Februari, 2009.

Mheshimiwa Spika, hata mimi nakubaliana na maelezo yaliyotolewa na Kamati ya Madini kuwa taarifa ya kwanza ya *TEITI* ya jumla ya shilingi bilioni 174.9 wakati Serikali imeonesha kupokea jumla ya shilingi bilioni 128.4 hivyo kufanya tofauti ya malipo na mapato kuwa shilingi bilioni 46.5 kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa dhana ya wananchi ya kuwa kumepita udanganyifu katika kasoro iliyokuwepo katika tofauti hii na mapato kati ya taarifa iliyooneshwa na makampuni makubwa na yale yaliyooneshwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wengi wa Tanzania hawashiriki katika kutoa huduma za ugani kwenye migodi na kwa kuwa huduma hii ina faida sana hasa katika kukua kwa Pato la Taifa. Hata mimi naungana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Nishati na Madini kwa kuishauri Serikali isaidie ili Watanzania walio wengi zaidi waweze kujikita katika huduma na kufaidi na hatimaye kunufaika na kuinua Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza hasa kazi iliyofanywa na Kamati ya Nishati na Madini. Naunga mkono hoja.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kuwepo ndani ya Ukumbi huu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, na mimi natoa mchango wangu kwa Wizara ya Nishati na Madini ambayo ni muhimu sana, imekuwa kama jambo la kawalda kwa Tanzania kuingia gizani ama kuwa na mgao wa umeme. Tatizo la mgao wa umeme limetokea mwaka 2006 kama haitoshi likatokea tena mwaka 2007 kama haitoshi na mwaka 2010 – 2011 bado tatizo hili lipo.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa umeme unasababisha hasara kwa Taifa, uchumi wa Taifa hushuka, Serikali inakosa mapato makubwa, viwanda vinafungwa havifanyi kazi na wananchi wanakosa ajira.

Mheshimiwa Spika, kutegemea chanzo kimoja cha kuzalisha umeme chanzo cha maji ni tatizo kwa sababu maji yanategemea mvua kama mvua hakuna na uzalishaji unapungua.

Mheshimiwa Spika, ili tuondokane na tatizo hili la kila mwaka, inapaswa juhudzi za makusudi Serikali ichukue. Serikali itafute njia mbadala za kuzalisha umeme badala ya kutegemea maji. Serikali ishirikiane na wataalamu kufanya utafiti wa njia mbadala za kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili ambayo Tanzania tunayo, kufanya utafiti kuzalisha umeme kwa kutumia upopo. Utafiti wa kina wa kutumia mawimbi ya bahari na nydingi nydinginezo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kufanya juhudzi ya kuondoa uchakachuaji wa mafuta. Uchakachuaji wa mafuta umekosesha mapato Serikali, umetia hasara wenye magari, injekta pampu zimekufa na matatizo mengi tu. Pamoja na kupandishwa bei ya mafuta ya taa ili yalingane na ya dizeli lakini kwa upande wa pili ni tatizo kwa wananchi hasa wa vijijini ambaeo ndio watumiaji wakubwa wa mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie kwa makini sana kutafuta njia mbadala ambayo itasidia wananchi wa vijijini ambaeo hutumia mafuta ya taa ambaeo ni karibu asilimia 80. Kutokana na kukosa umeme katika vijiji vingi Tanzania hutumia mafuta ya taa ambayo sasa yamekuwa ghali na hawamudu.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia madini. Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizobarikiwa kwa kuwa na madini mbalimbali. Pamekuwa na malalamiko makubwa kutoka wa wananchi hawafaidiki vizuri na ardhi yao. Wananchi ambaeo ardhi zao zinazalisha madini ni maskini sana, barabara zao ni duni na mbovu, shule zao hazina madawati, hamna maabara, hamna umeme, mali ambazo zinatoka katika ardhi zao zinaneemesha wawekezaji pamoja na nchi zao.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya kuangaliwa upya mikataba ya madini. Mikataba ya madini ni mibovu sana, hainufaishi Taifa letu wala wananchi ambao ardhi yao inachimbwa na kubakishwa mashimo matupu na mali inakwenda.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikisamehe kodi kwa wawekezaji wakubwa wakubwa na kupoteza pesa nyangi kwa Taifa letu, wakati sisi tuna matatizo mengi. Tunakaa gizani yaani mgao wa umeme, upungufu dawa katika hospitali, madaftari mashulen na mengi mengineo. Mimi nashauri Serikali yetu kuangalia upya mikataba kwa maslahi ya Taifa na watu wake. Mikataba yote mibovu ifutwe.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na watendaji wake wanavyoitajidi kufanya kila linalowezekana ili Watanzania waweze kupata umeme na waondokane na usumbufu huo.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa umeme ndani ya nchi yetu imekuwa ni tatizo ambalo linaathiri uchumi wa nchi yetu na pia linaendelea kuwaathiri wananchi wafanyabiashara kwani bila umeme saluni kwa wanawake zina suasua, washona cherehani wana athirika, wachoma nyuma, viwanda vidogo vidogo, saluni za kiume, viwanda na kadhalika. Hili ni tatizo kubwa sana lina mwelekeo wa janga la Taifa letu. Ushauri kama ushauri aliota Mbunge kwa Serikali sasa ichukue hatua ya umuhimu kwa udharura huu kutafuta pesa za uharaka na kuagiza hiyo mitambo na kunusuru hili Taifa kulizidishia umaskini kwani uzalishaji kwa wananchi umepungua sana.

Mheshimiwa Spika, umeme ni roho ya nchi yetu na Wizara hii ni muhimu sana. Ninaombwa Serikali iangalie sana Wizara hii kwa umuhimu wake na ifanye mabadiliko ya kuibagua sekta hii ya umeme ikawa yake ili tuweze kuiangalia kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukame umetufikisha pabaya kwani maji yakikauka tu na Taifa lina athirika kwa mambo mengi. Sasa Serikali iandae mipango mizuri ya kukopa au kutafuta fedha kwa njia yoyote ile tuondokane na umeme wa maji au tusipunguze utegemezi wa umeme wa maji ili wananchi waweze kufanya biashara zao bila ya usumbufu wowote na Taifa letu liendelee mbele kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, naomba nami nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme umeshawekwa Makao Makuu ya Tarafa ya Ndago kwa muda mrefu sasa na ukiacha Shule ya Sekondari ya Ndago iliyoko katika Kijiji cha Kibaya na pia kilomita chache toka Shule ya Sekondari ya Ndago kuna Magereza na pia kuna mashine ya kupampu maji kwa kutumia dizeli, je, ni lini Serikali itafikisha umeme Kibaya ambako ndiko anakoishi Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Singida Mheshimiwa Martha Mlata ili kumuondolea kero ya kulalamikiwa na kukejeliwa na wananchi wa eneo hilo kwamba Mbunge gani hata kwake anashindwa kutetea na kujenga hoja ya kuwekewa umeme na Serikali na kuonekana hafai, naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria ya Manunuzi inaonekana inatubana kununua vifaa ambavyo vimeshatumia na kusababishia watendaji kushindwa kutoa maamuzi ya kuokoa udharura unaojitokeza na mfano kwa sasa suala la kununua mitambo kwa ajili ya kutoa nchi gizani. Je, Serikali italeta lini Muswada wa Sheria hiyo kwa udharura ili tuweze kuiokoa nchi yetu toka gizani? Na pia kanuni ipi inayotakiwa kutenguliwa ili tuondokane na kero ya umeme?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali itachukua hatua gani kuwaelimisha wananchi wote kuhusu madini yapatikanavyo ardhini kwamba wanafaidikaje? Kwa kuwa walio wengi wanaonekana kutoridhishwa na madini yapatikanayo hasa kupitia wachimbaji wakubwa na kuonekana na kwamba mali yote inaporwa. Je, Serikali haioni kwamba sasa wakati umefika wa kuonyesha na kutangaza fedha zote ambazo zimepatikana toka wachimbaji wakubwa na wadogo na kwa kila

eneo na kilichotumika kwenye eneo husika na kilichoingia Mfuko Mkuu, ili kuondoa utata wa watu kudhani hakuna kinachopatikana pia kuepuka upotoshaji.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali wanipe orodha ya wawekezaji wakubwa kwenye machimbi ya Londoni na kama kuna mgogoro wowote na wachimbaji wadogo na kama upo kwa nini na Serikali inasaidiaje? Je, eneo la wachimbaji wadogo limeshatengwa? Na ni wangapi waliopewa maeneo?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. LAZARO S. NYALANDU: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Nampongeza Waziri Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuiongoza Wizara hii nyeti kwa uchumi na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wanajimbo wa Singida Kaskazini wanaomba yafuatayo kutoka Bajeti ya Wizara hii. Kwanza kusambaza umeme katika Tarafa ya Mgori ili ufile Sekondari ya Mwanamwema, Mgori, Sekondari ya Ngimu, Ngimu, Sekondari ya Pohama, Pohama na kituo cha Afya Nduamganga. Umeme huu pia utafaidisha zahahati na vituo vya afya katika Tarafa yote ya Mgori.

Pili, kusambaza umeme sekondari zote katika Tarafa ya Ilongero na Tarafa yote ya Mtiko, pamoja na vituo vyote vya afya ndani ya Tarafa hizi. Tatu, Wanajimbo la Singida Kaskazini wanaishukuru Wizara kwa kujenga njia ya umeme kutoka Singida Mjini hadi Ilongero, Ngamu na Mtinko hadi Nkungi. Tunaomba vijiji vinavyopitia na njia hii ya umeme, wananchi wapatiwe *step down trasformers* ili shule za msingi, zahanati na vituo vya afya navyo vipatiwe umeme huu.

Nne, wachimbaji wadogo wadogo wa Mpambaa wanaomba Serikali iwasaidie kupata hati miliki za machimbo yao ya dhahabu na kusaidiwa kama vikundi vya wazalishaji ili wawze kuzalisha kwa tija na kuwa na migodi midogo midogo endelevu.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kumpongeza Waziri Mheshimiwa William Ngelleja na naomba tena kuunga mkono hoja hii.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wa kuongea mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 15/7/2011 jioni naendelea kuchangia kwa maandishi nizibe mapungufu yaliyotokana na mapungufu ya muda.

Mheshimiwa Spika, naanza pale nilipoishia kwenye sekta ndogo ya mafuta na gesi asili. Nilisema kuna mapungufu katika mipango na kanuni itakavyotawala ununuzi kwa wingi na hapa nchini nafafanua.

Kama ilivyobainisha taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini, kanuni hizi zimeandaliwa kwa usiri na kificho bila kuwashirikisha wadau katika mchakato mzima hali inayowafanya wadau wafikiri kuwa zoezi zima lima nia mbaya.

Sehemu ya pili ya kanuni, *The Petroleum (BP) Regulations 2011, Part II*, inajikanganya na haionyesi ueledi na ujuzi katika kuendesha shughuli hii. Kanuni zinatoa tafsiri ya manunuzi yenye tija/ufanisi (*efficient procurement*) kuwa ni yale yaliyofanya chini ya mtindo wa *Bulk Procurement* kama kanuni zinavyooleza. Hii si kweli, manunuzi yenye ufanisi ni yale yatakayompatia mlaji mafuta yenye viwango (*TBS standard*) na kwa bei nafuu. Hapo uwezekano mkubwa chini ya mtindo huu bei ya mafuta kuwa kubwa zaidi kulinganisha na mfumo wa sasa. Je, hiyo itakuwa *efficient procurement*? Hakutakuwepo na uhakika wa ushindani katika kununua wakati wote inawezekana mzigo wa Taifa ukulanunuliwa katika dirisha ambapo bei zipo juu, inawezekana *supplies* akashindwa *ku-tender* kama ilivyotarajiwu kwa sababu mbalimbali. Bado yote hayo yaktolea ununuzi utakuwa na ufanisi?

Mheshimiwa Spika, ukisoma *Part II* na *III* pamoja Waziri anajaribu kutumia nguvu kutekeleza mpango huu. Njia ya busara na kwa kuazima uzoefu wa Zambia ni kuruhusu asiyekubali utaratibu huu aagize kivyake lakini aweke tozo maalum, nchini Zambia mafuta yote hutoka kiwanda cha kusafisha mafuta cha Indeni. Kutokana na ukweli kuwa mafuta yachujwayo *Indeni Refinery* ni gharama kubwa kuliko waagizaji wa moja kwa moja, lakini Serikali ya Zambia inayo dhamira ya kulinda kiwanda hicho kwa sababu za kihistoria, usalama na kiuchumi. Kampuni yoyote inayoagiza hulazimika kuilipa Serikali tofauti ya gharama kama *cost differential*. Mfano, iwapo kuagiza tani moja dizeli ni USD 1350 mpaka Zambia kabla ya kodi na faida ya kampuni na gharama ya *Indeni Refinery* ni USD 1450 basi muagizaji atailipa Serikali USD100 kwa kila tani pamoja na ushuru, kodi na tozo nyinezo zinazoandamana na bidhaa ya mafuta. Lakini wakati huo huo Waziri husika inapotokea kiwanda kikasimama hutoa ruhusa haraka makampuni yaagize na kuuza bila hiyo tofauti ya gharama (*USD100 cost differential*). Ukitafakari maelezo haya na *Part IV 16 (1)*, kanuni inazuia uingizaji wa mafuta nchini na kurejesha ukiritimba.

Sehemu ya tatu yenyе mapungufu makubwa ni *Part II 5(1) the Bulk Procurement Technical Committee*. Chombo hiki chenye mamlaka, kanuni inayokiunda inaishia kueleza watatoka Idara na sehemu zippi, haitaji ueledi, ujuzi na uzoefu wa wajumbe wake. Lakini kasoro nyinezo ni kuwa wajumbe wanateuliwa na Waziri kutekeleza majukumu haya makubwa na watalazimika kufuata maelekezo yote toka kwa Waziri atakayoyatoa kwa maandishi bila kuhoji, hii haiwezekani. Ipo mifano ambayo mikono ya viongozi au watu wenye nyadhifa wamesababishia hasara nchi zao kwa kuingilia vyombo vya utendaji kama hiki kinacholengwa kuundwa.

Sehemu ya nne nirudi nyuma kidogo ni uwezo au sifa za muagizaji wa mafuta (*Part II, 5 a & b*). Hii inazungumzia uwezo wa kiufundi na kifedha wa huyo muagizaji. Pia haja ya kanuni kushamirisha ushindani katika shughuli ambazo ni jambo jema. Mapungufu ya kanuni hii ni uwezo wa kifedha ambao *EWURA* ililuelea kwenye mkutano na makampuni ya mafuta na wataalam wa kibenki wa benki ya Baclays. Inadaiwa muagizaji awe na mauzo ya USD milioni 500 kwa mwezi. Hii ni sawa na mauzo ya shilingi bilioni 800 kwa mwezi. Kichekesho hapa ni kuwa mauzo ya mafuta kwa Tanzania hayafukii shilingi bilioni 600 kwa mwezi. Kwa mwezi tunauza/kununua takribani tani 200,000 tani moja ni wastani wa lita 1200 (dizeli) na lita iuzwe kwa wastani wa shilingi 2,200 kwa lita. Hii ina maana kampuni inayotafutwa ni ya nje kimantiki na kama ni ya ndani basi kanuni inahalalisha udalali. Kama haja ni hii kanuni itumike vinginevyo na kuweka kinga ya huyo dalali kumuumiza mlaji.

Sehemu ya tano ni miundombinu, kimsingi hapa mpishano wa kifikra ndipo ulipo na hii ndio dawa ya kumakata anayepinga mfumo wa *BPS* kwa sababu zake binafsi. *BPS* zitafanya kazi vizuri au tuseme inayotarajiva baada ya kuweka miundo inayoendana na dhana hiyo. Hapa tunazungumzia boyaa kuelekea bahari kuu *SPM* kwa ajili ya kupokeea meli za ukubwa wa tani 80,000 mpaka 120,000. Boyaa na mabomba yake yenyе uwezo wa kushusha tani 3,000 kwa saa na yakinaganisha mafuta ya ndege na mengine lazima yaunganishwe na matanki ya kupokelea. Matanki ya kupokelea mafuta kwa kasi hiyo hapo juu lazima yawe na ukubwa usioathiri ufanisi lengwa. Yote haya hayapo pamoja na uamuzi wa Serikali kutumia mfumo huu mwaka mmoja uliopita. Hifadhi ya *TIPER*, miundombinu yake mingi imechakaa na mmoja wa wamiliki ambaye ni mtaalam amekata tamaa na kuna uvumi kuwa anataka kuuza hisa zake na kuondoka. Huyu kama kweli angeondoka na Serikali kumiliki *TIPER* asilimia 100 na kuiboresha *BPS* ingezaa matunda halisi si matarajio hewa.

Kanuni inayojichanganya pale inapoelekeza uwepo wa mabomba ya inchi 10 au zaidi toka *KOJ*. Hii ina maana uwepo wa bomba za inchi 10 katika mfumo kunafuta uwezekano wa kupokeea mafuta moja kwa moja toka *SPM* kwenye hifadhi za Kurasini. Kanuni haitambui kasoro ya utandazaji wa mabomba kuwa ni moja ya sababu ya kupunguza ufanisi katika upakuaji. Utafiti wa kitaalam ulishafanyika na kubainisha haja ya kuyalaza kimkakati mabomba ili kupunguza *back pressure* na kuongeza ufanisi. Lakini kanuni inajichanganya kwa kuzungumzia matumizi ya *flow metre*! Ni nchi gani duniani ambako *flow metres* zinatumika kushusha mafuta toka melini? Hizi zinatumika kufunika mapungufu yaliyofanyika katika maamuzi ya kuzinunua ikiwemo gharama halisi ya kuzifunga. Idara ya Serikali inayosimamia vipimo mbona imeshasema kuwa *FM* ni bomtu. Tunaidanganya Serikali na Mheshimiwa Rais mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, hili lilizungumzwa katika Kamati lakini kanuni zikachepushwa huko na tusionyeshwe. Huwezi kubadili mfumo eti kwa faida ya kukusanya takwimu! Idara ya Vipimo na Mizani wameonyesha uwezo katika hili na wanatozo katika kila lita ya mafuta, kwa nini wasikidhi mahitaji hayo mpaka miundombinu yote iwe tayari. Na hili ni miundombinu, mbona hatuelezwi kinachoendelea na haja ya kuongeza kazi ili angalau basi iwe tayari Desemba tunapoanza *BPS*.

Mheshimiwa Spika, wakati nachangia kwa kuzungumza nilleleza haja ya kuwa na mawasiliiano na wananchi. Wananchi hawapewi maelezo ya kina bali wao wanabaki wadandie hili na lile kujaza ombwe la ufahamu. Hii ni kwenye mafuta na sekta ya madini. Haitoshi kusema bei ya mafuta ipo juu hapa nchini kutokana na udhoofu kwa shilingi. Unapaswa uonyeshe kuwa tarakimu na namba jinsi tunavyofikiwa hapo. Aidha, ipo haja ya kwenda mbali na kueleza kwa nini shillingi inadhoofu? Hilo nalisema kutokana na kauli za waliopewa dhamana kueleza kila kukicha kuwa *BPS* italeta unafuu katika bei kwa asilimia 30. Thubutu, nasema haiwezekani! Matumizi ya Meli kubwa kama *SPM* ikitumika yatatutoa katika *Premium* ya USD 39 – 54/MT mpaka USD 15 – 25/MT. Punguzo hili ni asilimia 2.8 ya *cost & freight*. Sasa *SBM* haipo tayari hiyo 2.8% nayo haiwezekani.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mafuta ni nyeti, mabadiliko ya ufanisi yanatakiwa lakini maandalizi stahili lazima yafanyike. Natanabaisha kuwa baadhi ya wadau wanafikiri kanuni zimeandalishi kwa kulenga kunufaisha kampuni au kundi fulani la watu. Rai yangu ni kuwa tuondoe janga la giza kabla ya kuchezea mfumo wa sasa wa uagizaji wa mafuta bila kuwa na maandalizi stahiki.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie Shirika la *TANESCO* katika kipindi hiki ambacho tutalazimika kutumia kwa wingi mafuta ya ndege, dizeli na mafuta mazito kama nishati ya kuzalishia umeme. Aina hii ya nishati ni ghali sana ukiliganisha na umeme wa maji na gesi asili. Hoja yangu hapa ni kuwa umakini unaoandamana na weledi unatakiwa ili kukabili maumivu yanayomeza kutokana na gharama za ununuzi wa mafuta pamoja na kuwa *TANESCO* ni shirika huru, kanuni ya kukokotoa kiwango cha *tarrif* ni vema iwasilishwe Serikalini na kwenye Kamati ya Nishati ili tuihakiki tusije kulia, majuto ni mjukuu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mashaka ya mchango wa mafuta katika bei ya umeme lipo suala la mfumo wa manunuzi ya mafuta mazito yatumikayo *IPTL*. Mfumo huu umefungwa hali inayoondoa ushindani katika kupata *tender* ya kuleta mafuta hayo. Kwa kuwa sasa *IPTL* si mtambo wa dharura tena njia wazi za ushindani zitumike ili tumpe faida au unafuu mlaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika lenyewe *TANESCO* janga la giza linatulazimu kujengwa/kuimarisha Shirika katika mfumo wake wa sasa na kuachana na fikra za kuligawa. *TANESCO* isilingiliwe bali ishauriwe, kuimega vipande kutapelekeea kipande kisichovutia wawekezaji kidhoofu ilhali sehemu nzuri imeshanunuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuongeleaa kidogo sekta ya madini. Madini kwa ujumla wake uendeshaji wake hauna mapokeo mazuri kwa Watanzania walio wengi. Ushauri wangu ni kama hivi, Serikali iendelee kipitia upya mikataba ya zamani na iweke jitihada za kuwasihii wawekezaji wakubali wazo jipya kwa manufaa ya Serikali na wawekezaji, migodi mipya ianzishwe chini ya mikataba mipya aliyowekwa wazi kwa umma, sekta ya madini itoe elimu kwa kufuta dhana potofu kama uhamishaji wa mchanga, watu wanahabari si za kweli. Iwapo chombo chenye dhamana ya kuhakiki madini kina uhakika na ushahidi kuwa hatuibiwi basi kwa nguvu kubwa kibebe jukumu la kueleimisha Taifa.

Pua upo ushahidi kuwa gharama kubwa za kuendesha migodi ni ugavi (*supplies*) ikiwemo vyakula, maji, chumvi, matunda kwa kutaja baadhi. Kama kipande cha ugavi kingachukuliwa na soko la ndani ni dhahiri uchumi ungechangamka na lawama toka kwa wananchi kupungua. Lakini huko ukweli kuwa viwanda, mashamba na kampuni yetu hayajajipanga kukabili mahitaji haya/mapendekezo na kushauri kuwa ofisi ya uwekezaji ichukue jitihada za makusudi kuwawezesa Watanzania kuteka fursa hii ya ugavi kwenye migodi ya madini.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nimalizie kwa kutoa jibu kwa nini shughuli za biashara ya mafuta zimejaa uvumi, mashaka na kutoaminiana, sababu ni makosa ya Serikali kukataa kuanzisha kampuni ya Taifa ya Mafuta (*National Oil Company*), bila kujali ukubwa wa kampuni kuwemo katika shughuli kwa kampuni ambayo ni ya Kitaifa, kunatoa fursa ya Serikali kupata taarifa za kwanza juu ya nini kinafanyika. Tunapata kigugumizi juu ya kwa nini bei ya mafuta haikushuka, jibu ni kuwa watendaji wa Serikali hawajui sawa sawa na kuushiriki mchezo/shughuli za mafuta kila uchao.

Mheshimiwa Spika, niliunga mkono hoja na naendelea kuunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Waziri Mheshimiwa Ngeleja, Naibu Waziri Mheshimiwa Malima, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa hotuba yao walioiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nianze na masikitiko yangu makubwa kwa Wizara hii kupatiwa Bajeti isiyokidhi haja kwa sababu sasa hivi Wizara hii inakabiliwa na janga kubwa la mgao wa umeme. Tatizo hili sina uhakika kama Serikali imelichukuliaje

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa makini utatuletea matatizo makubwa sana. Wananchi wengi wanashindwa kufanya biashara na kusababisha hali mbaya sana na ngumu ya maisha ya kila siku, pia Serikali itakosa mapato makubwa sana. Naomba Serikali iweke mkakati maalum wa kuhakikisha tatizo hili linatatuliwa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji. Vyanzo vya maji vingi havina matunzo, vimeachwa kiasi kwamba wananchi wanafanya kilimo cha umwagiliaji na kusababisha Bwawa la Mtera kutojaa kabisa pamoja na mvua nyingi sana zinazonyesha Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Bwawa la Mtera kuna kilimo pale kinaendelea cha mradi wa umwagiliaji sio rahisi bwawa lile kuishiwa maji kama lisingekuwa linatumwiwa visivyo halali.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupeleka wataalam katika vyanzo hivi ili kuona jinsi gani vinaweza kutunzwa ili vituletee mafanikio na kupeleka maji hayo katika Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu uchakachuaji, tatizo hili limekuwa kubwa sana kote hapa nchini, naomba uwepo mkakati wa kuhakikisha adhabu kubwa inatolewa kwa hawa wachakachuaji na uwepo udhibiti maalum kwa *EWURA* kuhakikisha kuwepo kwa ubora wa mafuta na kupata kodi inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa kulichangia ni kuhusu Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*). Wakala huu ni muhimu sana katika nchi yetu kwa sababu zaidi ya asilimia 86 za kaya hapa nchini hazina umeme.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwepo na mpango madhubuti wa usambazaji umeme na utaratibu wa usambazaji umeme vijijini uharakishwe ili nchi yetu ipate maendeleo ya uwiano sawa katika maeneo yote ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo naomba kuunga mkono hoja.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Spika, ninapenda nami nichangie hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia suala la umeme katika Tarafa ya Mpimbwe kata ya Mamba, Maji moto, Mbede, Usevya na Kibaoni. Ni muda mrefu sana kata hizi hazina umeme na wananchi wamekuwa hawana imani na Serikali iliyopo madarakani kwani wamekuwa wakilalamika kwani wamekuwa wakichelewa kupata maendeleo kutohana na Serikali kutowapelekea umeme. Wananchi hao wamekuwa wale wenye uwezo wa kujinunulia mitambo

ya umeme wa juu ambao ni wachache na wamekuwa wakiwauzia wananchi wenzao kwa bei kubwa.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuweza kuwapunguzia kero wananchi hao kwa kuwapatia mfumo wa umeme unaotumia juu hasa maeneo ya hospitali (zahanati na vituo vya afya) na maeneo muhimu kama mashulenii na vituo vya polisi? Ninaishauri Wizara husika iangalie upya mchakato wa namna ya kuwasaidisa wananchi hao ili kuondokana na adha za ujambazi na wizi unajitokeza sasa hasa kutokana na kukosa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, naiomba Serikali kuitia Wizara husika iangalie namna ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo kama wachimbaji wa madini ya dhahabu (Mpanda) kwa kuwapatia mafunzo na vifaa vya uchimbaji ili waweze kujinasua na umaskini na pia waweze kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta ya taa kupanda bei, ninaombaa Serikali kuitia Wizara husika kwa namna yoyote ile iweze kupunguza bei ya mafuta ya taa ili mwananchi wa kijijiini hususani Rukwa/Katavi waweze kupata mwanga kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, ninaombaa kuunga hoja mkono.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, katika hotuba za Kamati ya Bunge, pamoja na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, pamoja na mambo mengine imeonekana kwamba mradi kabambe wa kusambaza umeme katika Mikoa 16 unasuasua kutokana na Serikali kutokupeleka fedha kwa *REA*. Mfano mpaka Mei, 2011 Serikali kikuwa imepeleka billioni 23.3 kati ya billioni 78.3 kwa ajili ya malipo ya makandarasi. Halikadhali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mpaka mwezi Mei, fedha za *REA* zilizotolewa ni billioni 13.6 tu ambayo ni sawa na asilimia 23 ya Bajeti iliyotengwa. Ni kwa nini kumekuwa na tatizo hili sugu? Tatizo ni wafadhili au Hazina?

Mheshimiwa Spika, suala la pili, tarehe 1 Aprili, 2011 Rais Jakaya Kikwete alitoa ahadi kuitia hotuba yake kwa Taifa kwamba mitambo ya *MW 260* ingekodishwa na kuanza kufanya kazi mwezi Julai kukabiliana na mgao wa umeme. Huu ndio mwezi Julai unaishia, ahadi hii ya Rais utekelezaji wake umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kuna tuhuma nzito ambazo pia zimejadiliwa kwa kina na Kamati ya Nishati na Madini pamoja na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya ukwepajji kodi wa Kampuni ya *Pan-African Energy*. Msingi wa taarifa hii, pamoja na mambo mengine ni ripoti toka kwa Shirika la Misaada la Kimataifa la *Action Aid* lenye tawi nchini Swedien.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Pan African Energy* iliyosajiliwa kwenye visiwa vya Jersey na Mauritius inavuna gesi ya Songsongo huku ikiwa imeingia mkataba wa miaka 25 kuitia Shirika la Nishati na Madini la Taifa (*TPDC*). Ni mkataba ambao unaifanya Kampuni hiyo kutolipa kodi ya faida ya mapato wanayopata kutokana na mauzo ya umeme unaotokana na gesi asilia wanayovuna Songsongo. Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na hili?

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, kumekuwa na hili suala la usafirishaji wa michanga ya dhahabu nje ya nchi na hili limekuwa likizungumza sana na Wabunge/wanaharakati/wanasiasa mbalimbali. Lakini kwa taarifa zilizopo ndani ya mchanga huo kunakuwa na madini mengine kama *copper*, *silver* pamoja na madini mengine yenye thamani.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo ni kwamba taarifa ya nini kilichopatikana katika mchango husika ni dhahabu, madini mengine aghali kama *copper* na *silver* hivyo kulipotezea Taifa mapato kutokana na madini hayo na zaidi kama wange-process hoja hapa nchini *copper* ingejulikana!

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anielezee usahihi wa hoja hii ya mchanga wa dhahabu, inaposafirishwa kwenda nje, nini ambacho kinakuwa *declared*.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya mwisho kuhusiana na usambazaji wa umeme katika baadhi ya maeneo ya Jimbo langu la Kawe. Nimepitia kitabu cha Wizara, sijaona hata dalili wa mradi wowote katika Jimbo langu hususan Kata za Mabwepande, Wazo, Bunju, Mbweni na baadhi ya maeneo ya Makongo Juu!

Mheshimiwa Spika, naomba nipate taarifa sahihi kuhusiana na Jimbo langu.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kutoa masikitiko makubwa kwa Mheshimiwa Waziri Ngeleja na Wizara kwa ujumla kwa ahadi za uongo za muda mrefu zaidi ya miaka minne za kupeleka umeme Sepuka - Singida Vijiji. Nimefuatilia sana na kupata ahadi za uongo inasikitisha sana. Kumbe uungwana wangu ndio unenifikisha hapa na kwamba ili ufikiriwe kupata mradi wa umeme ni wajibu kusema ovyo na maneno ya kashfa.

Mheshimiwa Spika, nimeahidiwa na uongo wa *REA* kuwa kabla ya mwezi wa Juni Sepuka wangepata umeme, lakini leo ni Julai, mwishoni hakuna dalili zozote ingetosha kuwa muungwana. Hivyo sitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Singida kumegundulika kuwa kunafaa kuwa na umeme wa upepo. Makampuni mawili yalijitokeza yaani *Power Pool East Africa Ltd.* na *Wind East Africa*. Hadi sasa mradi huu haujaanza rasmi/wananchi wa Singida waliweka matumaini kuwa umeme huu wa upepo ungepatikana kiasi cha zaidi ya *MW 50* na hivyo kupunguza upungufu wa umeme nchini. Je, tatizo liko wapi la kuanzisha umeme huu wa upepo Singida? Nitashukuru kupata maelezo.

Mheshimiwa Spika, nchi ipo gizani – Dkt. Idrisa alitutahadharisha juu ya hilo lakini tulimpuuza na kumbeza sasa yametufika. Tujifunze kuheshimu ushauri wa wataalam wetu. Mtambo wa *Dowans* ulikuwa batili kwa mwarabu lakini halali kwa Mmarekani.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili niweze kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, nishati na madini ni sekta muhimu sana katika kukuza uchumi na ustawi wa nchi yetu. Licha ya kuwa nchi yetu imebarikiwa kwa kuwa na rasilimali nyingi za nishati na madni ya kila aina, kwa bahati mbaya sana wananchi na nchi kwa ujumla imekuwa haifaidiki kwa namna yoyote kutokana na rasilimali hizi. Aidha, utendaji mbovu wa wakuu wa Wizara umeliingiza Taifa katika hasara na giza nene kutokana na ukali wa mgao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme limekuwa ni tatizo sugu na la muda mrefu katika nchi yetu, hivyo tatizo la umeme liliopo hivi sasa japokuwa nakubali kuwa ni janga la Kitaifa lakini si la dharura kama Serikali inavyotaka kutueleza kwani nchi haiwezi kuwa katika dharura kwa miaka bila Serikali kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, wakati Naibu Waziri wa Nishati na Madini akijibu swalii la matatizo ya umeme hapa Bungeni, alitueleza kuwa tatizo la umeme liliopo hivi sasa ni la dharura na ndiyo maana Serikali inalishawishi Bunge kubadilisha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 ili iruhusu ununuzi wa mitambo na mashine chakavu.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa kubadili Sheria ya Manunuzi ambao pamoja na mambo mengine ulihitaji kuiruhusu Serikali kununua mitambo na mashine zilizotumika. Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi ambayo mimi ni mjambe ilipinga vikali mabadiliko hayo kwa kuwa Serikali ilishindwa kujibu hoja zilizotolewa na Kamati juu ya jambo/mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, awali Serikali ilikuwa inanunua mitambo chakavu lakini kutokana na ukosefu wa uadilifu katika Manunuzi ya Umma Bunge katika Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 ilikataza ununuzi wa mitambo na mashine zilizotumika. Je, Serikali inapotaka kuruhusu ununuzi wa

mitambo chakavu ili kutatua tatizo la umeme, ni kwa vipi itawezekana ilhali mazingira yaliyokuwepo zamani ndio yaliyopo na pengine sasa hali ni mbaya zaidi?

Mheshimiwa Spika, sekta ya manunuzi kutohana na ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za kila mwaka imegubikwa na ubadhirifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama nchi maskini vilevile ipo nyumba kiteknolojia katika dunia iliyoendelea kisayansi na teknolojia, ni mitambo gani mipyambayo Serikali yetu itahitaji kununua ikosekane kwa wakati muafaka? Tangu tatizo la umeme litukabilii zaidi ya miaka mitano iliyopita Serikali imeshindwa kuchukua hatua na sasa wanatuambia umeme ni dharura waitatue kwa kununua mitambo chakavu.

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali iachane na mpango wa ununuzi wa mitambo chakavu kwani wananchi wamechoshwa na manunuzi yasiyo na tija na yanayotafuna hela za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Wizara hii kama iliviyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu, katika mradi wa kupeleka umeme vijiji nimeshangaa kuona kuwa Mkoa wa Singida ambao upo nyuma kwa kila jambo haujapewa mradi wowote wa umeme vijiji isipokuwa vijiji viwili tu vya Wilaya ya Manyoni! Katika Mkoa mzima ni vijiji viwili tu ndio vipo katika mpango wa Serikali mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naitaka Wizara ielete ni kwa nini hajatenga Bajeti ya kupeleka umeme Singida Vijiji hususan Jimbo la Singida Mashariki ambao hawajapangiwa hata kijiji kimoja katika Bajeti hii?

Mheshimiwa Spika, kutohana na sekta ya madini na nishati kushindwa kulinufaisha Taifa letu, kukumbatia wawekezaji wanaonyonya uchumi/utajiri wetu na Serikali kuendelea kuwakumbatia na wala Serikali haionyeshi nia ya kuchukua hatua na Mawaziri kushindwa kuwajibika kwa utendaji wao mbovu, nalitaka Bunge lako Tukufu lisipitishe Bajeti ya Wizara hii ili Serikali ijpange upya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa masikitiko makubwa kabisa kutoa salaam zangu za rambirambi kwa msiba mkubwa uliotupata Watanzania hasa sisi wakati na wazaliwa wa Kata ya Susuni kwa kuondokewa na aliyekuwa Diwani ya Kata ya Susuni hadi mauti yalipomkuta siku ya Ijumaa, tarehe 15.7.2011 mnamo majira ya saa mbili baada ya kuuawa kikatili katika eneo ya Nyandoto au Nyamisi sehemu iliyopo kati ya Kijiji cha Korotambe na Magena. Nashangaa hawa Kanda Maalum wapo wapi sababu wiki hiyo hiyo iliyopita kijana mmoja aliuawa na kutobolewa macho pale Tarime Mjini au hawa Kanda Maalum ni wa kulinda mgodi na kuwapiga Wanatarime risasi na kuwabambikia kesi na sio kulinda usalama wa raia?

Mheshimiwa Spika, baada ya salam za rambirambi napenda sasa kuchangia katika Bajeti ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Katika hotuba yake Waziri hakutaja kabisa Mgodi wa Nyamongo yaani *North Mara (Barrick African Gold Mine)* licha ya madhila makubwa yanayowapata Watanzania waishio katika maeneo hayo na cha ajabu kabisa ukurasa namba 6 na 7 Waziri anaainisha baadhi ya mambo yaliyotekelizwa kuwa ni pamoja na kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini. Sasa hapa Nyamongo wenyewe hawaitaji uchimbaji mdogo mdogo au wenyewe ni wanyama au hawana thamani ya kuishi sio?

Hii ni dhara kubwa kwa Wanatarime (Wakurya) na hasa Watanzania wote ambao yale madini yamekuwa ni moja ya vyanzo vikuu vya kujipatia *income* maana ardhi ile ilishaadhihirika na shughuli za madini na hivyo *their soul source of income* ni shughuli kubwa za madini na si vinginevyo. Hii inaashiria dhara na inapelekea kukosekana na amani, kwani sisi Wanatarime tutaendelea kuvumilia ndugu zetu wanauawa *at the expense of few people and the government getting permit about of it. How can the government dare at the expense of his people's blood, government is comfortable* na inaendelea *as if nothing happening.* Hivi ni Tarime (Nyamongo tu au)? Mbona huko kwingine hatusikii manyanyaso kama Tarime?

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tarime na Watanzania wote wamenituma kusema kuwa wamechoka na uwepo wa mgodi ule maeneo yale kwani walidhani maliasili ile ambayo Mungu ametupatia Watanzania *a natural resources* imegeuka kuwa ni madhila makubwa sana kwao, kwani kabla ya uwekezaji Watanzania walijichimbia madini na kupata kipato, sehemu inayoitwa Nyarugusu ambapo maendeleo mengi yalionekana na bila vifaa vyoyote. Hivyo basi, Wanatarime wanaomba Serikali kama ndio inaona ni fedheha Mungu kutupa madini yale katika ardhi yetu inakuwa Serikali kuwa wao wanavifa vya kijeshi, polisi na vyombo vingine vya maamuzi na ndio maana inadharau wananchi wake. Wanatarime wanataka Serikali ihamishe ule mgodi na kuupeleka kwingine na wao kuwaacha waendelee na ardhi yao kwa shughuli kama kilimo na vinginevyo kuliko kushuhudia vifo vya wapendwa wetu, madhara kwa mifugo na mimea na hili lifanyike haraka sana.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwani ni kwa nini Serikali inashuhudia wananchi wanalipwa laki mbili hadi tano kama fidia. Jamani *are we serious au joking?* Shughuli za maendeleo hadi leo hamna kitu *tangible* kilichofanyika, ni bla bla tu. Ni juzi ndio nasikia kuwa wanatoa dola 100,000 kwa kila kijiji, mimi nasema hii haitoshi na ni dharau kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nataka Waziri anieleze ni kwa nini wanadharau Wanatarime, na kwa hili napenda kujua ni lini wachimbaji wadogo watapewa maeneo yao yaliyofanyiwa *exploration* na siyo changa la macho. Nani kwa ukubwa gani na maeneo yapi? Na ni lini hawa wachimbaji wadogo wadogo watapewa?

Mheshimiwa Spika, inaudhi sana, sababu wakati mwekezaji anakuja aliwakuta wananchi (Wanatarime) wakichimba madini na kuendesha biashara pamoja na maisha yao kama nyumba imara za kujengwa kisasa, watoto kusoma bila matatizo yoyote na pia shughuli zote za kijamii.

Mheshimiwa Spika, nilizungumza na Waziri wa Mambo ya Ndani kuhusu unyanyaswaji wa wananchi katika Mgodi wa *North Mara* ni nini *justification* ya uwepo wao. Nashukuru Waziri ameahidi kulishughulikia na kwamba wanaondoka, cha ajabu wiki iliyopita vijana wamepigwa risasi na kuvunjwa miguu na mikono na baadaye polisi kuwatelekeza tena bila hata kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria na kwa nini wanawapiga risasi tu, na hawa vijana hawatumii silaha na walikuwa wanaokota mawe kwenye *pits* zilizomwanga. Huu sio uongozi, tunashachoka sana naomba majibu ya yote haya wakati wa majumuisho na nini kinafanyika kuhakikisha kama mikataba inafungwa. Hakuna huduma yoyote ya jamii, kama shule, hospitali, barabara, umeme vyote vimeduwa ni usanii tu!

Mheshimiwa Spika, pia napenda kujua mkataba wa *North Mara* uliacha *loop hole* yaani bila kuainisha *boundary* za Barrick kuchimba, maana tumeshuhudia *extension* za ajabu wakisikia madini yapo hapa wanaenda, kama ulivyokuwa kwenye kitongoji cha Mirito na ni dhahiri kabisa maeneo ya Nyamongo sehemu nyingi ni madini, sasa hapa wanadhibiti vipi wizi huu. Serikali inakosa pato kwenye madini na ni bora yafungwe kwa kweli ni aibu tupu. Eti wanafaidika baadhi *at the expense of others*.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa Waziri aniambie nin nini kigezo cha mgao wa kupeleka umeme vijijini, maana naona kuna *bias* kwenye mgawanyo huu. Haiwezekani Mkoa wa Mara unapata *allocation* kwa Majimbo matatu tu na tena ni kijiji katika Jimbo la Tarime na Hospitali ya Ranya na upendeleo kwa Jimbo la Bunda *why?* Au ni *distribution by comrade just* Waziri? *This is not fair at all.* Igawe umeme kwa uwiano sawa na ukizingatia mafuta yanapanda bei inabidi umeme ndio *solution*.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, nchi yoyote yenye umeme legelege maendeleo yake huwa ni ndoto. Nazungumza hivyo kwa sababu ninaona matatizo katika sekta hii ya nishati. Umeme ndio kila kitu katika maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote na jinsi nionavyo mimi umeme utabakia historia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ianglie suala hili kwa macho mawili. Tumeshuhudia jinsi gani ajira zimepotea kwa baadhi ya Watanzania, viwanda vimepunguza uzalishaji kwa asilimia kubwa sana na kuwaacha Watanzania wakirandaranda bila kujua mustakabali wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, mgao wa umeme umekuwa wimbo kila mwaka katika nchi yetu, pamoja na mipango mizuri ya Serikali kumaliza matatizo ya umeme lakini utekelezaji wake naona umwkuwa mgumu. Kwa nini sasa Serikali ioneeri haja ya kubadili chanzo cha umeme kisiwe maji bali iwe kitu kingine mfano, gesi, upopo. Tuna mikoa ambayo inazalisha upopo wa kutosha kipindi chote cha mwaka kama Mkoa wa Dodoma, kwa nini Serikali haloni sasa wakati umefika kama upembuzi yakinifu umefanyaika kwa nini sasa umeme usizalishwe? Na kama bado Serikali ina subiri nini ili Tanzania iondokane na giza nene?

Mheshimiwa Spika, nimeona utitiri wa miradi ya umeme katika hotuba ya Waziri hii maana yake nini? Kuna miradi ambayo ina zaidi ya miaka kumi na mpaka sasa haijaanza kuzalisha umeme. Naomba niombe Serikali kwa nini isiweke msukumo kwenye mradi mmoja kuliko kuendelea kukumbatia miradi ambayo haina tija?

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie sasa kuhusu madini ambayo tunayakanyaga kila kukicha na kulala juu yake. Tanzania imejaliwa kuwa na madini ya kutosha lakini wananchi wake ni maskini wa kutupa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikikumbatia wachimbaji wakubwa amba o kazi yao ni kudandia maeneo ambayo wachimbaji wadogo wadogo wanayavumbua na baadaye kuwafokuza wachimbaji hao amba o ndio wazawa katika maeneo husika. Maeneo mengi ambayo Serikali imeingia mkataba na makampuni hayo makubwa ya uchimbaji ambayo yanakandamiza wananchi wanaozunguka maeneo ya migodi tunajionea madini mengi yakisafirishwa nje ya nchi yetu bila Serikali kupata chochote, huku baadhi ya viongozi wachache wakineemeka na familia zao huku Watanzania wengi wakibakia hawana chochote mkononi.

Mheshimiwa Spika, makampuni haya yamekuwa yakikwepa kodi na Serikali inaendelea kuyaangalia. Hii inadhahirisha jinsi gani Serikali haikuwa makini kwa mfano mgodi wa Buzwagi, wafanyakazi wa *TRA* waliopo pale wanaishi ndani ya *compound* ya mgodi na wanapatiwa kila kitu na mpaka usafiri pia. Sasa hapa kuna kazi kweli? Madini yetu yataendelea kuibiwa na mwisho wa siku Tanzania itabakia na mashimo, mali hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isifute leseni kwa makampuni haya ya uchimbaji ili sasa utaratibu wa kuititia mikataba upya ifanyike kwa makini.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii mpaka nipate majibu ya kuridhisha kutoka kwa Wizara husika. Wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakinyanyasika sana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke jitihada mahususi ili wachimbaji hao wadogo wadogo waweze kujidesha wenyewe na ikiwezekana wapewe mikopo ili waweze kununua vifaa kwa ajili ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakiondolewa bila kulipwa fidia, naiomba Serikali ihakikishe au ipange utaratibu amba o itasaidia wachimbaji wadogo kulipwa fidia mara maeneo yao ambayo yanakuwa wanachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu wa kuajiri watoto wadogo kwenye migodi ya madini. Ninaomba Serikali ihakikishe suala hili la ajira kwa watoto inakomesha katika maeneo ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. Wizara hii haina mipango mizuri. Umeme umekuwa taabu kubwa sana. Wakati wa ukame tunaambiwa hakuna

maji katika mabwawa, wakati wa mvua pia hakuna umeme sababu hazielezwi kikamilifu. Tunatumia pesa nyingi sana katika sekta ya umeme bila kupata umeme. Uchumi wa nchi umedorora kutokana na ukosefu wa umeme. Utata mkubwa umezingira mikataba yote ya umeme. *Richmond, Dowans, IPTL* na kadhalika, kwa nini? Mbona nchi hii imejenga barabara nyingi nzuri? Tumejenga shule nyingi, zahanati nyingi? Tunapiga hatua katika huduma za maji! Kwa nini umeme ndio tatizo? Wizara hii ina matatizo sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini tazama uozo uliopo katika sekta ya madini! Nchi imeuzwa, wageni wamekamata maeneo yote yenye madini, mikataba mibovu inatawala. Nchi haipati kitu katika mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja, pia ni rai yangu kuwa viongozi wote wa Wizara (Katibu Mkuu, Naibu Katibu, Makamishna, Wakurugenzi na kadhalika) waonDELETE. Tujiipange upya. Vinginevyo Wizara hii itatuangamiza kabisa. Serikali ionyeshe makucha yake. Tusioneane haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na siungi mkono hoja.

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri yeye binafsi pamoja na Naibu Waziri kwa juhudhi wanazozifanya ili nchi iondokane na tatizo la umeme. Pamoja na pongezi hizo naomba niwasilishe ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi katika mpango kabambe wa kusambaza umeme wa Gridi vijiji, pamoja na juhudhi zilizochukuliwa na Wizara kusambaza umeme vijiji katika mikoa 16 bado tunahitaji kuona mkakati Kitaifa na siyo mikoa 16 tu. Naomba Mheshimiwa Waziri kupata mpango huo Kitaifa ukoje?

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme kwenye maeneo/vijiji vikubwa Kiwilaya, kuna vijiji vikubwa sana katika Jimbo langu la Kalenga ambavyo vinakaribia kuwa miji midogo kwa ukubwa wake lakini havina umeme. Vijiji hivyo ni Magulilwa, Mgama, Kiiponzelo na Wasa. Vijiji hivyo vina shule, zahanati, sekondari, taasisi kubwa za dini na taasisi zingine za jamii pamoja na shughuli nyingine za uchumi. Naomba kujua kama vitapewa umeme lini?

Mheshimiwa Spika, naomba tena nikupe mchango wangu mwingine katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bajeti ya Fedha kwa Wizara. Ni kweli kuna nyongeza ya *Capital Development Vote* ya shilingi bilioni 141.5 kutoka shilingi bilioni 184 of last year (2010/2011) mpaka shilingi bilioni 325.5 ya mwaka 2011/2012. Hoja yangu kuu hapa ni kwamba bado Bajeti yetu haionyeshi kipaumbele chetu kwamba ni umeme ukilinganisha na Bajeti ambazo Wizara zingine zimepewa ni kubwa kuliko hii ya nishati na umeme. Tunahitaji mpango wa haraka kutafuta fedha ili mahitaji ya kuwekeza kwenye umeme. Kuna mkakati gani kulikabili hili?

Mheshimiwa Spika, suala la udhaifu wa Taifa kuwekeza kwenye vyanzo vya umeme vilivyopo. Tanzania ina fursa kubwa sana kuliko Mataifa mengine ya Afrika katika vyanzo mbalimbali vya umeme kama ifuatavyo; makaa ya mawe, maji, upepo, gesi na kadhalika. Je, kwa nini hatukuwa na mipango endelevu kuanza mwaka 2006 wakati dalili za upungufu wa umeme zilizanza. *There are too many excuses which the Ministry should now avoid for the interest of the country.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa sheria, kanuni na sera za madini mbalimbali nchini, kuna dalili kubwa ya upungufu wa sheria na *regulations* kuhusu mambo muhimu ya umiliki, utafutaji na uuzaaji (*marketing*) ya madini mbalimbali yanayopatikana nchini mwetu. Nitatoa mfano mmoja hapa kuhusu madini ya *Uranium*. Je, ni kwa nini watu wanachimba haya ambayo ni *highly classified* bila nchi kuwa na *regulations* muhimu ambazo zinalekeza masharti, usalama, utaratibu na wapi iuzwe nani kwa kufuata usalama gani?

MHE. SHAFFIN A. SUMAR: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti imeainishwa mikoa kadha ambayo itafaidika na mpango wa usambazaji umeme vijiji kupitia REA ukifuatilia kwa mfano mkao ambao natokea mimi Mkao wa Tabora ni Wilaya mbili tu ambazo zimetengewa Bajeti ya kupewa umeme hata hivyo katika Wilaya hizo mbili ni vijiji vinne tu ambavyo vitafaidika, kwa mantiki hiyo kama umeme utasambazwa kwa vijiji vinne kwa mwaka kwa mkao ina maana ifikapo mwaka 2015 ni vijiji vichache sana vitakuwa vimepatiwa umeme wakati jimbo langu la Tabora Kaskazini lina vijiji 99. Naishauri Serikali longeze kasi ya kusambaza umeme na iendelee na Mikoa ambayo imeshaanza utekelezaji.

Pia naishauri Serikali kwamba kwa kuwa Serikali imeshaongeza bei ya mafuta ya taa basi hizo fedha za ushuru wa ziada wa mafuta ya taa zitumike kwenye kusambaza umeme vijiji pia Serikali ilikuwa inapoteza takriban bilioni 25 – 33 kwa mwezi kutokana na mafuta na kwa sasa uchakachuaji utapungua hivyo Serikali kupata fedha za ziada ambazo awali zilikuwa zinapotea, ni bora hizo fedha zitumike kusambaza umeme vijiji.

Mheshimiwa Spika, pia imefahamika kwamba bomba la gesi asilia linaloleta gesi kutoka *Songas* tayari limefikia ukomo wa usafirishaji wakati mahitaji bado ni makubwa na kuna mpango wa kuongeza kuweka bomba lingine la kusafirisha gesi asilia lakini kama bomba jipya litakuwa na ukubwa kama bomba liliopo ina maana baada ya miaka mitano au sita tutajikuta tena kwenye hali hii ya kushindwa kutumia gesi kutokana na bomba kuwa dogo ukilinganisha na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, miradi ilioainishwa ya kufua umeme ni mingi sana kiasi ambacho inanipa wasiwasi na utekelezaji wake, nashauri Serikali ijikite katika miradi michache lakini mikubwa ili tufanikishe haraka lakini pia Serikali inatakiwa iwe na mtazamo wa mbali na kujua hali itakavyokuwa miaka ya usoni tangu mwaka 2005 ilishafahamika kwamba hali ya uzalishaji umeme itakuwa tatizo lakini Serikali haikupanga au kufanya maandalizi ya kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mungu kwa kutujalia kuhudhuria Bunge hili Tukufu nami nichangie machache.

Mheshimiwa Spika, nianze na Wizara hii kwa kuwa Bajeti ni chombo cha kutekeleza sera na maamuzi ya Serikali kufikia malengo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, sera hii huonyesha Serikali inavyowezesha kukusanya mapato, rasilimali mbalimbali na kuzitumia maeneo yanayochangia kufikia malengo ya nchi pamoja na vipaamble vitakavyopangwa wakati maalum pamoja na maendeleo yanayoainisha Dira ya Taifa 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala, Mpango wa Taifa, MKUKUTA II na Malengo ya Milenia.

Mheshimiwa Spika, nianze na madini kwa kuwa Serikali ina chombo cha kutunza mazingira katika maeneo ya migodi, kwa Bajeti iliyotengwa na matumizi ya fedha kwa ajili ya ukarabati endelevu wa mazingira niungane kwa Bajeti hii ili kuzuia utoroshaji wa madini na ukwepaji wa kulipa mirahaba na kutathimini thamani ya madini yaliyozalishwa kupata mirahaba stahiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ndio yenye dhamana ya nchi hivyo sina budi niseme ichukue fursa sasa ya kuwadhamini vijana wapate mafunzo ya elimu ya juu ya uchumi wa madini na ukaguzi na udhibiti wa mapato ya madini kwa mwaka hasa wale ambao ndiyo kwanza wanaanza uchimbaji madini.

Mheshimiwa Spika, huko Wilayani Kondo mwaka 2009/2010 kuna eneo ambalo limefumuka dhahabu hasa kwenye mpaka wa Kata ya Suruke eneo la Tungufu kutokea Kata ya Kondo Mjini eneo la Mtaa wa Maji ya Shamba, hivyo uchimbaji huo ulipelekea aliyejekwa Mkuu wa Wilaya, Mpembwene kutamka hali ya kiusalama hivyo alisitisha uchimbaji uliojitozea holela pamoja na wachimbaji hao kulipia vibali vya muda na kupelekea wachimbaji wadogo wadogo kuachwa bila kujua hatima ya uchimbaji huo watapata lini baraka za kurithiwa na wananchi wa Kondo na vijana wapate kunufaika na uchimbaji na uuzaji wa dhahabu hiyo kuiletea Serikali ya mapato na nchi kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nishati na Madini afike huko na kutoa maelekezo kwani hakuna mtaalam yeote aliyefika hapo kuelewesha uchimbaji huo unahitaji wachimbaji wakubwa au wadogo wadogo, kwani kuko kimya tu na wananchi wanataka washirikishwe na si watoke nje ya Wilaya yao kama ilivyotokea mwanzo walikuwa wachimbaji kutoka sehemu mbalimbali kuchimba dhahabu na kuondoka nayo bila Serikali kupata mapato wala wilaya haijanufaika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali na Wizara kwa kuwa Chuo cha Madini kipo hapa Dodoma na ndiyo Makao Makuu ya nchi yetu na Wilaya ya Kondoaa ni Makao Makuu yake hivyo wataalamu hao wawezeshwe kufanya kazi zao za uchunguzi madini hayo kuwaachia wananchi wanaoishi eneo husika kwani ni wazawa wa hapo Kondoaa wanufaika na kuwaunganisha kwenye vikundi na kurahisisha azma ya Serikali ya kuwawezesha.

Mheshimiwa Spika, niongelee umeme, ulianza kupatikana kati ya miaka 1982 huko Kondoaa. Umeme umekuwa ni kero kubwa kwa nchi nzima lakini tuangalie na maeneo mengine ambayo yanaweza yakaleta tija kwa Taifa letu na kuweza kuongeza pato kwa kuharakisha maendeleo hasa kwa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, wilaya ya Kondoaa ni wakulima wa zao kuu la biashara kwa kuitia zao hili la alizeti na ufuta, kungekuwa na umeme hasa kwenye kata zinazotoa kwa wingi zao hili basi naamini tungeinua kilimo hicho kukawa na kukamua mafuta ya alizeti na ufuta yanepatikana kwa wingi na bei ingepungua hasa kwa wanunuzi wa rejareja na wa jumla. Hivyo umeme wa Wilaya yetu umeanza kata ya Kondoaa Mjini na maeneo ya karibu tu na kata hiyo lakini maeneo mengi hayana umeme na ukaelekea Wilaya mpya ya Chemba hivyo ulifuata njia hiyo na kuitia Wilaya ya Kiteto kata tano tu kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, ningependa Wizara iwashakikishie wananchi wa Wilaya hiyo itapatiwa lini umeme wa kutosha na hasa ukizingatia wilaya hii pia ina watu wanaotakiwa watumie umeme huko vijiji na vitongoji kwani hakuna nishati mbadala hasa wakati huu wa utandawazi ukizingatia bei ya mafuta ya taa ghali na huku tunawahitaji wananchi vijiji wasiharibu mazingira kama vile ukataji kuni/mkaa na wa matumizi mengine. Serikali iwaangalie wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na mpango wa wafadhili wa MCC Wilayani Kondoaa kupeleka umeme kutokea Kondoaa Mjini kuitia kata ya Suruke, Tungufu, Mlua, Chemchem, Iyoli, Kingale hadi Gereza la King'ang'a kwa ufadhili huo mpaka leo hii haujakkamilika hivyo Wizara ifutatilie na ijue tatizo ni nini na ni lini umeme huo utapatikana?

Mheshimiwa Spika, sitounga mkono hoja hii iwapo umeme hautapatikana Wilayani humo na tamko la uchimbaji madni utatolewa lini ili wananchi hao wanufaika na matunda ya nchi yao?

MHE. SAID R. BWANAMDOGO: Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa mwaka 2010/2011 naomba maeneo yafuatayo yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta ya taa, ingawa Serikali ilikuwa na nia njema ya kuongeza bei ya mafuta hayo, lakini bado kuna haja ya kuangalia upya uamuzi huo kwani wananchi wetu wengi wanatumia sana nishati hiyo na uwezo wao ni mdogo sana. Mpaka muda huu wananchi wengi hasa Jimbo la Chalinze, wameumizwa sana na uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ufuaji umeme, ni kweli kuwa Serikali imepanga kufua umeme katika miradi mbalimbali. Kwa maoni yangu badala ya kutawanya sana fedha hizo kwenye miradi mingi ambayo inaweza isikamilika, ni vema Serikali ikaamua kuweka nguvu kwenye miradi michache ambayo inaweza kukamilika na kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha, ni vema Serikali ikapeleka fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali ya umeme. Ukamilishaji wa miradi kwa wakati utakisaidia sana CCM kushinda tena kama kawaada yake katika chaguzi mbalimbali zijazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogo wadogo, Serikali iendelee kuwapa uwezo wachimbaji wadogo ili waweze kuyapata madini mbalimbali. Kule Chalinze kuna wachimbaji wadogo wadogo na madini ya *Green Tormaline Sarfire* na kadhalika. Naomba Wizara ishirikiane na wataalam waliopo wilayani katika kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, chumvi kuingizwa kwenye kundi la madini, kwa mtazamo wangu si jambo zuri na wala halina mantiki yoyote kwa chumvi kuingizwa kwenye kundi la madini ukiondoa chumvi inayotoka Uvinza ambayo ni sahihi kuitwa madini, chumi nyingi inayotoka kwenye Bahari ya Hindi haistahili kuitwa madini kwani mchakato mzima wa kuipata hiyo chumvi ni wazi kabisa kuwa haistahili kuitwa madini.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuiweka chumvi kwenye kundi la madini kuna kodi mbalimbali zinazoingizwa kwenye hiyo chumvi na hivyo kuifanya chumvi iwe ghali sana. Ni vema, kwa kuzingatia kuwa chumvi huliwa na watu wengi wakiwemo maskini pia, kuondoa chumvi kwenye mlolongo wa madini.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, kwanza naiopongeza Serikali kwa juhudii kubwa za kuishughulikia suala la umeme, lakini ninao ushauri huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue mradi mmoja kwa wakati mmoja, ukiangalia katika hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, anaeleze miradi kumi kwa wakati mmoja.

- (a) Miradi wa kufufua umeme wa *Mnazi Bay MW 300*;
- (b) Mradi wa kufua umeme wa *Songas Fungu MW 230*;
- (c) Mgodi wa mradi wa kufua umeme Kiwira *MW 200*;
- (d) Mradi wa kufua umeme wa *Ngaka MW 400*;
- (e) Mradi wa kufua umeme Mchuchuma *MW 600*;
- (f) Mradi wa kufua umeme wa *MW 63* wa Rusumo;
- (g) Miradi ya kufua umeme ya *Stigler's Gorge MW2100* na Mpanga *MW165*;
- (h) Mradi wa kufua umeme wa Rumakali *MW 222*; na
- (i) Mradi wa Dharura wa kufua umeme Dar es Salaam na Tanga.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isianze na miradi ya kufua umeme ya *Stigler's Gorge MW 2,100* na Mpanga *MW165* kuliko kuchukua miradi kumi kwa wakati mmoja na usiishe mradi hata mmoja. Mradi huu utazaa na *MW 2100*, wakati uhitaji wetu ni *MW 500*, kwa nini kutapanya hela huku na huku na wakati tukiweka nguvu sehemu moja tunaweza kufaulu na kulinda fedha zetu na kupata usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Nkenge Rais alituahidi kwamba umeme katika kata za wilaya hii zitaongezwa kata tano kufungiwa umeme na kata zenyewe ni Buyango, Nsunga, Ishunju, Ishozi na, Gera. Kuna barua toka kwa Waziri akieleza kuwa umeme utaletwa, barua inazungushwa kila mahali, kila nikifanya mikutano inaletwa barua hiyo. Je, Serikali inasemaje juu ya barua hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi wamefunga nyaya za umeme na kwa bei kubwa sana, kama kata ya Kitobo walitozwa shilingi 400,000 wakielezwa kuwa tataletewa umeme, umeme haujaletwa nimeshangaa kupata habari kuwa wananchi wa vijiji wanatakiwa kuchangia shilingi 60,000/= tu lakini sasa hivi wananchi wametoa 400,000/= na umeme hawajapata.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleza kuwa sitarudi Nkenge bila kupata jibu na ukizingatia kuwa katika Bajeti hii haiongelei kijiji hata kimoja hakijawekwa, kuna vijiji vingine ni *trasforma* tu na hata hivyo havikuwekwa, kuna umeme kutoka Uganda unapita juu ya Nsunga na Mtukula, wamechoka hawatakulali kuendelea na giza.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Spika, awali namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo kwangu hapa katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba nielekeze mchango wangu katika hoja hii, kwenye wachimbaji wadogo wadogo, wachimbaji wengi wadogo ni wazawa katika nchi na wengi wapo katika maeneo ya migodi ya wachimbaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, kutohana na hali hii ni dhahiri kwamba wananchi hawa wananyimwa haki zao kwa sababu hawashirikishwi na wachimbaji hawa wakubwa. Jambo ambalo ardhi hii na kilichomo ni haki yao.

Mheshimiwa Spika, kwa matokeo hayo yamesababisha wananchi kupoteza imani na Serikali yao, jambo ambalo linasababisha uvunjifu wa amani na utulivu uliopo na kufikia kupoteza maisha ya wananchi hao. Kwa mfano mauaji ya raia huko Nyamongo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naishauri Serikali kupitia Wizara husika iandae upya mikakati ya kuweka njia bora ya usimamizi utakaoleta tija kwa wananchi na maeneo yanayozalishwa madini. Kwenye misitu ya hifadhi ambayo ipo karibu na wananchi vijiji ardhi zinazohodhiwa na Serikali ambazo wananchi hawa ni haki zao.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka huu, mfuko wa Bajeti walitengewa wachimbaji wadogo shilingi 1,189,630,000 kwa ajili ya kuwasaidia ni ndogo mno ukilinganisha na mahitaji makubwa ya wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima ya Bunge lako hili Tukufu, naomba niishauri Serikali mambo yafuatayo:-

- (a) Wananchi waliopo katika uchimbaji waongezewe fedha hizi; na
- (b) Wananchi waliopo maeneo yanayoelekezwa walipwe fedha kabla ya wawekezaji hawaanja shughuli zao za uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu naomba nimalizie juu ya mradi wa uendelezaji wa gesi ya Songosongo na Mnazi Bay. Mradi huu umetengewa kiasi cha shilingi 8,373,000,000. Hata hivyo kati ya fedha hizo shilingi 1,820,000,000/- ni kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha polisi Songosongo na shilingi 5,173,000,000 ni kwa ajili ya ruzuku kwa kampeni binafsi ya *Went Worth Resources* ya kuuza umeme Mtwara wa Lindi ili iuze umeme sawa na bei ya *TANESCO*. Miradi hii miwili haihusiani kabisa na gesi ya Songosongo na Mnazi Bay.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliyo mbele yetu ya Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nytingine kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, naomba nianze kwa kutoa mchango wangu katika sekta hii kama ifutatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uzalishaji umeme nchini, pamoja na kuipongeza Serikali kwa jitihada zote za kuweka mipango ya kuzalisha umeme na kupunguza tatizo la umeme nchini naomba kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilichukulie tatizo la umeme kama tatizo la dharura na kuchukua hatua thabiti kwa kutafuta mkopo wa fedha kwa ajili ya kuendeleza mipango ya kuzalisha umeme wa kutosha ili tuondokane na tatizo hili.

(b) Umeme vijiji, katika mwaka fedha 2010/2013 Serikali itenye fedha za kutosha ikiwezekana asilimia 50 ya Bajeti yote ili kuwe na fedha za kutosha kusambaza umeme katika vijiji vyote vyenye kuzalisha mali na kuchangia katika Pato la Taifa.

(c) Serikali iangalie upya gharama za kuunganisha umeme katika makazi ya watu hasa wale wa vijiji wenyewe kipato kidogo.

(d) Serikali ifanye kila linalowezekana kusambaza umeme katika zahanati na vituo vyote vya afya ili kuweza kupunguza vifo vya wanawake na watoto wanaofariki kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini na wachimbaji wadogo wadogo, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, wachimbaji wadogo wadogo kuwa wamekuwa wakikosa fursa ya kutumia rasilimali zao wakati wageni wakichukua wao binafsi na nchi zao kitu ambacho kimeleta mgogoro kati ya wawekezaji na wananchi wazawa amba ni wachimbaji wadogo wadogo wa madini.

Mheshimiwa Spika, ushauri, Serikali ichukue hatua za haraka za kuhakikisha inatenga maeneo yenye madini na kuwakabidhi wananchi wanaozunguka maeneo yenye madini waweze kuitumia rasilimali yao kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeshindwa kumudu jukumu hilo kubwa la Kitaifa katika kuleta manufaa makubwa kwa Taifa la Tanzania. Kimsingi mabadiliko makubwa yanahitajika ili kumpa nguvu Mheshimiwa Waziri. Suala hili siyo la Wizara peke bali linahitaji wadau wengi katika kufanikisha.

Mheshimiwa Spika, aidha, inaonekana jitihada zinazofanyika bado hazitoshi kutatua tatizo hili la msingi. Katika kuleta mafanikio yenye tija kwa Taifa nashauri mikataba iliyofanywa katika sekta ya madni irudiwe upya kwani kuna uhalifu mkubwa, mikataba mingi inaonekana kuwanufaisha wawekezaji zaidi kuliko hali halisi ya mategemeo ya Watanzania. Je, Serikali ipo tayari sasa kuona wananchi wazalendo na hasa wanaishi katika maeneo yenye uchimbaji wa madini wanaandaliwa mazingira ya kuwawezesha kuchimba madini? Je, Serikali haioni kuwa kuwawezesha wananchi wa Tanzania na hasa wanaozunguka maeneo ya migodi wanapatiwa maeneo ya kuchimba madini badala ya kupewa wawekezaji pekee?

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme ndiyo pekee inayotoa ajira kwa vijana wengi kwa kuanzisha miradi midogo midogo ambayo vijana hujajiri. Aldha, yapo maeneo mengi hapa nchini ambayo Watanzania wamewekeza, viwanda vingi vinasimama kuzalisha kutokana na tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbarali ni mionganoni mwa maeneo makubwa ya kilimo cha mpunga. Ni lini Serikali itasaidia kupatikana kwa umeme maeneo ya vijiji vya Mlangali – Uturo – Ukwavila, Igurusi – Utengule, Ilongo - Igalako ambayo yana uzalishaji mkubwa wa zao la mpunga lakini wanashindwa kuwekeza kwa kuweka mitambo mikubwa au viwanda vya ukoboaji kwa kukosa umeme? Je, Serikali haioni maeneo haya ungepatikana umeme vijana wengi na akina mama wangepata ajira?

Mheshimiwa Spika, naomba nijiridhishe ni lini maeneo hayo yatapata umeme ili na mimi niweze kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linalofanya nchi hii isifanikishe mipango mbalimbali ikiwemo madini na nishati ni kutokuwa na ufuatilaji wa karibu, kutofanya tathmini ya mikataba na maamuzi mbalimbali yanayofanywa na Serikali. Nashauri umakini uwepo katika maamuzi na tathmini ifanyike mara kwa mara.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Waziri Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Adam Malima, uongozi mzima wa Wizara kwa matayarisho na uwasilishaji mzuri wa Bajeti yao ya mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba hii katika suala la gesi asilia ambayo kama itatumika vyema inaweza kwa kiasi kikubwa sana kubadilisha hali ya umeme Kitaifa kwa sababu ya utajiri mkubwa wa chanzo hiki cha nishati. Changamoto kubwa katika gesi asilia kwa kutoa mchango wake kwa kutumika kama chanzo cha nishati ni suala la usambazaji toka katika visima (vyanzo) hadi kwa watumiaji wakiwamo mitambo ya kuzalisha umeme. Hivyo basi jitihada za dhati zinahitajika katika kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi, kwa kuwa na wawakilishi/wakandarasi zaidi ya mmoja.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie katika suala la umeme vijiji, kwanza naipongeza sana Wizara kwa kuanza kutekeleza mradi wa kusambaza umeme vijiji katika baadhi ya vijiji katika Jimbo langu la Ulanga Magharibi. Ombi langu katika mradi huu ukamilike katika kipindi kifupi maana wananchi kwa muda mrefu wameteseka kwa kukosa huduma hii jumboni.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa katika umeme vijiji ni gharama kubwa za uunganishaji umeme majumbani kwa watumiaji. Naomba na kuishauri Wizara na taasisi ya TANESCO na kadhalika kupitia upya gharama za uunganishaji umeme majumbani ili hata wanyonge nao waweze kufaidi matunda ya nchi na kunusuru mazingira ya maeneo yetu ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niitaarifu Wizara kwamba tayari katika maeneo nyeti katika Jimbo lango Ulanga Magharibi (maeneo ya vyanzo vya maji) wachimbaji wadogo wadogo ambaao baadhi tayari wanavyo vibali wameanza kuchimba na kuathiri mazingira bila hata kuanza uchambuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa Bajeti yake hasa kwa uwasilishaji mzuri, ingawa hana lolote kwa ajili ya Kyerwa na Karagwe, pamoja na ahadi nzuri zote za Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, nakumbushia umeme wa Kyerwa na Karagwe. Mheshimiwa Waziri, suala la umeme Kyerwa analielewa vizuri na ahadi ilikazia baada ya Mheshimiwa Rais kulitamka wakati wa mkutano mkubwa pale Nkwenda Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wa *T/N* wasibugudhiwe, wasaidiwe waelekezwe.

MHE. BRIG. JEN. MST. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja iliyowasilishwa baada ya kupata maelezo ya kuniridhisha kuhusu tatizo la umeme lifuatalo.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Lushoto katika Jimbo la Mlalo umeme ulifikishwa Mlalo sambamba na mradi huo umeme ulikuwa ufikishwe pia katika Tarafa ya Mtae ambayo ni maarufu kwa uzalishaji wa matunda, mboga mboga na mbaao. *Design* ya mradi ilikwishatengenezwa tokea 1995 na wakati huo mradi huo ulikuwa ugharimu shilingi bilioni moja tu, ni miaka 15 tokea wakati huo. Cha kushangaza tokea wakati huo, mradi huo umesahaulika. Lakini miradi inaendelea kujengwa sehemu zingine za nchi yetu. Mwaka huu, wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha hoja yake pamoja na kuorodhesha vijiji vitakavyopata umeme chini ya miradi kama *MCC* na *REA* bado mradi wa kupeleka umeme Tarafa ya Mtae umesahaulika.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri wananchi wa Jimbo la Mlalo waielewe vipi CCM na Serikali yake? Wizara yako iliniahidi mradi huu kupeleka umeme Tarafa ya Mtae utatekelezwa lini? Nawasilisha.

MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR: Mheshimiwa Spika, umeme ni janga la Taifa, Serikali ichukue hatua ya dharura kumaliza tatizo hili sababu kuna Watanzania wengi ambao wamekopa pesa sehemu mbalimbali ili kuijendeleza. Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale tumeahidiwa kupata umeme mnamo mwaka 1999 Mzee John Malecela aliahidi mnamo mwaka 2008 mwezi wa nane Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima aliahidi mwaka 2009 mwezi wa tatu umeme ungewashwa. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete mnamo mwezi Agosti, 2010 aliahidi kuwa umeme utawaka na Waziri wa Nishati na Madini aliahidi kuwa mwezi Mei, 2011 umeme utakuwa tayari lakini hadi leo hii hakuna umeme. Naomba wajibiwe wana Nyagh'wale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini naomba kujua mikataba ya migodi ifuatayo iletwe Bungeni ili isomwe mikataba ni lini imeanza na itaishia lini ili Watanzania wanaoishi kando kando ya migodi hiyo wafahamu:-

- (a) *Geita Gold Mine;*
- (b) *Bulyanhulu Gold Mine;*
- (c) *Buzwagi Gold Mine;*
- (d) *Tulawaka Gold Mine;*
- (e) *North Mara Gold Mine;* na
- (f) *Golden Pride Gold Mine.*

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni Watanzania wangapi ambao wamedhurika na sumu za migodini ni Watanzania wangapi wamepigwa risasi na kuuawa na pia kujeruhija na kulipwa fidia?

Mheshimiwa Spika, napenda kujua kwa nini *Bulyanhulu Gold Mine* inalipa dola 200,000 kwa Halmashuri ya Kahama pekee kwa wakati. Uchimbaji umeelekea Halmashauri ya Geita kwa kilomita 25 za chini kwa chini?

Mheshimiwa Spika, napenda kujua kwa nini wanatoa ahadi halafu hawatekelezi kama kuchimba visima na kadhalika ahadi *KGM* waliahidi katika jimbo langu la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua kwa nini *GGM* waliahidi kusambaza umeme na kujenga sekondari lakini mpaka sasa zaidi ya miaka nane hawajatlimiza ahadi zao?

Mheshimiwa Spika, napenda kujua je, Watanzania wangapi wameajiriwa katika migodi niliyoitaja? Ni kwa nini wafanyakazi wa Kitanzania wanalipwa pesa za Kitanzania wakati wafanyakazi wa kigeni wanalipwa pesa za kigeni? Kwa nini wote wasilipwe dola kwa sababu dhahabu inauzwa kwa pesa za kigeni?

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko toka kwa wafanyakazi wa migodi kuwa pesa zao wanazokatwa kwa kuchangia mfuko wa *NSSF* haziwakilishwi kwa wakati je, ni kweli?

Mheshimiwa Spika, ni tani ngapi za dhahabu ambazo zimezalishwa na kusafirishwa nje ya nchi tangu uliopanzishwa uzalishaji katika migodi hiyo? Je, Serikali na Wizara ya Madini na Nishati ina taarifa kuwa mgodi *KGM* unazalisha madini aina ya *copper*?

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa leseni za utafiti na uchimbaji mdogo, leseni hizo zinatolewa kwa upendeleo zaidi kwa wageni na wazawa wanakuwa watazamaji hiyo ni hatari kubwa hapo baadaye kuwa na migogoro mikubwa hata mauaji. Naomba kutoa ushauri ya kuwa yatengwe maeneo ya wachimbaji wazawa kila kijiji ambapo kuna dalili ya kuwa na dhahabu.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka nipate majibu ya kuridhisha.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Nachukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa maandalizi ya hotuba ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji umeme, naungana na maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge na Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya tatizo kubwa la upungufu mkubwa wa nishati. Naungana nao kukubali kuwa tatizo la umeme ni janga la Taifa. Ukosefu wa umeme umeleta adha kwa wananchi, umeleta athari kubwa kwa uchumi, kuchangia ukosefu wa ajira, umesababisha gharama za uzalishaji bidhaa zimeongezeka hivyo bei za bidhaa zimepanda.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ifanye maamuzi magumu ya namna ya kumaliza tatizo la nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini juu ya maeneo ya utekelezaji katika sekta ya nishati, imeeleza miradi mbalimbali inayotegemewa kutekelezwa katika mkakakti wa kupunguza tatizo la umeme.

Mheshimiwa Spika, katika miradi yote hiyo iliyoitajwa (kuanzia ukurasa 16 – 20), ni mradi wa kufua umeme wa *Stigler's Gorge MW 2,100* ndio mradi pekee wenyewe *MW*nyingi sana kuliko miradi yote ambayo kama Serikali ingekuwa na dhamira ya dhati, ingewekeza katika mradi huu tu ambao ungeondoa tatizo lote la uhaba wa umeme. Ni kwa nini Serikali/Wizara ya Nishati na Madini kwa takriban miaka 50 ya Uhuru imeshindwa kabisa kutumia maporomoko hayo (*Stigler's Gorge*) kuzalisha umeme! Kwa kweli kwa hili Serikali imechelewa sana.

Mheshimiwa Spika, naipongesa Wizara ya Nishati na Madini kwa kukamilisha mradi wa umeme wa Somanga Fungu uliozinduliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Agosti, 2010. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Pwani, naishukuru sana mradi huu wa kutufikishia umeme katika maeneo ya Bungu, Muhoro, Nyamwage, Kindwiti, Kibiti, Utete, Tingi na Hospitali ya Mchukwi. Hata hivyo pamoja na huduma hiyo ya umeme kuufikia vijiji/maeneo hayo lakini kutokana na gharama kubwa ya uunganishaji umeme huo huduma hiyo hajjawafikia walengwa hasa wananchi wa vijijini. Hivi Serikali halioni gharama zinazoambatana na uunganishaji wa umeme ni kubwa na wananchi wengi wa vijijini hawawezi kumudu gharama hizo.

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa umeme Makao Makuu ya Wilaya na Vijijini. Naishauri sana Serikali kuititia *REA* kwa kuanza utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme katika maeneo ya Kiwangwa (Bagamoyo), Magindu (Kibaha), Kisarawe, Mwanambaya, Dundani na Mipeko (Mkuranga). Naendelea kuiomba Wizara ya Nishati na Madini kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais alilotoa wakati wa ziara yake Wizarani hapo la Wizara kupunguza gharama za uunganishaji wa umeme ili wananchi wa kawaida na vijijini waweze kupata huduma hiyo kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa bei na uchakachuaaji mafuta. Ninayo masikitiko makubwa ya kuendelea kupanda kwa bei za mafuta pamoja na Serikali kupunguza tozo mbalimbali kwenye mafuta hasa dizeli na petroli. Jambo linaloshangaza ni kuona bei mpya ya mafuta ya taa imeanza kutumika, wakati bei mpya ya dizeli na petroli haijaanza kutumika na bei ya mafuta hayo inazidi kupanda.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* kimsingi imeshindwa kabisha kudhibiti bei ya mafuta. *EWURA* imeshindwa kudhibiti bei kwa vile *EWURA* inafaidika sana kwa kupanda kwa bei za mafuta, inafaidika kuititia makusanyo ya mapato. Kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2009/2010 ya *EWURA* ukurasa 96 mapato yanayotokana na *petroleum* yalipanda toka bilioni 5.1 mwaka 2009 hadi bilioni 11.5 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, tunachoshuhudia *EWURA* ni kufanya kazi ya kutoa bei elekezi tu, kazi ambayo haina tija kabisa. Mapato yanayokusanya na *EWURA* hayana tija kwa vile hakuna uwekezaji wowote unaofanyika kutokana na mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kuona ni *SUMATRA* tu inayochangia kwenye mapato ya Serikali Kuu mfano kwa mwaka huu 2011/2012 *SUMATRA* imechangia bilioni moja ukurasa 74 wa kitabu cha *Volume I*, lakini hata hivyo *EWURA* pamoja na kukusanya mabilioni ya pesa, katika kitabu hicho hicho hakuna mahali popote pale panapoonyesha *EWURA* itachangia kiasi gani, hata kwenye Bajeti ya Wizara ya Nishati *Volume I* ukurasa 92 – 93 hakuna kiasi cha mapato yoyote toka *EWURA*.

Mheshimiwa Spika, kwenye ripoti ya mwaka ya *EWURA* (2009/2010) inaonyesha pesa nyingi zinatumika kwenye maeneo yasiyo na tija mfano safari za nje.

Mheshimiwa Spika, ni *EWURA* hii iliyokesha Serikali msaada wa *Euro* takriban milioni 28 zilizokuwa zitolewe kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa maeneo ya Msimbati, Mtwara kuunganisha umeme wa gesi kwa shilingi 60,000/=. Mpaka sasa Serikali haijamchukulia hatua yoyote Mkurugezi wa *EWURA* kwa uzembe mkubwa uliokosesha Serikali msaada huo. Mpaka leo wananchi wa maeneo hayo yanayotoa gesi huko Msimbati wamekosa matumaini ya kuunganishiwa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja hii endapo wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atatoa majibu ya kuleta matumaini kwa Watanzania.

MHE. DUSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Naunga mkono hoja hii kutokana na ukweli kuwa nishati ni nyenzo muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi. Umuhimu wa nishati unaweza kufananishwa na mishipa ya fahamu katika mwili wa binadamu, bila nishati ya uhakika uchumi hauwezi kukua na ni kwa msingi huu naona kuna umuhimu mkubwa wa kuunga mkono hoja hii pamoja na upungufu mkubwa wa Kibajeti wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa umeme wa uhakika mjini na vijiji una uhusiano wa moja kwa moja na jitihada zetu kama Taifa katika kupambana na umaskini iwe katika sekta za uzalishaji mali, kukuza ajira na kuongeza kipato kwa wananchi wanaojajiri katika sekta rasmi na zisizo rasmi, huduma za afya, upatikanaji wa huduma ya uhakika ya maji salama na hivyo kuepuka magonjwa, elimu katika mashule na kupashana habari kuititia matumizi ya redio na televisheni kwa masuala ya kiada na hata burudani.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa tumejisahau kuwekeza katika miundombinu ya kuzalisha umeme. Ni vema tukachukua hatua za makusudi sasa kuwekeza kwa nguvu zetu zote katika miundombinu ya kuzalisha umeme. Hii ni kutokana na ukweli kwamba umeme hususani vijiji kama ilivyo kwa barabara ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi. Hatuna jinsi, lazima tuwekeze katika kupeleka umeme vijiji, kwa sababu hii ni mojawapo ya njia za kuondoa umaskini, kwa sababu kwa kupeleka umeme vijiji tutaibua fursa nyingi za kiuchumi na uzalishaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewaaahidi wananchi wa Mkinga kuwapatia umeme kuititia *REA* tangu mwaka 2007/2008 katika vijiji vya Gombero, Mapatano, Bwiti, Kigongoi, Hemsambia, Daluni, Kwale na Mkinga wakati ambapo tayari baadhi ya maeneo ya Mkinga tayari umeme umeanza kupatikana, watu wa Mkinga wanaona utekelezaji wa ahadi ya kuwapatia umeme kwenye vijiji tajwa unakwenda polepole mno na wangependa kujua lini miradi hii itakamilika?

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mwakijembe imejengewa muundombinu ya umwagiliaji nao wangependa kujua ni lini umeme utafika kwao ili waweze kutumia vema fursa za kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, shule nyingi katika Wilaya ya Mkinga zipo mbali na umeme wa Gridi ya Taifa hivyo inakuwa vigumu kuzipatia umeme. Nashauri kupitia *REA* zifanyike jithada za makusudi kuzipatia shule hizi umeme wa mionzi ya jua ili tuweze wenzetu ambao tayari wana umeme. Mkinga tumesubiri kwa muda mrefu, kwa *speed* hii tunayokwenda nayo ya kupeleka umeme vijijini hatuoni ni vipi kwa kipindi kifupi kijacho tunaweza kupata umeme na ni dhahiri tunatazidi kuachwa. Ni aibu ilioje kuwa hadi leo hii shule zetu na vijana wetu wanashindwa kutumia kompyuta. Inasikitisha kuwa vijana hawa wanaomiliza elimu yao ya kidato cha nne bila kujua jinsi ya kutumia kompyuta, hii ni hatari. *Let us take electricity to our rural school. So that we can introduce computer literacy in our schools.*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuwa na mkakati madhubuti wa kuongeza uzalishaji wa umeme nchini. Lengo linaloonekana katika Mpango wa Taifa wa miaka mitano la megawati 2700+ bado ni dogo sana. Tusirudie kosa tulilolifanya kwa miaka 30 iliyopita. Lazima tuwe na lengo kubwa zaidi la kuwa na zaidi ya megawati 6000. Hii ni kutokana na ukweli kwamba katika nchi zinaloendelea mahitaji ya matumizi ya umeme yanafikia megawati 1000+; sisi tunazungumzia megawati 600+, kwa nchi nzima. Majirani zetu wa Kenya mwaka 2009 tayari walikuwa wamezalisha megawati 1200, kwa hali kama hii si ajabu kuona wenzetu wanapiga hatua za haraka katika ukuaji wa uchumi wa nchi zao hususan katika kuvutia uwekezaji wa kiviwanda.

Mheshimiwa Spika, hivyo tunapozungumzia mpango wa maendeleo hususan katika sekta ya nishati uangalie mbele zaidi tufikirie kuwa na ongezeko la zaidi ya mara kumi ya uzalishaji wa umeme tulionao leo. Hii ndio *challenge* tulionayo.

Mheshimiwa Spika, fedha tulizotenga kwa Wizara hii hazitosh, tunatakiwa *ku-invest* kwenye umeme sasa, huu ndio wakati wa kushirikisha sekta binafsi kwa miradi ya *Public Private Partnership (PPP)* kigugumizi katika hili kinatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, tunaposherehekeea miaka 50 ya Uhuru wetu tunajiuliza na kuangalia mbele kwamba miaka 50 ijayo tunataka kuwa na Tanzania ya aina gani? Tanzania ambayo ikifika usiku inashabihiana na ule usemi wa kutukejeli wa bara jeusi (*black continent*) kutokana na kutokuwa na maendeleo au tuwe na Taifa linalojivunia kupiga hatua ya maendeleo kiviwanda yanayogusa watu wote popote walipo iwe vijijini au mijini na kuwa na fursa sawa katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa Pato la Taifa na kuwa na uwezo wa kuishi maisha bora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utegemezi wa maji kama *source* pekee ya umeme. Kama tunavyofahamu, nchi yetu imekuwa ikitegemea maji kutoka mabwawa ya kuzalisha umeme ambayo yamekuwa yakitegemea mvua. Mabwawa haya yamejengwa muda mrefu tangu enzi za Uhuru na mengi yanasadikika kuwa yamekuwa na *siltation* ambayo inapunguza kina cha mabwawa hayo na hii ni kutokana na ukweli kwamba kipindi mvua zinaponyesha ukomo, mabwawa haya hujaa mfano Mtera na hivyo kulazimika kutapishwa maji ili kuepusha kupasuka kingo zake. Lakini cha kushangaza, baada ya muda mfupi tu, hata msimu mwininge wa mvua haujafika tunatangaziwa kwamba maji yamepungua na mgao wa umeme unaanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua hii ni sawasawa au ni *sabotage*, haingii akilini. Mabwawa kutapishwa na baada ya muda mfupi mgao wa umeme unaanza. Kwa nini yasijengwe mabwawa mengi ya kuhifadhi maji ya ziada ili baadaye yatumike wakati wa ukame?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyanzo vya maji vimeshindwa kutosheleza mahitaji ya umeme, vyanzo vingine kama gesi, makaa ya mawe (Kiwira) na chuma – Liganga, upemo (Kanda ya Kat) vitumike ili kulondolea Taifa janga hili la umeme.

Mheshimiwa Spika, matatizo mengi katika sekta ya madini na nishati yamekuwa pia yakichangiwa na usiri mkubwa unaokuwa katika mikataba inayoingiwa na watendaji. Ni vema mikataba hii na yote mingine iwe inawekwa wazi ili wananchi wote wajue na wafanye maamuzi sahihi kwa mali za nchi yao na hii inatakiwa ipitie kwenye Bunge ambalo ndilo wawakilishi wa wananchi. Mikataba hii imekuwa ikiingiwa na kugubikwa na wingu kubwa la rushwa maana mingi imekuwa ikisainiwa nje ya nchi (mkataba wa Buzwagi ulisainiwa Marekani), na hivyo matokeo yake ni kukiukwa vipengele vingi vinavyotakiwa kuelewa ili kuinufaisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi yenye madini, wananchi wamekuwa wakiishi kama wakimbizi katika nchi yao wenyewe. Maeneo mengi hayana hata service muhimu kama shule, umeme, hospitali, barabara na kadhalika lakini unaishi umbali mdogo tu toka eneo ambalo madini yanachimbwa. Wananchi hao wanachobaki nacho ni kifusi na si hicho tu, makampuni mengine kama Barrick, yamethibitika kumwaga sumu (inayotokana na kazi zao za uchimbaji dhahabu) kwenye vyanzo vya maji kwa mfano, Ziwa Victoria na matokeo yake wananchi wengi walipata madhara makubwa kwenye ngozi na wengine kufa. Si binadamu tu na hata wanyama wafugwao nao waliathirika kwa kiasi kikubwa. Naitaka Serikali kutimiza wajibu wake kwa kuhakikisha mikataba hiyo ya simu angalau inatoa huduma ipasavyo kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Spika, naungana na Kambi ya Upinzani kuitaka Serikali kutenga shilingi biliioni 150 kwa ajili ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya uzalishaji wa umeme toka vyanzo vidogo vidogo vya umeme na usambazaji wa umeme katika maeneo ya vijijini. Naungana na Kambi ya Upinzani pia kwamba chanzo cha nyongeza kiwe fedha zitakazotozwa na zinazoendelea kutozwa katika kodi ya mafuta ya taa takriban shilingi milioni 70 kama itaendelea kutozwa kwa mwaka mzima. Umeme vijijini utasaidia pamoja na mambo mengine utunzaji wa mazingira vijijini kwa wananchi kuondokana na kukata miti hovyo kwa ajili ya kuni na kuwapunguzia akina mama mzigo mzito wa kutembea umbali mrefu kutafuta kuni na hivyo kutulua na kuweza kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na hivyo kujiongezea kipato chao wenyewe na Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, bei ya kuunganisha umeme ambao pia si wa kudumu na haupo ni kubwa sana, gherama hii zinawafanya wananchi kushindwa kuunganisha umeme katika nyuma zao na hivyo kuendelea kuharibu mazingira. Naitaka Serikali iangalie suala hilo la gherama za kuunganisha umeme ili wananchi wengi waweze kunufaika na umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Spika, na mimi napenda kuchangia katika Bajeti ya Wizara hii ya Nishati na Madini mwaka wa fedha 2011/2012 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika upande wa nishati, kero ya umeme imekuwa kubwa sana kiasi cha kushusha uzalishaji katika Pato la Taifa. Umeme hata kama ni wa mgao basi Serikali au wahusika wangetoa muda maalum wa mgao huo ili watumiaji waweze kujipanga katika matumizi ya nishati hiyo, kama wanafunzi ambao wanahitaji kujisomea kwa ajili ya kufanya vizuri katika masomo yao kama wakijua muda nishati hiyo inapatikana wakati gani wataweza kujipanga hata muda wa mchana wasome kutumia mwanga wa juu. Hivyo hivyo kwa mafundi wa kuchomelea mbao wanategemea kazi hiyo tu kwa ajili ya kujipatia kipato. Bei ya mafuta iko juu sana kiasi kwamba hakuna mbadala kwa upande wao kila kitu hakishikiki *either electricity or fuel*. Mimi naomba Serikali ifanye utaratibu wa haraka wa kuleta umeme wa dharura hata kama kununua hizo mashine chakavu ambazo zitasaidia katika ku-boost nishati hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea suala la madini, kumekuwa na uonevu kubwa katika machimbo ya madini hapa nchini. Wachimbaji wadogo hawa wamekuwa wakinyanyaswa

sana na wachimbaji wakubwa. Mfano katika machimbo ya madini ya *Tanzanite* huko Arusha, kumekuwa kunatokea maafa mengi sana na wanaoathirika ni wanaozama migodini na bado kipato chao ni kidogo sana na isitoshe kumekuwa na maafa yanayotokana labda na mvua/mafuriko au kukosa hewa wakati wapo ndani ya migodi.

Mheshimiwa Spika, watu hawa familia zao hazilipwi baada ya ndugu zao kupoteza maisha. Vile vile wachimbaji hawa wamekuwa wakipekuliwa katika mili yao wakati wa kutoka katika mashimo hayo na imekuwa ni fedheha kwani vijana hao wanakaguliwa hadi sehemu za siri na sehemu ya haja kubwa eti kama wameficha madini hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba matajiri hao watumie vyombo vya kisasa vya kuwakagua wafanyakazi hao kuliko kuwadhalilisha na pia tabia hii inaweza kuwabadilisha tabia vijana hao na kuanza tabia zingine ambazo ni kinyume na maadili na kuwaleta athari katika afya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu kwa kuchangia hotuba ya Makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani ninachangia kama ifuatavyo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, upande wa madini, madini ni rasilimali isiyooza na muhimu sana ndio maana nchi za Iraq, Libya Kongo na kadhalika zina mivutano kutokana na nishati, madini na rasilimali walizonazo. Ndio maana Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere alisema madini hayaazi na ni muhimu yatunzwe mpaka tutakopata teknolojia ili yanufaishe vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na Sheria ya Madini (*The Mining Act 2010*) ambayo inaeleza namna gani inaratibu masuala ya madini lakini kuna mambo ya kutazamwa upya kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, leseni za utafiti, hizi huitwa *prospecting licence*, leseni hizi humfanya mwekezaji kufanya utafiti yaani *survey and trial mining* hivyo *trial mining* huhusisha uchimbaji. Naomba kupata majibu ya Wizara licha ya Serikali kutoa *Prospecting Licence PL 3233*, je, Serikali inajua watafiti hawa wanachimba kiasi gani hasa wakati wa utafiti? Maana utafiti unahusisha uchimbaji kwani hata katika hotuba ya Wizara sijaona katika utafiti madini yanayopatikana yanakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanja vya ndege katika maeneo ya migodi, sitaunga mkono hoja mpaka njue kwa nini na kwa namna gani Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inahusika vipi katika kodi na kukagua dhahabu kabla ndege hajiaruka?

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 inayoeleza kwamba itahusika katika uwekezaji wa madini na petroli kwa kuwa Wizara hii ina mambo mengi ningependa kupata majibu ni lini. Sheria hi itafanyiwa marekebisho ili uwekezaji huu uende *T/C* ili kupunguza mzigo kwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, mikataba mibovu ya siri na msimamo wa Serikali juu ya *IMF* na *World Bank*. Kamati ya *Richmond* mwaka 2007 ilitoa maoni kwamba mikataba yote mibovu iletwe Bungeni na iwe *accessible* kwa Wabunge, kwa nini hili halitekelezwi. Aidha, Serikali itoe msimamo kwa *IMF* na *World Bank (WB)* juu ya masharti wanayotupatia kwani Tanzania ni nchi iliyoongiza harakati za ukombozi Barani Afrika. Hivyo itoe msimamo juu ya masharti haya kwa mustakabali wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, jmboni Muhamwe, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema umeme utawaka Kibondo kabla ya mwezi Novemba, 2010 kauli hii ikarudiwa tena na Waziri wa Nishati na Madini mwezi wa pili kuwa ifikapo mwezi wa tatu, 2011 umeme utakuwa umewaka Kibondo lakini mpaka leo mwezi wa saba, 2011 umeme haujawaka hivyo Rais na Waziri wametoa kauli ambazo hazitekelezeki?

Mheshimiwa Spika, ubaguzi katika miradi Ibara ya 8 na 9 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 maelezo kuwa rasilimali za nchi hii zitagawiwa kwa usawa. Lakini leo hii Mawaziri wanajipendelea katika kupanga miradi ya umeme, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivyo siungi mkono hoja.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, awali ya yote siungi mkono hoja hii ya kupidisha Bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, umeme, katika hotuba ya Waziri imeonyesha maeneo, majimbo na vijiji ambavyo Mheshimiwa Waziri anaviombea fedha kwa ajili ya utekelezaji. Kinachoonekana ni namna watendaji wa Wizara hii wasiyyo makini na jinsi ambavyo waifanye Serikali ionekane inafanya upendeleo wa kimajimbo na umaarufu/upeo/cheo cha mtu.

Mheshimiwa Spika, rai yangu ni kuwa namwomba Waziri arejeshee watendaji taarifa ile wairekebishe na kuondokana na hisia mbaya zilizojitokeza mionganoni mwetu sisi Wabunge na ajisafishe ye ye Waziri pamoja na Serikali kamili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini tendo la uendelezaji/uso na tija wa kusafirisha mchanga wa madini kupelekwa nchi za nje, limewahi kuzungumzwa sana katika Bunge hili. La kushangaza hadi leo Wizara/Idara hata Serikali kwa ujumla inaendelea kupuuza mawazo ambayo yanatolewa na Waheshimiwa Wabunge kana kwamba inakuwa wanapiga porojo na hii inathibitishwa na watendaji wakuu wa Wizara hii wanavyosema; "waache wapige kelele tu ni kawaida Bajeti itapita tu." Maneno haya ya watendaji wa Wizara hii yanaonesha ni namna gani watu hawa walivyo washenzi wa kutojali maisha ya wanyonge wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, umeme wa *Geothermal* kwa kuwa Wizara imepanga kutumia zaidi ya shilingi billioni 4.8 kwa matumizi yasiyo na maelezo (*other operating expenses*) ni wakati muafaka kwa Wizara kupunguza matumizi haya na fedha hizi kuzielekeza katika vilima vya *Volcano* na Bonde la Ufa ili kuzalisha umeme. Nchi jirani ya Kenya wanatumia mfumo huu wameweza kuzalisha umeme hata ziada isitoshe hata *technology* yake ni nyepesi kuitumia na vilevile ni teknolojia ambayo haichafui mazingira.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, naomba katika majibu ya Serikali mpate majibu juu ya malalamiko ya wananchi Mkoani Kigoma katika sekta ya madini.

Kuna utata ulio mkubwa kwamba Barrick wamehodhi maeneo ya vijiji vya Kinazi, Janda, Muhunga, Malumbo, Kasangezi, Kasuku, Nyamori, Mahembe, Kalinzi. Hili jambo linatokana na wananchi wakienda kwa Afisa Madini wanajibu hawezu kuwapa leseni katika maeneo hayo kwa kuwa Barricks wamehodhi maeneo hayo. Naomba nipate majibu kwani hilo jambo lasumbua sana wananchi wanaotaka kuchimba madini.

Pili wananchi wameomba leseni za *PML* toka hawajapewa na wao wameomba leseni hizo za uchimbaji wa *copper* na sio madini mengine. Je, kwa nini Aafisa Ardhi anawazungusha kuwapa leseni hizo, leseni tatizo ni Mkoani Kigoma au liko Wizarani?

Mheshimiwa Spika, msamaha wa kodi katika mafuta kwa wachimbaji madini. Hili ni tatizo na Wabunge wameshasema sana kuhusu suala hili lakini Serikali ipo kimya, ifike wakati tulione hili na tuache kusamehe kodi kwenye mafuta kwa wachimbaji madini.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji madini ya urani, nashauri Serikali ikamilishe Sera na Sheria ya Uchimbaji wa *Uranium* (urani). Ili tuepuke matatizo yaliyopo hivi sasa kwenye sekta ya madini mengine.

Mheshimiwa Spika, tatizo la migogoro baina ya wachimbaji wadogo wadogo na wale wakubwa. Mfano mzuri ni mgogoro wa Winza Wilaya ya Mpwapwa ambapo toka 9 Julai, 2010 Serikali ilisema itamaliza mgogoro huo lakini mpaka sasa bado halijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naitaka Serikali ihakikishe inawatengea wachimbaji wadogo wadogo maeneo yao na iwave leseni ili kuondoa mgogoro baina ya wachimbaji wakubwa na wadogo. Rejea tatizo la Nyarugusu kama Serikali ni sikuvi basi isikilize kilio chao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa *MCC* Kigoma, ni jambo zuri kuona angalau Serikali inatilia mkazo tatizo la umeme Kigoma. Kwa kuwa Serikali itajibu swali langu la tarehe 13/7/2011 kuhusu mradi wa *MCC*. Serikali ilijibu eneo la Igamba tatu ndani ya mto Malagarasi imegundulika tutapata megawati 41 za umeme. Naishauri Serikali ijithabidi kutafuta pesa haraka ili mradi huo uanze mara moja kwani tutasaidia Mkoa kuwa na umeme wa uhakika na mikoa ya jirani ya Tabora, Rukwa na Katavi wanaweza kunufaika pia. Serikali itoe majibu ina mpango gani wa kupata pesa za ujenzi wa mradi huo mara moja.

Mheshimiwa Spika, umeme wa jenereta Kibondo na Kasulu nashauri Serikali ikamilishe kuweka nyaya ili iwe rahisi kwa wananchi kuvuta umeme katika nyumba zao na ni lini kazi hiyo itakamilika kwani wamechoshwa na giza.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, matatizo ya umeme yameanza zamani na hadi sasa inaonekana Serikali bado haijui wapi tumekosea na hivyo ndio maana tokea mwaka 1992 hadi hivi leo tunayo matatizo ambayo hayaonekani kumalizika.

Mheshimiwa Spika, wapo Wabunge wamependekeza mkataba baina ya *Songas* na Serikali uvunjwe. Mimi napenda kuweka sawa suala hili ili libakie katika rekodi. Matatizo ya umeme Tanzania kwa kiasi kikubwa yamesababishwa na mikataba mibovu inayokwangua uchumi wa Tanzania. Hata hivyo baadhi ya Wabunge wamependekeza kuvunjwa kwa mkataba wa *Songas*.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa sio kukatisha mkataba na *Songas* ila kama hawa *Hunton & Williams* kweli ni watu wazuri kwa Tanzania basi wawalazimishe *Songas* kubadilisha mkataba katika mazingira ya leo.

Mheshimiwa Spika, *PSA* ya kwanza *TPDC* kusaini kwa niaba ya Serikali ni uzalishaji wa gesi ya Songosongo. Tanzania haikuwa na uzoefu wa mikataba ya namna hii. Mkataba huu mmoja ndani yake imo mikataba 21, mfano *Songas/TPDC*, *Songas/TANESCO*, *Pan African/TPDC* na kadhalika. *Law Firm* hii ya Kimataifa bado inatumiwa na Serikali, inatumiwa na *TANESCO* inatumiwa na *Songas* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hawa *H & W* walishindwa kesi baina ya *TPDC* na *Adults* na kusababisha Serikali kulipa fedha nydingi kwa *Adults and Hunton & Williams*. Lini tutasoma makosa haya?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumsadia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini Bajeti hii ni vema isipitishwe ina makosa mengi. Nitoe mifano miwili, kwanza *TPDC* – Matumizi ya Kawaida ni shilingi 2,276,587,500/= ukitoa mishahara shilingi 1,308,615,800/=; Matumizi Mengineo ni shilingi 967,971,700/= lakini ukilinganisha na *REA OC* ni shilingi 15,802,498,100/= na ukienda upande wa Wizara jumla ya *OC* ni shilingi 34,766,803,300/. Lakini Bajeti nzima ya maendeleo ya *TPDC* ni shilingi bilioni tatu, je, tuangalie kweli itakidhi utafutaji wa mafuta, usambazaji wa gesi asili Dar es Salaam, hifadhi ya mafuta ya Taifa 20 millioni na uwekezaji katika miradi ya Mnazibay?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kitengo cha mazingira, kifungu hiki kinazo jumla ya shilingi 430,026,000/= lakini katika mchanganuo zinazoonekana ni shilingi 212,366,600/= ziko wapi shilingi 217,659,400/=?

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa ofisi yake kwa mwaka 2011/12 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, Wizara hii ni robo ya uchumi wa nchi yetu. Hivyo majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji, ni kheri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kuboresha na kuondoa mapungufu yanayojitekeza kila siku maana sidhani kuwa ni busara kukosoa tu bila kutoa suluhisho.

Mheshimiwa Spika, ni vema sote tukaelewa kuwa matatizo ya umeme yaliyopo sasa ni makubwa na ukubwa wake unatokana na historia ya nchi yetu kwa maana wakoloni hawakuwekeza hata kidogo katika sekta ya umeme. Tutafakari pia ongezeko la mahitaji ya umeme pia linatokana na ukuaji wa kazi wa uchumi wa nchi yetu. Lakini pia utamaduni wa kutokuheshimu sheria miongoni mwetu maana kwa kipindi kirefu tumekuwa wagumu sana katika ulipaji wa ankara za umeme ambaa ilipelekea Shirika la Umeme (*TANESCO*) kushindwa kuijendesha kwa ufanisi kutokana na ukata. Kwa maana hiyo haifanani hata kidogo kulinganisha Tanzania na nchi nydingine duniani. Lakini napenda nielewe tatizo la mikataba ya madini ambayo imerithiwa katika vipindi vilivypita, si haki kuwabebesha waliopo sasa kwa maana ni kheri tuwahukumu kwa dhambi walizotenda wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jimbo la Kilwa Kaskazini hatuna tatizo la mgao wa umeme ila matatizo yetu ni mengine kwa maana kuwa vijiji vingi kama Tingi, Mtandango, Miteja, Sinza, Manzese na Marendego ambapo *line* ya umeme imepita lakini hawajapata fursa ya kuunganishiwa. Halikadhalika pia katika eneo la Somanga ambapo umeme unazalishwa pamoja na agizo la Rais la tarehe 16.8.2010 kuwa wananchi wafungiwe umeme lakini mpaka sasa agizo hili halijatekelezwa ila imeonekana ni bora kuendelea kupoteza pesa kwa kuweka *Load Bank (Dumb Load)* na kulipa gharama kubwa kuliko kuwafungia wananchi umeme kuongeza matumizi, hivyo katika hili ningependa nipate majibu.

Mheshimiwa Spika, nimepitia Bajeti yote kwa upande wa *REA*, hakuna kijiji hata kimoja ndani ya Jimbo la Kilwa Kaskazini, Wilaya ya Kilwa na hata Mkoa wa Lindi kwa ujumla ambacho kitapata na kunufaika na miradi wa umeme vijijini. Huku ikikumbukwa pia katika maeneo ya Kipatimu, Chumo, Mingumbi, Njinjo na Kibata kuna mahitaji makubwa sana ya umeme kwa shughuli za kiuchumi na kushindwa kuzitumia vema fursa zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kutokea gesi ilipoanza kuchimbwa mpaka sasa sisi kama wananchi wa Kilwa hatujapata kuona faida yake kwa maana hakuna gawio (*royalties*) ama vinginevyo, huku maeneo mengine ya nchi yananufaika katika madini na kadhalika. Naomba hili nalo lipatiwe ufumbuzi wa haraka ili kuondoa kero na malalamiko kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki. Nakutakia kila la kheri naomumba Mungu atulinde sote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kushukuru kwa kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Na kwa kuanza nitaanza na masuala ya Jimbo langu la Gairo na hasa katika masuala ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe tarehe 26.6.2008 Mheshimiwa Rais alipotembelea Jimbo la Gairo, katika maeneo ya Makao Makuu ya Kata za Kibedya na Chakwale na kufanya mukutano Chakwale, Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kipekee katika maeneo hayo kupatiwa umeme na hasa kutokana na maendeleo makubwa ya hali ya kiuchumi kwa wananchi wa kawaida na idadi kubwa ya wananchi katika maeneo hayo ndipo Mheshimiwa Rais alitoa agizo la haraka kwa kupatiwa umeme kata ya Chakwale kuititia kijiji cha Ngiloli na Makao Makuu ya Kata ya Kibedya hadi Chakwale na vilevile kupeleka umeme katika Kata ya Rubeho kuititia vijiji vya Luhaji, Msingisi, Kwipipa na Rubeho yenye na Mheshimiwa Rais aliona umuhimu huo baada ya kuzingatia idadi kubwa ya wananchi wanaoishi katika maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na agizo la Rais lakini viongozi wengi miaka mingi maeneo haya yamekuwa yakipigwa kelele na hata Waziri wa Nishati na Madini kwa maagizo amefika na

amefanya mkutano wa hadhara na kuwaahidi wananchi wa Chakwale na Rubevo kupatiwa umeme haraka iwezekanavyo. Serikali kwa kuona umuhimu wa maeneo haya kupatiwa umeme tayari imeshafanya tathmini zote za upelekaji umeme, cha kushangaza mpaka leo Bajeti hii hajaonyesha sehemu yoyote ya upelekaji umeme katika maeneo hayo na sijui *REA* wanafata vigezo gani. Na hii inaonyesha wazi kushindwa kazi na kutimiza wajibu wao. Ukiangalia sehemu nyingi zilizopewa kipaumbele na *REA* zina watu wachache sana ukilinganisha na maeneo kama Rubevo na Chakwale ambapo umeme haupo mbali na maeneo hayo.

Nimeuliza maswali mara mbili hapa Bungeni na majibu yallionyesha matumaini lakini bado, maneno maneno hayatoshi kutoka *REA*, *TANESCO* kuititia Wizara yenyewe. Mimi sitounga mkono hoja hii mpaka nipate majibu ya kutosha. Ahsante.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta hotuba ambayo ina maelezo ya kina ambayo yametuwezesha Wabunge kupata michango ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, tukianzia na ukurasa wa 122 Wizara imeonyesha ni kiasi gani cha unafuu Serikali inapata kutokana na matumizi ya umeme wa gesi asilia ya Songosongo badala ya mafuta mazito. Kiasi hicho ni takriban dola za Kimarekani 400,000,000 kwa mwaka. Kwa mikoa ya Mtwara na Lindi kiasi cha unafuu kwa mwaka ni takriban dola milioni 12 kwa mwaka. Lakini umeme unaozalishwa ni *MW 18* ambazo zinazotumika ni *MW 12* tu. Matatizo mengine ni yale ya uchakavu wa miundombinu yanayopelekea *technical loss*, lipo tatizo la *poor billing system* ambalo linasababisha watumiaji wa umeme kulipia gharama kubwa za umeme pasipo sababu na hivyo kipelekeea kuongezeka kwa umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo napenda nichukue fursa hii kuishauri Serikali ichukue kile kiasi cha unafuu kinachotokana na matumizi ya gesi asilia ikiwekeze katika kuboresha sekta ya umeme na huu ndio ubunifu katika kutumia fursa tulizonazo kama Tume ya Mipango ilivyotushauri. Kwa Mtwara na Lindi kwa miaka minne tangu mwaka 2007 Serikali imeokoa *USD* milioni 48 hivyo zipelekwe huko kuunganisha umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 126 na 127 Wizara imetoe makadirio ya gharama za mifumo mbalimbali ya umeme. Ningependa kuishauri *TANESCO* iwe na kitengo cha ushauri ili iwasaidie wale wote wanaoomba kupata umeme na baadaye kushindwa kupata kutokana na gharama kuwa kubwa. Kwa mfano shule ya *St. Aquinas* ya Mtwara waliomba umeme na wakaambiwa kulipa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 100 na waliposhindwa wakaamua kuwatafuta Wachina wakawafungia umeme wa *solar* kazi ambayo ingefanywa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, vilevile mahakama ya Mitengo pamoja na Ofisi ya Kata ya Mitengo walipoomba umeme nao wameambiwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 20 hawa pia wangeshauriwa kutumia umeme wa *solar*. Shule ya Sekondari Sino pamoja na jela ya watoto hawana umeme kwa muda mrefu na hali wao wapo ndani ya Manispaa. Serikali iangalie utaratibu wa kuwapatia nishati mbadala kama *solar* kwa kutumia ule unafuu unaopatikana kutokana na matumizi ya gesi asilia ya Mnazi Bay.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nichangie kwa kifupi tu katika eneo la madini. Nilipokuwa katika Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira nilipata fursa ya kutembelea Migodi ya Nyamongo, Buzwagi na Geita. Wananchi karibu na maeneo haya walikuwa wakilalamikia nyumba zao kupata nyufa kutokana na milipuko ya baruti. Lakini kutokana na maelezo ya wahusika wa migodi walidai kwamba vipimo vya baruti walivyokuwa wakitumia vilikuwa ni vya viwango vya Kimataifa na hivyo haviwezi kusababisha nyufa.

Naiomba Serikali isipuuze kilio cha wananchi hawa kwani inawezekana vipimo hivyo vya baruti ni kwa ajili ya zile nyumba ambazo ni imara na pengine kwa umbali fulani kutoka kwenye makazi. Haiwezekani wananchi wa maeneo tofauti wakalalamikia tatizo hilo hilo la alia moja. Serikali ilitazame, isikae kimya.

Mheshimiwa Spika, mwisho naishauri Serikali iwe makini na utafiti wa mafuta hapa nchini kuhakikisha hayaibiwi kama ilivyokuwa kwa wanyamapori wetu katika mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la nishati limekuwa sugu, tata na ni janga la Kitaifa. Ukosefu wa nishati ya uhakika umesababisha kudorora kwa uchumi wa nchi yetu. Mikataba mibovu ambayo imekuwa ikifanywa na viongozi ndiyo imelisababishia Taifa hasara na upotevu mkubwa wa mabilioni ya pesa. Hali hii imechosha katika masikio ya wananchi ambaeo ndio walipa kodi kwa kutokupatiwa huduma au majibu ya kuridhisha kutoka kwa Serikali yao ambayo ni sikivu.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika madini yanayopatikana hapa nchini hayawanufaishi wananchi na hasa ikizingatiwa kwamba ni rasilimali ya asili na urithi na Taifa hili na wananchi wake. Wananchi wengi raia wa nchi hii wamekuwa wakinnyanyasa na hata kuuliwa wakiwa katika harakati za kujitafutia riziki.

Mheshimiwa Spika, nionavyo Mawaziri wahusika wa Wizara hii wameshindwa kuiendesha Wizara, hivyo basi wawajibike, wajiu zulu pamoja na viongozi wengine wenye uwezo wa kuongoza waiongoze Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuimarisha na kuboresha sekta ya nishati na kuungeza fungamanisho la sekta ya madini. Ili kuwawezesha wananchi kuendesha shughuli za maendeleo kwa ufanisi na kuungeza mchango wa sekta hizo katika Pato la Taifa. Je, kama ndivyo hivyo ni kwa nini Wilaya ya Hanang isiwe na miradi ya kupeleka umeme wakati vijiji vingi havina mwanga wa umeme wa aina yoyote? Vijiji ambavyo havina umeme ni kama ifuatavyo, Laghanga, Gawidu na Dajamed vipo jirani na Mkoa wa Singida kilomita tatu toka Ngamu na wana umeme.

Mheshimiwa Spika, Dangaida, Mulbadew, Basoku kuna umeme ni kiasi cha kusambaza umeme katika vijiji hivyo. Bassodesh, Gaghata, Gijetamuhog upande wa Babati kuna umeme ni kiasi cha kusambaza tu.

Hirbadaw, Mwanga, umeme upande wa Singida upo haizidi kilomita mbili lakini inashindikana kupeleka umeme toka Singa ya Iramba?

Gridi ya Taifa inapita kuelekea Babati lakini kijiji cha Gehendu, Mogitu, Gabadaw, Endasiwold, Barjomod, Getaghud, Masqaroda, Masakta mpaka leo hii hadithi, hakuna mradi unaofikirwa ili wananchi nao wapate umeme.

Kijiji cha Gisambaleng na Waranga, Qalosendo, Sirop na Ayaona umeme ukipita utasaidia sana kupampu maji, usagishaji (mashine za kusaga), *welding machine* ili vijana waweze kujiajiri. Mwanga unasaidia kwa kurahisisha maendeleo, je, Serikali inasemaje kuhusu suala la huduma wilayani Hanang?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, wachimbaji wadogo wadogo kukosa nguvu ya kuwezeshwa na Serikali ili waweze kujipatia kipato mfano Mwanga ya upande wa Hanang na kijiji cha Mwanga upande wa Singida (Iramba Magharibi) walikuwa wanachimba madini ya dhahabu sasa je, ni kwa nini hakuna kwenye kitabu cha orodha ya aina ya madini yaliyopo? Ukurasa 156.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MADEYE: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Waziri Wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana David Jairo kwa

jitihada kubwa wanazofanya kuongoza wadau wa sekta ya nishati kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa kero ya upungufu wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati, baada ya kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010/2011 na mpango wa 2011/2012 nimebaini yafuatayo:-

Katika mwaka wa fedha 2010/2011 kupitia *REA* Serikali ilitenga kiasi cha bilioni 7.6 kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye vijiji vya Jimbo la Arumeru Magharibi. Hata hivyo nimesikitika kuona kuwa thamani ya miradi inayotekelizwa na iliyotekelizwa na iliyopangwa kutekelezwa katika miaka miwili yaani 2010/2011 (Jedwali Na. 2) na 2011/2012 (Jedwali Na. 3) ni shilingi 454,000,000.00 tu ili kulinda heshima ya Serikali na Chama cha Mapinduzi, nashauri kuwa miradi iliyokuwa imeidhinishwa na ikatumika kufanikisha Kampeni ya Uchaguzi Mkuu 2010 itekelezwe. Hivyo naomba kuwa fedha zote zilizobaki kati ya shilingi bilioni 7.6 na shilingi milioni 454 yaani shilingi bilioni 7.1 zitolewe na zitumike kutekeleza miradi ya umeme vijijini kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Arusha (Jimbo la Arumeru Magharibi). Naomba Serikali itimize ahadi yake kwa kuhakikisha kuwa miradi iliyoidhinishwa 2010/2011 inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, nimefuatilia taritibu za ugawaji wa maeneo ya machimbo kwa wachimbaji wadogo na kubaini kuwa ugawaji hauwashirikishi wadau muhimu hususan viongozi wa wilaya bali hufanywa na Ofisi ya Madini peke yao. Utaratibu huo una mapungufu kwani umesababisha uchimbaji kufanyika bila kuchukua tahadhari za kulinda mazingira. Matokeo yake sehemu kubwa ya nchi hasa maeneo ya miinuko imeharibika.

Nashauri kuwa ugawaji wa maeneo ya machimbo ufanywe kupitia kamati zinazoundwa na wataalam wa Wizara pamoja na wawakilishi wa wilaya husika wakiwemo Madiwani na Wabunge wa Majimbo yanayohusika.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na wachimbaji wadogo wadogo wa Mpanda kilio chetu cha muda mrefu Wizara inafahamu. Kilio chao pamoja na kufika mara kadhaa katika ofisi na kuongea na kupewa ahadi nyingi na Mheshimiwa Waziri pamoja na kukutana na kuwatemeblea wachimbaji hao na kusikia Kilio chao lakini ahadi hizo bado kutekelezwa pengine huu ndio utamaduni na utendaji kazi wa Serikali hii ambayo kwao wachimbaji wadogo wadogo hawana thamani kwao, lakini napenda kuikumbusha Serikali hii imewekwa madarakani pamoja na kura za wachimbaji wadogo ambao wanaendelea kupuuzwa, matokeo yake sasa wanaletwa Machinga toka nje wanazagaa katika mapori yetu kwa kisingizio cha uwekezaji, nitapenda kupata maelekezo ya kina juu ya hawa Wachina na Waturuki ambao wamezagaa kule Mpanda na hata kufikia leo Waturuki wanapeperusha bendera ya nchi yao katika nchi yetu inakuaje sekta hii ya madini kuridhia na kuruhusu wageni kupeperusha bendera za Mataifa yao katika nchi yetu. Ni ujinga au umaskni wetu?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo ni kwa nini Mkoa wa Rukwa hadi sasa haujaunganishwa katika Gridi ya Taifa na kutokuwepo hata mradi mmoja wa nishati vijijini hivi dhambi na kosa letu Rukwa ni nini? Vlijiji vyote Rukwa vipo gizani lakini wananchi hawa wanahitaji umeme pia na ni kwa sababu hata miji iliyopo katika Mkoa wa Rukwa Sumbawanga, Namanyere Mpanda hawana umeme wa uhakika na hii inapelekea hata vijiji vilivyo kando kando ya miji hii haina umeme pia achilia mbali Namanyere ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naitaka sasa Wizara kupitia *TANESCO* kuhakikisha maeneo yaliyohitaji umeme katika Mji wa Mpanda *TANESCO* ianze kujenga njia za kusafirisha umeme ili uwafikie wananchi wengi katika mji wa Mpanda husuan kata ya Illembu, Shanwe, Misunkumilo, Kawajeuse, Nsemliwa na vijiji vya Kakese Mbugani Kata ya Kakese kupitia mfuko wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kujadili matatizo na changamoto zinazosababisha tuendelee na mgao wa umeme, umeme vijiji kutoenea vijiji kwa haraka na madini kuendelea kutupatia mapato kidogo kinyume na thamani yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa umeme wa kutosha, tumekuwa na miradi mingi mno ya uzalishaji wa umeme yenye megawati kidogo kidogo mingi ikiwa haizidi megawati 300 na mingi inazalisha chini ya uwezo wake. Kwa mfano *IPTL* imekuwa ikizalisha chini ya uwezo wake, Songas na Tegeta na Ubungo nayo imekuwa ikizalisha chini ya uwezo wake. Kama miradi hii inayotumia gesi asili na mafuta mazito ambayo tayari ipo na bado inazalisha umeme chini ya uwezo wake ni kwa nini tena tuendelee kuagiza mitambo mingine ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili na mafuta mazito Dar es Salaam na Mwanza? Nasema iliyopo kwa nini isiwezeshwe ili izalishe *full capacity* yake?

Mheshimiwa Spika, miradi hii midogo tuachane nayo kwa miradi ya muda mrefu na tuamua sasa tuwekeze *Stigler's Gorge* ili tuanze na uzalishaji wa *MW 300* na baadaye *MW 2,100*. Naamini *environmental impact assessment* ilishafanyika na kuonekana kuwa mradi huo hautaathiri wala kuharibu mazingira. Hata hivyo wenzetu wa Brazil na *DRC Congo* wana miradi kama hii kwenye hifadhi, nendeni mkajifunze huko na Serikali isiwe na woga wa kuamua kuwekeza *Stigler's Gorge*.

Mheshimiwa Spika, umeme vijiji bado tuna safari ndefu sana kama tutategemea Bajeti ya fedha za kodi ya wananchi. Miundombinu ya umeme vijiji kuititia *REA* inahitaji fedha nyini sana. Nashauri kwamba Tanzania inakadirwa kuwa kaya za vijiji zipatazo 6,600,000 na hivyo kuiongezea uwezo kifedha *REA* tumeamua tutunge sheria ya kutoza shilingi 500 tu kwa mwezi kila kaya ambapo kwa mwaka tutapata shilingi 39,600,000,000 na miaka mitano tutakuwa na shilingi 198,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa umeme umepita kwa kutumia ardhi ya Jimbo la Mwibara na kupelekwa Wilaya ya Ukerewe. Ni aibu kwa Serikali kutowapa umeme wananchi wa Mwibara ambapo ardhi yao imetumika, je, Serikali haioni hii ni aibu? Ni aibu kwa Serikali kutowapa umeme wananchi wa kijiji cha Bulamba – Mwibara ambapo kuna *ginery* ya kuchambua ambayo ni peke yake ina umeme, je, Serikali haioni hii ni aibu? Ni aibu kwa Serikali kutowapa umeme wananchi wa Mwibara ambapo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais mbele ya Nishati na Madini Mheshimiwa Ngeleja, je, Serikali haioni hii ni aibu?

Ni aibu kwa Serikali kutowapa umeme wananchi wa Mwibara wakati wenzao wa Jimbo la Bunda vijiji wanao umeme na katika Bajeti hii vijiji vitano vimepata umeme wakati Wilaya yetu ni moja, je, Serikali haioni hii ni aibu? Vitendo hivi vyote vilimkera Magembe Ngirya Aloyce wa Kijiji cha Kasahunga ambaye sasa ni marehemu kuamua kujunganishia umeme kutoka waya zenye umeme mkubwa na kufa hapo hapo. Ni lini Serikali itaondoa aibu hii?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini naishauri Serikali itazame upya maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza mikataba ya uchimbaji na utafiti wa madini itazamwe upya bila woga wowote kwani ina matatizo kuhusu ulipaji wa kodi na mirahaba. Mikataba ya madini ni ya kinyonyaji na ukandamizaji.

Mheshimiwa Spika, pili wachimbaji hasa migodi mikubwa wapewe ukomo wa uchimbaji wa mwaka (*maximum exploitation*) vinginevyo watachimba na kumaliza mali yote hata kabla ya muda wa mkataba kuisha.

Tatu ni vema Serikali ikawa na uangalifu juu ya *greenstone belt* Kanda ya Ziwa Victoria na kutazama upya suala la mchanga wa madini kwenda kusafishwa nje ya nchi. Kiutaalam madini ya dhahabu yana madini rafiki (*indicator minerals*) kama vile kopa na silver. Kitendo cha mchanga kupelekwa nje ni sawa na kupeleka madini ya dhahabu, kopa na *silver* wakati wawekezaji wanalipia kodi na mirahaba ya dhahabu tu. Kwa nini Kampuni isiyo na uwezo wa kuwa mitambo wa kusafirisha mchanga hapa nchini ipiwe mkataba?

Mheshimiwa Spika, nadhani kigezo cha Kampuni kuingia mkataba na Serikali ni lazima iwe na uwezo wa kifedha (mtaji) pamoja na teknolojia. Sipo tayari kuunga mkono hoja mpaka nipate maelezo ya kina juu ya hoja zangu. Ahsante.

MHE. WARIDE BAKARI JABU: Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini kwa uwasilishaji wake. Pia nachukua fursa hii kumshukuru Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme ilikuwa ikiendeshwa na *TANESCO* na *ZECO* kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kusikitisha *TANESCO* ilikuwa ikipandisha bei ya umeme bila ya kuwashauri na kuwashirikisha Shirika la Umeme za Zanzibar hii inasababisha kutolewana katika kuendesha biashara hii. *EWURA* iliamua kupatisha kodi au tozo hiyo ya abiria 168 kwa Wanzanzibar na 21.7 Tanzania Bara hivyo bila kushirikisha *ZECO* na kuwasababishia deni la 50 bilioni hizi zimetoka wapi? Wakati deni linalojulikana ni bilioni tisa tu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kuhusiana na gesi asilia inayozalishwa katika Bahari ya Hindi kwenye Kisiwa cha Songsongo. Naomba sana Serikali iangalie kwa kina mapato na faida ya kupatikana gesi hii ambayo hainufaishi wananchi wa Kisiwa hicho ambacho ni maskini sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kunufaisha wananchi kwa kuwawekea boti ya kisasa ya kuvusha abiria na mizigo kutoka Kisiwa cha Songsongo mpaka Kilwa Kivinje na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kisiwa hicho hawana hospitali ya kisasa wala shule nzuri au mahitaji mengine muhimu. Lakini pia ajira za vijana bado ni ndogo ukilinganisha na wageni wanaopata ajira. Hivyo tunaiomba Wizara iangalie hili ili wananchi wa eneo hili na wanaozunguka wafanufaike.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba tarehe 18 Julai 2011, Waziri Mkuu alitoa hoja ya kuahirisha mjadala wa makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa kipindi kisichozidi wiki tatu na hoja hiyo iliafikiwa na Bunge hili.

Aidha, Kamati ya Uongozi ilikutana siku hiyo tarehe 18 Julai 2011 na kupanga mjadala huo uendelee leo Jumamosi tarehe 13 Agosti, 2011 baada ya Kanuni zinazohusika kutenguliwa.

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka pia kwamba tarehe 5 Julai, 2011, Bunge lilitengua Kanuni kadhaa zinazohusu utaratibu katika Kamati ya Matumizi ili kuleta uwiano sawa wa michango na kupata idadi kubwa ya wachangajji na hivyo kuepuka kuingia kwenye utaratibu wa *guillotine*. Kanuni zilizotenguliwa ni kama ziufuatazo:-

Kanuni ya 101(5) ilitenguliwa kwamba muda wa Mbunge kuomba ufanuzi wa Waziri wakati wa mjadala wa Kamati ya Matumizi usizidi dakika tatu badala ya dakika tano. Kanuni ya 103(4) ilitenguliwa kwamba muda wa kutoa hoja kuondoa shilingi usiozidi dakika tatu badala ya dakika tano. Kanuni ya 103(5) ilitenguliwa kwamba muda wa kuchangia hoja ya kuondoa shilingi usizidi dakika mbili badala ya dakika tatu.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka pia kwamba tarehe 1 Agosti, 2011 Bunge pia lilitengua Kanuni kadhaa ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge ambao ni waumini wa dini ya Kiislamu waweze kuswali na kufuturu kwa wakati muafaka na wakati huo huo kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, miongoni mwa Kanuni zilizotenguliwa ni kama ifuatavyo, Kanuni ya 28(2) ilitenguliwa ili kuruhusu Bunge katika kipindi cha asubuhi liendelee na shughuli zake hadi saa saba na dakika kumi na tano mchana badala ya saa saba mchana. Kanuni ya 28(4) ilitenguliwa ili katika kipindi cha jioni shughuli za Bunge zianze saa Kumi na zahirishwe inapofika saa kumi na mbili na dakika thelathini jioni badala ya saa moja na dakika arobaini na tano usiku.

Kanuni ya 104(1) na Kanuni ya 104(2) zilitenguliwa pia ili kuondoa mamlaka ya Mwenyekiti kuiongezeza muda Kamati ya Matumizi wakati wa kuitisha mafungu.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yaliyosababisha mjadala wa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kuahirishwa ni mazito na yamevuta hisia za Watanzania kuanzia ndani hadi nje ya Bunge, hivyo ni muhimu sana kwa Waheshimiwa Wabunge kupata muda wa kutosha wa kuhoji maeneo yote ili kujiridhisha na kazi iliyofanyika na itakayofanyika. Kwa mantiki hiyo, upo umuhimu wa kutumia taratibu zetu zinazoainishwa katika Kanuni za Bunge kuhusiana na mjadala katika Kamati ya Matumizi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kama nilivyoeleza hapo awali, Kanuni zinazohusu mjadala katika Kamati ya Matumizi zilitenguliwa na Bunge hili, na kwa kuwa Kanuni zetu hazijaweka utaratibu wa kutengua utaratibu uliotenguliwa, hivyo basi kwa mamlaka niliyopewa na Kanuni ya 2 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, napenda kuelekeza utaratibu utakaofuatwa katika kikao cha leo tarehe 13 Agosti, 2011 kama ifuatavyo:-

Utaratibu katika Kamati ya Matumizi utakuwa kama ulivyoainishwa katika Kanuni husika za Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 kwamba muda wa Mbunge kuomba ufanuzi kwa Waziri itakuwa ni dakika zile zile tano na siyo tatu na Mbunge asiporidhika na maeleo ya Waziri anaweza kusimama mara ya pili. Muda wa kutoa hoja kuondoa shilingi utakuwa ni dakika zile zile tano na siyo tatu na muda wa kuchangia na kujibu hoja ya kuondoa shilingi utakuwa ni dakika zile zile tatu na siyo mbili.

Waheshimiwa Wabunge, mtiririko wa shughuli za leo utakuwa kama ifuatavyo:-

Kwanza, mtakumbuka kwamba kabla ya kuahirisha tulishafunga uchangiaji wa mtu mmoja mmoja, kama isingekuwa siyo matatizo ya kuomba iahirishwe Naibu Waziri ilikuwa aanze kutoa ufanuzi halafu afuate mtoa hoja. Kwa hiyo, kwa leo pia tutafanya kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, ataanza Naibu Waziri wa Nishati na Madini ambaye atachangia hoja kwa dakika zake kumi na tano au zaidi kama Waziri wake ataamua kumwongeza dakika kutoka katika muda wa Waziri wa kuhitimisha hoja.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nirudie hapa, Waziri anachangia hoja ama anajibu hoja zetu kwa muda wa saa moja, Naibu Waziri wa Wizara ile anachukuliwa kama ni mchangiaji, kwa hiyo ni dakika kumi na tano, lakini Waziri anaweza akachukua dakika zake sitini na za Naibu Waziri kumi na tano zikawa sabini na tano akamgawia vile anavyofikiria anapenda kumgawia. Kwa hiyo, ndiyo tuna maana hiyo, naomba hilo zoezi mlifanye ili kusudi tuweze kuwapangia muda utakaohusika.

Waheshimiwa Wabunge, halafu atafuata Waziri mtoa hoja ili ahitimishe hoja yake. Kisha, Bunge litaingia katika Kamati ya Matumizi na kuendelea na hatua zinazofuata kama inavyofafanuliwa katika Kanuni za Bunge, Toleo la 2007.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyoeleza tutarudia utaratibu wetu uliopo kwenye Kanuni anayetaka kuhoji atatumia dakika tano kwa mara ya kwanza, kama atataka kurudia tena kuuliza atatumia dakika tatu. Kama mtaondo shilingi atakayeondona shilingi atakuwa na dakika tano, kama wenzake watataka kumuunga mkono katika hoja yake watatumia dakika tatu na vile vile yule atakayetaka kujibu atajibu kwa dakika tatu. Kwa hiyo tunarudia utaratibu uliopo kwenye Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, hii inatuwezesha kuwa na muda mwangi wa kuihoji Wizara hii vizuri mpaka muda utakaohusika. Tunategemea kwamba itakapofika saa saba na nusu kama tukiwa kwenye Kamati, nitaongeza dakika thelathini kama itakuwa lazima tufikie saa nane. Ndiyo maana tumeweza kujivuta hivi kwa sababu kazi kubwa itakuwepo kwenye Kamati ya Matumizi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo maelezo yangu kuhusu utaratibu wa kikao cha leo, isipokuwa ikumbukwe tu kwamba kuanzia Jumatatu Tarehe 15 Agosti, 2011 tutendelea na utaratibu ule ule kama ambavyo Kanuni husika za Bunge ziliviyotenguliwa.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo maelezo yangu. Sasa nitamwita Naibu Waziri, mmekubaliana dakika ngapi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Thelathini.

SPIKA: Naibu Waziri dakika thelathini na Waziri dakika arobaini na tano.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa Rehema, mwangi wa Ukarimu kwa kuniwezesha kuwa hapa mbele yenu leo kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yetu kwa mwaka huu 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kabla sijaendelea kwanza niwashukuru wazazi wangu, Mama yangu mzazi alikuwepo hapa leo lakini naona hajafika, naomba nimshukuru *post mostly* marehemu Baba yangu, bado nafuata nyayo zake na natarajia huko aliko ananitazama na ananiongoza. Naomba nimshukuru Mke wangu Mpenzi Naima, barafu wa moyo wangu, kipozeo cha moyo wangu na watoto wangu Amina, Ali, Adam, wako wengi, Abdallah, Mariam, Amin, Sambarat, Zulkifli. Naomba niwashukuru ndugu zangu, wadogo zangu, shemeji zangu wote wapo pale juu wamewakilishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wapiga kura wangu kwa kunirejesha kama Mbunge wa Mkuranga kwa kura nydingi na nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kunitfea kuwa mgombea wake wa Mkuranga na wananchi wameridhia.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniamini katika nafasi hii ya Naibu Waziri wa Nishati na Madini, naomba niwashukuru sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kutuongoza na kutushika mkono siku hadi siku, nakushukuru sana Waziri Mkuu. Mwishi, naomba nimshukuru Mheshimiwa William Ngeleja Waziri wa Nishati na Madini kwa ushirikiano tulikuwa nao katika kutekeleza majukumu haya magumu sana. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyopo mbele yetu ya makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini, wakati wa kufanya tahmini ina maeneo makubwa lakini yapo mengine ambayo Waziri nitayasemea kwa ufupi na mengine atayazungumzia yeye kwa urefu pamoja na kuwatambua Wabunge waliochangia.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja mbalimbali, ipo hoja ya dharura tunayokabiliana nayo hivi sasa ya umeme, ambayo ataizungumzia Waziri mwenyewe na namna ya kukabiliana nayo.

Mheshimiwa Spika, wakati Wabunge wanachangia hoja zao mbalimbali na hoja za maandishi zaidi ya 185 jambo lilioljitozea ni namna ambavyo miradi ya Vijiji ya utekelezaji wa kupeleka umeme vijijini inavyoendelea. Jambo lingine liliikuwa kuhusu gharama za uunganishaji wa *TANESCO* lakini pia na matumizi ya gesi asilia katika kuondoa kadhia ya matatizo ya nishati ya umeme tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, upande wa Madini tulikuwa na masuala ya wachimbaji wadogo, tulikuwa na mapato yanayotokana na madini ambayo katika mgawanyo wetu hayo mengine atayazungumzia Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako nianze kuzungumzia hoja. Katika upande wa madini hoja ambayo napenda kuizungumzia ni suala la *STAMICO* kuwezesha ili iweze kusimamia uwekezaji wa Serikali katika sekta ya madini ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna tutakavyoona, kwanza Serikali itaendelea kuiwezesha *STAMICO* kwa hapo ilipokuwa, miaka mitatu iliyopita ilikuwa *ICU*, sasa hapa ilipo inakwenda vizuri, lakini tumekubaliana pia kwamba yale maeneo ambayo tunadhani ni *very critical also strategic mining areas* za nchi badala ya kuzitenga tu ziwe *openly*, mtu unakuja unapata *mining license* yako unaondoka, tunesema maeneo haya yatengwe kwa ajili ya *STAMICO*, ili Mwekezaji atakapokuja kutoka huko anakusudia kufanya uwekezaji katika maeneo yale, kwanza kabisa apitie katika eneo hilo lakini atakumbana na *STAMICO* sasa kwa niaba yetu sisi wote, watawasilisha hoja ya *free carried interest* kwa maana ya maslahi yale au hisa zitakazokuwa za Watanzania kwa niaba ya Watanzania wote zitamiliikiwa na *STAMICO*. Utaratibu huo, ni kwa wale ambao wanaonekana kwa sasa hivi wanataka kuja kuwekeza Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa mwaka jana ilikuwa ni mgogoro kidogo, nakumbuka hata tulipokwenda kwenye *mining Durban and Cape Town*, wawekezaji na wafanyabiashara wakubwa wa madini walitaka kuanza kulifanya kuwa ni jambo kubwa lakini tulismama *delegation* iliyokuwepo pale tulijenga hoja za kutosha na kusema kweli katika hili hatutatetereka kwa sababu ni namna pekee ya kuhakikisha kwamba na sisi huko mbele maslahi yetu katika sekta ya madini yanaangaliwa kwa karibu zaidi kwa kuwa na ushiriki wa karibu.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni kuongeza uwazi na usimamizi wa rasilimali za madini, gesi asilia, mafuta katika *natural resources* mbalimbali ambayo ni kupitia utaratibu wa *AITI*. Utaratibu huu unahusu kuwa na uwazi zaidi kuhusu mapato lakini na malipo yanayotokana na makampuni mbalimbali yanayoshiriki katika sekta hizi mbalimbali na sisi kama Tanzania tumesharidhia mkataba wa *AITI* na pamoja na Serikali tumebaini mambo mbalimbali lakini bado taarifa za *AITI* zinaendelea na tunaendelea vizuri katika hilo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyininge ilikuwa kwamba Serikali isitishe hatua za utafutaji na uchimbaji wa madini ya Urani hadi ikamilishe maandalizi ya kisera, kisheria, kikanuni na kitaasisi ambayo yatahakikisha kunakuwepo na maandalizi ya msingi yatakayohakikisha umiliki wa migodi hiyo nchini unanufaisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya 1998 iliyofutwa na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ya sasa, zinaruhusu uwekezaji katika madini ya aina yote yakiwemo madini ya urani. Utafutaji wa madini ya urani unaruhusiwa kisheria na Sheria na Kanuni za utafutaji na usafirishaji za nchi za madini ndio hizo ambazo sasa hivi zinafanyiwa kazi. Shughuli za utafutaji wa Urani zina Sheria ya Madini kama tulivosema, lakini pia usimamizi wa Urani una Sheria ya Mionzi, *Atomic Energy Act* na Kanuni za madini ya mionzi (*The mining radiation Minerals Regulations*). Kwa hiyo, taratibu za menejimenti ya madini ya urani, maana ina awamu mbili, kuna awamu ile ya kwanza ambayo ni madini ya *uranium*, halafu awamu inayofuata baada ya *development process* ile inakuwa sasa ni *source of energy* na kwa maana hiyo sasa, hiyo yote imezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa uchimbaji mdogo nchini, ni hoja ambayo ilijitokeza kwa Wabunge walio wengi, Serikali inatambua umuhimu wa sekta ndogo ya uchimbaji mdogo wa madini, uchimbaji mdogo umekuwa ni chanzo cha kutoa ajira na kipato kwa Watanzania walio wengi. Mfano, Serikali tumeamua kutenga maeneo kwa ajili ya uchimbaji mdogo na kuanzisha Mfuko wa kuwasaidia wachimbaji kupata mitaji. Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo lakini siku hizi pia kuna ule mradi wa *sustainable mining resources* ambao unakusudia pia ujieleze huko ili kuboresha hali za wachimbaji wadogo lakini pia kuwafungulia namna ambazo wanaweza wakafanyakazi yao katika mazingira yaliyo bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Wachimbaji Wadogo unaendelea, kwa sasa Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kusaidia vikundi vyta wachimbaji wadogo kama ambavyo tumeweza kueleza katika Bunge lako, ambako *STAMICO* pamoja na kampuni za *TAN Discovery* ya Kilimo *NG Supplies Limited* zimepewa jukumu la kutoa huduma kwa wachimbaji wadogo. Bado mchakato wenyewe umeanza *it is in preliminary stage* mwaka jana zilitengwa shilingi 1.3 billion lakini zikatoka shilingi 600 milioni lakini bado ni jambo ambalo *it is in process* na tulitarajia kwamba tutaendeleza kuwekeza pesa katika Mfuko huu, lakini pia labda baadaye tutatengeneza mfumo wa wadau wengine wa sekta ya madini kuchangia katika Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi waliochangia kwa kuongeza Wabunge kama 30 kama tulivyosema hoja zile za maandishi zilikuwa hoja karibu 185 na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atawatambua walioleta hoja hizi pamoja na wale waliochangia kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha lakini pia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, wachangiaji ni wengi kidogo.

Mheshimiwa Spika, sitawataja wachangiaji kwa kila hoja isipokuwa nitajaribu kujielekeza kwenye hoja zenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la migogoro ndani ya maeneo ya uchimbaji na Serikali inaendelea kutatua migogoro na kuboresha mahusiano baina ya wamiliki wa migodi na wananchi wanaozunguka migodi kadri inavyojitokeza. Kuna suala la Kijiji cha Nyarugusu kule Busanda ambako ni kijiji kilichoanzishwa ndani ya maeneo yenye dhahabu. Utengaji wa maeneo hayo na maeneo yanayozunguka ni sahihi, tumekubaliana, lakini ni ngumu, kijiji kimesimama pale na kuna maeneo labda kuna uchimbaji ambaao unakuwa hauko kwenye mfumo wa leseni. Lakini tumekubaliana tutenge leseni kwa sababu kuna maeneo ya Mgusu, kuna maeneo mengine kule Ruangwa na Nachingwea, kuna watu ambaao wameshakaa kwenye maeneo hayo mpaka wanajukuu. Leo ukija ukisema waondoke inakuwa ngumu kidogo hasa kama uchimbaji wenyewe ni uchimbaji mdogo, ni bora zaidi kuwatengenezea mazingira ambayo yatawawezesha kufanya kazi yao katika mazingira mazuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna hatma ya wachimbaji wa *Tembo Mine* pia kule Geita waliondolewa, wachimbaji hawa walikuwa wanachimba bila ya kuwa na leseni, lakini Serikali itaendelea na utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya uchimbaji mdogo kadri itakavyowaridhia lakini na maeneo ya kuwapatia makazi wananchi hao wa *Tembo Mine*.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo pia ambalo tumeliona katika shughuli hii, ni utoaji wa leseni au watu wenye leseni za madini wanapokwenda kwenye maeneo bila kutoa taarifa. Sasa hilo tumelikuta nadhani kule Manyoni na maeneo ya Bahi kwa Badwel, tulipokwenda tumekuta malalamiko haya ya kwamba, kuna baadhi ya watu wanachukua leseni huku halafu akifika pale kijjini anavamia tu eneo lake anaanza shughuli zake bila kutoa taarifa, tuseme haya ni makosa. Ukipika una leseni yako lazima ukaripoti kwanza kwa Mkuu wa Wilaya mpaka ngazi husika, ili ukiwa unataka kufanya shughuli yako ya *exploration* lazima uanze kuwasiliana na wale walioko pale. Sasa ukienda tu wewe umetoka huko unavamia mashamba ya watu *it is wrong* na tumelisema hili na tunaendelea kulisisitiza na hata tulipokuwa tukienda kwenye ziara tumewaambia wananchi hivyo, isionekane ni jambo ambalo Serikali imeliridhia.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni masuala ya fidia na kuboresha mahusiano baina ya wamiliki wa migodi na wananchi wanaozunguka migodi, masuala ya fidia yanaongozwa kwa mujibu wa sheria zipo lakini pia tumeona kwamba kwenye menejimenti ya masuala ya fidia, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alinielekeza niende Buzwagi mwaka 2008/2009 kwenye kusimamia masuala ya mgogoro pale na pamoja na kwamba kuna masuala ya ule mgogoro wa fidia unagundua kabisa wazi kwamba kuna matatizo mengine, ni matatizo yanayotokana na wajanja wajanja kwenye pande zote kutaka kuwadhulumu wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa pale tumekubaliana kwamba labda pawe na usimamizi wa karibu wa Wizara, lakini pia tuliwajibisha Halmashauri, sekta ya ardh, maafisa mahusiano wa jamii na kadhalika ili mambo haya ya wananchi kudhulumiwa kwenye masuala ya fidia yasioneckane kama ni jambo linalojirudia sana.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lilitokeza pia ambalo lilikuwa linahusu marekebisho ya sheria kuleta manufaa kwa wananchi. Wabunge wawili au watatu wamelizungumzia suala hili. Sheria ya Madini ambayo tumeleta mwaka 2010 imeridhiwa hapa kwenye Bunge lakini *is a working progress*. Kwa hiyo, fikra yangu ni kwamba kwa sisi Wabunge hapa kwa sababu ndio tunaishi na wananchi, tunakwenda kwenye maeneo ya uchimbaji, tunakaa na makampuni haya kwa ujumla, pale ambapo tunaona sheria hii inatukwaza na haituelekezi kufikia malengo yale tunayokusudia, hakuna sababu ya kuendelea kuwa na vipengele hivi ndani ya sheria na sisi ndio Bunge tuendelee kuboresha sheria yetu ili ikidhi mahitaji yale ambayo tumeyakusudia.

Mheshimiwa Spika, kuna suala kule Mererani mwaka 2008, baada ya mafuriko kulikuwa na suala lile la mtaro wa Disuza Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka analijua vizuri kwa sababu tulikuwa wote kwenye kusaidia matatizo yaliyoko pale. Tumetenga fedha kwa utaratibu wa *re-allocation* kama tulivyosema jana kwenye Kamati kiasi kama cha milioni 400 au milioni 500 ili zianze kufanya kazi hiyo kwa sababu tunamwombea Mwenyezi Mungu lakini isitokee tena ikapatikana dharura nyingine kabla hatujatengeneza ule mtaro. Utasaidia ku-*divert* maji kuondoka huku kwenye machimbo kwa wachimbaji wadogo, iende sehemu ambayo yale maji hayatasababisha athari kwa wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji kutokuchangia huduma za jamii kadri ya makubaliano yaliyoingia na jamii husika, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau katika maeneo ya wachimbaji kwa maana ya wadau wa pande zote ili kuboresha huu msingi wa *social cooperate responsibility* ili kupunguza malalamiko yanayojiteze. Nadhani pia kuna udhaifu katika hii mikataba ambayo tumeingia kwenye awamu ya 1997/1998, lakini tumeliangalia. Ukiangalia hawa wachimbaji wakubwa wanapokuwa kwenye maeneo mengine, ukienda kuangalia mikataba yao wanaingia Peru, Apado na kwiningko, unaona kabisa kwamba element ya *social cooperate responsibility* siyo issue ambayo ni ngeni kwao, kwa hiyo, hakuna sababu kwa Tanzania sasa element hii ionekane ni kitu kigeni. Hili tumeliangalia na tunaendelea kulifuatilia na limetiliwa mkazo kwenye Sheria mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa njielekeze kwenye masuala kwa haraka haraka yale ambayo nimekusudia kuyasema kwenye sekta ya nishati. La kwanza kabisa, miradi ya REA ambayo Wabunge wenzangu walismama wakasema kwa ukali kabisa na wakasema mengine imekuwa ni kama hadithi, ni kweli. Kwa ukubwa wa nchi yetu 140,000 Square Kilometer na vijiji viliviyokuwemo, kazi ya kufikisha umeme Tanzania nzima ni kubwa sana. Kwa hiyo, tutaifanya kwa awamu. Sasa labda niseme tu kwa mwaka jana tulilisema hili mwaka jana fedha zilizokadiriwa kwa ajili ya kufanya yale malengo tuliyokusudia mwaka jana ilikuwa kama bilioni 50, bado ni fedha ndogo sana kwa kazi kubwa iliyokuwepo. Lakini katika hizo zikapatikana bilioni 13. Kwa hiyo, utaona kwamba pamoja na nia nzuri ambayo Serikali ilikuwa nayo ya kuhakikisha miradi hii ya REA inatekelezwa, *it was impossible* kufanya kwa fedha hizo katika maeneo yote. Sasa mwaka huu tumekubaliana kwamba katika fedha za mwaka huu bilioni 54 zile fedha ziko *ring fenced* ili zisifanye kitu kingine isipokuwa miradi ya kijijini.

Mheshimiwa Spika, pia na sisi tumemwomba Waziri wa Fedha kwamba kwenye fedha hizi atoe *displacements schedule* ili jijikane kabisa kwamba katika hizi bilioni 54 labda bilioni kumi na ngapi zitatoka baada ya miezi mitatu na zisiache kutoka kwa sababu zikiacha kutoka tutachelewa kukubaliana au REA watachelewa kukubaliana na wakandarasi. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo Wizara ya Fedha tumekubaliana nao na tumefikiria kwamba ni njia sahihi ya huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi sana wamechangia kwenye miradi yao mbalimbali. Mheshimiwa Vita Kawawa amezungumzia suala la Namtumbo, Mheshimiwa Keissy amezungumzia suala la kuwepo kwa nguzo katika mradi wa upelekaji Nkasi, Mheshimiwa Zedi amezungumzia suala la miradi ya Bukene, Ahmad wa Solwa amezungumzia la miradi inayozunguka. Kwa hiyo, ukiangalia kusema kweli Wabunge wote zaidi ya 200 waliochangia kila mtu amezungumzia miradi yake na hasa wanapokuwa Wabunge wa Vijiji wamezungumzia utekelezaji wa miradi ya REA. Tumewaomba REA watupe tathmini *plan* yao kwamba kwa mwaka huu wanatarajia kufanya nini au *ideally* wafanye nini?

Mheshimiwa Spika, ukiona ile miradi yao yote kwa ujumla kwa mwaka huu wanatarajia kama tungkuwa *we are leaving an ideal society*, wapewe hela wanayotaka wangeomba bilioni 170 kwa miradi mpya waliyokusudia. Bilioni kama 25 kwa ajili ya miradi ya Makao Makuu ya Wilaya mpya zilizojiteze na wangeomba kama bilioni 25 au 30 kwa ajili ya kumalizia miradi ile ya mwaka jana ikijumuisha na bilioni 11 ambayo iko *outstanding* kutoka mwaka jana za wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *you can see the magnitude of the problem* ni bilioni 40 plus kwenye miradi ya REA ili tuanze kuwa na *a significant approach* ya kupeleka umeme kwenye

maeneo ya Tanzania na *why is this so relevant?* Kwa sababu kama *access to power* ya Tanzania sasa hivi ni asilimia 15, tusipokwenda na mkakati huu mkubwa wa kufikisha umeme kwa wananchi kwa kiasi hiki tutabaki kwenye viwango vya asilimia 17, 18, sasa tukijiridhisha kwamba ni viwango vya wastani kwa nchi zingine zote *fine*, lakini kwa sisi Watanzania kwa *resources* tulizokuwa nayo pia na hii mipango mkakati tunayokuja nayo tunadhani kwamba ni jambo ambalo linawezekana. Ukiondoa hizi bilioni 54 ambazo ni fedha za *REA* zilizokusudiwa, kuna fedha zingine zimeonekana zinatoka kwenye tozo la *TANESCO* kwenye fedha za *REA* za matumizi ya ndani, na kwa ujumla wake wamepata kama bilioni 90 ambazo wataanza nazo.

Mheshimiwa Spika, kutoka bilioni 90 mpaka milioni kama 180 bado ni nusu, kwa hiyo, sis humu ndani Bungeni tukae tujuje wazi kabisa kwamba, tukiboresha kazi ya usambazaji wa umeme ndio pia tunaweza kuwafikia Watanzania walikuwa wengi. Kwa hiyo, natarajia kwamba, pamoja na kuwa kuna miradi mingi sana ya umeme vijiji ni iliyotajwa, Mheshimiwa Ndassa ametaja miradi yake ya Taro na kadhalika, nafikiria kwamba miradi hii itakuja kuzungumziwa wakati wa kupitisha vifungu kwa sababu kwa sasa hivi siwezi kuitaja yote ni mingi sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine liliozungumzwa ni suala la upatikanaji wa vifaa. Wabunge wamelikemea sana hili kwamba, wanapata nguzo zinakwenda, halafu nguzo zinakaa tu pale, nyaya zinakwenda baada ya miezi mitatu. Tumekubaliana na *TANESCO*, waendelezaji wa miradi kwamba, walifanye kwa utaratibu ambao unawapa matumaini kidogo wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala pale ya Kasulu na Kibondo ambayo kwa mfano, kwa sasa hivi umeme kweli umekwenda, jenereta zimekwenda, nyanya zimekwenda lakini sasa hivi umeme unashindwa kuunganishwa Kasulu na Kibondo kwa sababu hakuna *meter*. Sasa tumesema *this is the problem wide, and we see this problem kwamba kuna tatizo la meter*. Hata hivyo, mwendelezaji amekubaliana na *TANESCO*, kwamba, wampe *meter* zake. *Meter* za *TANESCO* ziko bandarini wiki ya tatu, kama meter 25,000 au 30,000. Sasa hivi ndio vitu ambavyo kusema kweli tumekubaliana *within* kwamba ni lazima tuboreshe *efficient especially* kwenye namna ambayo huduma hii ya umeme itawafikia Watanzania, vinginevyo tutakuwa tunachelewesha uwezekano wa kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja iliyokuja ambayo nimeelezea, Serikali iharakishe ujenzi wa miradi vijiji, Serikali kupitia *TANESCO* iweke mikakati ya kupunguza ghamara za kuunganisha umeme kwa wateja hilo tumelizingumza mara kwa mara na Wabunge wengi sana wamelizingumzia. Sasa kwa ghamara tulizonazo sasa hivi ni 470,000, 450,000 kuunganisha umeme ndani *average*, lakini *TANESCO* wenye ukiwaliza wanasema ghamara zenyewe *actually* hata hivyo ghamara zinatakiwa kuwa kubwa zaidi kama shilingi 600,000 kwa sababu kama ghamara za *copper* zimepanda, wakati shaba ndio kiungo kikuu kwenye vifaa na nini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunajaribu kusema kwamba lazima tuangalie kwenye maeneo ambayo *TANESCO* wanaweza kupunguza ghamara za kuunganisha umeme, tumekubaliana watafanya hivyo. Lakini *alternatively* ni kuhakikisha kwamba tunaweza kuunganisha kwa awamu, hilo nalo katika kupita kwa wananchi wengi, wameonekana wanaweza kupokea, kwamba badala ya kwenda na kulipa 450,000 kwa wakati mmoja, ulipe kwa awamu ili uanze labda na 150,000 halafu ndani ya miezi mitatu au miezi sita kulingana na *cash flow* za *TANESCO* watafanya tathmini. Hili tunaona ni jambo ambalo pia linaweza likaongeza *connectivity* kwa wateja walio wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni hili kwamba sasa hivi utaratibu huo wa kwenda benki kuchukua au kupeleka fomu zako za *TANESCO* na kurudi linahusisha Akiba *Commercial Bank* peke yake. Jana nimewauliza *TANESCO* na wamenihakikisha kwamba wameanza kuzungumza na mabenki ili kwa mabenki yale ambayo yana *access* kwenye maeneo mbali zaidi kwa mfano, wakiweza kufanya hivyo na *NMB* na *CRDB* that is better kwa sababu ina maana hata Watanzania wengi walioko vijiji wataweza kufanya *connection* za umeme kupitia utaratibu huu wa mabenki kuliko kwa sasa hivi unakwenda Akiba *Commercial Bank* nayo ina matawi machache sana ni ngumu kupata *connectivity*.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *TANESCO* ipanue wigo wa vyanzo vyatuzi kuzalisha umeme ili ipunguze utegemezi katika umeme wa maji. Hili tumelipokea na kwa sasa hivi vyanzo vikuu ambavyo vinaonekana vitatutoa kwenye kadhia hii haraka ni gesi asili kutokea Mnazi Bay na Songsongo na chanzo kingine ni makaa ya mawe. Tumewasikia Wabunge wamesema sana maeneo makubwa matatu yaliyojitokeza ni Ngaka, Mchuchuma na Liganga na Kiwira. Matatizo yaliyokuwepo labda tuseme tu kwamba, yote pia na matatizo ya maeneo yaliyopo ukiondoa Kiwira ambayo imefikika kwa nyanya lakini Ngaka inabidi uje Songea, uingie kwenye *grid* ya Taifa kwa msongo ambao unatarajiwa kuja kutoka Makambako 132 Kv.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa hivi kwa mfano, jana kulikuwa na fikra ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa nini tusizalisha Ngaka kwa MW 200 tukazipeleka Songea, *well and good* lakini huyu atakayezalisha (*developer*) akikaa anazalisha umeme wa Megawatt 200, hana pa kuzipeleka kwa sababu msongo wa Makambako, Songea unaendelea vizuri kwa mkandarasi, lakini unategemea kuingia Januari, 2014. Kwa hiyo, kwa sasa hivi miradi ya haraka ni hii ya kutumia gesi ambayo tunatarajia kwamba, kama bomba la gesi hili ambalo utaratibu wake wa dharura ukiingia kutoka Songsongo mpaka Dar es Salaam ndani ya miezi 12 mpaka 14 ijayo, maeneo mengi haya ambayo tunatarajia vyanzo vinavyotumia mafuta vitabadiilisha na kutumia gesi ili kushusha gharama ya umeme kwa zaidi ya asilimia sitini ndio tofauti ya mafuta na gesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima niseme hilo ndipo tunapojielekeza na Mheshimiwa Waziri atakuja kulisemea vizuri zaidi baadaye.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, Serikali ije na mkakati wa kurekebisha sekta ya umeme kwa madhumuni ya kuweka mazingira wezeshi. Haya mazingira yapo tayari Wabunge wameyazungumzia lakini yako tayari kwenye Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 *grid* ya Tanzania na *grid* za nchi jirani ziunganishwe kuimarisha upatikanaji wa umeme. Kuna *program* ya kutoka Arusha kwenda Nairobi, lakini kuungana moja kwa moja mpaka Singida – Iringa na mradi huu unaitwa ZTK, utaunganisha *East African Power Pool* kwa upande na *South African Power Pool* ni mradi ambao kwenye pande zote mbili, *South African Power Pool* tulikuwa kule Botswana mwezi wa tano wanauhimiza na *East African Power* wanauhimiza sana tulipokuwa Kigali na wao wanasema ndio *lifeline* unapita Tanzania na una-connect power pool mbili zote hizi. Kwa hiyo, hili peke yake tunajaribu kulifanyia kazi, wenzetu wa Kenya wanaonekana wana haraka zaidi, wenzetu wa Zambia wako kwenye uchaguzi, kwa hiyo, sasa hivi kidogo hawapatikani sana.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo hili la usambazaji wa umeme uzingatie Jiografia ya nchi ni kweli hili jambo pia tumeliangalia na ndio maana kuna mikakati ya makusudi ya Serikali kama hii, Mtwara Electricity Project na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuna maelezo kuhusu umeme wa upepo. Mmezungumzia umeme wa gesi ambao kwa sasa hivi kwa miundombinu tuliyokuwa nayo leo hii inachangia MW 400 katika MW kama 620 zinazozalishwa. Kwa hiyo, utaona kwamba *we real have dependency* kwenye *gas* na lengo letu ni kupanua zaidi uwezo huu ili gesi izalishe hata kufika MW 1000 ikifika mwaka 2012 mwezi wa Tisa au wa Kumi ndio lengo.

Mheshimiwa Spika, kuna upepo pale Singida na wiki iliyopita tulikwenda kwenye eneo la *Wind East Africa* walikuwa wameomba Serikali twende tukaangalie wanachofanya pale. Mpaka sasa hivi tulikwenda na Mheshimiwa Mohamed Missanga, mpaka sasa hivi wanachofanya ni kwamba wanatarajia, wanaweza kuingiza MW zinazotumika pale Singida *as soon as June, 2013*, lakini pia kuna mradi mwingine ambao unaweza kuingiza Makambako MW 50 za umeme. Sasa lilitokuwa jambo la kusisitiza sana hapa ni kwamba, miradi yote hii kwa bahati *Alhamdulillah*, yote iko karibu na *grid* ya Taifa. Huu mmoja uko kilomita nane tu kutoka *grid* ya Taifa kituo cha Singida, ule mwingine wa Makambako uko kama kilomita 10 nadhani kwenye *grid* ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukizalisha 50 huku na 100 huku, *transmission* zake kwenda *sub station* tena kwenye *line* unakuwa karibu sana jambo ambalo tumezungumza tulipokutana nao na tunazidi kuwahimiza *developers* wa *wind* waje wengi zaidi pale Singida pana *capacity* ya

kuzalisha mpaka *MW* 300, *MW* 400 za *wind* kabla ya mwaka 2014. Lakini gharama ya mitambo ya *wind* lazima tuseme ukweli ni kubwa zaidi kuliko mitambo mingine.

Tofauti ni moja kwamba miradi ya gesi au mafuta ukipeleka na *operational cost* ya kuweka mafuta kila siku, hii ya *wind* unapeleka pale labda kwa dola 2.5 au dola 3.0 kwa *MW* 1 lakini ukishaiweka pale unaanza kufanya dua ili *wind* iendelee kuwa kali zaidi. Sasa kwa upande wa Singida vipimo vilivyoonyesha pale vimeonyesha kwamba hata ukipeleka *wind* pale ya *MW* 200, 300 ni jambo ambalo litachangia sana kwenye *grid* ya Taifa, Serikali imejielekeza hapo, imeonekana kuna mgogoro wa mwendelezaji mmoja na *TANESCO*, niseme tu kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alinielekeza nikae nao, nimekaa na *Wind East African*, tumekaa na watu wa Makambako, wale wengine wa *East African Wind* nao tumewaambia waje tuzungumze nao na kama kuna vikwazo vingine ambavyo vinaonekana vipo katika daraja zetu za uundaji, tutaviondoa ili miradi hii iingie haraka iwezekanavyo kwa sababu itapunguza utegemezi kwenye vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mradi wa Ngaka, tumelizungumzia na kwa kumalizia, naomba nijielekeze na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa hii hatua tuliyofikia leo. Nimesimama hapa mbele yenu hii ni mara ya nne sasa, nikija kuunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. Mara nydingi tumekuu tunazungumzia kwamba suala hili *we need to protect ourselves* dhidi ya *dependence* ya maji lakini tunahitaji tufanye *investments* za haraka, kwa sababu umeme unaweza ukaonekana kwamba, leo upo lakini hili jambo ambalo tutalifikia kwenye hatua tuliyokuwa nayo tulikuwa tunalifahamu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pia tungeweka tahadhari na ambalo sasa hivi naomba niwahimiza Waheshimiwa Wabunge wenzangu tukubaliane kwamba tuishi katika mazingira ya kuwa katika mfumo wa tahadhari. Turidhie tukiwa na *forecasted planning* kwamba huko mbele tutahitaji kitu fulani na kitu fulani kisionekane kwamba kwa sasa hivi hatukihitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa tunajua kabisa kwamba kwenye mfumo wa *transmission* ya Tanzania, huko mbele tunakokwenda na uzalishaji huu wa ziada ni lazima tuongeze nguvu kwenye mfumo wa *transmission* na eneo moja ambalo lazima tuongeze nguvu ni kwenye vituo vya Iringa, lakini pia kwenye kituo cha Singida. Pale kituo cha Singida ndiyo *substation inayo-branch off* kwenda Kanda ya Ziwa yote na Kanda ya Babati mpaka Arusha yote. Kwa hiyo *at some stage* kwa uwezo wake uliopo sasa hivi ni lazima tuongeze uwezo. Lakini hilo jambo hatuwezi kuli-plan system ikishakuwa *overloaded*, ni lazima tuelewane kwamba, tuanze kuli-plan sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakuja kwa Wabunge tuseme tunahitaji kuongeza nguvu kwenye *system* ya *transmission* pale Singida. *Of course back borne* hii Iringa-Shinyanga 400 KV inaendelea sasa hivi. Lakini pia kuna umuhimu wa kuiongeza *transmission line* ile Makambako-Songea inakwenda. Lakini kuna kipande kwa kwenda Mbeya ili iungane na *transmission* ya Pensulu Zambia. Hii ni miradi ambayo inahitajika ili kuweka uhimili wenye nguvu kwenye mfumo mzima wa umeme, vinginevyo uzalishaji wetu wataalam wanasema utaendelea kuwa *squalid*.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikusudia kulisema na ambalo Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atakuja kulisema zaidi ni kwamba hili suala la kutegemea mafuta kwenye uzalishaji wa umeme ni gumu. Kwa sababu gharama zake *operationally* ni kubwa. Kwa hiyo hakuna namna isipokuwa kwamba lazima tutaridhia na lazima tulete mipango ya makusudi kabisa ili gesi iingie haraka iwezekanavyo. Kama nilivyo sema kwa hesabu tu gesi itapunguza gharama za umeme unaozalishwa na mafuta kwa zaidi ya asilimia 60. Kwa hiyo, kusema kweli ndiyo *the way forward* kwa maana ya umeme unaotokana na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, hili kwa ruksa yako niliseme kidogo. Kuna maneno ambayo tunaona baadhi ya wanaoitwa wanaharakati wanasema Tanzania isizalishishe makaa ya mawe kwa sababu makaa ya mawe yanachafua mazingira. Jamani tuache maneno haya. Tunawapa sababu watu wengine ya kusema kwamba Tanzania msizalishishe kwa makaa ya mawe. Afrika ya Kusini wanazalisha makaa ya mawe *megawatt* 25,000. China wanazalisha umeme wa makaa ya mawe *megawatt* chungu nzima. India pia wanazalisha umeme wa makaa ya mawe sisi hatujazalisha hata *megawatt* tano, wanaharakati wanaanza kusema ooh *ozone layer*.

Mheshimiwa Spika, tulichokubaliana kwenye Mkutano wa *Renewable Energy* na sisi Tanzania tumeweka *position* yetu kwamba Mwenyezi Mungu ametujalia makaa ya mawe ya kuleta umeme wa kutosha kwa wananchi wetu na kuondoa kadhia hii. Sasa tutakachofanya tutashirikiana na mtu yoyote ambaye atakuja kutupa *the best ways* za kupunguza *environmental degradation* inayotokana na makaa ya mawe. Kwa bahati nzuri watu wa kule *Mumbay Institute of Technology* na kuna baadhi ya *institutes* za India ambazo tumeanza nazo mawasiliano, tumekutana nao kwenye mikutano. Wao kwa makusudi kabisa wanafanya utafiti wa namna ya kupunguza athari za matumizi ya makaa ya mawe kwenye mazingira.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri katika hizo *forum* za Kimataifa imeonekana na South Africa ambao ndiyo watumiaji wakuu wa makaa ya mawe Afrika wametuunga mkono sana. Kwa hiyo, katika ule msafara wa mamba na sisi tumo. Lakini maana yake ni kwamba, katika hili lazima tuseme kwamba wenzetu ambao wanakuja wanasema wao ni wanaharakati, *NGO* sijui ni nini, wanatukwaza. Hii ni *resource* ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu. Hatuanzi sisi kuzalisha umeme kwa makaa ya mawe. Watu wameshaanza kuzalisha makaa ya mawe huko miaka 100 iliyopita iwe sisi Tanzania leo kwa vi-megawatt 2,000 ndiyo tunachafua mazingira. Tukubaliane kwamba Ngaka itaingia, Kiwira itaingia, Mchuchuma na Liganga itaingia kusaidia kwenye matumizi ya gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anayekuja tutamwambia tukae tupunguze namna ya kupunguza athari, siyo kuondoa uzalishaji wa makaa kwa wingi wa *resource* tulyokuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia. Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushirikiano wenu. Pia naomba niwashukuru Wabunge wenzangu kwa haya yote ambayo wametuletea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa nitamwita Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Dakika 45 hazitahusisha wale utakaowasoma kwa majina. (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na pia kwa kutuongoza katika kipindi chote cha wiki tatu tulichopewa kuandaa mkakati wa kuondoa mgao wa umeme na kuiamarisha Sekta ya Nishati na Madini. Lakini pia kupata muda kwa ajili ya kutoa ufanuzi kwa hoja ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili hotuba yetu ya makadirio na taarifa ya utekelezaji kama tulivyoiwasilisha tarehe 15 na tarehe 18 Julai.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, kabla ya kuanza kutoa ufanuzi ambao kimsingi utatanguliwa na mkakati maalum ambao ilikuwa ni sababu maalum ya kuahirisha hitimisho la majumuisho ya Wizara ya Nishati na Madini, naomba nitambue wale wote waliopata nafasi ya kuchangia mjadala wa hotuba yetu kwa kuzungumza ama kupitia maandishi.

Mheshimiwa Spika, katika hili wachangiaji sisi tume-classify katika sehemu mbili. Kwanza wale waliochangia kwa kuongea lakini pia kwa kuandika wakati wa mjadala wetu wa tarehe 15 na tarehe 18 mwezi wa saba. Lakini pia waliochangia masuala yanayohusu Sekta za Nishati na Madini wakati wa mjadala wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara ambazo zilichangiwa au kujadiliwa kabla ya kuwasilisha hotuba ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii, napenda niwatambue waliopata nafasi ya kuchangia kwa kuongea tukiongozwa na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini pia Mheshimiwa Januari Yussuf Makamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa John Mnyika, Msemaji wa Upinzani na Waziri Kivuli katika Sekta ya Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine waliopata nafasi ya kuchangia kwa kuongea ni pamoja na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Mheshimiwa Freeman

Mbowe, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Mansoor Hiran, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Charles Mwijke, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Omar Badwel, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Rebecca Mgodo, Mheshimiwa Dokta Hamis Kigwangalla, Mheshimiwa Naomi Kaihula, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Lolecia Bukwimba, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Hussein Amour na Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Nishati na Madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, waliopata nafasi ya kuchangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Dokta Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Ali Mohamed, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Madelu, Mheshimiwa Hussein Mzee, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Dokta Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Saidi Mtanda, Mheshimiwa Zaynab Vullu, Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge, Mheshimiwa Dokta Mary Nagu, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Clara Mwatuka na Mheshimiwa Suleiman Bungara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Nassib Omar, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Dokta Christina Ishengoma, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Gosbet Blandes, Mheshimiwa Salum Hemed, Mheshimiwa Dokta Augustino Mrema, Mheshimiwa Eng. Athuman Mfutakamba, Mheshimiwa Dokta Festus Limbu, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Jaji Fredrick Werema, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Masoud Salim na Mheshimiwa Saidi Zubeir. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, Mheshimiwa Gregory Teu, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Benedicto Ole-Nangoro, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Dokta Antony Mbassa, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Suleiman Omar, Mheshimiwa Josephine Genzabuke pamoja na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba radhi endapo nitakuwa nimekosea kutamka vizuri kwa usahihi majina ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, hayakuwa makusudio yangu. Pia kwa ufupi nilikuwa napenda wakati naendelea kuwasilisha, kutoa ufanuzi na majumuisho ya hotuba hii, nikushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Bunge lako Tukufu, kwa nia thabiti ya kutaka kuondokana na janga hili la umeme ambalo milionyesha wakati tunajadiliana tulipowasilisha bajeti yetu tarehe 15 na mjadala uliendelea mpaka tarahe 18 Julai, 2011.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu mngeweza kupitisha mpango na bajeti yetu kama iliyopangwa tarehe 18 Julai, 2011, lakini kwa uzalendo wenu mkaona ni vyema kuahirisha kwa muda hitimisho la hoja yetu, ili tupate fursa ya kuandaa ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mkakati wa kuondoa mgawo wa umeme nchini. Kwa kuelewa dhamira yenu njema, tulipokea kwa moyo mkunjufu na kuifanya kazi kwa kadiri ya uwezo wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wepesi wake wa kusoma hisia za Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia

hoja ya Wizara yetu na kuchukua hisia hizo kwa mtazamo chanya. Kutokana na hekima zake, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliona ni busara yeye akiwa Klongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, kuchukua dhamana ya kutoa hoja ya kuliomba Bunge kuahirisha majumuisho ya mjadala wa hoja ya Nishati na Madini. Kwa niaba ya wenzangu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kutuongoza na kusimamia vyema shughuli za Serikali Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa pia, nitumie nafasi hii kwa ufupi kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri wote na Watendaji wa Serikali, walioshiriki kuandaa mkakati huu ambaa tumeufanyia kazi baada ya kupewa muda huu wa kipindi cha wiki tatu. Kwa namna ya pekee napenda kuishukuru sana Kamati ya Nishati na Madini kwa namna ambavyo imetoe ushirikiano, maoni na ushauri, ikiwa ni pamoja na Wabunge wote kwa ujumla, ambaa leo umetufikisha hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niendelee kuwashukuru wapigakura wenzangu wa Jimbo la Sengerema, ambaa kwa hakika bila wao, mimi nisingekuwa hapa. Lakini kwa nafasi ambayo haimithili, kwa mara nyiningine tena namshukuru sana mke wangu Blandina, kwa kuendelea kunivumilia, lakini pia kunitia moyo hasa katika kipindi hiki na kusimamia familia yetu, watoto wetu Brian, Brigete pamoja na Bill Junior. Nawashukuru wazazi wangu, ndugu na jamaa na wote ambaa kwa kipindi hiki wamekuwa wakituunga mkono kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo ujumbe mfupi wa simu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda kuwasilisha mkakati wa kuondoa mgawo wa umeme nchini. Katika hili, nitajielekeza zaidi kwenye hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali na hatimaye kushirikisha Waheshimiwa Wabunge, kupitia Kamati za Bunge, kuandaa mkakati ambaa tunaamini kwamba, utatuondoa hapa tulipo na kutumalizia mgawo wa umeme.

Mheshimiwa Spika, historia ya mgawo tunaifahamu na tusingependa kutumia muda mwangi kueleza haya. Lakini niseme kwamba hatua za makusudi ambazo zimechukuliwa kuhakikisha kwamba tunakuwa na umeme wa uhakika kwa kipindi hiki kati ya sasa na mwezi wa 12, Serikali kwa kushirikisha wadau mbalimbali imekaa na ikaja na mkakati ufuataa.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaomba kuahirisha majumuisho ya Wizara hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwaarifu Watanzania kipitia Bunge lako Tukufu kwamba, katika muda ambaa tulikuwa tunakwenda kuufanya kazi mkakati wa kuondoa mgao Tanzania, tulikusudia angalau tuje na mkakati ambaa unatuhakikishia upatikanaji wa kiwango cha umeme kisichopungua *Mega Watt 300* ili tuwe katika nafasi nzuri ya kukabiliana na hali ya hewa inavyokuwa. Kwa sababu, sasa hivi umeme kwa asilimia 55 unategemea maji kwenye mfumo wetu wa usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hili, mkakati tuliojua nao umejielekeza na tumeibua miradi ifuatayo:- Kwanza kuna mradi wa kampuni ya *Symbion Power* ambaa hata wakati tunawasilisha taarifa yetu, tulisema kampuni hii ilishafunga Mkataba na Shirika la *TANESCO* wakiwa wanatakiwa kuzalisha kiwango cha umeme usiopungua *Mega Watt 112*, wakati huo walikuwa wanazalisha *Mega Watt 75*. Tuliahidi na tulisema kwenye kitabu chetu kwamba, ilikusudiwa kufikia mwishoni mwa mwezi huu, watakuwa wameongeza uzalishaji. Kwa sababu, kipindi kile ilikuwa ni *Mega Watt 75*, watakuwa wameongeza *Mega Watt 37* ambazo zilikusudiwa zitumike kuzalisha kwa kutokana na mafuta ya ndege.

Mheshimiwa Spika, ninapoongea hivi, leo kampuni ya *Symbion*, kwa kile kiwango kilichokuwa kimebaki cha *Mega Watt 37*, wameanza jana majaribio ya kuwasha, hivyo kutimiza lengo la kuzalisha *Mega Watt 112*. Hatua ya pili tuliyokuja nayo wakati tunawasilisha bajeti yetu tarehe 15 na hata tarehe 18 Julai, 2011 tulipoomba kuahirisha hitimisho la mjadala huu, mtambo wa *IPTL* ulikuwa unazalisha kiwango cha umeme usiozidi *Mega Watt 20*. Tumeshapata fedha za kununulia mafuta; kati ya kipindi ambacho tulahirisha na sasa na itakuwa hivyo kuendelea siku zijazo. Mtambo ule sasa unazalisha *Mega Watt 100*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwaarifu Watanzania kwamba, ule unafuu ambaa sasa hivi unaonekana wa mgawo, tofauti na siku tulipokuwa tunawasilisha hapa hotuba yetu tarehe 15 Julai na hadi terehe 18 Julai, 2011 umechangiwa na ongezeko la hizo *Mega Watt 80* kutoka kwenye mtambo wa *IPTL*.

Mradi wa tatu ni ule ambaa tuliutolea taarifa kwenye kitabu chetu cha hotuba kwamba, mwishoni mwa mwezi wa sita Shirika la *TANESCO* lilikuwa limefunga Mkataba na Kampuni ya *AGGRECO International*. Hii ni kampuni inayofanya kazi ya kukodisha mitambo ya kuzalisha umeme, kama ambavyo wengi wetu tumeshuhudia jana, tuliahidi hapa kwamba, itakapokuwa imefika mwezi wa Nane, hasa mwishoni, mitambo hii itaanza kuzalisha *Mega Watt 100*, mitambo imewasili jana. Sasa hivi wanaendelea na harakati za ufungaji na tumewaambia wafanye kazi usiku na mchana. Kwa hiyo, matarajio yetu kama tulivyoahidi kwenye hotuba kipindi kile, ni kwamba, kufikia mwisho wa mwezi wa Nane tutakuwa na ongezeko pamoja na vyanzo vingine pia la *Mega Watt 100* kutoka Kampuni ya *AGGRECO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mradi mwininge ulioibuliwa ni kuhusu Kampuni ya *Symbion*. Kwa mara nyininge tena, kampuni hii imeonyesha uwezo wa katuongezea uzalishaji wa *Mega Watt* zisizopungua 205 kati ya kipindi cha mwezi wa Tisa mpaka mwezi wa 12. Kinachoendelea sasa hivi, ni maandalizi hayo. Tunataraja kwamba, mwezi wa Tisa wataleta *Mega Watt 45*, mwezi wa Kumi wataleta *Mega Watt 110* na mwezi wa 12 watafunga mitambo ya *Mega Watt 50*, hivyo, kukamilisha jukumu lao la kimkataba waliloingia na *TANESCO* la kuzalisha *Mega Watt 205*.

Mheshimiwa Spika, mradi wa tano tulioibuni katika maandalizi ya kuundoa mgawo huu wa umeme, tumeona tujielekeze katika fursa zote ambazo zinapatikana ndani ya nchi yetu. Uwezo wa kiserikali, lakini pia tutumie taasisi au mashirika ya umma yaliyopo nchini pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika hili, tunafurahi kuutaarifu umma kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, ile hamu ya Shirika letu la Jamii (*NNSF*) la kuwekeza katika Sekta ya Nishati pamoja na sekta nyininge kama ambavyo inaendelea, wamekubaliana na *TANESCO* kwamba, *NNSF* itanunua mtambo wa kuzalisha umeme wa kiwango cha *Mega Watt 150*. Mtambo huu utakuwa umekamilika ufungwaji wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi wa Tisa watafunga mitambo ya *Mega Watt 50*, mwezi wa Kumi watafunga mitambo ya *Mega Watt 50* na mwezi wa 11 watafunga mitambo ya *Mega Watt 50*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miradi yote niliyoitaja kwamba, kampuni ya *Symbion* kwa ule mkataba wa kwanza ambaa walipaswa kuzalisha *Mega Watt 112*, zile *Mega Watt 137* zitaongezeka mwezi huu. Kama nilivyo sema kwamba, kutoka tulipoahirisha mjadala wetu kampuni ya *IPTL* imeongeza uzalishaji wa *Mega Watt 80*, hivyo kufikia *Mega Watt 100* kwamba, Kampuni ya *Symbion* pia imefunga Mkataba wa kuzalisha *Mega Watt 205* kati ya sasa na mwezi wa 12. Kwa kuzingatia kwamba kampuni ya *AGGRECO* imeshaleta mitambo ambayo kufikia mwisho wa mwezi huu itakuwa inazalisha *Mega Watt 100*, na kwa kutambua kwamba *NNSF*, shirika letu ambalo litawekeza *Mega Watt 150* ifikapo mwezi wa 11, hatua hii inatuhakikishia ongezeko la umeme usiopungua *Mega Watt 572* kwa kipindi kati ya sasa na mwezi wa 12 mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika tutaona kiwango hiki cha umeme ni zaidi ya *Mega Watt 272* kutoka makusudio ambayo tulidhania kwamba *Mega Watt 300* zingeweza kutufaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la kusisitiza hapa. Tunapata faraja kuwa na uwezo huu kwa sababu, ukweli umethibitika kwamba, kwa kadiri unavyokuwa na umeme katika mifumo ya usafirishaji na usambazaji umeme, mahitaji yanaongezeka kwa kasi sana. Kwa hiyo, inawezekana ikawepo fikra, siamini ndani ya nyumba hii, lakini sisi ni wawakilishi wa wananchi, wakadhani kwa nini kama dhamira ama kusudi lilikuwa ni *Mega Watt 300* mmekwenda mpaka *Mega Watt 572*? Ni ukweli mmoja tu kwamba, uhitaji wa umeme ni kama vile ilivyo kwenye mahitaji ya simu.

Mahitaji ya simu ukishaweka miundombinu, ukawahakikishia wananchi kwamba, mawasiliano yatapatikana, na hilo limethibitika tangu tulipofungua soko la mawasiliano ya Watanzania, wananchi wana uwezo wa kutumia simu. Wataalamu wamethibitisha pasipokuwa na mashaka kwamba, ukishakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme na ukawa na mfumo unaowafikia Watanzania, wananchi wengi, *automatically* matumizi yanaongezeka. Kwa hiyo, basi, sababu za msingi na faraja tunayoipata sisi ni kwamba, ziada hii tunayoisema leo ya *Mega Watt* 272, kimsingi inatuongeza uwezo wa kuwa na uhakika zaidi, lakini inatuongeza uwezo wa kuwafikishia wananchi wengi zaidi umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hapa ikumbukwe, kuna miradi mingi ambayo sasa hivi inatekelezwa, na Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu. Kwa mfano, mradi wa *REA* uko katika Mikoa 16, miradi mingi inakamilika kati ya mwezi wa 11 na mwezi wa 12 na michache sana mwanzoni mwa mwaka kesho. Hii nayo itatuongeza uwezo wa wananchi kuhitaji umeme zaidi. Kwa hiyo, kufikia mwezi wa 12 tutakuwa na *Mega Watt* 572, ukijumlisha na zilizopo, sasa tunakuwa na uhakika wa kuwa na *Mega Watt* zisizopungua elfu moja, mia moja, kumi na kitu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua umeme wetu leo ni zaidi ya asilimia 55 kutokana na maji. Lakini hakuna anayeweza kusema kwa uhakika tunakoelekea, hali itakuwaje? Kwa hiyo, sisi mpango wetu wa dharura, ama huu mkakati maalum wa kukabiliana na mgawo, hatukuishia mwezi wa 12 peke yake. Mvua ikinyesha, tutamshukuru Mwenyezi Mungu, lakini isiponyesha kitatokea nini? Serikali imekwenda zaidi ya hapo. Hivyo kuna mradi mwengine ambao utatekelezwa. Kuna Kampuni ya *Jacobsen* ambayo Serikali italidhamini Shirika la *TANESCO* kununua mitambo mingine ya *Mega Watt* 100 ifikapo mwezi wa tatu mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika awamu hii tuna mradi ule wa Mwanza. Mradi wa Mwanza wa *Mega Watt* 60 ambao tumekuwa tukileta hizi taarifa, utakamilika ifikapo mwezi wa Sita mwaka kesho. Mradi mwengine ambao sasa hivi nao upo katika hatua za utekelezaji, ni mradi ambao tumekuwa tukiusema sana, utafungwa Dar es Salaam wa *Mega Watt* 100 ambao umenunuliwa na Serikali na tunaukabidhi kwa *TANESCO*, mitambo yake nayo imefika juzi. Kwa hivi sasa mitambo ya *Mega Watt* 100 iko bandarini. Sasa hivi wanakamilisha taratibu za kuitoa na kuifunga Ubungo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kati ya kipindi cha mwezi wa kwanza mwaka kesho na mwezi wa 12. Pia tumejiwekea lengo la kuongeza *Mega Watt* nyingine 310. Lengo ni kutokuwa kabisa na nafasi ya upungufu katika uzalishaji wa umeme katika mfumo wetu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, liko jambo lingine. Umeme wetu mwengine huu tunaoujadili hapa, mitambo hii ambayo sasa hivi itatusaidia kututoa hapa tulipo kufikia mwezi wa 12, mitambo hii inatumia mafuta mazito na mingine inatumia mafuta ya ndege na pia inatumia gesi asilia. Sisi tumejaliwa kuwa na rasimali nyngi za kutuwezesha kupata umeme kwa bei nafuu sana na wa uhakika zaidi kutokana na gesi asili. Tumekuwa tukitoa taarifa hapa kwamba, Serikali ina dhamira ya dhati kuondokana kabisa na utegemezi wa umeme unaozalishwa kutokana na maji kwa sababu mabadiliko ya tabia ya nchi hayatupi uhakika wa kuwa na umeme wa uhakika kwa kadri miaka inavyokwenda. Kwa hiyo, tumebuni mradi ambao tumeutolea taarifa hata kwenye hotuba yetu, wa ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asili kutoka Mtwara, *Mnazi Bay* kupitia Wilaya ya Kilwa eneo la Somanga Fungu na kuja mpaka Dar es Salaam na kuelekea Tanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida, mradi ule ulikuwa ukamilishwe mwaka 2013. Mradi huu ni wa Serikali, tunapata mkopo wa masharti nafuu kutoka China. Tumesema, kwa dharura tuliyonayo, ujenzi wa bomba hili la gesi ambalo litatuhakikishia upatikanaji wa gesi ya kuzalisha umeme zaidi ya *Mega Watt* elfu moja na kitu, tuuharakishe. Tumewaambia wenzetu wa China, sisi tuna matatizo ya umeme ambayo yanahitaji ufumbuzi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunakusudia ujenzi ule wa lile bomba, ukamilishwe kabla ya mwisho wa mwaka kesho na wiki ya kwanza ya mwezi wa Tisa, Waziri wa Fedha pamoja na wawakilishi wa Wizara ya Nishati na Madini na watalaamu wengine pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, watakwenda China kukamilisha utaratibu wa Mikataba, ili ujenzi wa bomba lile uanze mara moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? Pamoja na kwamba sasa hivi tutakuwa tunakwenda kwa mitambo inayozalisha umeme kutokana na gesi, mafuta na mafuta ya ndege; lengo letu ni kwamba, mitambo hii kwa sababu mitambo yote hii ambayo *TANESCO* wamefunga mikataba na huwa, ina uwezo wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili ama mafuta mepesi, mgingi yake ipo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sisi tunachosema, tukishaharakisha ujenzi wa bomba lile mitambo yote ambayo kimkataba itakuwa inaendelea kuzalisha umeme hapa. Itanza kuzalisha kwa kutumia gesi. Tathmini ya kitaalamu inaonyesha ukishaanza kutumia gesi asili kuzalisha umeme, unakata gharama kama asilimia 50 ambazo unazitumia kwenye mafuta. Ndiyo maana tunasema tunakuja na uharaka huo wa ujenzi wa bomba lile, ni jambo la dharura sisi kiserikali na kwa niaba ya watanzania pia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mradi mwine ambao tuliutolea taarifa kwenye hotuba yetu kwamba, kampuni ya *SONGAS* kule Songo Songo kisiwani kwa Mheshimiwa Mangungu, walikuwa na mradi wa upanuzi wa ile mitambo ya kusafisha gesi ili nayo iongeze uwezo wa kuleta gesi asili kwa miundombinu iliyopo sasa. Mradi ule ulikuwa ukamilike mwaka 2013 mwezi wa Pili, kikao cha mwisho tumekaa nao tarehe 11 hapa Dodoma, tumekubaliana na tumewaambia kwa dharura tulionayo na kwa jinsi wananchi wanavyopata mateso, kunapokuwepo na mgawo, Taifa linavyoumia kiuchumi na kijamii, mradi ule uharakishwe.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kwamba ule mradi nao utaharakishwa wao, wameshatangaza tenda, saa hii wameshafungua tenda wanafanya uchambuzi kwa sababu ile ni *private sector*, ukamilishwe kabla ya mwisho wa mwaka kesho uunganishe nguvu na hili bomba letu la Serikali linalotoka Mnazi Bay.

Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu, tukishakuwa na hiyo miundombinu miwili, Watanzania wawe na imani, tunawahakikishia tatizo hili ambalo tunaona leo tutakuwa tumelidhibiti kiasi cha kutosha na sasa tutakuwa na uhakika wa kuunganisha utekelezaji wa mipango yetu ambayo tumekuwa tukiisema hapa kwa muda mrefu ambayo imefikia mahali wakati mwine ambayo imetufanya tuwe *nick named*, "wazee wa ku-download." Somanga Fungu *Megawatt* 230, Kinyerezi *Megawatt* 240, Kiwira *Megawatt* 200 pamoja na miradi mingine yote ambayo tumekuwa tukitaja hapa. Tutakuwa tumeunganisha sasa tukienda kwa uhakika zaidi katika kutekeleza miradi hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mpango huu una gharama zake, una gharama kubwa na kwa kuonyesha tu gharama ziliyyo, nataka niseme, kati ya sasa na mwezi wa 12, kwa hii Mikataba ambayo Shirika la *TANESCO* kwa niaba ya Watanzania imeingia na hawa wazalishaji wa umeme kwa mtazamo huu wa dharura, umeme huu utatugharimu sisi Watanzania kiasi kisichopungua Shilingi bilioni 523, tathmini iliyofanywa uzalishaji wa *TANESCO* kwa mapato wanayopata kutoka mauzo ya umeme utakaozalishwa na *TANESCO* kuititia mitambo yote hii ambayo nimeisema, inayotupa ziada ya *Megawatt* 272 mauzo yote ya *TANESCO*. Watakayokuwa wamekusanya ni makusanyo ya Shilingi bilioni 115 tu. Kwa hiyo, tuna upungufu wa fedha kuhimili huu mzigo wa Shilingi bilioni 408. Sasa nani anabeba gharama hizi?

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaarifu Watanzania kuititia Bunge hili kwamba Serikali kwa kutambua uchungu iliyonayo kwa wananchi wake, imejitwisha mzigo huu, inaubeba mzigo wa Shilingi bilioni 408. Huo ni mpango kati ya sasa na mwezi wa 12, kwa sababu tunasema dharura hii hatuna uhakika nayo kama itaishia mwezi wa 12 tu. Gharama halisi kutoka mwezi wa kwanza mpaka mwezi wa 12 endapo hali itakuwa mbaya, na wataalam wa uchumi wanasesma ukitaka kupanga mambo vizuri, usijipangie kwa matumaini ambayo hayana tahadhari. Gharama zake kama mpango huu utakwenda mpaka mwezi wa 12 mwaka kesho, gharama zake ni Shilingi *trillion* 1.2 kama tutakwenda mpaka mwezi wa 12 mwaka kesho. Tukiishia mwezi wa 12, gharama zake ni hizo kwa upungufu ukiondoa kwa kukokotoa, kuiondoa ambacho *TANESCO* watakuwa wamekusanya ni shilingi bilioni 408.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua zifuatazo, wakati ikijitwisha mzigo huu. Kwanza, Serikali imesamehe kodi zote kwenye mafuta wakati huu wa kipindi cha dharura. Tunafahamu kodi ni sehemu ya mapato ya Serikali. Kodi hiyo ndiyo iliyo sababisha kuwekeza katika maeneo mbalimbali kuhudumia sekta mbalimbali. Lakini tunasema kwa hali tuliyokuwa nayo, leo hii gharama ya kutokuwa na umeme ni kubwa kuliko kuwa na umeme ambao ni ghali kiasi. Kwa hiyo, tumeondoa kodi katika mafuta yote yatakayotumika na hili nataka niliweke sawasawa, yatakayotumika kuzalisha umeme peke yake katika mikataba ambayo imefungwa na *TANESCO*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia wakati huu, kwa sababu kuondoa kodi ni moja, lakini mzigo huu wa Shilingi bilioni 408 hauwezi kumalizwa na kuondoa tofauti ya kodi tu, Serikali imesema *TANESCO* kama shirika la kibashara likakope na Serikali iliwekee dhamana ndiyo ilichokifanya. Serikali imeridhia, *TANESCO* imekopa, na Serikali imebeba jukumu lile kwa kuweka dhamana.

Mheshimiwa Spika, Iakini lingine ambalo tumelifanya kama Serikali, tumekuwa tukitoa taarifa hapa kwamba *TANESCO* inawadai wengi, kutoka taasisi za umma, hata baadhi ya Wizara, Iakini pia kutoka kwa wateja wao wa kawaida, wananchi wa kawaida na mashirika ya binafsi. Tumesema kwa kuanzia, sisi huku Serikalini kwa sababu madeni ya *TANESCO* mpaka ilipokuwa imefika mwezi wa Tano mwaka huu, *TANESCO* walikuwa wanaidai Serikali Shilingi bilioni isiyopungua 86. Serikali imesema fedha hizi tuzilipe ili kuipa nafuu *TANESCO* na malipo yameshaanza kufanya *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, nasema mpango huu ni wa gharama, na katika nchi zozote zile zinazofanya shughuli hizi kama ilivyo kwa sababu tunafahamu kweli nishati ya umeme ni nyenzo muhimu sana katika ustawi wa Taifa lolote. Hatua nyingine ambayo nilikuwa naomba Bunge lako lifahamu, Serikali inachokusudia na kwa kweli tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge na ninafahamu Waheshimiwa Wabunge wengi wametushauri kwa namna hiyo, lakini tuombe wananchi watuelewe tunapoelekea naona kuna umuhimu. Itakapofikia kwamba sasa umeme umekuwa wa uhakika zaidi kutoka na mipango hii tulioisema, kila mwananchi akapata umeme anaostahili kupata kwa jinsi anavyotaka kuutumia tutafanya marekebisho kwenye bei za umeme. Ili bei za umeme ziwe zenye uhalisia uliwezeshe Shirika la *TANESCO* liendelee kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tathmini imefanywa, ulinganifu wa nchi za Afrika Mashariki kwa sisi Kenya na Uganda, sisi ndio tunaotoza chini sana na kwa kweli wengi wetu tunafahamu. Ukiangalia kwa namna nyingine, b Bashara inayofanya *TANESCO*, ni kama hisani, unanunua bei ya umeme kwa bei ya juu sana, Iakini anawauzia wateja kwa bei ya chini, imetusaidia siyo jambo la kulaumu, Iakini tunasema hatuwezi kwenda mbele zaidi kwa mwenendo huu. Tutaweka marekebisho. Tunaomba *TANESCO* wapeleke maombi kwa mdhibiti wa masuala ya Nishati na Maji *EWURA*. Tutafanya hivyo baada ya kujiridhisha kwamba umeme huu umekuwa ni wa uhakika, wananchi watakuwa nao na tutafanya marekebisho kwa kuzingatia uwezo wa vipato nya wananchi.

Bei za *TANESCO* ziko katika makundi manne, kundi la chini ni la wananchi wa kawaida, hilo hatutaligusa hata kidogo. Mnafahamu umuhimu wa kuendelea kuiwezesha hiyo kada ambayo ina zile *tariff* ina vile viwango nya chini kabisa wasiotumia zaidi ya *unit 50*. Lakini tunasema kwa watumiaji wakubwa, makampuni ya uzalishaji, migodi, na watumiaji wa kada ya kati, na niseme tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge, ninaamini kwa mahesabu ya kitanzania mambo yetu ni afueni kidogo, tutaweka marekebisho siyo ya kuumiza mwananchi yoyote, Iakini ya kuliwezesha Shirika la *TANESCO* liendelee na sisi tuendelee kuwa na umeme. Kwa hiyo, tutafanya marekebisho hayo wakati muafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuliwe vizuri katika hili, na ndugu zangu Waandishi wa Habari twende kwa pamoja, kwamba bei hazitarekebishwa mpaka mahali ambapo tutakuwa tumejiridhisha kwamba wananchi wanapata umeme wa uhakika kusipokuwapo na mgao, tufanye marekebisho tusonge mbele. Wataalam wa uchumi wanasema umeme ukishakuwa nao hata kama ni ghali kiasi gani, Iakini unapata manufaa kutokuwa na umeme kabisa kila siku, unapoteza. Wanasema kwa ile *unit* moja, ni dola moja na senti kumi za Marekani unaipoteza katika uchumi. Sasa sisi tunaomba tusifikie hapo, ni Taifa linalokua na tunaamini tukishafikia hapo tutakwenda vizuri.

Kwa nafasi hii, naomba nitumie kuwashukuru Shirikisho la Wafanyabiashara Tanzania *CTI*, wamekuwa wa kwanza kuonyesha hili, wamesema, mkishatuhakikishia kwamba mtakuwa na umeme wa uhakika *TANESCO* na Serikali tuko tayari kuongeza viwango. Wamekuwa wa kwanza, napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza sana. Wameonyesha uzalendo wa kweli na ninaamini kwamba Watanzania watatuelewa katika kada zile nyingine kwa sababu hatutaweka mabadiliko ya kuwaumiza Watanzania, bali tutakuwa na nia ya dhati ya kuwhakikishia kwamba nchi yetu imetoka hapa iliposonga mbele kwa sababu tuna nia njema ya kuboresha maisha na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambayo tutaifanya, tunakusudia mfuko wa kuendeleza nishati ya umeme utakaotumika kama mtaji wa kuendeleza uwekezaji katika Sekta ya Umeme na Serikali inafanya kazi. Tunadhani kodi ya ongezeko la thamani upande wa *VAT*, itokanayo na mauzo ya umeme ilipwe moja kwa moja kwenye mfuko huu badala ya kwenda Hazina. Nadhani tutafikia muafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kodi ya kuagiza vipuli na mafuta ya kuendeshea mitambo, *import and exercise duty* ya kufua umeme iwe inalipwe moja kwa moja katika mfumo huo badala ya kwenda Hazina.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tukifika hapo, ninaamini kwamba tutakuwa tumefikia pazuri, na ikitokezea kwamba mvua zimenesha, itakuwa jambo la heri zaidi. Lakini hii ndio mipango tuliyonayo. Tutafanya marekebisho ili kuhimili huo mzigo tuliusema kwamba Serikali imepewa dhamana ya Shilingi bilioni 408 sasa, lakini tuendelee pia kuona namna gani Watanzania, watumiaji wa umeme kama wanavyofanya nchi nyingine, wanaweza kusaidia kuendesha uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kuelezea yale ya jumla katika eneo hili, ya mpango huu, Serikali kwa nafasi yake pamoja na kubeba dhamana ya Shilingi bilioni 408, imefanya nini? Sisi katika Wizara ya Nishati na Madini tumefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, *addendum* imesambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge, sisi tulikuwa na miradi kadhaa ambayo tulikuwa tunadhani ingetekelezwa katika mwaka huu wa fedha tumeiondoa. La kwanza, ni ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki Dar es Salaam, Shilingi bilioni 3.8, tumeufuta huo mradi. Fedha hiyo tunaelekeza kwenye Mfuko wa Umeme Vijiji (REA). (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoona, pia tumefuta miradi mingi na tumefuta kwa nia njema na hatujafuta kwa nia mbaya. Tumesema tuahirishe kwanza miradi hiyo ili iwe sehemu ya kukabiliana na hali ya udharura ambayo tunayo sasa. Matokeo yake sisi katika Wizara ya Nishati na Madini, hiyo ya Shilingi bilioni 3.8 tulikuwa na ujenzi wa Kituo cha Polisi kule Songo Songo kisiwani cha thamani ya Shilingi bilioni 1.8 kwa sababu ni kama kakijiji fulani hivi. Tumesema tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, tuone namna bora ya kutekeleza ule mradi, na kwenyewe tumeiondoa hizo fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, fedha hizi kwa ujumla, pamoja na posho mbalimbali katika ile kasma ambayo tulikuwa tumepewa, tumeiondoa Shilingi bilioni 10.3 kwenye Wizara yetu ya Nishati na Madini, tukazisambaza katika maeneo mengine likiwemo eneo la Mtaro mmoja, tuliahidi siku nyingi kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mererani, mfereji wa Disuza, ndugu zangu wachimbaji wa pale Mererani mwelewe Serikali inadhamiria. Tuliomba fedha miaka miwili iliyopita, tunafahamu matatizo ya bajeti yetu hatukuwahi kupata zile fedha, safari hii tunapeleka Shilingi bilioni 500, tukamalize kazi hiyo. Fedha nyingine tutaipeleka *TPDC* kuwaimarishia uwezo, lakini pia tunachangia katika ununuzi wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii, wakati nahitimisha kutoa ufanuzi kuhusu makakati wa kuondoa mgao Tanzania, nilikuwa napenda nitumie nafasi hii kutoa shukrani za dhati kabisa kwa wadau ambao wametuwezesha kufikia na kwenye mpango huo wa kutuhakikishia kwamba tunaiondoa mgao wa umeme. Wadau hawa ni pamoja na Shirika letu la Ugavi wa Umeme Tanzania *TANESCO*, *TPDC*, *EWURA*, *NSSF*, Benki ya Maendeleo ya *CRDB*, Kampuni za *Symbion*,

General Electric (GE) wa Marekani, Jacobsen SEMCO, Songas, IPTL, AGGRECO, na Wentworth ambao wamenunua ule mradi uliokuwa unajulikana kama ARTUMAS kule Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kufikia hapa kwa mikataba ambayo imefungwa na *TANESCO*, *TANESCO* ilikuwa imefanya majadiliano na makampuni mengi, na niseme kwa dhati kabisa, makampuni hayo, mengine bado hata leo wataendelea na mazungumzo baada ya mjadala huu. Kampuni mojawapo ambayo ilikuja kuonyesha na sisi na tulikuwa tumefurahishwa na jinsi ambavyo inaweza kusaidiana na juhudzi za Serikali kuondoa huu mgao uliopo sasa ni kampuni moja ambayo yenewe ilikuwa imekusudia kuzalisha umeme kwa kutumia meli, inaitwa *Karpowership* ya Uturuki. Wamefanya mazungumzo na *TANESCO*, mazungumzo yamechukua muda mrefu kidogo kwa sababu mitazamo na għarama ziliwu zinapishana. Lakini sisi hatujafunga dirisha la majadiliano, na tumewaambia *TANESCO*, baada ya mjadala huu, leo wanaendelea na majadiliano hapa Dodoma, tuone namna gani kama inawezekana kuingia nao mikataba.

Mheshimiwa Spika, Makampuni mengine yalikuwa yamejitokeza kama *Mantrack* nao wameoneyesha nia na wengine makampuni mengi ambayo wengine Waheshimiwa Wabunge wanayafahamu kwa sababu mengine yalikuwa yanajaribu kuwatumia nyie kuwasiliana na *TANESCO* ama kuona *TANESCO* walitambulisha kwa *TANESCO* kwamba na wenyewe wanawenza kuchangia kwenye mkakati huu wa kuondoa mgawo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la mkakati wa kuondoa mgao Tanzania, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana ndugu yangu wa karibu, Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima - Mbunge wa Mkuranga, na Naibu Waziri wa Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi naweza kusema, ukiondoa hili la kwamba ye ye tunapokuwa uwanjani ye ye anacheza katikati ya dimba, mimi ni *back*, tumeshafanya kazi nzuri sana na Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima. Tunafurahia sana. Amenisaidia sana, amekuwa ni mtu mahiri katika kutekeleza yale ambayo Watanzania wanakusudia kuyaona na kuyasikia. Ananikumbusha kule uwanjani mimi kapteni na ye ye ni nahodha msaidizi, mambo siyo haba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili liliikuwa ni eneo la mkakati wa kuondoa mgawo Tanzania. Kwa kifupi sana tena kwa mara nyingine naomba radhi, kwa muda tulionao, haitatosha kutoa ufanuzi wa hoja zilizochangiwa na Wabunge wote. Wabunge wote waliochangia mpaka sasa ni Wabunge 258, kwa hakika tunafahamu kwamba kwa taratibu za kawaida siyo rahisi kuweza kufanua kila hoja iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ziko hoja chache ambazo ningependa kusema na kwa nafasi hii napenda kumpongeza Mheshimiwa Adam Kigoma Malima kwa jinsi ambavyo ametoa mchango wake kwa njia ya ufanuzi katika baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Tunashukuru sana na mimi kwa utaratibu huo nitapitia baadhi ya hoja. (*Makofi*)

Hoja ambazo kwanza kabisa nitazipitia ni zile zilizotolewa na Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini chini ya uongozi wake Mheshimiwa January Yusuf Makamba, wametoa maoni na ushauri mzuri, tumekuwa nao kwenye Kamati. Katika mengi waliyoyasema, moja liliikuwa ni hili la mgao wa umeme, wamelisemea kweli na tunashukuru kwamba wao wamekuwa mmojawapo ya wachangiaji waliotufikisha hapa tulipo kwa maana ya mkakati huu tuliojuwa nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia walijielekeza sana kwenye eneo la uongezaji kasi ya usambazaji wa umeme kwenda vijjini, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshalielezea vizuri sana. Tuna vyanzo vingi vingine ambavyo Serikali imebuni, ambavyo sisi Serikali tunavifanyia kazi. Ukweli ni kwamba, tutafika mbali kwa muda siyo mrefu ujao wakati tunaonjeza uwezo wa kukusanya mapato na kusogea mbele kwenye huduma katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyotolewa ni Mkataba katika mradi wa Songo Songo, udurusiwe kama ambavyo Kamati ya Nishati na Madini, pamoja na Bunge hili tumekuwa tukitoa taarifa tangu mwishoni mwa mwaka jana, tulianza zoezi la kudurusu mikataba hii kwenye sekta ya

nishati. Tulilisema hili wakati tunakutana na Kamati ya Nishati ya Madini Dar es Salaam na hapa hapa Dodoma. Kimsingi, zoezi hili linaihusisha Serikali ikiwemo pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Tumeshabaini maeneo ambayo sisi tunadhani ni muhimu sana tuyafanyie kazi, tuyarekebishe, na tunalifanya hivyo kwa nia njema na wala siyo kwa nia ya kuogofya wawekezaji, hapana hata kidogo. Tunafahamu sera zetu, ziko wazi kwamba maendeleo ya ukweli ya Taifa hili yatafikiwa kwa kushirikisha sekta binafsi pia na ndiyo imani yetu mpaka kesho.

Mheshimiwa Spika, tunasema, kwa yale maeneo ambayo tunadhani kwamba kuna kasoro kadhaa tuzifanyie kazi kwa pamoja. Katika mojawapo ya hatua tulizozichukua wakati tukiendelea na zoezi la kudurusu, mikataba iliyofungwa kihalali kisheria kabisa, na tuna idurusu kwa sababu pia ni *legitimate* pia kudurusu mikataba, ni halali pia kudurusu mikataba, siyo jambo geni, hatua mojawapo tulioichukua. Kwa sasa tuna endelea na zoezi hilo la kudurusu mikataba hiyo. Leo hii miundombinu ya kusafisha na kusafirisha gesi kuja Dar es Salaam iliyopo kutokea Songo songo Kiswani mpaka Dar es Salaam inamiliikiwa na makampuni ya *Songas* pamoja na *Pan Africa Energy*. Sisi kama hatua ya haraka na ya dharura tumewaondolea ukiritimba utumiaji wa miundombinu hiyo kwa sasa. (*Makofi*)

Tumekubali tuondoe ukiritimba huo ili wazalishaji wengine wa gesi waliopo sasa, wakati sisi tunajenga bomba letu na wakati zoezi la kudurusu mikataba hii linaendelea, nao waruhusiwe kutumia miundombinu hiyo ya usafirishaji na usambazaji wa gesi. Hapa tuna kampuni ilio tayari ya *Ndovu Resources*, tumewaambia *Ndovu Resources* nao watumie hiyo miundombinu kuingiza kwenye mfumo wa usafirishaji wa gesi kuja Dar es Salaam ili itupe uhakika zaidi wa kuwa, gesi wakati wowote endapo mitambo ya *Songas* ama hata visima ambavyo vinaendeshwa na Kampuni ya *Pan African Energy* vitapata kasoro kama ilivyojiteza mwezi wa Desemba, 2010. Tumeona kwa nia ya dhati kwa hilo tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati ya Nishati na Madini ilitukumbusha umuhimu wa kuweka mkakati endelevu wa kuboresha miundombinu ya gesi na hasa Serikali kuwa na miundombinu yake, hili nimelisemea. Ilikuwa inatukumbusha kwa hatua ambazo tulizitoa kwenye Kamati. mradi wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka *Mnazi Bay* mpaka Dar es Salaam na baadaye kwenda Tanga, hilo tunakwenda nalo vizuri.

Pia Waheshimiwa Wabunge na Bunge zima walitukumbusha sana kwa ujumla umuhimu wa kuwa na kampuni yetu wenyewe kwenye upande wa Nishati inayoshiriki katika biashara ya mafuta. Hili tulilitolea ufanuzi juzi na nitumie nafasi hii kuyapongeza sana makampuni ambayo yametii amri ya Serikali na minarudia kwamba katika hili haturudi nyuma. Tanzania tunabaki kama Taifa lililo huru. Tunawakaribisha wawekezaji, waje kuwekeza hapa Tanzania kwa sababu ya kuongeza juhudhi, *ku-complement* na *ku-supplement* juhudhi zinazofanywa na Serikali, siyo kuja kuhujumu uchumi wa Taifa letu.

Sheria hizi ambazo zimeyafanya makampuni ya mafuta leo, wawe na faida wanazopipata leo, ndiyo Sheria ambazo zimewafanya waje Tanzania kuwekeza. Zisingekuwepo Sheria hizi ambazo leo mionganii mwao wanazikaidi, wasinge kujua kuwekeza Tanzania. Ndiyo maana tunasema wana haki ya kufanya biashara ya mazingira ya kisheria na *policy* iliyopo, lakini wana wajibu wa kuitii Sheria kama ilivyo. Kuna maamuzi yametolewa na *EWURA* ambayo ni chombo cha Serikali. Sitaki kulisema sana, lakini kama Sheria hiyo hiyo ya *EWURA* ndiyo imewajengea mazingira ya wao kufanya kazi vizuri na imetoa utaratibu wa kupeleka malalamiko yao, iweje leo inapofikia eneo ambalo wanahisi kwamba wao linawagusa wakatae kuitii Sheria ambayo inawafanya wafanye biashara Tanzania? Hilo halitakubalika hata kidogo!

Mheshimiwa Spika, naipongeza *EWURA*, kwani jana ilichukua hatua ya kuisimamisha miezi mitatu kampuni ya *BP* na Serikali tunaunga mkono jambo hilo na wote ambao watachezea mkono wa Sheria na wananchi nawahakikisha kuwa Serikali iko makini, tunachukua tahadhari zote kuhakikisha kwamba nchi haitumbukii katika mgogoro wa ukosefu wa mafuta. Yako mambo ya kuyasema hapa na mengine hatutayasema hapa, lakini tahadhari ambazo Serikali inazichukua na wasitikise kiberiti wakidhani katika hili kuna kurudi nyuma, tunawaambia wachukue hatua za kweli za kisheria, waende wakate rufaa kwenye *Fare Competition Tribunal*, siyo *ku-lobby* kuitia

kwa baadhi ya Watanzania ndani ya nchi yetu. Sheria ni msumeno, itakata pande zote, haitabagua na wala hawana pa kujificha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya COPEC, Bunge hili Tukufu la Tisa liliishauri Serikali tuanzishe, na ni kweli tulikuwa na mchakato, umekamilika, ina leseni. Itaagiza mafuta kwa niaba ya Watanzania. Nataka niseme kwamba kampuni ya COPEC ambayo ni kampuni tanzu kupitia Shirika la Maendeleo ya Mafuta ya Petroli na TPDC haiendi kuondoa uhalali wa wafanyabiashara binafsi waliopo katika soko, inakwenda kushindana nao. Hofu ya nini? Taifa hili litaendelea kujengwa na wenye moyo na wanaopenda maslahi ya wengi. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inapenda maslahi ya wengi, haitarudi katika hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru kwa maoni na ushauri mzuri tulioopata kutoka kwenye Kambi Rasmi ya Upinzani na Upinzani kwa ujumla. Yako mengi wameyasema hapa, sitapata muda kupitia hoja kwa hoja na kwa kusema hivyo sijaribu kuhalalisha kwamba wakati wa vifungu shughuli nzima ifanyike. Ninaomba twende kwa pamoja, lakini kwa nafasi hii naomba niseme, wakati tunawasilisha bajeti yetu, Waheshimiwa Wabunge kama ilivyo kibinadamu mmebaini baadhi ya makosa mbalimbali kwenye hotuba yetu. Mimi ndiye mwenye dhamana, sina pa kujificha katika hilo, iwe nimesababisha mwenyewe au imesababishwa na Watendaji wangu. Naomba radhi sana kwa makosa ya kiuchapaji na vinginevyo mliyoyabaini katika hotuba yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie kwamba leo nawasilisha bajeti ya nne katika Serikali na ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, ni ngumu kuamini lakini kwa yale ambayo yamejitokeza pengine yamenigusa kuliko ambavyo yamewagusa Waheshimiwa Wabunge. Yapo mambo ya ajabu yametokea nikiwa katika Wizara hii ya Nishati na Madini, lakini tunaamini kutenda kosa siyo kosa, lakini naamini kurudia kosa ni tatizo kubwa. Tumejifunza kutokana na ushauri na maoni yenu. Ninawaahidi mara nydingine, Mwenyezi Mungu akijaalia, tutafanya bora kuliko ilivyo sasa. Kwa dhati kabisa nakuomba radhi Mheshimiwa Mama Anna Malecela. (*Kicheko/Makof*)

MJUMBE FULANI: Ya chai! (*Kicheko*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Ya chai sisemi mimi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, haiingi akilini kutaja Jimbo linguine, lakini miradi ikawa mingine. Katika akili ya kawaida tunaomba radhi sana. Lakini tumeyaona, Mheshimiwa Anna Malecela miradi yako ipo umeitaja, inatekelezwa.

Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed alinyanya baada ya mimi kuwasilisha, akapiga utaratibu! Mheshimiwa Keissy nakushukuru, ulisaidia kubaini kosa. Habari ya nguzo inabeba dhamana hiyo kwa dhati, ina gharama zake kicutendaji. Lakini kama nilivyosema, sina pa kujificha, katika hili, ni la kwangu na mimi na Watendaji niachieni, tutaendelea kulifanya kazi.

Pia Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, alisema kwa uchungu, nafahamu! Lakini miradi inatekelezwa, kasoro zilizoonekana kwenye taarifa jinsi ilivyoripotiwa haikuwa kwa nia mbaya, ilikuwa ni kwa nia njema tu kwamba tunaendelea kufanya kazi kwa kuzingatia yale ambayo kweli katika maeneo ya kazi yanafanya.

Katika hili la Mheshimiwa Anna Malecela, hoja ilikuwa kwamba katika Jimbo la Same Mashariki hakuna miradi ya umeme inayotekeliza na REA. Aidha, vijiji viliviyotajwa katika miradi wa usambazaji wa umeme vijijini viko Same Magharibi na siyo Same Mashariki. Ni kweli miradi inayotekeliza na REA na TANESCO fedha zinatoka Serikalini, katika Jimbo la Same Mashariki TANESCO imeshaanza kutekeleza miradi ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme kijiji cha lvuga ambayo *transformer* ya KVA 100 imeshafungwa na mradi unakaribia kukamilika. Kupeleka umeme Kijiji cha Mpini ambapo *transformer* yenye uwezo wa KVA 100 imeshafungwa na mradi unaendelea. Upelekaji umeme katika Kijiji cha Bwambo umekamilika. Maombi ya kupeleka umeme kwenye maeneo mengine

aliyoyataja Mheshimiwa Anna Malecela yameshapokelewa na kuwekwa kwenye mipango ya utekelezaji kwa ruzuku kutoka *REA* ambapo utekelezaji wake utafanyika. Hapa nina jedwali lingine ambalo kwa sababu ya uwezo amba mmetuongezea tukachukue fedha kwenye vyanzo mbalimbali, vyanzo ambavyo kwa utaratibu wa kawaida haviwezi kuonekana katika bajeti hii, lakini tutavitolea taarifa wakati wa utekelezaji wa mwaka huu wa fedha. Miradi hii ni pamoja na miradi ya Waheshimiwa Wabunge itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la madini, yako mambo mengi yamesemwa lakini hoja moja kubwa ilijojiteza ni kwamba Taifa halifaидiki na migodi ya madini. Naomba kwa dhati niseme kwamba wapo wataalamu wengi wamefanya kazi kwenye Sekta ya Madini hapa, sisi pamoja na uchanga wetu, pamoja na kasoro zilizokuwepo, bado yako manufaa tuliyoyapata kwenye migodi iliyopo.

Mtakumbuka kwenye mpango wa maendeleo amba Bunge hili limeuridhia, lakini pia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete wakati anazindua Bunge hili la Kumi mwezi Oktoba, 2010 alitukumbusha kwamba kati ya mwaka 2005 mpaka 2010 Sekta ya Nishati ilikuwa imechangia mapato kwa Serikali kwa niaba ya Watanzania kwa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 4.7. Ukizipiga kwa hesabu za Kitanzania ni shilingi triliioni kadhaa. Ninachotaka kusema ni nini?

Pamoja na kasoro zilizokuwepo, kikubwa ni kwamba mikataba iliyofungwa kipindi kile, kwa vyovyyote vile ilikuwa na kasoro kadhaa, lakini tulikuwa tunatoka kwenye mfumo tofauti wa uendeshaji wa uchumi kutoka kwenye uchumi amba Serikali ndiyo inadhibiti shughuli za uzalishaji uchumi hodhi tukawa tunakuja kwenye uchumi huru wa kushirikisha sekta binafsi. Kwa hiyo, kwa sababu ya hofu ya kilichokuwepo miaka ya nyuma na ilikuwa kwa nia njema tu, tukajikuta wakati mwingine tumetoa *over protection* kwa makampuni ya uwekezaji katika sekta hii. Tullilibaini hilo. Kumekuwa na Tume kadhaa zimeundwa ili kupitia Sera ya Madini ya mwaka 1997 na Sheria yake ya mwaka 2008, ndiyo maana ilipofika mwaka 2009 na hitimisho la mapitio hayo ilifanywa na Tume ilioongozwu na Mheshimiwa Mzee Jaji Mark Boman na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu walikuwa Wajumbe wa Kamati hiyo.

Tukaja na Sera ya Madini mpya ya mwaka 2009 na mwaka jana tukatunga Sheria mpya ya Madini ili pamoja na mambo mengine kuboresha zile kasoro ambazo tulikuwa tumezibaini miaka ya nyuma. Ni kweli yapo mambo hapa tumekuja nayo hayakuwepo kwenye Sheria na sera za zamani. Kwa mfano, ushiriki wa Serikali kama mwekezaji tofauti na ilivyokuwa zamani, sasa kwenye Sheria mpya tumesema Serikali kwa migodi yote inayokuja sasa lazima iwe na kiasi ambacho inakishikilia na sababu kubwa moja tu kwamba madini haya kwa Tanzania hata kama hatuna uwezo wala taaluma hiyo ya kuyachimba sisi wenyewe, bado haya ni ya kwetu, hayako nchi 'X', bali yako hapa Tanzania. Hilo linatupa uhalali wa sisi kushiriki kwenye sekta hiyo, tumefanya hivyo na vifungu tumeviweka.

Mheshimiwa Spika, pia tumewaambia, unapoanza kuzalisha tu na hasa ukishamaliza kurudisha gharama zako haraka haraka ujisajili kwenye soko la ndani ili Watanzania wengi waweze kununua hisa kama ambavyo wanafanya kwenye makampuni mengine, ni mojawapo ya maingizo mpya ya vifungu vya Sheria ambavyo huko nyuma havikuwepo, lakini tumebadilisha formula ya ukokotoaji wa mrabaha.

Mheshimiwa Spika, tumesema mrabaha uliokuwepo kwenye baadhi ya madini ubadiilike. Kwa mfano, kwenye dhahabu, tumetoka kwenye 3% mpaka 4%, lakini ile formula yake tukasema zamani mzalishaji au mgodi unaondoa gharama zake zote za usafirishaji na usambazaji, lakini sasa tunasema tuna calculate on gross, inatuongezea.

Kwa mikataba iliyopo sasa kwa utaratibu wa kisheria, huwezi ku-*impose*, sisi ni nchi ambayo inathamini utawala wa Sheria, yaani *Rule of Law* na hii ni sehemu ya utawala bora, yaani *Good Governance*. Kwa yale makampuni ambayo yalikuwa na mikataba, tumejhajiliana katika Mikutano ya mwisho, makampuni haya yaliyopo hapa Tanzania kuwa wanapeleka taarifa za kampuni zao kwenye stock of exchange, tumejbaliana kwamba wiki ya kwanza ya mwezi wa Tisa ndiyo mwisho wa ratiba ya kumaliza huu mjadala ili waanze kulipa mrabaha kwa formula

mpya na hilo ni jambo la kheri. Nafahamu yapo mawazo wangesema, kwa nini tusingefanya *imposition*? Kwa nini tusingeweza tu tukatamka, mkishaingia katika utaratibu wa kuendesha nchi kwa kuzingatia utawala bora na Sheria ikawa ndiyo mwongozo mkubwa katika kuongoza jamii? Lazima pia ukubali wajibu na majukumu ambayo katika wakati mbalimbali umeshajifunga.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Watanzania kwamba hili linakwenda vizuri na sioni namna yoyote ya makampuni haya hatimaye kwa njia ya mazungumzo, narudia kusitiza tena kwamba sioni namna yoyote kwa njia ya mazungumzo makampuni haya kushindwa kuingiza katika utaratibu mpya wa kulipa mrabaha kwa utaratibu mpya. Hakuna namna hiyo, kwani mazungumzo yanakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, katika hili pia nataka nisema kwamba tumefanikiwa kuyafanya baadhi ya makampuni yaanze kulipa kodi ile *Cooperate Tax* ambayo ndiyo ilikuwa kilio cha Watanzania wengi. Kampuni ya *Resolute* kwa Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla inalipa sasa kodi ya mapato ya 30%. Kampuni pia...

(Hapa Kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

SPIKA: Kengelel ya pili hiyo!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, hoja ni nyingi kweli! Wachangiaji ni 258. Kwa hiyo, kumjibu kila aliyechangia kwa nafasi yake, haitawezekana kwa wakati huu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa jinsi ambavyo kwa kipindi hiki mmetupa *support*, mmetuunga mkono, mmetutia moyo na mmetutia faraja na hatimaye tumefikia hapa tulipo. Tuko tayari kutoa ufanuzi kwa hoja zote zilizotolewa kwa utaratibu wa kawaida...

SPIKA: Haya ombo kutoa hoja!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Kabla hatujaingia hatua nyingine, napenda kwanza niwaache muweze kutafakari ili niwatambulisse wageni.

Wageni tulionao hapa Bungeni ni Balozi wa Marekani - Mheshimiwa Balozi Alfonso Lenhardt, ameongozana na Ndugu Elizabeth Pelletreau - *Chief Political and Economic Section*, halafu yupo na msaidizi wao *Political Assistant* - Ndugu Tina Mdobilu. (*Makofii*)

Pia tunaye Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) -Mheshimiwa Ludovick Uttoh anaafuatana na Mkaguzi Mkazi, Ofisi ya Bunge - Ndugu Fortunatus Donge.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini ambaa ni Kaimu Katibu Mkuu, Ndugu Eliakim C. Maswi, Mwenyekiti wa Bodi ya *TPDC* - Ndugu Gen. Robert Mboma (Rtd), yupo Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO* - Ndugu Ramadhani Hatibu. Pia yupo Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO* - Mheshimiwa Semindu Pawa. Mheshimiwa Semindu Pawa alikuwa Mbunge machachari humu ndani siku zake. Pia yuko Mwenyekiti wa Bodi ya *GST* - Prof. Idris Kikula na pia yuko Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Madini - Prof. A. H. Mruma. (*Makofii*)

Halafu Mheshimiwa Naibu Waziri ye ye mgeni wake ni Mama yake mzazi na familia yake, Mama yake anaitwa Lenasia Mariam Vivao, lazima ni-declare *interest* huyu ni Dada yangu. Yupo na wageni wengine waliofuatana na Mama.

Pia wageni walifika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, ni wanakwaya 26 wa *Kilimanjaro Revival Choir* kutoka Moshi. Karibuni sana. Ahsanteni sana.

Tuna waandishi wa habari 10 kutoka Kampuni ya *Made in Africa TV* inayoandaa kipindi cha Daladala wakiongozwa na Ndugu Christina Mbunda au Bi Kiroboto, ameongozana na mtangazaji mwenzake Ndugu Daniel Kijo. Hawa watu ni Maarufu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu tuna wanakwaya wengine 35 wa Usharika wa Nkuhungu pamoja na wageni wao kutoka Dayosisi ya Kaskazini Arusha, jimbo la Karatu. Hapo walipo wasimame. Okay! Nkuhungu ni hapa Dodoma, kwa hiyo, wamekuja na wageni wao kutoka Arusha. Karibuni sana na tunawapongeza kwa kuweza kupata nafasi ya kufika hapa. (*Makofi*)

Kuna Mkurugenzi wa Mfuko wa Habari Tanzania (*TMF*) ndugu Ernest Sungura ameambatana na mke wake. Yuko wapi? Aah, Wako pale. Huyu ni Mkurugenzi wa Mfuko wa Habari Tanzania. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunao pia wachimbaji wa madini wadogo wadogo 32 kutoka Kijiji cha Sambaru, Kata ya Mangonyi, Jimbo la Singida Mashariki kwa Mheshimiwa Tundu Lissu. Wako wapi? Aah, Okay! Ahsanteni na karibuni sana. Mmekuja wakati mzuri wa kuweza kusikiliza maelezo ya mambo yanayowahusu. Karibuni sana na tunawatachia heri. (*Makofi*)

Namtangaza Mheshimiwa Ramadhan Dau, kutoka *National Social Security Fund (NSSF)* kwa sababu yeye pia ni mdau katika huu mpango mkakati hapa. Yuko wapi? Aah! Leo tumekusahau kwa sababu umeavaa uliviyovaa. Basi karibu sana! Tunaomba hilo kusudio lenu liweze pia kufanikiwa ili lioneze nguvu katika shughuli zetu. Nadhani wageni wengine sikuwatangaza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya shughuli hii, Kamati yetu ya Kudumu ya Nishati na Madini, imewaruhusu kuijunda katika Kamati ndogo, kusudi waweze kufuatilia suala zima la matumizi ya gesi na hiyo hiyo kampuni inayoitwa *Pan African Energy* ya *Songas*. Nimewaruhusu baada ya kuahirisha Bunge hili, hiyo Kamati ndogo itakwenda kufuatilia yale yaliyokuwa yanazungumzwa kuhusu kampuni hii, kuhusiana na matumizi ya *Songas*. Kwa hiyo, nimewaruhusu watafanya hivyo. Kutokana na hiyo shughuli nydingine, wataripoti kwangu kwa sababu siyo Kamati teule.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunajadili bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, *Inspector General* wa Polisi (*IGP*), aliahidi kugawa vipeperushi kwa Waheshimiwa Wabunge wote, vinavyoelezea kampeni inayoendelea sasa hivi ya kushawishi utii wa sheria bila kushurutishwa ili kudumisha amani, usalama na utulivu nchini.

Baada ya kushauriana na sisi, tukaona kwamba, kugawa vipeperushi ni vizuri, lakini tulifikiri kwamba muwe na kikao na yeye kesho kuanzia saa 4.30 katika Ukumbi wa Msekwa, aweze kueleza kwa undani juu ya hiyo kampeni na nyie muweze kutoa maneno machache au ushauri itakavyohusika. Kwa hiyo, kesho saa 4.30 Wabunge wote tutakuwa na hicho kikao pale katika Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kusikiliza huu mpango ambao, *IGP* ameuanzisha, halafu na nyie muweze kushiriki kwa kutoa changamoto zenu.

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo huo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo - Mheshimiwa Boniface Simbachawene, anawatangazia wajumbe wa Kamati yake kwamba hiyo kesho wawe na kikao. Nadhani muda, watakubaliana wao kwa sababu kutakuwa na hii shughuli, basi watakubaliana wakutane wapi, kwa sababu wana wageni wao walioalika waje kuwasikiliza. Kwa hiyo, hawana namna ya kuahirisha. Kwa hiyo, mtapanga kadri mtakavyoona inafaa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, tunaendelea na hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini

Kif. 1001 - Administration and General Sh. 3, 960,303,500/=

MWENYEKITI: Simameni wote tu, simameni wote. Hata sijui nianze wapi! Haya nitakuwa nataja kwa row. Nyie mnaweza kukaa kwanza, nakwenda kwa row kwa sababu hii inanisaidia mimi nikienda row ya kwanza, ya pili, najua nikiita hapa inakuwa rahisi. Kwa hiyo, naomba mkae nianze na row hizi. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Wengine ni wafupi siwaoni. (*Kicheko*)

MHE. FREEMAN E. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia hoja hii muhimu. Wakati Waziri Mkuu anaahirisha hoja hii hapa Bungeni, tarehe 18 Agosti, 2011 alisema kwamba Serikali imetambua na imethamini michango ya Wabunge na kwamba Serikali inaiondoa hoja ama inaomba *extension of time* ili wawze kwenda kurekebisha na kuchukua mawazo ya wadau, jambo ambalo ilikuwa ni la msingi sana. Lakini Waziri Mkuu katika kauli yake alisema kwamba watashirikisha Kamati mbalimbali zinazohusika za Bunge, ikiwa vilevile ni pamoa na kujaribu kutafuta mafungu ya fedha kutoka vyanzo mbalimbali, kuwezesha kupata fungu la kutosha kusimamia miradi ya umeme kuondoa mgao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi na hili suala linalohusu bajeti, nilitegemea kwa wakati mmoja au mwingine Kamati yetu ingeshirikishwa katika kujadili suala hili, lakini kwa bahati mbaya hali hiyo haikujitokeza. Sasa ningependa tu Mheshimiwa Waziri atuhakikishie jambo moja la msingi sana. Kwa njia nyininge Serikali imekirikisha Kamati mbalimbali zinazohusika za Bunge, ikiwa vilevile ni pamoa na kujaribu kutafuta mafungu ya fedha kutoka vyanzo mbalimbali, kuwezesha kupata fungu la kutosha kusimamia miradi ya umeme kuondoa mgao wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ni Serikali hii hii na Wizara hii hii iliyotufikisha tulipofika leo. Katika huu mpango wa dharura unaozungumziwa hapa halijajitokeza kwa njia yoyote swalii la kwamba Serikali inakwenda ku-*manage* hili tatizo vipi, kwa sababu tatizo lipo, mipango imeletwa je, ni watu hawa hawa ambao bado tuna hofu nao wanaokwenda kulisimamia jambo hili kikamilifu mpaka hatua za mwisho za utekelezaji wake au kuna mpango wa dharura basi kama ambavyo tunakuwa tunashauri mara kwa mara Serikali ikajaribu kuunda *A National Task* ambayo ingeweza kuisaidia Serikali kusimamia jambo hili kiukamilifu ili lisiwe na madhara makubwa sana na mapana kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo tunakopa fedha nyingi sana. Ni kweli tunahitaji umeme na ni lazima hatua zichukuliwe. Lakini kiwango kinachokopwa ambacho Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa kwamba Serikali inabeba mzigo huu. Serikali ina fedha kwa niaba ya wananchi, sio fedha zenu, sio fedha za Serikali ni fedha za Watanzania. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tunapobeba mzigo wa fedha kusema ni Serikali inabeba ina maana tunakiri kwamba tunawabebesha wananchi mzigo na ni mzigo unaotokana na uzembe katika *planning*, hakuna *planning* tunafanya mipango ya dharura, Bajeti inakataliwa hapa tunakwenda tena kufanya *plan*. Katika kipindi cha wiki tatu tunakuja na mipango kama vile Serikali mwanzoni ilikuwa haipo au pengine ilikuwa likizo. (*Makofii*)

Sasa tunakopa fedha nyingi mno na hatujaeleza kwa kina *impact* ya mikopo hiyo ni nini? Hii mikopo tunayoikopa kutoka kwenye Benki za Biashara katika *terms* za kibashara, hatujapewa kwa kinagaubaga hapa, hii mikopo ni ya kitu gani, kwa riba ya kiwango gani. Kwa sababu TANESCO hata kama ni TANESCO inakopa, TANESCO ni Shirika la Umma na TANESCO kama ni Shirika la Umma ikikopa mzigo hatimaye unakwenda kwa mlaji na mlaji ni Tanzania wa kawaida na hata TANESCO ikishindwa kulipa maana yake kama *government* imetoa *guarantee* ina maana kwamba Serikali itawajibika kulipa deni hilo, huo ndio ukweli wa mambo. Kama ikilipa TANESCO ikilipa Serikali wote ni Watanzania wanalipa. Sasa Mheshimiwa Waziri atuhakikishie katika upande wa pili kinafanyika nini basi kwa misingi hiyo kutekeleza hilo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante umemaliza vizuri, lakini moja hatukukataa makadiro tuli-suspend. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi kwenye swali la Mheshimiwa Mbewe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kama ifuatavyo:-

Kwanza namheshimu sana Mheshimiwa Mbewe, hoja zake naelewa anachokisema. Lakini nataka niseme tu, Serikali imebeba dhamana hii kwa niaba ya Watanzania. Ni kweli ni fedha za Watanzania lakini kwa manufaa ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mbewe ni mfanyakishara, tena mfanyakishara maarufu, anafahamu taratibu za mikopo, mkopo haukopwi kama huwezi *justify* kusudio la mkopo huo. Kwa hivi mikopo ambayo Serikali imedhamini *TANESCO* imezingatia vigezo vyote vya kibiashara na hatimaye kuzingatia manufaa ya kiuchumi kutokana na mikopo hiyo. Lakini Mheshimiwa Mbewe anasema nani anakwenda kusimamia. Tumesema sisi kama Wizara, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kuhakikisha kwamba Shirika la *TANESCO* linafanya yaliyokusudiwa kwa niaba ya Watanzania pamoja na washiriki wengine kuitia sekta binafsi. (*Makofii*)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya msingi. Lakini nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba wakati Waziri Mkuu anaomba hoja hii iahirishwe hapa Bungeni alisema; "Serikali inakwenda kuangalia namna ya kupata fedha kutoka kwenye Bajeti yake kwa kujaribu kwenda kuchukua mafungu mbalimbali yasiyo ya lazima katika matumizi ya Serikali."

Sasa tunakwenda kukopa ni tofauti na kauli aliyokuwa ameitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba hatukwenda kupunguza yale matumizi ambayo hayakuwa ya lazima Serikalini, ila tumekwenda kuingia mkopo na deni kama Taifa. Lakini vilevile nimwambie pamoja na kwamba kuna *justification* ya mkopo, mkopo huo lazima uchukuliwe kwa tahadhari. Kuna hofu kwamba mikopo hii imechukuliwa kwa hatua za haraka haraka kwa ajili ya *ku-solve* tatizo, lakini ninachotaka kuwatahadharisha Waheshimiwa wa Serikali ni kwamba tusitatuve tatizo kwa *ku-create* matatizo mengine mapana zaidi. Tu-*solve* matatizo kwa kuyapunguza zaidi na sio kuya-*amplify*. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na la pili. Sehemu yake ya nyongeza ya maswali ilikuwa na sehemu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwathibitishie Watanzania kuitia Bunge lako Tukufu imani aliyonayo Mheshimiwa Mbewe ni potofu kuhusu matumizi na uhalali wa mikopo ambayo dhamana ya Serikali imeichukua. Nawahakikisha Watanzania kwamba Serikali ipo makini na kwa sababu nafahamu kibinadamu wapo wanaoamini baada ya kuona, lakini wapo wanaoamini kwa kutumainishwa. Mheshimiwa Mbewe kama utapenda kuamini kwa kusubiri kuona, subiri uone. Lakini Watanzania nawaomba waendelee kuamini kwa kutumainishwa. (*Makofii*)

Hili la kwanza kuhusu mikopo iliyochechukuliwa, nataka nithibitishe ile misamaha tulioisema Serikali imeiondoa kwenye mafuta yatakayotumika kuzalisha umeme, kwa upande mwininge Serikali imeamua kwa dhati kuondoa uwezekano wa kupata mapato kutoka kwenye vyanzo vya kodi kwa ajili ya kuwa na umeme wa hakika ili hatimaye utuongezee uwezo wa kuzalisha umeme zaidi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nataka nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali kwa kuja na mpango huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Ngeleja mpango huu uliouleta kama ukiutekeleza na naamini utautekeleza umeme ukawaka, mgao ukaisha, ugomvi na mimi umekwisha na hutansikia nakuandama tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu sisi ilipendekeza kwamba Serikali jje na mpango wa dharura wa megawati 500. Serikali imekuja na mpango wa dharura wa megawati 572. Sasa kuna mihimili mitatu tofauti iko Bunge, Serikali na Mahakama. Sisi Bunge tumefanya kazi yetu ya kuishauri Serikali kuchangia mawazo, kutoa maoni na ushauri. Nataka niwahakikishie kwamba kwenye Kamati yetu kazi hii tumeifanya vizuri mno na kwa kina na kwa umakini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kiasi kikubwa sana imezingatia yale tuliyoyasema, sasa watekelezaji ni wao. Mimi naomba niwasihii Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa mpango huu kwa jinsi uliviyotengenezwa na Serikali tuwape nafasi wakautekeleze. Kwa sababu hapa tutachangia, tutashika mshahara, lakini hasa katika mpango huu hakuna cha kupika, umeshapikwa huu ni kwenda kuutekeleza tu. (*Makof!*)

Sasa isipokuwa kuna maangalizo ambayo ndio lazima tuyatoe kwa Wabunge kwamba mpango mmeutengeneza, lakini suala la gharama ailosema Mheshimiwa Mbewe ni suala sahihi kabisa, kwamba umeme tunautaka lakini ni kwa gharama gani. Majibu ni rahisi tu kwamba umeme katika mpango huu ambaao ni wa gharama kuliko wote ni umeme wa *Aggreko* ambaao ni senti 42 za dola za Kimarekani kwa kila *unit*. Kiuchumi kwa kila umeme ambaao hauzalishwi, kwa kila *kilowatt hour*, kila *unit* moja ambayo haizalishwi gharama yake ni dola 1.10. Kwa umeme aghali hapa bado ni rahisi kuliko usipokuwepo. Kwa sababu umeme ukiupima tu kwa *transaction* unavyoununua lakini huupimi kwa thamani kwa uchumi wake unakuwa vilevile unakosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachowashi wenzetu Serikalini kwamba ni kweli katika kipindi cha miezi minne shilingi bilioni 408 ni nyingi na sehemu kubwa kama asilimia 80 ya fedha hizi zinaenda kwenye ununuzi au gharama ya mafuta kwa ajili ya kuendesha mitambo hii. Kwa hiyo, cha kutazama hapa kwanza ni utaratibu wa kupata mafuta ya kuendesha mitambo hii kwa sababu hapa ndipo penye tatizo, bei ya umeme ni ndogo. Kwa mfano hapa *Aggreko* umeme wao wanauza senti 5, *IPTL* senti 4, *Simbion* senti 5, gharama kubwa ni kwenye mafuta na kwa sababu kwenye mpango huu mafuta ni wajibu wetu sisi Serikali... (*Makof!*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Dakika tano zako tayari.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Ohooo! Nilikuwa sijamaliza.

MWENYEKITI: Dakika tano tu sio nydingi sana kwa hiyo, mijipange vizuri.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Mheshimiwa January Makamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kama ambavyo amekuwa akiusisitiza tumeupokea. (*Makof!*)

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nadhani Mbunge mwenzangu aliyetangulia kuongea, ameongea kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la *logistics*. Kwenye mpango huu Serikali imepanga kuleta megawati 110 hapa Dodoma, megawati 50 Arusha za mafuta. Ukitaka umeme uzalishwe wa megawati 100 kwa mafuta maana yake ni kwamba uwe na malori 25 yanapakua na 25 yanapakia. Maana malori 50 kwa wakati mmoja yapo barabarani ili mtambo huu hapa Dodoma ufanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Serikali naomba Mheshimiwa Waziri mlitazame kama hili linawezekana kuwa na malori 50 kwa wakati mmoja yanayoleta mafuta. Vinginevyo mnaweza mkaweka mpango huu lakini ukashindikana kutokana na *logistics* kuwa ngumu. Vilevile Arusha *distance* ni ndefu. Mheshimiwa Magufuli ataruhusu malori ya mafuta 50 yawe kila siku yapo barabarani yanaleta mafuta Dodoma na kwa mazingira ya barabara zetu hizi, kwa hiyo ilikuwa ni angalizo lingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, dharura sasa ifike mwisho. Mpango huu wa dharura uwe wa mwisho usiwe na dharura tena. Kuanzia sasa hivi ni mipango endelevu. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu utoe kauli Bungeni hapa kwamba mpango huu wa dharura uwe ni wa mwisho kwa sababu dharura ndio vichochoro vyta rushwa, wizi na ufisadi. Ahsante. (*Makof*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ningependa kupata ufanuzi nianze kwa kunukuu kwa kifupi sana kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anatoa hoja hii kuahirishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri nilioutoa ni wa msingi sana. Moja mmesema Serikali nunueni mitambo na tusitafute visingio vyta fedha kwamba tafuteni kila mbinu huko kateni posho zenu, kateni vitu gani, nendeni mkatazame magari mnayotumia, punguza, tazameni *OC* kikamilifu mtaona kule ndani matumizi mengine ambayo mkiamua kwa dhati mkayaondoa tunawenza kununua mitambo ya uhakika na kusaidia kuongeza uwezo wa mafuta. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa dharura tulioletewa mbele yetu auhusishi kukata posho, kupunguza magari, kupunguza matumizi yote ya dharura bali inahusisha kukopa. Sasa ningetaka kupata ufanuzi. Nakubali kwamba Serikali imetoa ushauri wa Kamati na imechukua ushauri vilevile kwa kiwango kikubwa sana kwa Kambi Rasmi ya Upinzani. Lakini kuna ushauri mmoja wa msingi sana hamjauchukua kabisa. Bajeti mbadala illeleza vilevile vyanzo mbadala vyta fedha ambayo Serikali ingeweza kuitumia bila kuongeza mzigo kwa walipa kodi kujikwamua katika hii dharura. Tilitaja kwa kiwango, mapato ya madini ambayo yangeweza kukusanya kwa haraka shilingi bilioni 100. Tulizungumza fedha za nchi yetu za umeme zilizoko kwenye *extra account* ya *BOT* shilingi bilioni 200. Tulizungumza kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kile kifungu ambacho hakijapangiwa matumizi. Tulizungumza vilevile mapato yanayotokana na ongezeko ambalo hatuliungi mkono la kodi kwenye mafuta ya taa, tulizungumza vilevile maeneo mengine ya anasa ya posho ya kupunguza ambayo kwa ujumla wake yangezidi kiwango cha shilingi bilioni 500 kinachohitajika kwa mpango huu.

Sasa uamuzi wa Serikali umeacha haya mapendekezo yote umeona pendeleko la haraka la kuchukua ni kwenda kukopa Benki. Katika mkakati amba pamoja na maelezo yote mimi nautafsiri kama tusipokuwa makini kwenye *ku-manage* na ningependa Wizara ikubali tu kwamba pamoja na hili litakalopitishwa hapa kwenda kufanya kazi kupunguza kiwango cha *terms* za mikopo na kadhalika kama usipokuwa *managed* vizuri unaweza kunyonya damu na rasilimali za Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukubali maelezo ya kiuchumi kwamba kutokuwa na umeme kunaweza kuwa ghali kuliko kuwa na umeme. Ni ukweli ulio wazi umeme wa gesi unazalishwa kati ya senti tano mpaka saba kwa gharama ya kuzalisha umeme wa gesi. Umeme wa mafuta unatoka kuanzia senti 30 mpaka senti 42 katikati hapo kiwango kikubwa cha fedha *in between* ni kiwango cha *capacity charges* na kiwango cha mafuta kutokana na kutoshughulikia udhaifu kwenye mfumo mzima wa uingizaji na uhifadhi wa mafuta. Kwa gharama za shilingi bilioni 408 tunazokwenda kuziingia ni gharama ambazo kama Taifa tunawenza kuziepuka. (*Makof*)

Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufanuzi pamoja na kuwa ameleta ombi hapa la shilingi bilioni 408 ni mkakati gani wa nyongeza amba Serikali inao kwenda kupunguza ili katika kipindi hiki cha dharura cha miezi minne tusitumie shilingi bilioni 408 badala yake tuwe na namna ya kupunguzia mzigo mkubwa sana amba utaliangukia *TANESCO* na hatimaye utakuja kuangukia wateja siku za usoni. (*Makof*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kwa swali la Mheshimiwa Mnyika, Waziri Kivuli katika sekta hizi za Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Kwanza tunakumbushana tu mpango huu ni wetu sote. Mpango huu ni kwa manufaa ya Watanzania, lakini pili, Mheshimiwa Mnyika anasema hajaona popote ambapo Serikali imefanya kwa kadri ilivyowezekana kuhakikisha kwamba yenyewe inashiriki katika utekelezaji wa mpango mpya kwa maana ya kutoka kwenye vyanzo vyake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mnyika ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini tumekuwa naye. Katika miradi niliyokuwa naisema na hasa katika miradi ambayo itatekelezwa kati ya mwezi Januari hadi mwezi Desemba mwaka 2012 kuna mradi unaitwa *Jackson* awamu ya pili megawati 150. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mnyika anafahamu, gharama yake ni kiasi kisichopungua shilingi milioni 165 dola za Kimarekani, Serikali imesema itadhamini, Serikali itaisaidia *TANESCO* kupata umeme na ule mradi unakamiliika mwezi Machi, 2012. Mheshimiwa Mnyika anajua ukweli huu, kwa nini hii dhana ya kutaka kuwaaminisha Watanzania hapa tunaongea kwa niaba ya Watanzania kwamba pengine kutumia mikopo si njia sahihi sana inanipa taabu kidogo kuelewa. Leo hii Taifa kubwa ambalo linafahamika duniani ndio Taifa la kwanza kwa nguvu ya kiuchumi Marekani wamefikia mahali wanaongeza uwezo wao wa kukopa katika Bajeti zao. Hivi sisi Watanzania tuna uwezo gani wa kushangazwa na hali iliyoko hapa ambayo imejitokeza. Naomba Mheshimiwa Mnyika uisemee miyo yetu. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake na ni kweli mimi ni Mjumbe wa Kamati na naelewa ninachokizungumza na nakizungumza kwa nia njema sana ya kujenga. Tuanze na hili la megawati 150 za *Jacobson* ambazo zitakuja mwakani. Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake ameelleza bayana kwamba Serikali itadhamini kukopa. Kwa hiyo, tafsiri yake ni kwamba bado hatujaamua kwa dhati kama Taifa kuangalia kwa rasilimali zetu tulizonazo tunaweza kupata pesa kiasi gani bila kukopa. Mikopo ya kibashara ina riba za kibashara, ina gharama kubwa za kibashara ambazo zitakuja kuwa mzigo kwa *TANESCO*. Sasa *TANESCO* ina mzigo wa ku-service deni la shilingi bilioni 300 mnakwenda kuongeza deni lingine kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana kabisa na maelezo kwamba tunahitaji kukopa na ni jambo zuri sana kukopa lakini tunakopa tukimaliza vyanzo vyetu. Marekani na nashukuru Balozi wa Marekani yupo hapa ananisikia na anachokisema. Marekani imefikia hatua ya kuweka *ceiling*. Ulisikia ubishani kule Marekani kwamba wanataka kuongeza *ceiling* ya kiwango cha kukopa ili kusije kukawa na kukopa kupindukia. Tatizo letu ni kwamba tuna kopa kupindukia, tunakopa kibashara. Tunao uwezo kabisa na mimi naunga mkono sana masuala ya umeme na nawapongeza *TANESCO* kwamba kule Jimboni kwangu wameshaanza kupeleka umeme maeneo kadhaa, ni jitihada. Lakini tunahitaji kabla ya kuamua kwenda kukopa tumalize vyanzo turudi kwenye maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na naona niyarudie tena kwa mara ya mwisho, alisema; "Mheshimiwa Spika, ushauri mlioutoa ni wa msingi sana, moja mmesema Serikali nunueni mitambo." Kwa hiyo, tungehitaji kuweka mkazo kwenye kununua. (*Makofii*)

Lakini anaendelea kusema; "na tusitafute visingizio vya fedha" hivi vya kukopa na nini ndiyo visingizo vyenyewe; "kwamba tafuteni kila mbinu huko kateni posho zenu, kateni vitu gani, nendeni mkatazame magari mnayotumia, punguza huko, tazameni *OC* zenu kikamilifu kule ndani kabisa mkaondoa na nendeni mkanunue mitambo ya uhakika." (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mitambo tuliyonayo sasa hivi tunakodi, mitambo ya *Simbion* tutakodi kwa miaka miwili, mitambo ya *Aggreko* tutakodi kwa mwaka mmoja na tutalipa *capacity charges* kipindi chote hicho na tungeweze kuwa na njia mbadala.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana rafiki yangu Mheshimiwa Mnyika. Nikukumbushe jambo la msingi sana kwamba uendeshaji wa nchi yoyote na hasa kwenye masuala ya Bajeti lazima izingatie suala la *ceiling*. Sisi kama Taifa na kama ulivyoukuwa unatukumbusha kilichotokea Marekani, yote tunayoyafanya yanazingatia *ceiling* na ndiyo maana sisi kama Taifa kuitia Wizara ya Fedha kuna *ceiling* ndiyo maana hata hii *addendum* ambayo tumeitoa pamoja na sisi kujipapasa kwa kupunguza na kufanya *reallocation* kwa zile bilioni 10.3 yote hii imezingatia *ceiling*. Mchakato ndani ya wiki tatu ambazo Bunge hili Tukufu lilituridhia tukajipange tumefanya mapitio Wizara kwa Wizara na kuitia Bajeti kuu iliyowasilishwa na Wizara ya Fedha tukizingatia *ceiling* ili kuwezesha Serikali iendelee kufanya kazili.

Lakini Mheshimiwa Mnyika amezungumzia jambo moja la kuhusu mrabaha. Nimesema hapa kwamba ratiba ya mazungumzo yanakwenda vizuri na nimesema kwa dhati kwa sababu nafahamu kinachoendelea pamoja na kwamba mazungumzo yatakamiliika mwezi ujao sisi kwa

mwenendo wa mazungumzo yalivyo hatuna shaka yoyote kwamba utaratibu wa kutozwa mrabaha na *formula* ya kukokotoa itabadiika na tutafikia muafaka. Lakini nilichotahadharisha nikawakumbusha rafiki za waandishi wa habari nchi hii inazingatia Sheria na taratibu zilizopo. Kwa mikataba ambayo ilikuwepo lazima tuzingatie mazungumzo kwa sababu tusingeweza ku-*impose* hii si nchi ya kidikteta, hatuendeshi nchi hii kidikteta kwa kuamua mambo. Sisi tunasema nchi hii tumepata heshima tuliyonayo duniani kwa sababu ya kuheshimu utawala bora. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mnyika kwa hilo usiwe na hofu tumejipanga vizuri, tunakwenda vizuri na hata hii mikopo tunayochukua imezingatia uwezo wa Kibajeti wa Kiserikali. Umegota kwenye *ceiling* sasa unakwenda kwenye vyanzo vingine kama ambavyo nchi nyininge zinafanya. Sisi si wakwanza na mpango unaenda vizuri. (*Makofii*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi pamoja na hali ngumu sana ya Taifa letu ikaona kwa kweli kuna umuhimu wa kuliokoa Taifa hili kutoka katika janga kubwa la giza. Naipongeza sana Serikali yangu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lwenge hupaswi kupita katikati ya mimi na anayezungumza. (*Makofii*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba dakika zangu hizi ziangaliwe na Makatibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono mpango huu wa dharura wa kuleta umeme nchini, nina amini kabisa kwa umakini, kwa udharura huo Serikali itakuwa pia makini katika utelekezaji. Nimefurahi pia kuona kwamba sasa hata Shirika letu la Hifadhi za Jamii (*NSSF*) wamekubaliwa na wao waanze kuwekeza katika nyanja hii ya umeme. Mimi sidhani kama kuna Mbunge atakuwa anashaka kwa kazi zilizofanya na *NSSF* naamini kabisa kwamba watafanya kazi nzuri. Lakini nirudi katika suala moja la msingi katika *formula* zozote za biashara unapoanza kuona umefanikiwa kwenda katika *peak* kwenye biashara yako ni lazima kuna kuanguka. Sasa tunapoanza kuona umuhimu wa dharura lazima tuanze ile ya mikakati ya utengenezaji na utayarishaji wa umeme kwa muda mrefu. Tusidharua sasa kuanza kushughulikia vyanzo vya kudumu kutokana na Makaa ya Mawe kule Mhukuru, Ngaka na Mchuchuma. Mimi nafikiri wakati tunatumia fedha hizi tulizonazo tuanze kujivekea matarajio ya mbele kule ambako kutakuwa na umeme wa kudumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo mimi sasa labda nipate ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri, hii miradi yote tunayosema ya dharura itaishia sana sana kwenye miji yetu mikubwa, kule kwenye Jimbo la Peramiho katika Tarafa ya Madaba tuna umeme wa maji kutoka katika kijiji cha Mahanje, mradi wa Lingatuta unaframika ndani ya Wizara kwa muda mrefu sana na tayari *REA* walionyesha nia nzuri sana na Waziri amesema hapa *REA* itaongezwa nguvu. Ninataka kuwa na ufahamu wa kutosha huu mradi ambao *REA* walishaupokea na wanataka *generate* umeme utakaolngiza tena nguvu kwenye Gridi ya Taifa. Lakini upo mradi wa Makambako Songea, miradi hiyo tukizungumza tu suala hili la dharura tusipoiangalia na hiyo miradi mingine nadhani tutakuwa bado hatujakwenda sawa sawa kwa sababu umeme huu wa gridi ukishia kuzungumza kwa udharura ile miradi kama hii niliyozungumza ya Makambako Songea, ya Lingatuta kule Mabada lakini pia kwenye kitabu cha Waziri ipo miradi midogo midogo ya kuweka *solar* kwenye vijiji vyetu na nini.

Kwa hiyo, nadhani tutengeneze udharura huu lakini Mheshimiwa Waziri atupe pia ufanuzi wa hii mradi mingine pia kwa sababu ni suala la dharura na kwa sababu Serikali imeweka nguvu kwenye suala hili la umeme na yenye we itapatiwa kipaumbele cha namna gani. Nimalizie kwa kusema ufanuzi huo nauhitaji lakini naipongeza sana Serikali na imefanya uamuzi sahihi, imetekeleza azma ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imetekeleza azma ya Tanzania na kwa kweli itainua uchumi wa nchi yetu kwa kiasi kikubwa sana. *Big up* kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa ushauri wake ameutoa na kwa kweli kwa kuunga mpango huu. Napenda kufafanua kwa hoja ambazo amezitoa, ni kweli mpango huu tunaongelea ni wa muda mfupi kwa sababu tatizo tulilonalo ni la sasa. Ndiyo maana nikasema ukiondoa mipango hii ambayo inatekelezwa kati ya sasa na mwaka kesho kwenye hotuba ya kitabu chetu tumelezea miradi ambayo itatekelezwa kuanzia mwaka 2012, 2013 na kuendelea mpaka mwaka 2015. Kwenye miradi ya muda mrefu ukurasa wa 135 wa Kitabu cha Mpango wa Maendeleo umeelezea miradi ambayo katika dhamira ile ya Serikali kwa kusema walau kati ya sasa na mwaka 2015 kwa uchache tuwe tumeongeza megawati 2780 ukiwemo mradi wa makaa ya mawe. Hili tunakwenda nalo lipo katika utaratibu lakini mradi ambaao ameusema Mheshimiwa Mhagama wa Mahanje upo kwenye utaratibu wetu wa Wakala wa Nishati (*REA*) kwa sababu ni mradi mdogo. Sasa kwa uwezo huu ambaao Bunge kwa pamoja linaonyesha linaunga mkono juhudzi za Serikali za kutanua wigo wa vyanzo vya mapato na kutunisha Wakala wa Nishati Vijiji tunaanzia na kuwa na fedha nydingi zaidi na tutakwenda kutekeleza pamoja miradi mingine pamoja na mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Makambako Songea tumeutolea taarifa kwenye kitabu chetu cha hotuba, ni mradi ambaao tunafadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lao la Maendeleo (*SIDA*). Katika hatua ya utekelezaji kwa sasa makablasha ya kuwapata wakandarasi yanaandalialiwa. Imechukua muda mrefu ni kweli, lakini ukweli ni kwamba mradi ambaao kwa sasa ulipofikia upo kwenye hatua za utekelezaji. Makandarasi wakipatikana tutaanza kujenga kutoka Makambako mpaka Songea, Mbanga mpaka Namtumbo. Lakini kwa sasa juhudzi zinazoendelea ni kuhakikisha kwamba ile *generator* ya pale Songea mjini pamoja na Namtumbo zinakamilika mwisho wa mwaka huu wakati wanasubiri mpango mzima wa miradi mikubwa ikiwemo mpango wa kuzalisha umeme kutohana na makaa ya mawe ya Ngaka. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kuna wengine wakati tunatengeneza utaratibu wa mabadiliko ya Kanuni yetu hawakuwepo. Kwa hiyo, tunatumia dakika tano mtu kujieleza kwa mara ya kwanza na dakika tatu mara ya pili.

La pili naomba msiniandikie vibarua, mimi nina *concentrate* kusikiliza, sasa si nitaacha haya nitasoma barua yako, jamani mniache sasa hivi nipo kwenye Kamati. Hivyo hivyo asiondoke mtu kuja kukaa kwa Waziri Mkuu. Huu ni wakati wa maamuzi hakuna mtu kwenda kukaa na kuongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa. Tunasikiliza watu wanachokisema kusudi tuweze *underline* mambo. Namwita Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa hakika nichukue fursa hii kupongeza sana hatua za Serikali katika mpango huu wa dharura. Imani yangu na ningependa Watanzania waamini kwamba mpango huu kwa namna ulivoandalialiwa nina hakika utatekelezwa na tatizo la umeme litaisha. Kubwa ni kuangalia tu sasa tatizo lisijirudie na kwamba dharura na yenye we iwe ina *limit* yake. Tuseme sasa dharura basi, maana dharura inaweza ikaendeleza na wengine wanapenda kweli mpango huu wa dharura. Kwa hiyo, tuwe makini kuhakikisha kwamba dharura hii haiendelei. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina jambo la ufanuzi ambalo Mheshimiwa Waziri anakumbuka katika michango yangu ya Bajeti zote ambazo yeye amekuwa Waziri wa Nishati na Madini nimekuwa nikizungumzia kuhusu suala la mradi wa *MCC* ambaao ulikuwa *designed* na kuwa *planned* wakati ambapo maendeleo ya *vijiji* vyetu hayakuwa kama yalivyo sasa na nilikwenda mpaka ofisi ni kake tukzungumza nikamueleza kwamba kutoa umeme kutoka Kibakwe kupeleka moja kwa moja hadi Pwaga hakuna tija kama hautapita katika Kijiji cha Ikuyu na Luhundwa ambapo kuna kituo cha afya, sekondari mbili na tofauti yake pale ni kilomita 12 tu. Lakini pia umeme kutoka Pwaga kama haujaflik Lumuma na Kitatye ambako kuna kilimo kikubwa cha umwagiliaji karibu hekta 2500 na Sera inasema hivyo kwamba umeme lazima ziangalie sehemu zenye huduma muhimu za jamii na sehemu zenye uzalishaji na Mheshimiwa Waziri ukanielekeza niende *REA* na *REA* nilikwenda na tumeongea na Mkurugenzi na kukubaliana. Lakini simo kwenye kitabu hiki. Sasa Mheshimiwa Waziri mimi hapa napata shida, sisemi lolote juu ya kutokuunga au kutoa shilingi lakini nikuombe na unipe ufanuzi wa jambo hili ambalo tumeshaongea mara kadhaa. (*Makof*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyojasema Mheshimiwa Simbachawene ni kweli tulikutana na tukaongea na kweli amekutana na watendaji wa REA na pia kwa suala lake kwa vijiji ambavyo ameviombea kwa kweli tumelishughulikia. Kama nilivosema kwenye hotuba ya kitabu chetu cha Bajeti si rahisi kuona miradi ile kwa sababu kwa kweli kutokana na upatikanaji wa fedha kwa miaka miwili iliopita miradi mingi inayoonekana kwenye kitabu chetu sasa hivi ni miradi iliyoombewa fedha miaka miwili iliopita na mingine ni zaidi ya hapo.

Kwa hiyo, tumekuwa tukilitolea ufanuzi kwa minajili ya utekelezaji kwa sababu tumekuwa hatupati fedha lakini kwa sasa hivi tunaamini kwamba itakamilika kwa mwaka huu na tunaanza raundi nyingine ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wameiomba. Sasa siku moja nilimdokeza Mheshimiwa Simbachawene kwamba miradi ambayo ameiongelea tayari imeshafanyiwa tathimini na bahati nzuri gharama ya utekelezaji wa miradi hiyo ni shilingi bilioni tatu na yeze nilishamwarifu. Nataka nitumie nafasi hii kuwathibitishia wananchi wa Jimbo la Kibakwe na hasa wananchi wanaishi maeneo haya ya mradi huo utatekelezwa kwa sababu vyanzo ambavyo Bunge limeridhia kwamba tukavitekeleze Kiserikali mtatuongezea uwezo wa kupata fedha zaidi kuliko kitabu chetu cha hotuba kinavyoonyesha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Simbachawene uwe na amani mradi wako unakwenda kutekelezwa. (*Makof*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa nia tu ya kuweka vizuri rekodi, miradi anayozungumzia Mheshimiwa Waziri kwamba angalau umeshafanyiwa utafiti ni ile inayozunguka Bwawa la Mtera ambako nimekuwa nikizungumza sana kilio chao lakini hii ni ile inayounganisha kutoka Kibakwe kwenda Ikyu, Luhundwa ile ya MCC na baadae kutoka Pwaga kwenda Kitate na Lumuma, Kitate na Lumuma kuna kilimo kikubwa cha umwagiliaji ambako kwa hakika ukipeleka umeme maana yake umetoa ajira, sera inasema hivyo. Lakini Luhundwa na Ikyu kuna sekondari mbili na kituo cha afya havina umeme. Kutoka Kibakwe mpaka Luhundwa ni kilomita 12. Kwa hiyo, napenda ufanuzi wa jambo hilo na sio kule Mtera ambako amenipa jibu lake hili la mwisho. (*Makof*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuahidi Mheshimiwa Simbachawene kwamba maeneo haya nayo tutayfanya kazi kwa sababu yapo maeneo mengi ya Waheshimiwa Wabunge wengi kuingizwa kwenye mpango. Kama ambavyo tulianza kwa kumuahidi hii miradi ambayo ipo kwenye utaratibu. Tunaichukua tutafanyia tathimini tujue gharama zake sasa kutoka kwenye hiyo *junction* ya miradi inayotekeliza kupitia MCC na tujiridhishe gharama zake halafu tuendelee na hatua za utekelezaji. (*Makof*)

MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MINYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi napenda nipaye ufanuzi na huu mpango wa dharura wa Serikali mimi sikuufurahia hata kidogo kwa sababu haujaondo tatizo la msingi. Serikali imeweza kujifunza kuanzia mwaka 1995/2006 na ikatolewa mifano mingi ya kuepukana na umeme wa dharura. Hadi hivi leo bado Serikali inaleta mpango wa umeme wa dharura, umeme wa dharura huu unaghali mu kiasi kikubwa sana. Mara nyingi sana Mawaziri wanapokuja hapa wakielezea namna ya Serikali kupata mitambo mipya inachukua miaka mitatu kitu ambacho si sahihi na huu mpango wa hivi sasa wa dharura bado tunaendelea na dharura ambayo haimaliziki ambayo itagharimu Serikali fedha nyingi sana. (*Makof*)

Hivi karibuni mimi mwenyewe nilichukua *initiatives* zangu nikaweza kupata uwezekano wa kupata mitambo kirahisi kwa muda wa miezi miwili na mwingine mwisho wa mwaka huu kwa gharama nafuu sana na mitambo hiyo ikawa inamiliikiwa na Serikali na gharama zake ni rahisi zaidi kuliko hii ya kukodi hata kwa mwaka mmoja. Taarifa hizo Mheshimiwa Waziri Mkuu anazo nilimpattia na nategemea hata Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini anazo, je, ni kwa nini mpaka leo tunaendelea na mipango ya dharura ambayo inatugharimu vibaya sana na inatukamua kama Taifa ambapo mpaka leo Serikali bado inaleta mipango ya dharura wakati uwezo wa kununua mitambo yetu ipo na kwa bei nafuu? (*Makof*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mnyaa kwa juhudzi zake ambazo amekuwa akifanya na kwa kweli wapo Waheshimiwa wengi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa namwona pale, Mheshimiwa Hamad

Rashid Mohamed na ni jambo jema kushirikiana na wawekezaji. Lakini mwisho wa yote ninachokisema ni kwamba inafanya tathmini na wataalam wetu. Mheshimiwa Mnyaa inawezekana kabisa kati ya maombi ambayo nimesema wakati tunakuja kutoa ufanuzi wa hoja yetu leo bado yapo makampuni mengi yameonyesha dhamira ama kuikodishia *TANESCO* kwa niaba ya Watanzania ama kuiuzia mitambo ya kufua umeme. Sasa ni jambo ambalo ni endelevu. Lakini hili la kwamba kwa nini muda wote huo Serikali imekuwa ikija na mpango ya dharura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe tu kwamba kuna jambo tumekuwa tukilisema na pengine hili halijaka vizuri sana kwamba leo hii tusingekuwa hapa kama miradi yetu miwili tu ingekuwa imetekelezeka kati ya kipindi cha mwaka 2005 mpaka 2010; Mradi wa *ARTUMAS MW300* ambao ulikwama kwa sababu ya mdoororo wa kiuchumi wa mwaka 2007 mpaka 2009. Lilikuwa ni jambo ambalo lilikuwa nje ya uwezo wetu. Mradi wa Kiwira wa Makaa ya Mawe, mradi huo wa *MW200*, kama ingeteklezeka, maana yake leo tungekuwa na *MW500* kujumlisha zile *MW145* ambazo tumeshazipata, kwa kipindi kile tungezalisha *MW645*. Yaliyotokea, yametokea, kiasi kikubwa yapo nje ya uwezo wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo muda wote hapa Serikali imekuwa ikifanya juhudzi za kuhakikisha kwamba tunaondokana na utegemezi wa umeme unaozalishwa kutokana na maji, tuhamie kwenye vyanzo vingine vya uhakika, vyanzo kama hivi tunavyosema vya gesi asili, lakini pamoa na makaa ya mawe na hata zaidi kama tunavyoendelea ku-*promote* miradi ya upepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni juhudzi za makusudi zimekuwa zikichukuliwa. Lakini tumekutwa na janga hili wakati ambapo miradi yetu hajakamilika na siyo sisi tu, hata wenzetu. Ni hivi karibuni watu walikuwa wanatolea mfano kwamba Kenya mbona hawana mgao? Uganda pia, jana nilikuwa na Waziri wa Uganda alikuwa ametutembelea hapa, wana mgao wa saa 16. Wapo Wakenya hapa majirani zetu, wametangaza mgao wa miezi saba ijayo. Ndiyo maana tunasema mambo haya yanatokana wakati mwingine mnakutwa ni kama vile mnafumaniba wakati mambo hayajakaa sawa. Kwa hiyo, ninacho sema, naomba Waheshimiwa waamini kwamba Serikali inafanya kazi. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofii*)

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameeleza, lakini kiini cha kwa nini Serikali inafanya hivyo hajatoa na kama maelezo yale ya mwanzo hajayafahamu, tukilinganisha na maelezo yako na mradi wa *MW60* wa Nyakato Mwanza ambao unategemea kukamilika mwaka 2012, halafu na mradi wa bomba la mafuta mliompa mwekezaji mwaka 2007 na mwekezaji hajafanya chochote mpaka hivi leo na leo bado mradi huo utegemee magari kutoa Dar es Salaam kupeleka *heavy fuel* Mwanza! Mmefanya nini kama Serikali kuanzia mwaka 2007, Kampuni ya Qatar ambayo mmeipa na hajafanya chochote kuhusu ujengaji wa bomba lile kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, nini kinaendelea? Je, haitakuja kuwa dharura tena? (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanuzi ni kwamba nashukuru kwa maswali ya Mheshimiwa Mnyaa, yanaipa fursa Serikali kuelezea na kuwafahamisha Watanzania kinachoendelea. Kwanza, kampuni anayo sema, anafahamu, inawezekana kampuni ya Qatar anayo sema pengine ni kampuni mojawapo katika sekta ya nishati iliyoonyesha nia ya kuwekeza inaitwa Ras Al Khaimah. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba ule mradi anaousema kwamba tulilipa tangu miaka ile, nadhani anaongelea habari ya mradi amba tulisema, kwa sababu ile kampuni ya *Lucky Gas*, hajawahi kupewa mradi ule iuendeleze. Illichofanya yenye na walikubaliana kwa sababu ile pia ina vitalu vya utafutaji wa gesi na mafuta, walikubaliana na Serikali kupitia Shirika la *TPDC* wafanye upembuzi yakinifu wa uwezekano wa kujenga bomba la mafuta kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam. Lakini wakakubaliana kwamba għarama hiso ziwe sehemu ya makubaliano kati ya *TPDC* na wao.

Kwa hiyo, si kusema kwamba labda waliambiwa kwamba watafikia kwenye */level* ya uzalishaji au ya ujenzi, hapana. Ni kati ya makampuni ambayo yameonyesha nia ya kushiriki katika

ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam na kuendelea mpaka Tanga. Lakini kilichofanyika ndicho hicho kwamba tulikamilisha upembuzi yakinifu wa mradi ule na ndiyo maana sasa ule mradi baada ya kukamilisha na baada ya kufanya tathmini kuona kwamba tukiwatumia wao, ilikuwa dhamira ya Serikali, bomba la kusafirisha gesi kutoka Mtwara kwenda Tanga limilikiwe na Serikali. Tukasema bora tuchukue mkopo kuliko kuendelea, kwa sababu tumejifunza pia kutoptaka na washiriki waliopo katika sekta binafsi sasa. Miundombinu ya sasa hivi, inamiliikiwa na sekta binafsi. Kuwepo na sekta binafsi ni jambo la heri, lakini pia katika mazingira fulani na hasa kwenye miundombinu nyeti ambayo unaweza hata kuhtarisha usalama wa Taifa, tukasema sisi Serikali tushiriki. Tulivyopata uwezekano wa kupata mkopo kutoka Serikali ya China, mkopo wenye masharti nafuu, tukasema tujenge wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilichofanyika ni hicho, siyo kwamba ile kampuni imezuilliwa. Ungeongelea habari ya Kampuni ya *Songas* iliyochelewesha mradi wa kupanua ujenzi au miundombinu ya kusafirisha gesi *Songsongo*, ningekuelewa kwa sababu ile ilikuwa ni suala la Mdhibiti *EWURA* na lilitfanyika vile kwa sababu kampuni hii ilikuwa inabadilisha gharama za mradi kwa kadri muda ulivyokuwa unakwenda na hatimaye *EWURA* ikawa imekataa, lakini baadaye walikuabaliana. Kwa hiyo, nataka nikuthibitishie Mheshimiwa Mnyaa na Watanzania kwa ujumla kwamba siyo kwamba Serikali imekaa tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mwanza, huu uwekaji wa mitambo mbalimbali ya kufua umeme katika Gridi ya Taifa unazingatia tathmini ya kitalaam. Nafahamu Mheshimiwa Mnyaa katika eneo hili una uelewa mpana sana. Lakini nataka nimwambie *Engineers* wenzako wametuthibitishia kwamba na ni suala la kweli, ukiweka uzalishaji katika eneo moja na mtandao wako ukawa ni mkubwa sana, kwanza unaudhoofisha mtandao wako kufikisha umeme kwa maeneo ambayo yapo mbali na vyanzo. Lakini pili, unajivekea mazingira mazuri ya kupoteza umeme mwingi zaidi. (*Makofî*)

Leo hii vyanzo vyetu nya umeme kwa sababu tunasema asilimia 55 ya umeme wa Tanzania umekuwa ukitegemea maji na vyanzo vyetu vingi viko Mikoa ya Kusini, kupeleka umeme mpaka Kanda ya Ziwa, kupeleka umeme mpaka Sirari, kupeleka umeme mpaka Mkoa wa Kagera, tumekuwa tunapata matatizo kwa sababu ya urefu wa njia. Ndiyo maana tumebuni mradi wa kuimrisha *transmission line* ya kutoka Iringa mpaka Shinyanga zaidi ya kilomita 600 ambayo fedha zipo na sasa *tender* zinashambuliwa ili tuimarishe, tutoe *KV220* mpaka *KV400* ili pamoja na mambo mengine tudhibiti uwezekano wa upotetu wa umeme huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba tutafikishaje mafuta Mwanza, leo hii mgodi wa *GGM* pale Geita unafanya shughuli zake kwa kutegemea mafuta mazito ambayo yanasaferishwa na magari. Katika kipindi cha mpito hiki na kwa kuzingatia hilo la kitalaam kwamba ni vyema ukasambaza uwekaji wa vyanzo vyako nya kufua umeme ili *network* yako iwe *balanced*, tunasema mafuta yatapelekwa kwa kutumia magari kwa sasa. Lakini zoezi hilo ndilo linalofanyika kupeleka leo mafuta. Mheshimiwa Serukamba anafahamu Kigoma kuna tatizo la mafuta sasa hivi, ndiyo hiyo hiyo, utaratibu wa kupeleka mafuta Kigoma, kupeleka Mpanda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupeleka Songea ambako Gridi ya Taifa haijafika. Kinachotakiwa hapa, pamoja na utaratibu mwingine, ni usimamizi wa kweli, lakini pia kupata msafirishaji wa mafuta hayo ambayo amepatikana kwa utaratibu unaokubalika, siyo wa kifisadi. (*Makofî*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na kutoa pongezi kwa Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya kuleta umeme wa dharura, ninapenda kupata ufanuzi katika maeneo mawili.

La kwanza, katika mchango wangu wa maandishi nilioomba Serikali kujua ni mikakati gani inayo kuhakikisha maeneo yote yaliyopitiwa na nyaya za umeme, wananchi wanachungu nguzo za umeme ni lini watashushiwa umeme, zinunuliwe *transfoma* za kutosha kuhakikisha vijiji vyote vinapata umeme? Vilevile, maeneo ambayo yanapelekewa umeme sasa, Serikali ihakikishe inamaliza tatizo, inashusha umeme kwenye vijiji vitakavyopitiwa na umeme huko unakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili, nahitaji ufanuzi, nilioomba Serikali kwamba kunakuwa na tatizo kwenye ofisi za *TANESCO*, kutokuwa na mita za umeme na mita za LUKU hasa

Mkoa wa Singida, wananchi wanasubiri kwa muda mrefu. Wananchi wameshaelewa matumizi ya hivi vitu. Sasa Serikali ina mkakati gani kuhakikisha vifaa hivi, mita za umeme na mita za LUKU zinakuwepo kwenye vituo vya TANESCO ili wananchi wanapohitaji huduma wapate mara moja? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili suala la kushusha umeme nyaya zinapopita, inategemea kusema kweli ni msongo gani wa waya unaopita, kwa sababu saa nyingine tunao labda vijiji hivyo vinapitiwa na *transmission line* kubwa za msongo wa labda KV132 na kadhalika. Huwezi kuushusha umeme pale bila kuweka miundombinu ya *sub-station* na kadhalika ambayo peke yake ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kisheria tunawajibika kwamba pale ambapo pana msongo kama wa KV33, tushushe umeme kwenda kwenye msongo wa KV11 ambayo ni *transfoma*, halafu usambazaji ufanyike kwa KV0.4 kwa maeneo ya kufikisha majumbani. Kwa hiyo, mkakati huo upo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama tunavyosema pia unazingatia vigezo vya kitalaam, wingi wa watu, mahitaji na kadhalika na nini, kwa sababu hata huko kushuka tu kutoka kwenye msongo wa KV33 kwenda kufikia kwenye usambazaji una gharama zake na gharama zenyewe kutegemeana na *transfoma* kama ni KVA50 au KVA100 ni gharama kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, nimelisemea wakati tunatoa hoja pale kwamba ni kweli kumekuwa na tatizo la vifaa vya TANESCO na hasa mambo ya nguzo, nyaya na hizi mita. Lakini nasema sasa hivi TANESCO wameagiza mita kama 30,000. Kuna wakati tulishakaa Serikalini na tulikubaliana kwamba vifaa hivi vya TANESCO vifanyiwe tathmini haraka ili visikae bandarini wiki tatu, wiki nne wakati wananchi wanavisubiri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nadhani hili ni jambo ambalo tutakumbushana wenyewe Serikalini ili vifaa vya TANESCO namna ile *especially* ambapo wananchi wanasubiri kuunga umeme, visikae bandarini wiki tatu, wiki nne wakati watu wanavisubiri kuvitumia. (Makofi)

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Lakini kipekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu amesikiliza kilio cha wananchi wa Same Mashariki, isipokuwa kidogo nim-*caution* kwamba ukiniahidi, ujue umeniahidi, nitakubana kikweli kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ielete kwamba leo tulivyokaa hapa, nchi nzima wananchi wote wamekaa kwenye TV, wanaangalia Serikali inasema nini. Wananchi wote wapo aidha ni kwenye redio au ni kwenye TV wanamsikiliza Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Waziri na wanaakisikiliza Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapitisha hii Bajeti leo ya shilingi triliuni 1.2, sijui kama niko sahihi. Lakini kuna jambo ambalo ningeomba kwanza liwe ni angalizo. Wizara ya Nishati na Madini imeomba hizi hela, Bunge hili litazipitisha leo. Hivi *commitment* ipi itatoka kwa Serikali kwamba Wizara hii itazipata hizi hela zote kama ilivyozomba? Kwa sababu kipindi kilichopita, pesa ambazo Wizara ya Nishati na Madini iliomba, sizo ilizopewa na Serikali. (Makofi)

Kwa hiyo sasa, sisi tukaendelea kuibana Wizara ya Nishati na Madini, lakini nao walikuwa hawakupata pesa zote kama ambavyo tulizipitisha. Kwa hiyo, hilo nalo ni tatizo kubwa. Ni vyema Serikali ijue kwamba leo tukipitisha hizi hela hizi, nafikiri shilingi triliuni 1.2, wahakikishe Wizara ya Nishati na Madini inapewa hizi pesa zote kwa sababu Watanzania wanaibana hii Wizara na wakati mwingine inakuwa siyo zenyewe yenye matatizo. Hilo la kwanza! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba tuzungumze hili jambo limezungumzwa na watu wengi, miradi ya dharura sasa iwe mwisho. Iwe mwisho kwa sababu tuna Hansard. Sasa Serikali ijikite, na hili nilizungumza wakati nachangia, kutafuta japo miradi mitatu mikubwa, iende ipeleke

nguvu zake huko ili hili tatizo liwe ni mwisho na sisi tuwe kama Msumbiji ambao wanaauza umeme nje, wanawauzia *South Africa*, uwezekano huo upo.

Naisihi Serikali ya CCM, dharura ndiko kuliko na mianya yote ya ufisadi, tusikatae! Tuache dharura, hii ya wakati huu tunaomba tuikubali, tunaipitisha kwa sababu nchi ipo kwenye kipindi kigumu, lakini basi iwe ni mwisho. Iwe ni mwisho, tunatatua tatizo na isiwe tunakwenda kwenye dharura tena. Tutatue tatizo kwa kudumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kidogo Waziri hapo azungumze. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa kukubaliana na mpango huu akiunganisha nguvu na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu, tunashukuru sana na ahsante sana. Lakini pia tunashukuru sana kwa angalizo lake kwamba mtuunge mkono tukatekeleze mipango ambayo tumeiwasilisha hapa kutoka kwenye vyanzo vyetu, mikopo na hatimaye ipatikane fedha ya kututoa hapa tulipo na kutusogea mbele na kwa hilo nalo tunashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatu ni kweli dharura hizi zimesababisha usumbufu kama nilivosema siyo wa kichumi tu lakini pia wa kijamii na kwa kweli sisi wengine, watendaji tumepewa hata majina mengine katika kipindi hiki cha dharura hii. Inatuma, inatugusa, tunafahamu adha yake. Nataka nitumie nafasi hii tena kuwashakishia Watanzania kwamba kinachofanyika hiki, lengo lake kwa kweli ni kudhibiti kabisa mgao usiwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo tayari kwenda kutekeleza mpango huu kwa manufaa ya Watanzania. Tunashukuru sana. (*Makofii*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa fursa niweze ku-request ufanuzi kidogo kutoka kwa Waziri wa Nishati na Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kuna miradi ambayo inaendelea katika Wilaya za Kasulu pamoja na Kibondo na ni muda mrefu sana Serikali imekuwa ikitoa kauli zake kuhusiana na utekelezaji wa miradi ile ili kusudi wananchi wa Wilaya hizo waweweza kuona umeme ukiwaka. Kwa sababu ukizungumzia umeme katika Wilaya za Kasulu na Kibondo, tuseme ni kitu ambacho hakijawahi kutokea. Kwa hiyo, wananchi wa Wilaya za Kasulu na Kibondo wanasubiri umeme ule kwa hamu. Ni muda mrefu sana tumekuwa tukiahidiwa tangu mwaka jana kwamba mwezi Desemba, 2010 *TANESCO* wangeweza kuwashaa *phase one*, lakini umeme haukuwashwa. Baadaye tukawa *promised* kwamba mwezi wa Februari, wewe Mwenyekiti kama Mheshimiwa Spika, uli-request Serikali iweze kutoa kauli juu ya miradi mbalimbali ya hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, alili-*promise* Bunge hili pamoja na wananchi wa Wilaya hizo kwamba umeme ungewaka mwishoni mwa mwezi Machi. Lakini umeme haukuwashwa. Tuliendelea kufuatilia, lakini bado mpaka leo hii haujawaka. Kauli ya mwisho ilikuwa umeme ungewaka mwezi Julai, 2010 umeme haujawaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona kama vile tunadanganyana wakati mwingine. Sasa niombe Mheshimiwa Waziri awathibitishie wananchi wa Wilaya za Kasulu na Kibondo ikiwemo na Bunge lako Tukufu, umeme huu *exactly* utawashwa tarehe ngapi? Na ingekuwa ni vizuri umeme huu ukawaka mwezi huu wa Agosti kwa sababu *promise* zimekuwa ni nyingi, tunapigwa danadana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri, naomba ufanuzi, ni lini, ni tarehe ngapi, ikiwezekana na siku gani ambapo umeme utawaka katika Wilaya hizo? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Hamna *diary humu* ndani ya Bunge! Hamna *dairy!* (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Machali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakati nachangia hapa hoja ya Mheshimiwa Waziri nilieleza kwamba Kasulu na Kibondo kweli Desemba, 2010 jenereta zilifungwa na matarajio ya kufunga jerereta, baada ya kufunga jenereta, kazi zile za usambazaji zingeenda na wakati, vifaa vilichelewa. Sasa kwa sasa hivi vifaa vimeendelea kufika na kazi za kufunga zinaendelea. Nimekwambia kwamba mkandarasi kwa wiki iliyopita, baada ya wewe kuniuliza swali na mimi kwenda kuongea na mkandarasi, nikamuuliza tatizo ni nini, akaniambia kwa sasa wanaendelea vizuri isipokuwa kwa sasa hivi tatizo lao ni mita, mita zao hazijaja. Tulichofanya, tumekubaliana kwamba mita ni mita, wachukue za *TANESCO*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mkandarasi za kwake zikija, atarejesha *TANESCO* ili kukamilisha hilo jambo la kwanza, kuunganisha umeme Kasulu na Kibondo. Kwa hiyo, tutarajie kwamba wameshakubaliana kwamba mita hizo zitakwenda Kasulu na Kibondo, zitaanza kufungwa sasa hivi ndani ya wiki moja, mbili wakati zoezi lile la kuunganisha umeme na Nyaza linaendelea. Kwa hiyo, mambo mawili yote yatakuwa yanaendelea kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba wakazi wa Kasulu na Kibondo, mita zikifika, huwezi kufunga umeme hata kama ukiwepo hapo bila mita. Kwa hiyo, mita zikifika, ndani ya wiki moja, mbili wataanza kuuona na zile kazi za kusambaza waya na nguzo zitamalizika mwezi wa Desemba. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, tarehe bado hujapata!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na majibu yake, japo kidogo nahitaji ufanuzi zaidi kwa sababu suala la kukosekana kwa vifaa limekuwa ni suala la muda mrefu. Hapo awali kisingizio ilikuwa ni nyaya na ambazo mli-*promise* kwamba mwishoni mwa mwezi Machi nyaya zingekuwa zimefika *site*, lakini kumekuwa na uchelewaji.

Leo imeibuka hoja ya mita kwamba hazipo, hili ni tatizo ambalo huko nyuma wakati ambapo nimekuwa nikiuliza halijawahi kuzungumzwa. Mnasema kwamba ndani ya wiki mbili, sijui kwamba ufungaji wa mita utachukua muda gani ni vizuri mtuambie wananchi wa Kasulu wanataka kujua, kwamba umeme utawaka lini, ni mwezi huu wa nane? Kwa sababu kuna majibu mengine tukizungumza huko unasema ni mwezi wa nane au ni mwezi wa tisa, sasa naomba kauli ya Serikali tujue umeme utawaka lini, ndiyo jambo la msingi na hoja ndiyo hiyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Umenikumbusha mwingine anasema anaomba kiatu na mwingine anasema anaomba mguu, haya Naibu Waziri majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema kwamba kwanza pale mkandarasi anayeendeleza ule mradi siyo *TANESCO*, Mkandarasi huyo ni mzuri kusema kweli lakini kazi yake aliyopewa na makusudio yake ya kukamilisha hiyo kazi anakwenda nayo kwa mwendo mzuri. Lakini tulipozungumza naye wiki iliyopita au kama wiki mbili zilizopita kutokana na haya tuliyoyawasilisha hapa Bungeni, wewe bwana kitu yako inakwisha lini akasema mimi naendelea kusambaza nyaya lakini inaonekana katika mambo nitakayokwama ni mita. Kwa kujua udharura na ahadi iliyokwenda pale na kwa sababu sisi wenyewe tumepelekana nalo hili sana. Tumewaambia *TANESCO* toeni mita za kwenu ziende. Sasa ndiyo maana nasema kwamba taarifa niliyokuwa nayo ya leo asubuhi, ni kwamba wanatarajia kufanya hilo zoezi ndani ya wiki moja au wiki mbili na ndiyo kipindi nilichokupa. Sasa ukiniambia tarehe na saa na wakati ambao watafunga nadhani hiyo kidogo itakuwa ngumu lakini ndani ya wiki mbili kwa taarifa ya leo ya *TANESCO* ni kwamba wao watatoa mita zao ziende Kasulu na Kibondo, hizo zilizokwama bandarini Dar es Salaam, kama za kwao zikifika watarudisha za *TANESCO* na kazi itakuwa imeendelea, ila kazi ya usambazaji inaendelea na yenyewe itakwisha Disemba. (*Makofi*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kwanza nizungumzie jambo la dharura, ukiangalia yote yanayozungumzwa hapa yanategemea mafuta ambayo yatatolewa na Serikali. Kwa hiyo, ukianzia kwenye *IPTL* Serikali ilijua tatizo la kutokuwa na umeme, imeweza kutoa fedha ya kununua mafuta baada ya Bunge hili kusema hawapitishi Bajeti hii na bado sijaelewa hiyo fedha ilitoka wapi.

Leo tuna *Aggreko* ambayo na yenyewe tutaipa mafuta, tuna *Simbion* tutaipa mafuta, tuna *NSSF* tutaipa mafuta na ukiangalia mteja ni *TANESCO* ambayo mmetuambia yeye anapata bilioni 115. Kweli ukiangalia kibiashara hii kitu kweli itafanikiwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sogea *microphone* yako tunakusikia kwa mbali.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kibiashara hii kitu kweli itafanyika? Maana yake mimi naanza kuogopa kwamba watu watakuwa wanakuita wewe Mheshimiwa Megawati kila siku, kweli hebu tuhakikishie hii pesa itapatikana na itapatikana lini, zaidi wakati huu ambapo Serikali haipati mapato ya kutosha kwa sababu ya umeme? Mpango upo lakini ni *sketch*. (*Makofi*)

Jambo la pili, kila wakati mimi nimezungumza kwamba labda pia tuangalie muundo wa Wizara yenyewe, leo hapa tunazungumza ni Nishati na Madini Waziri umetumia dakika tano kuzungumza madini, umetumia muda wote kuzungumzia nishati, hivi kweli hajafika wakati ambapo labda haya mambo mawili yangegawanywa, kukawa na Wizara ya mambo ya madini na tukawa na Wizara inayosughulikia mambo ya nishati na utapata muda? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hata ukiangalia mpango wako huu hujatueleza je, una pesa ya kuweza kuweka kwenye *transmission* kwa sababu tatizo siyo ku-*generate* tu, tatizo pia ni *transmission system* yetu ni ya zamani hajapata *repair* kwa miaka mingi, hata uki-*produce* umeme hautaingia kwa sababu hauna *system* ya *transmission*, sijaona pesa yoyote ambayo inatuambia itafanya hiyo kazi. Lakini mimi nafikiri pia *TANESCO is overloaded*, mimi nafikiri tulishasema pawepo na watu wanao-*generate*, wawepo watu ambaao wana-*transmit* na pawepo na watu ambaao wanaogawanya. Ni lini mpango kama huu utakuja ili utuwezeshe kutatua haya matatizo kwa mara moja na kwa miaka mingi. Lakini leo ukiangalia *TANESCO as it is, is top heavy!* Haiwezi ikakusaidia kwa hali halisi iliyopo kwa sasa hivi. (*Makofi*)

Mhehsimiwa Mwenyekiti, mwisho, bado mimi sijaridhika jinsi ambavyo umeshirikisha *private sector* zaidi kwa upande wa *generation*. Umezungumza juu ya *ARTUMAS*, hawa walishindwa kwa sababu Serikali haikuweza kutoa uamuzi *whether* yule mtu anayekuwa mteja wao, awe *TANESCO* au awe Barrick, kwa sababu *balance sheet* ya *TANESCO* kama unavyoijua haiuziki. Sasa kama umeshidwa kwa miaka minne 2004 kuna visima vinne vinasubiri, sisi tunakaa gizani, Serikali haifanyi kazi, *I think that mngetuambia ni nini zaidi?* (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Waziri maelezo.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa John Cheyo kwa maswali aliyoyauliza. (*Makofi*)

Ufafanuzi wake ni kwamba kuhusu fedha ya *IPTL*, fedha ya *IPTL* siyo kwamba ilitolewa kwa sababu Bunge liliridhia kuahirisha majumuisho ya Bajeti hii, hapana, wakati tunawasilisha huu mchakato wa Kiserikali wa kupata fedha kutoka Hazina ulikuwa unaendelea. Lakini kwa hili la kwamba pengine hii mitambo ambayo nimesema inakuja kuunganisha nguvu na mitambo iliyopo ya *Simbion*, *Aggreko*, *NSSF* kwamba pengine wote fedha hiyo itatoka Serikalini. Kinachofanyika ni kwamba kwanza manunzi hayatafanywa kama vile *IPTL* kwa sababu katika majadiliano ambayo yamekubaliana na *TANESCO* gharama za mafuta zipo ndani ya hayo makubaliano, kwa hiyo wanunuzi wa mafuta kwa mfano kwa *Aggreko* ni wao wenyewe. *Simbion* ambaye atatumia mafuta ya ndege kwa kuanzia, yeye mwenyewe atanunua kwa sababu gharama zote ziko *factored* kwenye makubaliano. Kwa hivyo kama ni suala la kununua linabaki kwenye mtambo wa *IPTL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Cheyo anahoji je, fedha hizi kweli zitapatikana? Kama nilivyosema tumeingia makubaliano ya kibiashara kupitia Shirika la *TANESCO* na Serikali imechangia kama nilivyosema kwa kupunguza kwanza mzigo wa kwenye kodi kwa maana ya kwamba tumejinyima kwa upande mwininge wa mapato. Lakini tukasema inadhamini mikopo, sasa ile mikopo yote inayokopwa itasaidia kuweza kuhimili gharama hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za *transmission*, Mheshimiwa Cheyo ningependa kumkubusha angepitia vizuri kile kitabu chetu cha hotuba kinasema tuna miradi mingi sana ya *transmission* sasa hivi inajengwa na nimeitaja hapa muda mfupi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anatoa ufanuzi alielezea lakini na mimi nimesema mojawapo ya mradi ambaa tunafanya kuiimarisha *transmission line* ili kweli zisidhoofike kama unavyosema, ni huu wa Iringa - Shinyanga. Mradi wa kutoka Kahama - Geita - Nyakanazi - Kigoma - Rukwa hadi Tunduma - Mbeya, miradi yote hii inatekelezwa lakini pia tunaboresha *transmission line* kutoka Morogoro - Chalinze - Tanga hadi Arusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii siyo kwamba tunaisema kinadharia, tayari tuna utaratibu wa kupata fedha kwa kutegemea vyanzo vya mikopo kama ilivyo kawaida kwa sababu hatuwezi kuwa na Bajeti ya kuweza kuhimili yote haya. Kwa hivyo Mheshimiwa Cheyo nimesema Mradi wa Makambako wakati nikimjibu Mheshimiwa Jenista Mhagama, ni mradi ambaa upo katika hatua za utekelezaji, bado hajafikia mwisho ndiyo maana pengine haionekani, lakini yote ni miradi ambayo ipo kwenye hatua za utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *ARTUMAS*, kilichokwamisha mradi wa *ARTUMAS* kama nilivyosema ni mambo mawili makubwa, kwanza ni mdodoro wa kiuchumi, kwa sababu ili mradi wa *ARTUMAS* utekelezwe na pale kulikuwa na fedha ambayo tulikuwa tumeomba tupate msaada kutoka kwa Serikali ya Uhlanzi, ulikuwa na masharti kwamba *ARTUMAS* mwenyewe na fedha yake apate mkopo, hakupata kwa sababu upo mparanganyiko ule wa tatizo la fedha duniani, ile ilimfanya asi-*qualify* kuweza kuwezesha hicho kitu kitokee. Lakini vingine ni kwa jinsi ambavyo yeye mwenyewe *ARTUMAS* alikuwa anawasilisha taarifa zake zinazotakiwa *EWURA* hazikuweza kukidhi, kama ungewahi kupata nafasi ya kuona mawasiliano kati ya Uhlanzi na *EWURA* haya ambayo yamejitokeza hapa ungebaini kwamba ninachokisema hapa ni cha kweli kwa sababu hayakuitokeza moja moja kwamba Serikali ilichangia mradi ule kuchelewa, ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi yangu.

MWENYEKITI: Nilikusahau maana yake muda umekuwa mwingi, tafadhalii Mheshimiwa Cheyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Nikae?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Waziri huku-*comment* kabisa juu ya *structure* ya Wizara, huku-*comment* juu ya *structure* ya *TANESCO*, kwa sababu haya mambo tutatoa pesa lakini kama hizi *structure* hazipo sawa sawa, ni kama tunatwanga maji kwenye *whatever*. Kwa hiyo, mimi ningependa pia wewe kama Mshauri Mkuu wa Rais u-*comment* juu ya mambo kama haya.

MWENYEKITI: Hawezi ku-*comment*, Waziri yeye ndiye mhanga mwenyewe, Serikali imesikia Mheshimiwa Cheyo.

MHE. PUDENCIA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunifapatia nafasi hii nami niweze kusema machache kuhusiana na Wizara hii. Kwanza kabisa napenda niipongeze Serikali kwa mipango yake mizuri kabisa iliyochochuka kutohana na tatizo hili la umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kupanga ni kuchagua na katika kupanga kunakuwa na *option* mbalimbali ambazo nafikiri kwa Serikali kukopa benki bado ninaona kwamba ni *option* nzuri na ni sawasawa kabisa na ni muafaka kabisa kwa sasa hivi, japokuwa kupewa ushauri haikatazwi na kutoa ushauri haikatazwi kwa hiyo, unaweza ukapewa ushauri mwingi lakini ukatafuta lile unalofikiri kwa wakati huo linafaa na ukalifanyia kazi na maamuzi

mengine yakaja kutumika kwenye maamuzi mengine kwa mambo mengine ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipo mbali sana na waliopita, tatizo langu nimekwishamfuata Waziri nikaongea naye kuhusu suala la Mpanda, mpaka sasa hivi Mpanda Mjini hatuna umeme takribani mwezi mmoja na nusu, wananchi wamekosa kuona vipindi vyao, wameshindwa kuwaona wawakilishi wao, wamelalamika sana kwani wanapenda sana kufuatilia ni namna gani pia Bunge linavyoendelea. Wananchi wa Mpanda wamesikitika sana kwa sababu wamekosa umeme kwa kipindi hicho na Waziri aliniahidi kwamba amekwishapata hizo *transifoma*.

Ninapenda aniambie ni lini atawapelekea wananchi wa Mpanda wa maeneo ya Mji Mwema na Majengo hizo *transifoma* ili waweze kupata umeme nao waweze kuangalia vipindi mbalimbali vinavyorushwa na TV zetu, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, analosema Mheshimiwa Kikwembe ni kweli, tatizo la Mpanda ni tatizo la *transfoma*, kwa hiyo palikuwa pana tatizo la *transfoma* na alishamuona Waziri, lakini na mimi ameniona tumeufuatilia na TANESCO anasema kwamba tatizo hili limeshughulikiwa, TANALEC wametoa *transfoma* zinaelekeaa sasa hivi Mpanda kwa ajili ya kukidhi tatizo la Mpanda na Majengo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani tunaweza tukampa taarifa baadaye kwa sababu TANESCO wenye we wapo hapa, tunaweza tukampa taarifa kazi hiyo ya kusafirisha na kuzifunga zitachukua muda gani. (*Makofii*)

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, mimi niseme kwamba kwa mara ya kwanza toka nimjue Waziri Ngeleja, leo amewasilisha vizuri sana, nampongeza kwa hilo, Waziri leo ametulia, ameongea kwa mamlaka, ametupa mpango wenyewe tija, na ameongea kama Waziri mwenye dhamana. Nakupongeza sana Mheshimiwa Ngeleja endelea hivyo, ndivyo tunavyotaka Mawaziri wetu mtende. Tunataka mfanye kazi kwa kujamini, msisubiri Wabunge wawakabe ndiyo mje na mipango mizuri hapa. Hili liwe ni fundisho, liwe ni onyo kwa Bajeti zijazo mkija na mipango ambayo haijakaa vizuri Wabunge tutawachana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka kusema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Ngeleja kwa ukomavu wake wa kisasa, maana yake amewaomba radhi Waheshimiwa Wabunge wote, ameomba radhi Watanzania wote kwa makosa ambayo au yeye mwenye we au watendaji wake wameyafanya ambapo kwake ilikuwa inapelekea Shirika lake la TANESCO liwe linawagawia giza Watanzania. Waziri ameomba msamaha, tumeupokea, Mawaziri wengine wajifunze, leo Ngeleja ameomba msamaha, hiki siyo kitu cha kawaida kwa Serikali yetu kuomba msamaha, tufike mahali sasa Mawaziri wengine siku nyininge mtendaji wako akikosea au wewe mwenye we basi Waziri uweze kujuzuru tuanze sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema hapo Wizarani kwako kuna mdudu yule anaitwa David Jairo, akina David Jairo bado hawajamalizika bado wapo pale Wizarani kwako, tunaomba upasafishe ufanye kazi vizuri, wadudu hawa wote lazima wamalizike ili Wizara yako iweze kwenda vizuri. Huyu mdudu ni lazima tumpinge kwa nguvu zetu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wako ulioleta hapa mbele mimi nina imani nao kwa sababu tu walau umetaja Shirika la NSSF, Shirika hili ni zuri, tuna imani nalo, hatuna wasiwasi tunajua kwa sababu mmeingia nao kwenye mkataba huu tunajua kabisa sasa Watanzania tutapata umeme na tuna matumaini na ninyi. NSSF endeleeni, muishike mkono Wizara ya Nishati na Madini. (*Makofii*)

Mhehsimiwa Mwenyekiti, miradi ya Ngaka, Mchuchuma pamoja na Kiwira nilzungumzia sana, nimeimba sana, wenzangu wamesema dharura sasa ifike mwisho, nataka kumuambia Waziri ufumbuzi pekee wa suala hili upo Ludewa, upo Mchuchuma kwa manufaa ya wana Ludewa wote na kwa manufaa ya Watanzania wote. Huu mpango ambao tumeuweka sasa wa dharura ni wa mwaka mmoja tu, mwaka mmoja siyo muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atufafanulie kuna mkakati gani hasa kwa ajili ya Mchuchuma baada ya mwaka mmoja. Naomba kupata majibu. (*Makof*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa nimshukuru rafiki yangu Mheshimiwa Filikunjombe, Mbunge mwenzetu kwa kutuunga mkono kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanaendelea kutuunga mkono kwenye hoja yetu. (*Makof*)

Pili nakubaliana na yeche kwenye kwamba hisia zake ni za kweli kuhusu adha hii ya mgao na sisi tutaendelea kuimarishe uwajibikaji wetu. Ninafahamu jukumu ambalo tunalo la kuwatumikia Watanzania, nafahamu dhamana tuliyonayo ni kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uimarishaji na hasa utekelezaji wa miradi ambayo Mbunge ameisemea, Mradi wa Mchuchuma, Ngaka na Kiwira. Mkakati tulionao kwanza ni kuhakikisha kwamba Makaa ya Mawe yanatumika kama nishati ya msingi ya kuzalisha umeme kama ambavyo tumekuwa tukisema hapa na kama vile ambavyo wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa sababu kimkakati madini ya makaa ya mawe na hasa inapoonekana kuna hali ya kuzalisha nishati ya umeme na matumizi mengine, tumelema kimkakati leseni zote za maeneo ambako madini haya ya mkaa wa mawe yanapatikana zitolewe kwa taasisi ya Serikali ambayo kwa sasa ni *NDC* lakini pia tunashiriki na *STAMICO*, huo ndiyo mkakati wa Kiserikali ambao tumeufanya ili sasa kuitia taasisi hizi tuendelee kuvuna rasilimali hizi kwa manufaa ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendelezaji wa miradi hii ya Mchuchuma kama ambavyo wenzetu Wizara ya Viwanda na Biashara walisema, mwendelezaji Kampuni ya Uchina ya *Sichuan Hongda Group* tuna uhakika kwamba mazungumzo yanakwenda vizuri na utekelezaji wake upo kwenye ratiba ambayo wenzetu waliifafanua hapa na nisingependa kutumia maneno mengi kurudia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngaka pia tumelema, lakini suala hili la Ngaka nafahamu juzi tumelizungumzia sana kuitia Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini sisi kama wadau kuitia Shirika la *TANESCO* tutafanyakazi pamoja na wenzetu kuhakikisha kwamba mradi ule tunautekeliza na hata Mradi wa Kiwira ambao kwa sasa hivi wenzetu wa *CHC* wanakamilisha utaratibu ili tuweze kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yote hii ni miradi ya Serikali kwa hiyo na Kiwira tumelema urudi mikononi mwa Serikali ili tuendelee na utekelezaji na mipango ya kupatikana fedha ilishafanywa na Serikali, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Hujaridhika jamani, haya! (*Makof*)

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata fursa hii. Wananchi wa Ludewa wamekuwa wakisikia sana kuhusu Liganga na Mchuchuma. Maneno haya yamesemwa kila siku lakini yamebakia kuishia kwenye maneno tu. Mheshimiwa Waziri, Wananchi wa Ludewa wanakusikiliza nataka uwape kauli thabiti kuhusu Mchuchuma na Liganga, naomba majibu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, nafahamu utekelezaji wake unafanyika kuitia Wizara ya Viwanda na Biashara lakini nataka niwakumbushe Watanzania popote walipo wakiwemo wa Ludewa wa Jimbo la Mheshimiwa Filikunjombe kwamba Serikali imewaaahidi Watanzania na Bunge hili likaridhia utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano, ule ukurasa wa 135 katika miradi iliyotajwa pale ambayo lazima itekelezwe na kwa sababu pia suala hili lina *element* za kisiasa kwamba sisi tusipotekeleza mpango huu kama Serikali iliyoundwa na Chama Tawala maana yake ni kwamba hatutakuwa tumetimiza ahadi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Filikunjombe kwamba Mradi wa Mchuchuma uko katika mpango na ndani ya miaka mitano utekelezaji wake umeshaanza kuitia miradi mbalimbali na Wanaludewa wawe na imani kwamba Serikali imesema

hivyo na Bunge hili limeridhia na ni ahadi ambayo lazima tutekeleze ili mwaka 2015 iwe pia ni mojawapo ya vigezo vya kuwaambia Watanzania tuliahidi, tumetekeliza, tunaomba tena nafasi nyininge ya kuendelea kuwatumikia Watanzania. (*Makof*)

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niseme nimevutika sana na kauli ya Mheshimiwa Waziri ya kuomba radhi. Hii ni kauli ya uungwana wa hali ya juu sana. Mimi naelewa kwamba ni kauli ambayo ameitoa kwa niaba ya Serikali. Sasa mimi nachotaka kusema ni kwamba Waziri aende mbele zaidi kwa sababu naamini kabisa kwamba Serikali inadhalilishwa sana na baadhi ya Watendaji wake hawa waliomfikisha Waziri hapa alipofika leo, napenda baadaye hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tatizo tulilonalo mimi nalifananisha na mgonjwa. Ukiwa na mgonjwa kitu ambacho unatakiwa ukifanye cha awali kabisa ni kumpeleka Hospitali. Kama huna kitu, utafanya kila njia hata kukopa ili mgonjwa aende hospitali kwa sababu asipokwenda hospitali atakufia. Sasa akifika hospitali, akishapona basi ndio utaanza kufikiria gharama zilizotumika kumfikisha hospitali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, nachosema ni kwamba huu mkakati wa Serikali, mimi nasema uendelee ili utuondoe hapa tulipo, sawa na mgonjwa ambaye tukisubiri atakufa baada ya hapo sasa tutaangalia nini tutakachofanya, ushauri uliotolewa utachukuliwa na utafanyiwa kazi. Ila tahadhari tu ni kwamba watakaompeleka mgonjwa hospitali wasinywe uji wa mgonjwa njiani. Ndio haya tunayosema kwamba hizi dharura na mikataba hii na ufisadi unawenza ukaingia. Sasa ufisadi usiingie kwa sababu ukiingia ni sawa na kunywa uji wa mgonjwa njiani matokeo yake mgonjwa atakufa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni uzembe uliopo *TANESCO*, upo wazi. Pamoja na matatizo mengi tuliyonayo, madeni na kadhalika, wale ambao wametembelea maofisi mengi ya *TANESCO* kuna uzembe wa hali ya juu sana huko, kuna rushwa nyingi zinazotembua huko. Watu hata waliojiandaa wanapata shida sana mpaka kuupata umeme pamoja na fedha zao mkononi. Kwa hiyo, tusizungumze kuongeza umeme tu na kuwalipa madeni yao, lakini vilevile, namwona Mheshimiwa Mwanri ananiangalia, wako Watendaji wengi sana ndani ya *TANESCO* ambao wanahujumu Shirika. Sasa tufikie mahali tuamue washughulikiwe kikamifu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nizungumze tatizo la umeme katika Jimbo langu la Rombo. Tumezungumza mgao Kitaifa lakini watu wa Rombo wana mgao wa umeme wa kudumu na hii ni kwa sababu *transmission line* inayokwenda Rombo ni ndefu sana, ni ile ya *TPC* inakwenda Boma Ng'ombe halafu ndio inakuja njia yote mpaka Rombo, kwa hiyo, umeme unaofika Rombo ni mdogo sana. Kwa hiyo, suala la kukatika kwa umeme Rombo ni kama wananchi wameshalizoea. Sasa nimesikia kuna tetesi sijazona kwenye vitabu vya bajeti, lakini nimesikia kuna tetesi kwamba kuna *line* itajengwa kutoka Kiungi kuja Himo kwenda Maloa na baadaye Wilayani Rombo. Napenda kujua kama kweli tetesi hizi zipo na kama zipo kazi hii itafanyika lini ili wananchi wa Rombo na wenye wawe na matumaini ya kuwa na umeme wa uhakika. Ahsante sana. (*Makof*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Selasini kwa kupongeza Serikali kwa hatua tuliyofikia na tunaendelea kusema sisi ni Watumishi wa Umma tunawajibika kwa Watanzania, mamlaka yote inatoka kwa wananchi. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuendelea kuwasheshimu na kuwaambia kile cha kweli ambacho tunadhani kwamba ni cha manufaa na chenye tija kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza na kumshukuru sana kwa kutuunga mkono katika mpango wenye na tatu tunazingatia ushauri wake kwa niaba ya wenzangu. Wako Watendaji wengi na kwa kweli hatua zinaendelea kuchukulia ndani ya Shirika letu la *TANESCO* hata sisi Wizara wapo ambao wanazidi kuvuta miguu, tunafahamu lakini kama nilivyosema wakati nafanya majumuisho, yako mambo mengine ambayo hatuwezi kuongelea hapa ndani, juhudhi zinafanywa kwa mujibu wa taratibu zilizopo kuhakikisha kwamba Shirika letu la *TANESCO* limefikia viwango vya ubora wa utoaji wa huduma kama ilivyokuwa miaka ya 1980 ambapo lilikuwa

miongoni mwa mashirika matatu Afrika yenyewe ubora wa hali ya juu kabisa. Huko ndiko tunadhamiria kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Selasini alivyosema, iko mipango mingi inayofanywa na TANESCO, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji kuboresha njia za usafirishaji na usambazaji katika maeneo mengi wala siyo katika eneo lake tu. Kwa hiyo, habari hizi ni kweli kwamba dhamira yetu ni kuboresha mifumo hii ya usafishaji na usambazaji umeme ili wananchi wapate umeme wa uhakika zaidi. Kwa hiyo, namthibitishia kwamba mpango huo wa kuboresha huduma hiyo upo na pia hata maeneo mengine tutazidi kuboresha ikiwa ni pamoja na kwa Mheshimiwa Lekule Laizer kwa sababu kuna miradi yake ambayo kwa jinsi wanavyopakana ameomba tuyazingatie na sisi tunayafanya kazi maeneo haya. Ahsante sana.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, la mabosi wangu wapigakura wangu, ahadi za Mheshimiwa Waziri katika kipindi cha miaka mitano iliyopita wakati nasema alikuwa bado *dynamic* pamoja na Naibu Waziri wake ukiacha hapa katikati, aliahidi kwamba Ofisi ya Madini itahama kutoka Handeni italetwa Kilindi ambapo wachimbaji karibu ni asilimia zaidi ya 80 lakini hadi leo ni miaka mitatu na nusu wananchi wa Kilindi tunauliza kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo umeme umepita hadi kufika Makao Makuu Songe lakini pia tunashangaa maeneo mengi, katika mchango wangu nilainisha mfano Kwamaligwa, Msanja na maeneo mengi ambapo umeme umepita bado hakuna *transformer*, ahadi zimekuwa nydingi tunaambiwa ziko Tanga hazifiki mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la pili nilitaka kuuliza pamoja na mpango mzuri waliokuja nao wenye tija na kama kila mtu alivyoisifu, mimi nawapongeza, naipongeza Serikali yangu, tatizo langu ni moja, Watendaji ni walewale, ukiacha yule wa juu ambaye najua mchakato wake unaendelea, nazungumzia ndani ya Wizara. Wanaweza wakaleta mipango mizuri, Watendaji wakawa wale wale mambo yasiende. Sasa sijui Waziri ana mkakati gani kufanya siyo *overhaul*/angalau mabadiliko makubwa kabisa ndani ya Wizara? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nilikuwa najaribu kufikiria lakini nadhani nikifikiria kwa nguvu siyo vibaya, COPEC ambaao tumewapa dhamana sasa ya kufanya biashara ya mafuta ambaao uwezo wao kidogo ni mdogo, nadhani wana vituo takribani, kama nimeelewa katika maeleo mbalimbali tuliyoyapata, wana vituo visivyozidi vitano ndani ya nchi lakini BP kwa taarifa ambazo zipo wamekuwa muda mrefu wakitaka kuuza *shares* zao 50 ambazo na sisi tuna *share* ili waweze kuondoka. Je, kwa nini basi Serikali tuisiwawezesha COPEC kununua *shares* za BP ili kwamba sasa waweze kuwa na vituo vingi zaidi tukawa *full-fledged*? Ahsante. (*Makof*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumshukuru Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, kwa ushirikiano ambaao amekuwa akitupa sisi Wizarani lakini pia nimpongeze kwa ufuatilaji wa masuala yake yanayohusu wapigakura wa Jimbo lake. Labda niseme tu kwamba Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, ni mojawapo wa wadau wa karibu sana wa Wizara ya Nishati na Madini kwa sekta zote, upande wa umeme lakini pia kwenye madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la uhamishaji wa Ofisi ya Madini, ni kweli tumechukua muda mrefu lakini changamoto iliyokuwa mbele yetu ni hiyo moja tu kwamba bajeti zimekuwa zikipita lakini mafungu kwa kweli na hili narudia tena kusema wala siyo la kumlamu mtu yejote kwa sababu ni makusanyo ndio hivyo hatukuwa tunafikia malengo. Kwa hiyo, kadri ambavyo inakuwa fedha hatupati kulingana na mipango ambayo Bunge hili limekuwa likipitisha ndivyo ambavyo tumekuwa tukiathirika kutekeleza miradi mbalimbali. Naamini kwa hatua tuliyofikia sasa na hasa huu mpango wa kufanya sekta hizi hasa sekta hii ya nishati iwe kipaumbele katika utekelezaji wa mpango wetu wa miaka mitano, mambo mengi yatafanya kama vile tulivyoeleza hapa kupitia REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya *transformer* haya ni mambo ambayo kwa kweli ni endelevu, yanafanyiwa kazi lakini nimwambie tu kwamba sisi na wenzetu tumejipanga kuhakikisha kwamba tatizo ambalo Mheshimiwa Beatrice Shellukindo limekuwa likimkabili kwa muda mrefu linaisha kwa sababu tunafahamu ni kero ya muda mrefu na yeye anabanwa na wananchi wake kama ambavyo sisi wengine tunabanwa kwenye Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuimarisha utendaji, kwa mara nyingine niseme tu ningekuwa mtu wa makamu kidogo ningesema kuishi kwingi ni kuona mengi. Sasa nataka niseme kwamba si haba hata Wizara ya Nishati na Madini yako mambo nimeyaona na tumeanza kuyafanya kazi. Nawaahidi Watanzania kupitia Bunge hili Tukufu, yako mambo wataona kiutekelezaji yataleta mabadiliko makubwa kwa jinsi ambavyo tumejipanga, ni sehemu ya utekelezaji wa mipango na uimarishaji wa utendaji Serikalini si kwa Wizara ya Nishati na Madini peke yake lakini pia hata kwenye Wizara zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la *COPEC* kama alivyosema ni kweli na hasa kuhusu hizi hisa asilimia 50 kwenye kampuni ya *BP*, ule mchakato wa mauzo kuhusu *BP* ulishafanyika mwaka jana kwenye hisa zao sisi asilimia 50 zetu bado ziko palepale. Nafikiri kwa sababu mchakato wenywewe ulishapita pengine niseme tu kwamba sasa hivi siyo rahisi, tumechelewa, *COPEC* tumeipa leseni yake ianze kazi juzi lakini wazo hili lilikuwa ni zuri sana lakini bado sisi kama Serikali tunasema tuna ule mpango wa kuwa na *Strategic Oil Reserve* ambao ndio sasa hivi tunaendelea kuufanya kazi na kuifufua *COPEC* mambo haya tunahakikisha yatatuifikisha mahali pazuri hasa mafuta ya Tanzania. Kwa hiyo, ni mambo ambayo tunayafanya kazi Serikali. Nashukuru sana.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa mpango mzuri. Wakati tunaahirisha kipindi kile tuliwaambia waje na Mpango wa Dharura wa sasa. Sasa wamekuja na mpango mzuri mpaka umesababisha baadhi ya Wabunge tumeishiwa hoja, tunasema tena hatutaki Mpango wa Dharura. Tulichotaka si ndio hiki? Tulichotaka ni waje na Mpango wa Dharura wa sasa na ndio wamekuja nao. Sasa tukianze tena kusema hatutaki Mpango wa Dharura, ehee, haya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilisema Jimbo la Mtera lina Vijiji 62 lakini vyenye umeme viwili, tena umeletwa na Kanisa la Anglican. Nilitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kuzipa walau Taasisi za Serikali zilizoko kwenye Jimbo lile ili wananchi wawze kunufaika na umeme Vijiji? Nini tamko la Serikali? Ahsante sana.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Lusinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Lusinde amekuwa anafuatilia sana upatikanaji wa umeme kwenye maeneo ambayo amesema. Amekuwa akiyasemea kwa kweli kupitia maswali ya nyongeza na maswali ya msingi hapa Bungeni. Mimi nilishaelekeza *REA*, *REA* wanafanya kazi miradi yake na kwa sababu kama nilivyosema wakati nafanua hoja zilizoulizwa na Waheshimiwa Wabunge, awali uwezo wa *REA* kwa mwaka huu wa fedha ulikwama sana lakini kwa sababu ya vyanzo ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmetushauri na Serikali inavifanya kazi, nimhakikishie Mheshimiwa Lusinde na wananchi kwa Vijiji ambavyo tumekuwa tukijadili, tutatekeleza kupitia Mfuko wa Nishati na Madini. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Serikali imeleta Mpango wa Dharura, nina mambo matatu. La kwanza, sote tunakubali kwamba Serikali ikope lakini ikope kwa maana ya kwamba huu mkopo utaweza kurejeshwa na wananchi wa Tanzania hawataweza kubeba hilo deni kubwa. Pili, vilevile Serikali iangalie kwamba inapunguza kuibebesha mzigo *TANESCO* kila wakati kwa gharama ambazo hazina sababu. Kwa hiyo, nilitegemea katika mchakato huu, moja lingefanyika kwamba kwa mfano sasa hivi tunavyochukua *diesel*, *generators* watakuwa *TANESCO* wananchi mafuta kwa si chini ya dola 1800 wakati ukitumia *heavy fuel* ni dola kama 600 au 700. Kwa hiyo, tayari una *different* ya chini ya dola 300, 400 hapo zinapotea bila sababu. Sasa kama kweli mnataka kuisaidia hii *TANESCO* katika hii dharura yenye, tungejielekeza katika mahali ambapo tutapunguza gharama za kuibebesha *TANESCO* na kwa maana hiyo Serikali, ushauri wangu wa kwanza ulikuwa ni huo kwamba katika mchakato huu kwa hii mitambo yote ambayo imechukuliwa, sehemu kubwa sana inatumia *diesel* ambayo gharama yake ni kubwa, nilifikiri Serikali ingekuwa wise *enough* kuipunguzia mzito *TANESCO*, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, wakati Waziri anatoa majumuisho hapa alizungumzia suala zima la kutoa kodi. Sina hakika wakati tunapitisha *Finance Bill* kama haya yalikuwemo ndani ya zile kodi ambazo Waziri wa Fedha alisema zinaondolewa, sina hakika. Kama amepata *mandate* hiyo na Kanuni yetu ya 102 haituruhusu hivyo, nataka tupate ufanuzi kama haya maeneo ambayo amesema yanatolewa kodi hivi sasa je, yamo ndani ya ile *Finance Bill* ambayo tulishaipitisha wakati wa bajeti au vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu nilitaka vilevile nipate ufanuzi kuhusu mikopo inayokopwa kwenye *Commercial Bank*, ni dhahiri kwamba hizi *capacity charge* na gharama nyingine zina-*include* hizo *interest* ambazo zitaingizwa kwenye kodi. Sasa ile 26, 30, 40 *cense* lazima u-*add* na ile *interest* tutakayokuwa *charged* mbele ya safari. Sasa sina hakika kama Serikali hayo nayo imeangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nilitegemea vilevile Serikali ingeangalia na ile Sheria yetu ya *PPP* ambayo imepitishwa katika mchakato mzima wa kupunguza mzigo kwa mashirika yetu, ilikuwa vilevile tuingie katika utaratibu wa *PPP*. Sina hakika kama mchakato huu, Serikali nalo hilo imezingatia, ningependa kupata maelezo. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwanza kwa kukubali kwamba Serikali *at anyone stage* lazima iingie kwenye *borrowing* ya aina yoyote na kwa maana hii tunataka tujielekeze kwenye *domestic borrowing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani katika mambo ambayo tumejaribu kusema lazima moja liwe *clear kwamba borrowing* hii inafanywa na tunajielekeza kwenye sekta ambayo tunatarajia ilekee kwenye uzalishaji lakini hata haya matumizi yenye ya umeme ikiwa umeme wenye unatumika kwa ajili ya *domestic use* tu, kuwashaa taa na nini, *then we have problem* lakini *right now* tunasema kwamba katika huu umeme ambao tunatarajia tutazalisha katika mfumo huu, mwangi uelekee kwenye uzalishaji wa *economic development* na *capacity building* kama viwanda na *economic activities* zingine. Sasa kwa maana hiyo, tunatarajia kwamba yenye itatafuta *justification* ya kukidhi hii. Kwa hiyo, tumepokea hii ya kwamba Serikali ikope na tuwe waangalifu hapa kwenye *Commercial Bank lending* na pia kwenye kukokotoa hizo gharama kwamba *there is some such interest* ambazo zimetokana na *Commercial Bank lending* ziwe reflected kwenye gharama. Ndiyo maana tukahimiza kwamba kwa mfumo huu tunategemea *operational cost* ishuke ili tuelekee kwenye matumizi ya *gas* ambayo ni *60% cheaper* kuliko kuendelea kutumia mafuta *for over period of 24 months* ambazo ni *more expensive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusema hayo ndiyo nasema kweli unavyosema, *HVO it is likely cheaper*, ni bei ya kawaida, kuliko *Jet A-1* na dizeli lakini kwa mitambo tuliyokuwa tunataka, tulikuwa tunataka mitambo ambayo *dual-fired* kwa maana kwamba hii mitambo tunayotafuta sasa hivi yote ni *switch* tu ya *24 hours*, *gas* ikiingilia tuhamie kwenye *gas* badala ya kuingia kwenye mitambo ya *H4* ambayo unapotaka kuibadilisha, wanasema *process* ya kutoka kwenye *H4* kwenda kwenye *gas technical* ni kubwa zaidi kuliko hii ambayo una-*switch off* leo unatumia dizeli. Kwa hiyo, hilo ndiyo lengo kwa sababu matarajio ni kuingia kwenye *gas* miezi 12 hivi wa mitambo hii.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Lile la kupunguza kodi sikujibisha sijui kama Waziri hapa alikuwa anasema kwamba kutakuwa na kodi za mafuta zinapunguzwapunguzwa. Nataka kuuliza je, katika ile *Finance Bill* tulioipitisha nazo hizi ziliwu zimetajwa au hizi ni za ziada na zitakuja baadaye katika utaratibu ambao pengine si wa Kikanuni, maana katika mfumo mzima bajeti itakuwa imevurugika, hajanijibu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie dakika zangu tatu kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba kuna miaka miwili ambayo tutakwenda nayo kwa kutumia hili *fuel* pamoja na dizeli wakati huo tuna kazi ya kuhakikisha kama *gas* inafika. Sasa ukichukua hiyo *period* ya miaka miwili, kila mwaka mmoja kwenye dizeli ni *about USD million dollars* zitatumika kwa mwaka. Kwa hiyo, una miaka miwili hapo unatumia huku unangojea *gas*, unatumia *that amount of money*. Sasa ndiyo

nasema pengine Serikali pamoja na huu udharura uliopo bado hamjaweza kukaa kitako mkaona hizi *heavy cost* ambazo hazina sababu mkawea kuzipunguza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lile la kupunguza kodi limeambatana na utaratibu huu wa udharura wenye mafuta na mafuta yenye tunajielekeza kwenye yale ambayo yanaelekea kwenye kuzalisha umeme tu. Sasa tunachosema ni kwamba kwa utaratibu huo tumekubaliana ndani ya Serikali kwamba Wizara ya Fedha kwa sababu ndiyo mhusika wa kodi atafuata taratibu za kisheria kuleta hoja hiyo kwamba tukubali kwa dharura mafuta yanayoelekea kwenye lengo hili tu ndiyo yatapunguzwa kodi yote kwa lengo la kushusha bei ya umeme ambayo tutafikisha kwa mtumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili la miaka miwili kila mwaka *900 million USD dollars*, nadhani ndiyo hilo tumesema, leo ni Agosti, mkakati ni kuwasih, TPDC imeshaanza kufanya mikakati na Wachina na tumesema mwezi ujao wiki ya kwanza, Mawaziri na timu nzima wanakwenda kumaliza *negotiations* ambazo zinatakiwa zimalizike by *23rd of September* ili kutoa siku saba kwa Wachina kuridhia pesa hizi ambazo zinaombwa kwa ajili ya utaratibu huo na kama kuna pesa ya ziada kwa ajili ya *ku-accelerate* mradi huu badala ya kupata kwa miezi 24 au miezi 18 tu tuiplate ndani ya miezi 12. Tumesema kwamba tunafanya mkakati ili kile ki-element cha *domestic funding internally* kifanywe na *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema kwamba katika hili tuondoe wasiwasi wa kwamba *900 USD million* mara *two years* sio makusudio yetu. Makusudio yetu ni kutumia hizi *trillion 1.2* hadi Desemba mwakani. Sasa kama tukiweza kuingiza *gas* mwezi wa nane siyo *trillion 1.2* tena ni pesa pungufu sana kuliko hizi tunazotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tushirikiane kwenye kuhakikisha kwamba mkakati huu wa kuleta *gas* unakamilika kwa haraka iwezekanavyo kwa sababu ndiyo mwokozi wa gharama zote hizi.

MWENYEKITI: Ahsante. Utaratibu wetu kidogo sio nzuri kwa sababu mlionomba mlikuwa 108 na toka tumeanza ni watu 16 tu wamepata nafasi, kwa hiyo, ni utaratibu mbaya kabisa. Namwita Mheshimiwa Masauni.

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa maoni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kuipongeza Serikali kwa kuja na mpango huu mzuri kabisa wa dharura. Wakati nikichangia nilikuwa nimejaribu kutoa mapendekezo ambayo nashukuru sana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameyatilia maanani kwa kiasi. Nilipendekeza kwamba matatizo ya umeme ambayo tunayo, moja katika ufumbuzi ambao utatusaidia sana ni kuwa na Mfuko wa Nishati. Pia nilipendekeza vyanzo ambavyo tunaweza tukavitumia kwa ajili ya kupata fedha kwa ajili ya Mfuko huo. Mfano matumizi ya asilimia 20 ya *Fuel Levy*, matumizi ya *VAT* kwa vyanzo vya nishati, fedha ambazo zinabaki kutohakana na makusanyo ya *EWURA*, ongezeko la kodi ya mafuta ya taa kwa asilimia, kutoka kwenye matumizi ya simu na kadhalika. Nashukuru Mheshimiwa Waziri katika haya mapendekezo sita mawili yapo katika mapendekezo yake lakini pengine akiona na haya yanafaa kwa baadaye anawenza akayatilia maanani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza na la msingi ni kwamba katika Mpango huu wa Dharura tuna upungufu wa *megawatt 300*. Nimesema ni mpango mzuri sana. Serikali inastahili sana pongezi kwa kuja na mpango huu lakini ni mpango ambao una gharama kubwa sana. Jambo zuri ni lazima liwe na gharama lakini kama kuna njia ambazo tunaweza tukapunguza gharama kuzitumia napo siyo jambo baya. Sasa kuna *Spring Reserve* ya wastani wa *megawatt 272* ambapo gharama zake ukichanganya na *capacity charge* na mambu mengine yote ni fedha nyingi sana. Sisemi kwamba fedha hizi ziingizwe katika mfuko lakini leo tuna Mfuko wa *REA* ambao unafanya kazi nzuri ya kusambaza umeme vijijini, nafirikia pengine tungetafuta njia za kuongeza uwezo kwenye huu Mfuko wa *REA* ili uweze kushirikiana na *PPP* kuweza kuibua miradi katika Mikoa. Nikizungumzia utaratibu wa kupeleka madaraka Mikoani

nikiwa na maana kwamba tunapokuwa na vyanzo vya uzalishaji katika Mikoa mbalimbali tuna *mini-hydro potential* kubwa sana katika Mikoa mingi ya Tanzania zingeweza kusaidia kupunguza ama kupunguza hii *grid stability* ambayo inatokana na kupeleka vyanzo vingi vya umeme eneo moja. Kama sasa hivi vyanzo vingi vya umeme viko Dar es Salaam, huu mpango unapendekeza vyanzo vingine vitapelekwa Mikoa mingine lakini ukiangalia mchakato unapata mashaka kidogo. Kwa hiyo, pengine utaratibu huu wa kuweza kuibua vyanzo kwa kushirikiana na *REA* na hizi *PPP* Mikoani ungesaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar, niligusia suala la bomba la mafuta ya *gas* ambalo Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba bomba hilli litaanza kutoka Mtwara kuelekea Dar es Salaam hadi Tanga lakini hakutilia maanani pendekezo la kuunganisha kipande kidogo cha kutokea Dar es Salaam kwenda Zanzibar ili na Zanzibar nao waweze kuzalisha umeme kwa kutumia *gas*. Hii ingesaidia sana kupunguza mzigo wa uzalishaji katika eneo moja. Mheshimiwa Waziri alizungumzia vizuri sana kwamba hatuvezi kuwa na vyanzo vyote katika eneo moja mbali ya *grid stability* lakini tunaweza kujikuta tuna matatizo ya upotevu mkubwa wa umeme. Naomba Mheshimiwa Waziri hili ni muhimu sana, la *pipe line* ya *gas* nalo pia litiliwe maanani katika kujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo pia nilijaribu kuligusia na pia nashukuru kwamba wachangiaji wengine nao waliliona ni kwamba kuna haja pia ya kuhakikisha tuna *improve efficiency* na *accountability* katika Shirika la *TANESCO*. Hii inaweza ikasaidia sana kwa kuangalia *structure* ya *TANESCO* kwamba sasa wakati umefika pengine kufikiria ni jinsi gani muundo wa *TANESCO* kwa maana ya kuligawanya Shirika lile ili *generation, transmission distribution* ziweze kufanya kazi kwa kujitegemea. Sisemi jambo hilli lifanyike sasa hivi kwa kurupuka. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Nadhani ni ushauri zaidi kuliko jambo lingine lolote. Wewe umetoa ushauri naomba jamani tusirudie maana muda unakwenda, Mheshimiwa Kibona.

MHE. ALIKO A. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Naomba nianze kuchangia kwa ufupi kama ifuatavyo.

MWENYEKITI: Naomba tuombe ufanuzi tukichangia ndiyo kosa tulilolifanya hapa ndani, watu wamechangia badala ya kuuliza maswali ya kutaka ufanuzi.

MHE. ALIKO A. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe kwenye Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, nimefanya ziara kutembelea migodi ya Kiwira na Ngaka. Kule Kiwira, Shirika la *NSSF* lilieta wataalam wake na tulikuwa nao pale wakionyesha nia ya kuingia ubia, kuchangia kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe. Wataalam wakatuambia kwamba duniani kote hakuna urahisi wa kuzalisha umeme kama ilivyo katika makaa ya mawe. Tetesi ambazo ninazo kuna vizingitizingiti vya kukwamisha *NSFF* isiingie katika mchakato huu wa kupewa mgodi wa Kiwira na kuzalisha umeme kwa Taifa letu. Naomba Waziri anipe maelezo ni kitu gani kinachelewesha takribani sasa ni miezi minane tangu *NSFF* waleta maombi hayo Serikalini? Kwenye majumuisho yake sikusikia kutaja *NSFF with connection* na Kiwira. Naomba atakapokuwa ananijibu anipe maelezo juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ileje haina umeme kwa sehemu kubwa. Naomba Waziri anisaidie kwamba ana mkakati gani kusaidia kuleta umeme hasa kwa kutumia Wakala wa Umeme Vijijini (*REA*) kwa Wilaya ya Ileje? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *NSSF* walionyesha nia ya kuingia kwenye kuendeleza mradi wa Kiwira wa kuleta umeme. Tatizo ni kwamba katika wakati huu wote mradi ule wa Kiwira bado ulikuwa kwenye mikono ya *Consolidated Corporations*, Wizara ya Fedha kule kwa *Treasury Registrar* kwa kuhakikisha kwamba unababilisha umiliki wake. Sasa *NSSF* nadhani walikuja Ofisini, Wizara ya Nishati na Madini

wameleta mapendekezo yao lakini na wawekezaji wengine wamekuja na mapendekezo yao, Wachina wamekuja na pendekezo la kukopesha pesa kiasi fulani kwa ajili ya kuendeleza mradi huu. Mimi nadhani tumepokea maoni ya Mheshimiwa Kibona ya kwamba ni vema *especially* katika *scenario* hii ya kukopa kwa utaratibu wa *PPP* kama akajitokeza mtu ambaye ana uwezo wa kuendeleza mradi huu wa Kiwira na kupunguza ule uzito wa kukopesha kwa Serikali basi tutakaa tutafikiria. Kwa hiyo, kuna suala la *NSSF* aje na mpango wake na huyo mwekezaji mwininge na Mchini waje na mipango yao, tutafanya tathmini na tutapata njia bora ya kuendeleza mradi wa Kiwira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *REA*, naomba nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kuendeleza miradi ya *REA*, lleje ipo katika ile miradi karibu 170 niliyoisema wakati nachangia ambayo kwa mpango wote wa *REA* jumla yake ni kama shilingi bilioni 170. Kwa hiyo, utekelezaji wake kusema kweli nadhani ni vema tuanze na ile miradi ambayo imechelewa kwa miaka miwili, mitatu lakini tutafikia.

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi hii. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa mpango huu iliokuja nao lakini ni matumaini mapya kwa Watanzania kwa kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilisema kwamba Serikali illahidi watu wa Mtwara watapata umeme kwa gharama nafuu na iliyahidi kuwaingizia umeme kwa shilingi 60,000 lakini mpaka sasa hivi hatujasikia kitu chochote Mheshimiwa Waziri akiongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine amesema kwamba ARTMUS imekosa mkopo lakini sasa hivi umeme unaozalishwa Mtwara unazalishwa umeme wa *gas* na zamani tulikuwa tunapata umeme wa genereta. Ule wa *TANESCO* ulikuwa ni dola senti 35 kwa *unit* moja, sasa hivi umeme tunaozalisha wa *gas* kwa *unit* moja ni dola senti 11 kwa *unit*. Ni tofauti kubwa sana na sasa hivi *TANESCO* inapata karibu faida ya dola milioni moja ambayo ni sawa na 1.5 bilioni. Kwa sababu Serikali imeshawaahidi watu wa Mtwara kuwapa umeme kwa gharama nafuu na kwa kuwa ARTMUS hawakupata mkopo, kwa nini sasa hivi faida hii kubwa *TANESCO* inayopata basi isitumiwe ili wananchi pale wakaingiziwa umeme kwa gharama nafuu ili ahadi hiyo itimizwe kwa watu wale? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri alikuwa anajibu majibu hapa ya Mheshimiwa Wambura na akasema sasa kampuni ya ARTMUS imeuzwa, yaani hisa zake zimenunuliwa *Wentwork Resources* lakini sasa hivi wakati Mheshimiwa Waziri amesimama hapa ana-wind up pia amesema kwamba ARTMUS hisa zake zimeuzwa lakini amenunu AGGREKO. Sasa tunataka kujua ni *Wentwork Resources* iliyonunua au ni AGGREKO kwa sababu Mheshimiwa Waziri anaongelea AGGREKO na Naibu Waziri anaongelea *Wentwork Resources*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mtwara sasa inakua. Sasa hivi Manispaa ya Mtwara tumegawa viwanja 1,500 katika Kata moja ya Mitengo ambayo kuna *Vyuo* vitatu vinakuja pale na Hospitali ya Rufaa inajengwa pale. Tuna tatizo la umeme, hakuna umeme pale na *line* ya umeme imepita, tatizo ni *transformer*. Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie ili atusaidie tuweze kupata umeme kwa gharama nafuu kwa faida hiyo inayopatikana pale *TANESCO* sasa na aangalie kwa ukuaji wa Mkoa Mtwara na hususani Manispaa ya Mtwara na eneo hilo la Kata ya Mitengo ili aweze kutusaidia ili tuweze kupata umeme.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri maelezo ya suala hili kwa kirefu tumejibu jana tu kwanza niseme Waziri hakusema kwamba ARTMUS wameuza hisa kwa AGGREKO, AGGREKO ni kitu kingine kabisa na ARTMUS wameuza hisa kwa *Wentwork Resources*. Hapa katikati walikuwa na kampuni tanzu ya *Umoja Light* ambayo ndio ilikuwa inafanya kazi zile za kusambaza umeme lakini kwa sasa hivi baada ya mambo yao kwenda kombo kidogo wameuza hisa zao kwa *Wentwork Resources* na *Wentwork Resources* wenywewe wamekuja Wizarani kuleta mpango wao kuendeleza mradi huu. Mheshimiwa Waziri aliwaelekeza kwangu na mimi nimekaa nao, nimekuja kugundua kwamba gharama zao za kuendeleza mradi ni kubwa. Kwa hiyo, bado tunawasiliana nao ili kuangalia namna ya kuweza kusambaza huduma

hii na ikibidi ifanywe na *TANESCO* ambao nao wana ubora huo lakini walishaanza kujitoa kwa sababu ya mikataba ambayo tulafikiana kabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema jana na hili naomba niliseme ili Watanzania wenzetu wa Mtwara na Lindi walielewe. Ni kweli chini ya utaratibu uliokuwa umekubaliwa, awali walikuwa waunganishe umeme kwa shilingi 60,000/- ambapo ni gharama za *VAT* katika jumla ya gharama laki tatu na elfu tisini na tano ambazo gharama hizi zingefidiwa na pesa za msaada kutoka mfuko wa *ORET* wa Serikali ya Uholanzi. Sasa katika yale majadiliano baina ya *ORET* na *EWURA* waliposhindwa kuafikiana ule mkopo umekaa kwa muda kama miezi 24 hivi, wale Waholanzi wakasema wameshindwa kuafikiana basi. Sasa katika kule kushindwa kuafikiana baina ya *EWURA* na ile kampuni na ndiyo na sisi tukashindwa kupeleka umeme kulingana na msaada ule ambao ungepatikana ambao haukuwa wa kuunganisha tu lakini pia tulisema jana kwamba kulikuwa na *element* ya kuboresha miundombinu lakini pia kulikuwa na *element* ya kuongeza *sub-stations* moja pale Mnazi Mmoja na nyagine nadhani kule Nyangao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Serikali imesema jana na leo tunarudia tena na naomba ndugu zetu wa Mtwara wa Tandahimba kule na Newala na kote mpaka Mangaka na Mnazi Bay, Lulindi na kwa sababu ni Mkoa wa Lindi pia Nachingwea, mradi huu unaenda kote kule mpaka Mchinga, ni lazima Serikali tutafute utaratibu mbadala kwa sababu hii ni ahadi ya Serikali na tumekubaliana kwamba, kwa sasa hivi tunaangalia namna ya kuwaunganisha wananchi kwa awamu au kutafuta namna ya kupunguza gharama ili tuweze kuendana na ile ahadi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile lingine la kusema gharama za uzalishaji na gharama za uwekezaji, alichokuwa anasema Mheshimiwa Murji ni kweli, ni gharama za uendeshaji kwa maana ile *production unit cost* sasa hivi ni *11 cents*, lakini bado kuna uwekezaji mkubwa ambao ulikuwa umefanywa kabla ambao inabidi katika mfumo ule mzima wa umeme ambao pesa zake inabidi zirudishwe na ndio maana pana *tariff equalization fund* ambayo inalenga kuwapa wananchi umeme ule kwa *tariff* ya nafuu kidogo wakati ambapo pesa za kurudisha gharama za uwekezaji wa mradi zinafidiwa.

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua tu kwamba, Serikali ilitoa dola milioni saba kwa kampuni ya *ARTUMAS* na hiyo kampuni sasa hivi inauza hisa zake, je, zile fedha ambazo Serikali iliwapo zitarudi au viper?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba, uwekezaji uliofanywa na Serikali katika kutoa zile pesa, pesa zile zilitolewa kwa namna mbili, kwanza ilikuwa ni mchango wetu katika uwekezaji lakini pili nasema kuna pesa za makusudi zilitolewa na Serikali ili kuweza kufidia gharama zile kama *stimulus* fulani kwa ajili ya kuwezesha *tariff*, kwa maana ya kiwango kinacholipiwa na wateja kuwa ni chini zaidi. Kwa hiyo, haya mawili yote nadhani Mheshimiwa aelewé tu kwamba, moja lilikuwa ni kwa ajili ya kuchangia katika uwekezaji na lingine lilikuwa kwenye *tariff equalization fund*.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipatia nafasi. Kwanza, naomba niipongeze Serikali kwa kukubali kusikiliza hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani na kuona kwamba tatizo la umeme ni tatizo kubwa, ni janga la kitaifa ambalo linahitaji utatuzi wa kidharura, naipongeza Serikali. Pia nawapongeza Wabunge wote kwa jinsi tulivyoichukulia hoja hii. Kwa kweli wote tumekuwa na msimamo mmoja kuonesha jinsi gani tunakerwa na matatizo ya umeme. Nina hakika Bunge likiendelea hivi, kwa hoja za msingi, kushikamana kuibana Serikali ili iweze kuwajibika vizuri, nafikiri tutakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitoe mchango wangu kama ifuatavyo. Tatizo la umeme limetokana na matatizo ya kiungozi na mikataba mibovu kuanzia kwenye *IPTL*, ubinafishaji wa *TANESCO*, matatizo ya ujisadi wa *RICHMOND*, ujisadi wa Kiwira. Matatizo haya yalisababishwa na mikataba mibovu na hivi sasa tunaelekea tena kwenye mkataba mpya ambao utatumia mafuta. Kwa maelezo yaliyosemwa hapa ni kwamba, umeme utapatikana kwa gharama kubwa sana, kwa malori 50 kila siku ya mafuta kupelekwa Mwanza, Tanga, Arusha, kitu ambacho ni gharama kubwa sana. Wakati huohuo sijui itakuwaje katika kusafirisha hayo mafuta ukizingatia

miundombinu yetu ilivyo, usalama wa hayo mafuta ukoje? Ni kitu ambacho kinaashiria kwa vyovoyote vile inaweza ikatokea tena aina nyingine ya ufisadi humo ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza vilevile Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, eti gharama zote hizi za upatikanaji wa umeme ambazo zitakuwa ni kubwa kupita kiasi, hazitamgusa mwananchi wa kawaida! Sasa sijui hapa anatueleza nini? Utakwepaje kumhusisha mwananchi wa kawaida, ukaongeza gharama hizo upande wa viwanda na maisha ya Mtanzania yanategemea viwanda, mahitaji yake yote atayanunua madukani ambayo yanatengeneza bidhaa hizo kwa kutumia umeme ambapo viwandani utakuwa umepandishwa bei kutokana na gharama za uendeshaji. Sasa Mheshimiwa Waziri, mimi hili limenisumbua, anaposema kwamba hatahusishwa mwananchi wa kawaida kwa gharama hizi za umeme, je, mahitaji yake muhimu ambayo yanatokana na viwanda, atayapata kwa njia zipo? Ama sasa kutakuwa na bei tofauti ya wananchi wa kawaida na wananchi wa madaraja mengine kwamba wao watapata bei nafuu, watatolewa kodi, watatolewa gharama za uzalishaji na wengine watalipia gharama hizo za uzalishaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, atueleze hili, mwananchi wa kawaida atakwepeshwa vipi kuhusishwa na matatizo ya umeme? Kwa sababu, tunapozungumzia tatzito la umeme, sio la taa tu kuwaka nyumbani, ni pamoja na mahitaji ya msingi ambayo yanahitaji umeme viwandani na ndio hasa ukali wa maisha umetokana na hayo kwamba, mahitaji yetu tunayapata kwa gharama kubwa sana madukani kiasi kwamba, maisha yanazidi kuwa magumu sana! Sasa Mheshimiwa Waziri, angetueleza hilo ili mwananchi wa kawaida yule anayetusikiliza ajue huo unafuu atakaoupata yeye kama mwananchi wa kawaida, ukoje. Hiyo ahadi ya Mheshimiwa Waziri ambapo hatamhusisha mwananchi wa kawaida kwa gharama hizo itatekelezwa vipi? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nimsaidie Mheshimiwa Chiku Abwao, nadhani hakumuelewa Mheshimiwa Waziri. Alichosema ni hivi kuna namna nne za kuchaji. Kile kima cha chini kabisa cha *TANESCO* ni pale ambapo mtumiaji yule anakwenda anasema mimi nataka *tariff* hii na kwa matumizi hayo sitazidi *unit 50*. Sasa kwa maana Watanzania wengi amba ni wale watumiaji wadogo, kwa nyumbani kwake, hatumii zaidi ya *unit 50*, ana feni, ana taa na kadhalika. Tunasema hivi, kuna wale Watanzania wa kat, amba nyumbani kwake ana *AC* nne, ana friji tano, yeye usipompunguzia umeme, anao uwezo wa kulipa hii nyongeza ya umeme. Kwa hiyo, kama sasa hivi analipa kwa *unit 157/=*, sasa hivi aliipe labda 190/=, ana uwezo huo. Kwa hiyo, achangie kwenye ile gharama ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisha tukasema wale kule viwandani, wanapozalisha sasa hivi, kuna wengine wamefunga kabisa uzalishaji, wale wanaozalisha kwa kutumia majenereta, sasa ule uzalishaji wenye, kile anachozalisha kwa maana hiyo tayari kina gharama kubwa zaidi kinapokwenda sokoni. Kwa hiyo, wanachosema *CTI*, ndio alichosema Mheshimiwa Waziri, *CTI* wamesema kama mtatuhakikisha umeme wa uhakika, tukaondokana na utegemezi wa haya majenereta yanayopiga kelele, gharama hiyo ongezeni kidogo sisi tutafidia kwa sababu, itawapa unafuu wa kuzalisha, kwa hiyo, unafuu huo kwanza kule kwenye *tariff*, lakin pili hapa kwenye uzalishaji ndio utakuwa *passed over* Watanzania wote wa kima cha chini na wale *middle income economy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani hii ya gharama kubwa na usalama wa mafuta na ufisadi wa uongozi, mimi napata tabu kidogo! Labda niseme tu kwamba, mafuta yote haya, tungesafirishaje kwenda Arusha na Dodoma na wapi, tayari tunajua kwamba, hata sasa hivi *GGM* wanasaferisha mafuta kutoka Dar-es-Salaam kupeleka kule, sasa ni utaratibu amba upo mafuta yanakwenda Kigoma, mafuta yanakwenda Mpanda kwa magari, mafuta yanakwenda Songea mpaka Rwanda na wapi, kote yanakwenda na magari!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nachosema ni kwamba, tuaminiane na utaratibu wa mafuta haya huwezi kuiba kwa sababu, wewe unachukua mafuta unaenda kuzalisha umeme *Megawatt 100*, unazalisha *megawatt 20*, tutakuuliza mafuta ya kuzalisha *megawatt 80* umepeleka wapi? Kwa hiyo, mimi naomba tu kuhakikisha kwamba, sisi wenye, tumejipanga kusimamia zoezi hili kwa nguvu zetu zote. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi nachokifanya ni kuongeza zile dakika zangu 30, katika dakika zangu 30, mkumbuke ikifika kasoro 10 ya hizo, tunaingia kwenye *Guillotine*, ni bahati mbaya.

Mheshimiwa Ndassa, aah, Mheshimiwa Chiku, nilifikiri ilikuwa ni maelezo tu hivi, haya.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la ukali wa maisha ni tatizo kubwa sana ambalo linasababishwa na umeme. Tatizo hili lingeweza kuwa na suluhu kwa kuturahisishia pia maisha ya Watanzania kama kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo ndio ilikuwa hasa *solution*, kwa sababu huwezi kutatua tatizo wakati uleule unaishi maisha yaleyale ya kawaida. Hata katika familia kama mna malengo mazito yanayowakabili mnajibana, kama mlikuwa mnaishi kwa anasa kidogo, mnajibana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitupa ahadi nzuri ambayo ilisababisha tukaamini tatizo hili la umeme lingetatuliwa bila kuleta madhara makubwa ya gharama. Sasa iweje leo badala ya kung'ang'ania kauli ya Kiongozi Mkuu, Waziri Mkuu, ambaye ni Sauti ya Serikali, ambaye aliletta matumaini makubwa sana kwa Watanzania kwamba, sasa Serikali imeangalia hata namna ya kujibana ili iweze kuleta nafuu kwa maisha ya Watanzania, sasa leo tena wanakuja kupewa huu mkakati ambao tunahitaji huruma tu ya kupunguziwa na wenye viwanda, hatuna hakika nao maana nao wakija kufanya mahesabu baadaye wanawenza kukataa kwamba hatuwezi kuendelea kufanya kazi ya hasara! Tunawaambia nini Watanzania na ukali wa maisha huu, pamoja na matatizo yanayosabishwa na umeme? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nareje tena. Sidhani kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema kwamba huu umeme utatolewa bure au kadhalika, sidhani! Nachosema ni kwamba, katika mfumo tulikuwanao sasa hivi, ukosefu wa umeme, kila *unit* moja inapotea dola 1.1 na ndio maana *analysis* ile ya Mheshimiwa January Makamba ilikuwa inasema pamoja na kwamba umeme huu ni ghali, kutokuwanao huu umeme ni gharama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema tumejipanga ili gharama hii ya mafuta iliyozidi sana kwa sababu ya kutumia mafuta isiendelee kwa kipindi cha miezi 18, 24! Tumekusudia na tumesema Mpango wa umeme wa Dharura kutoka Songosongo, Somanga mpaka Dar-es-Salaam ukamilike ndani ya miezi 12 ili majenereta haya ambayo yamenunuliwa kwa mfumo wa kwamba yatumike baina ya gesi na mafuta, yaweze kufanya kazi kwa gesi ndani ya miezi 12 ijayo. Kwa maana hiyo, ile hofu yote tuliyokuanayo ya gharama za ziada katika uzalishaji, itashuka kwa sababu kama tulivyosema, gesi ni zaidi ya 60% pungufu kwa gharama hiyo. Kwa hiyo, nakushukuru Mheshimiwa lakini naomba kusitisiza kwamba, tumejipanga na huo ndio mwelekeo wetu. Tunaomba tushirikiane ili tufike hapo tunapotaka kufika.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii lakini naomba na mimi nianze kwa kuipongeza sana Serikali, kwa kuleta mpango huu na tukijipanga vizuri, tunaweza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri asubuhi ulisoma dua lakini dua hiyo naomba niinukuu baadhi ya maneno, *"Utuongezee hekima na busara, sisi Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utupe uwezo wa kujadili kwa dhati mambo yatakayotolewa mbele yetu leo, ili tufanye uamuzi sahihi wenyewe manufaa kwa watu wote na ustawi wa nchi yetu."* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya uliyasema asubuhi na kweli tunajadili suala hili kwa manufaa na ustawi wa nchi yetu. Niombe sana ndugu zangu, upande wa pilii, kama kweli haya tumesali asubuhi na wote tukaitikia, *Amina*, nitashangaa endapo Waziri mhusika au Mheshimiwa Mwenyekiti, atakapopanda pale kutuhoji wengine waseme '*Hapana*' Nitashangaa! Hili ni letu sote, naomba sana Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wenzangu wote, kwa dhati kabisa tukubali mpango ulioletwa na Serikali yetu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote iliyokaa kuleta mpango huu. Naomba tuendelee na utaratibu huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana kama utaridhia Kamati ya Nishati na Madini, ikiwezekana kwa kuridhia kwako, kila tunapokutana kila Mkutano wa Bunge, kwa mfano sasa hivi, labda inaweza ikawa mwezi wa 11 au wa 12 au Januari, Kamati hii ya Nishati na Madini, iwe inatuletea Taarifa ya yale yaliyoteklezwa, yanayoendelea, ili tuweze kujua nini kinaendelea kwenye umeme. Tukifanya hivyo kwa sababu Mikutano mingine mbali na huu wa bajeti tunajadili bajeti lakini Mkutano ujao mingi ni Miswada, suala la umeme si ajabu tusilijue lakini kama tutai-task Kamati ya Nishati na Madini kutuletea Taarifa katika kila Mkutano, tutakuwa tunajua mwendelezo wa shughuli zinazoendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu jana wakati anajibu swal langu la umeme kupeleka Talo mpaka Marigisu, Nyashana, Kadashi mpaka Kabilia Centre, alisema ataniambia na wananchi wa Marigisu, Ibindo, Kadashi, Kabilia Centre, wanasikiliza sasa nataka nipaye maelezo, ni lini umeme wa eneo hilo utapelekwa kupitia REA? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Haya, labda nilikosea kusali asubuhi! Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli jana wakati tunazungumza tulizungumzia mradi huu, hii miradi iko pande mbili, kuna huu ambao anauzungumzia Mheshimiwa Ndassa ambao unaanzia kwake pale unakwenda mpaka Kabilia Centre, unapita pale Idindo, Marigisu, Kadashi, Nyashana na maeneo yale. Mradi huu umefanyiwa tathmini, ni mradi sio mrefu sana ni mradi wa kilometra kama 36, 37, lakini unapita kwenye maeneo mengi na una kazi kubwa ya usambazaji na kushusha *transformer* na nini. Umekadiriwa kama una shilingi bilioni tatu hivi. Kwa upande wa pili kuunganika na huo mradi kuna huu mradi wa Magu, kule kwa Mheshimiwa Festus Limbu, kutoka Magu kule kuja mpaka Kabilia Centre na huo nao una shilingi bilioni tatu, lakini huu mwingine una vijiji vinne. Kwa hiyo, kwa ujumla ukitekeleza miradi yote hii miwili ni kama shilingi bilioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kuipakia yote REA, imekuwa ngumu kidogo lakini tutakachofanya, namwomba Mheshimiwa Ndassa, kama nilivyochukua ahadi kwakwe tukaenda Ngudu mpaka Malya, Lioma kule, tukasimamia na ile miradi imekwisha, basi na hili tutafanya; tufanye kwa awamu. Kama tulivyofanya kutoka Ngudu kwenda Lioma baadaye tukaenda Malya na hii miradi ifanywe kwa awamu ili ipate utekelezaji lakini kuji-*committ* kwa shilingi bilioni sita kwa miradi miwili inayounganika, kwa muda huu kidogo inaweza ikawa *unrealistic*. Nia ya kukamilisha mradi kama tulivyosema jana iko palepale na tunataraja tuanje kwa awamu mwaka huu wa fedha.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Mimi nitatumia muda mfupi sana kumuuliza Waziri, maswali yafuatayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Waziri, pamoja na pongezi nyingi sana ulizopewa na mimi nakupongeza lakini vilevile naomba unijibu maswali haya. Moja, ni ahadi zilizotolewa na Mwekezaji katika Mgodi wa Nyamongo, zitatekelezwa lini? Namba mbili, Mgodi wa *North Mara*, walituhahidi kwamba, watatujengea barabara ya lami ya kilometra 53, naomba Mheshimiwa Waziri, kupitia Wizara yako, mutie nguvu pale waweeze kutekeleza ahadi ile. Namba tatu, fidia halali kwa waathirika wa maji ya Mto Tigite, Waziri unasema nini kuhusiana na hilo? Namba nne, mradi wa umeme...

MWENYEKITI: Mmh! Yanakuwa ni matatu tu, mawili tena! Pamoja na dakika zako, Mheshimiwa naomba ujibu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Chacha Nyambari Nyangwine, kwa jinsi ambavyo ameuliza swal lake, ni swal la msingi sana. Kimsingi, tulitakiwa tulitolee ufanuzi mwanzoni kabisa kwa sababu nafahamu eneo la Nyamongo ni kati ya maeneo ambayo yamevuta hisia kali. Tunafahamu historia ya mahusiano ya wawekezaji na wananchi kule lakini kikubwa ambacho nilitaka nimuahidi Mheshimiwa Nyangwine, ni kwamba ahadi ambazo zimetolewa na Mwekezaji na kwa kweli hizi zimetolewa kwa kuishirikisha Serikali, chini ya uratibu wa Serikali pamoja na wananchi kwa ujumla, zitatekelezwa kama tulivyokubaliana. Unakumbuka Mheshimiwa Nyangwine, kumekuwa na mawasiliano kati ya

Serikali, kupitia Wizara yetu lakini pia Wizara ya Mambo ya Ndani, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na hata Vijiji ambavyo vinazunguka Mgodi huu. Tumejipanga kusimamia kwa dhati utekelezaji wa ahadi ambazo zimefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe kama anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata zile ahadi za mwanzo kwa mfano ile 1% iliyokuwa inapaswa itolewe kwenye vijiji ambavyo vinazunguka mgodi, ilikuwa inatolewa lakini bahati mbaya Viongozi wale hawakuwa wanaziflisha kwa wananchi. Sasa utaratibu tuliookujanao ni wa kuwashirikisha wananchi na Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kushirikiana Vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la fidia, tumejibu swalii hivi karibuni, tukasema taarifa inayoshughulikiwa na Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais kupitia Waziri anayehusika na Mazingira itakapokuwa imekamilika kama itakuwa taarifa ambayo inaelekeza ama ina-*justify* hiki ambacho amekiulizia, Serikali haitakwepa wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kutumia nafasi hii kusema ule mradi wa kuwasaidia wachimbaji wadogo katika eneo la Nyamongo, katika Wilaya ya Tarime, mradi ule ambao thamani yake ni Dola za Kimarekani milioni tatu, utatekelezwa ndani ya mwaka huu na kama unavyofahamu, uratibu wa shughuli hiyo umeshaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu niunganishe hapa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mdau kutoka katika Wilaya hiyo. Tatizo alilonalo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hawezikusimama hapa akakamata kifungu...

MWENYEKITI: Aaah! Sasa anaingiaje, hakusimama!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Lakini ana ombi kwa wananchi wake ndiyo maana nikasema...

MWENYEKITI: *Please,* Mheshimiwa Waziri nimesema hapana. Waheshimiwa Wabunge yaani nasikitika sana, cha kufanya sina, hata ningetamani na sasa tumejifunza kwamba utaratibu wetu ule wa Kanuni kwa kundi hili haiwezekani, kwa hiyo, tarehe 15 tunarudi kwenye utaratibu wetu ule, tungkuwa tumetumia utaratibu ule wote nyie mngepata nafasi lakini sasa asilimia kubwa hawajapata nafasi kwa sababu wengi wamemsingizia Waziri Mkuu kwa mambo ambayo sijui alisema au hakusema, naomba ujaribu kujitetea sasa hivi kwa dakika kumi tu. Naomba usogee mbele Mheshimiwa. Naomba usogee pale, ndiyoo! Ndiyo uliposemea hapo, kwa hiyo naomba umalizie hapo. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii angalau na mimi niweze kusema mawili, matatu. La kwanza, nataka nikushukuru wewe kwa kukubali pamoja na Kamati yako ya Uongozi kutoa fursa mimi nadhani nzuri, kubwa ambayo imewawezesha Waheshimiwa Wabunge wengi kuweza kuchangia vizuri na kushauri, kwa maoni yangu vizuri sana, kwa hiyo kwa hili kwa kweli nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake, wamejitätidi sana katika kujaribu kutoa ufanuzi wa maeneo mbalimbali, hawawezi kuyamaliza yote, lakini napenda niamini kwamba kwa mambo ya msingi wamejitätidi sana. Kwa hiyo, nawapongezeni sana kwa kazi hiyo nzuri mliyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jumla niwashukuru Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo kwa kweli mimi mmenipa faraja sana kwamba katika mambo makubwa haya mawazo yetu yamefanana. Ni imani yangu kwamba mwenendo huu tukienda nao nadhani utatusaidia sana kuimarisha Bunge hili kwa kadri ambavyo mimi nimeona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu yafutayo, kwanza, yako mawazo au ushauri wa kisera ambao umetoka kwa baadhi ya Wabunge na moja ni hili la kugawa Wizara kutokana na majukumu yake mengi. Mie nafikiri ni jambo zuri. Wote tunajua uzito wa madini na uzito wa nishati na kwa kweli vyote vinahitaji usimamizi wa karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili liko chini ya mamlaka ya Rais lakini washauri wake ni sisi na Baraza lake. Mimi nimewasiliza kwa uangalifu mkubwa, nadhani ni jambo jema, wacha tulibebe, tutamkabidhi Bwana Mkubwa kwamba haya ni mawazo mazuri yaliyotoka ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko vilevile la muundo wa *TANESCO*, wako wengine wamezungumza *aspect* ya *unbundling* ya *TANESCO* kwa maana ya uzalishaji, ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya usafirishaji wa umeme pamoja na *distribution*. Nadhani rai iliyotoka ni nzuri na si vibaya kwa Serikali kulitazama kwamba jambo jema kama hili tufanyeje ili pengeni tuweze kuongeza ufanisi kwenye chombo hiki ambacho ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengine kadhaa ambayo vilevile yamejitokeza hapa ya kisera, kubwa mimi nadhani tuyapokee, tutajaribu kuyazingatia na muda unavyokwenda tutaweza kuona matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni la gharama za umeme hususan kwa Mpango huu wa Dharura. Ni kweli una gharama kubwa, lakini sisi tuliliangalia eneo lote la gharama, tukafikiri vilevile kwamba ni lazima tukumbushane unapopima gharama hizi tunazoiangalia muangalie na gharama ambazo zinatokana na kuwepo kwa mgao wa umeme. Mwanzioni mwa mwaka huu mwezi Februari, kama mtakumbuka *TRA* waliwahi kutoa angalizo kwamba kwa namna mgao sasa wa umeme ulivyo, *TRA* ingepoteza mapato ndani ya miezi sita, kwa kiwango cha shilingi bilioni 840, kiasi hiki ni kikubwa mno! Kwa hiyo, lazima upime ama uache, ama utafute njia hata kama itaonekana kimtaalamo ina gharama kubwa lakini uondoe hii hali ambayo athari zake ni kubwa zaidi na huyo alikuwa ni *TRA* anazungumzia upande wake wa makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati uleule *CTI*, walituambia tayari viwanda 50 vilikuwa vimefungwa, acha sasa bugudha na kero kwa Watanzania, jambo ambalo hamwezi mkaliacha likaendelea kusemwa. Kwa hiyo nadhani gharama hizi ni za dharti. *TANESCO* nao vilevile kwa kukosa kuingiza umeme katika uchumi, wao wamepoteza karibu shilingi bilioni 466 kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba ni lazima tupime haya yote na mimi nadhani *trust* tuliyokuja nayo kwa kuzingatia hali halisi tumeona ni bora tuwe na umeme huu hata kama itaonekana pale kuna bilioni 400 na kitu ambazo itabidi tuzibewe kwa maana ya uendeshaji wa shughuli zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimeona niliseme hili kwa sababu wengine wamelisema na nilijaribu kueleza kwa namna mbalimbali tumekubali mzigo upo, lakini tusipofanya hivi mzigo ni mkubwa zaidi. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge, Serikali itajipanga vizuri, tutaona yale mawazo ya namna ya kupunguza gharama na hasa kwa kuzingatia ushauri mpana wa kwenda katika matumizi ya gesi na zaidi ya mkaa wa mawe kwa sababu zote ni rasilimali tulizonazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili la ahadi za Waziri Mkuu, tulipokuwa tumeombwa tufikirie jambo hili mimi niliseme kwa niaba ya Serikali tutajitahidi kuona kila litakaloonekana, tuje na mpango lakini mpango ambaa utazingatia vilevile kidogo *sacrifice* kwa upande wa Serikali. Sasa tulipotoka si kwamba tulikaa tu, tumeliangalia sana, tumekaa, tuliunda timu maalum, Katibu Mkuu Kiongozi alikuwa ndiye kiongozi, kujaribu kuititia vyanzo vyetu kwa namna moja au nyingine tuone ni namna gani tunaweza tukasaidiana katika mzigo huu na kazi ile ilikuwa ni nzuri lakini liliobainika tu la wazi maana mimi nilikuwa nimekodolea macho yangu kwelikweli kwenye magari, nikaambiwa mwaka huu hatukutenga fedha kwa ajili ya magari kwenye maeneo mengi tu. Kwa hiyo, eneo lile nikawa sina mahali pa kushika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa la pili, ikawa ni kwamba angalieni basi hata na hivyo vipocho vilivyopo lakini baada ya kupima suala hili la mafuta na namna tukavyosaidiana kubeba mzigo, tukasema hivi posho hizi pamoja na maeneo mengine pengine tuviweke akiba hasa kwa sababu kusaidia kutua mzigo upande wa *TANESCO* kwa kuwa atahitaji msaada wa Serikali muda wote. Kwa hiyo, tulijaribu kulitazama lakini tukaona tu liingizwe katika maeneo kama haya kwa kuwa kwa upande mwingine chombo chetu cha Serikali *NSSF*, tayari kilikwishakujitoa kwamba kina uwezo wa kuweza kuchangia *megawatt* 150. Mimi nataka niwapongeze sana, chombo hiki

kimefanya kazi nzuri, kimesaidia kutua mzigo na mimi naamini huko tunakokwenda, vyombo vingine vitaiga vilevile tuweze kutumia jambo hili kwa nguvu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, yako mambo mawili yamesemwa, moja wana sema sasa Serikali dharura hizi ziwe mwisho na mimi nasema tutajitahidi. Dharura hizi ni matokeo ya historia ya muda mrefu, lakini zaidi ilikuwa ni kutegemea mno kitu kinaitwa maji yatokanayo na mvua, sasa wote tumejifunza na mimi ninahakika hata ndugu yangu Mheshimiwa January Makamba pale asingependa tukarudi huko. Sisi kama Serikali tutashirikiana, Bunge, Watanzania kwa ujumla, *private sector in particular* kuhakikisha kwamba jambo hili linakuwa ni letu sisi wote na tuhakikishe kwamba kama Taifa basi tunaondokana na mwelekeo huu wa umeme ambao kwa kweli hauna tija, si wa kutegemea kiu hakika kwa maana ya chanzo cha maji, tukiondoka huko tukaingia katika hatua hizi zinazopendekezwa, mimi naamini jambo hili litakwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nikuhakikishieni tu kwamba tutajitahidi, tutashirikiana na ninyi kwa kadri tutakavyoweza, mmetuasa tuhakikishe Wizara hii ya Nishati na Madini wanapewa fedha yao yote kwa kadri itakavyowezekana, ni jambo jema na mimi nakubali na rai yangu ni kwamba wala si Nishati tu ni Wizara zote. Msingi wake itakuwa ni kama *TRA* wataweza kukusanya mapato yote na hivyo kuweza kuyaingiza katika huduma za uendeshaji wa shughuli za Serikali. Athari mojawapo ambayo inaweza ikasababisha hilo lisifanyike ni kukosekana kwa umeme, kwa hiyo, tukiwa na umeme *TRA* atakusanya mapato yanaweza kurudi Serikali na tukayatumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kurejea kukushukuru tena na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri, michango ambayo imesaidia kujenga na mimi nina hakika tukifanya kazi kwa namna hii hapa tulipo, tutatoka vizuri bila matatizo makubwa. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Tsh.1,419,987,300/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Tsh.1,095,885,000/=
Kif. 1004 - <i>Internal Audit Unit</i>	Tsh.525,367,300/=
Kif. 1005 - <i>Legal Services</i>	Tsh2,882,616,800/=
Kif. 1006 - <i>Information, Education and Communication</i>	Tsh.647,990,800/=
Kif. 1007 - <i>Procurement Management Unit</i>	Tsh.537,134,500/=
Kif. 1008 - <i>Environment Management Unit</i>	Tsh.430,026,200/=
Kif. 1009 - <i>Management Information System</i>	Tsh. 405,515,100/=
Kif. 2001 - <i>Minerals</i>	Tshs.15,611,694,000/=
Kif. 2002 - <i>Madini Institute</i>	Tshs.1,579,268,700/=
Kif. 2003 - <i>Research and Laboratory Services</i>	Tsh.0/=
Kif. 2004 - <i>Tanzania Diamond Sorting Agency (TANSORT)</i>	Tsh.1,086,389,500/=
Kif. 2005 - <i>Eastern Zone</i>	Tsh.1,113,127,400/=
Kif. 2006 - <i>Western Zone</i>	Tsh.872,587,200/=
Kif. 2007- <i>Lake Zone</i>	Tsh.983,258,200/=
Kif. 2008 - <i>Northern Zone</i>	Tsh.981,893,500/=
Kif. 2009 - <i>Southern Zone</i>	Tsh.932,135,300/=
Kif. 2010- <i>Central Western Zone</i>	Tsh.963,553,500/=
Kif. 2011 - <i>Central Zone</i>	Tsh.954,329,100/=
Kif. 2012 - <i>Southern Western Zone</i>	Tsh.917,934,600/=
Kif. 3001- <i>Energy and Petroleum</i>	Tsh.39,052,936,500/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila mabadiliko yoyote*)

MATUMIZI YA MAENDELEO

Kif. 1001 - *Administration and General*..... Tshs. 0

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake*)

Kif. 1003 - *Policy and Planning* Tsh.980,000,000/=
Kif. 1008 - *Environment Management Unit*.... Tsh.1,651,106,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2001 - *Minerals*.....Tsh.16,272,870,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake*)

Kif. 2002 - *Madini Institute*.....Tsh.1,350,000,000/=
Kif. 2003 - *Research and Laboratory Services*...Tsh.1,200,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 3001 - *Energy and Petroleum*....Tsh.303,994,161,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake*)

(*Bunge lilitrudia*)

SPIKA: Mheshimiwa mtoha hoja taarifa!

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge Walipiga Makofi*)

TAARIFA

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Mkadirio ya Mtumizi ya Fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2011/2012 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na mabadiliko yake. Hivyo basi, naliomba Bunge lako liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012
yalipitishwa na Bunge*)

(*Hapa Wabunge Walishangilia kwa Makofi na Vigelegele*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hatimaye Wizara ya Nishati na Madini tumepitisha hesabu zake na kama mlivyosema nadhani mmesema kwa vitendo. Katika historia ya Bunge hili, nafikiri mimi ni mmojawapo niliyekaa sana, sikumbuki kitu cha namna hii, shilingi ilikuwa inatoka lakini Wizara nzima kwamba mkakae kwanza, ni mara ya kwanza. Kwa hiyo, tumeputa mafunzo mengi sana, Serikali yenye, sisi tunasema Serikali yenye jamani fanyeni kazi zenu, kama mtafanya nusunusu haya yatawapata na wengine na si jambo ambalo linapendeza na nyie mnafahamu, wanaotafuta Uwaziri hapa wapo wengi, mnajua kwa vilemba, Waarabu wa Pemba. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, fanyeni kazi ili wananchi waweze kuiona kwamba ni kazi iliyosahihi na *transparency*. Mimi nadhani tatizo kubwa hapa ni *transparency*. Mjithabidi sana, haya mliyoahidi ni makubwa, mazito, matumiani ya Watanzania ni makubwa sana kwa suala hili. Kwa hiyo, napenda sana kwa kweli muweze kuonekana na nyie kwamba mnawenza kusema kitu kinachotekelze, msimamie wakati wote.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kwamba Waziri Mkuu atakuwa na shughuli, kuna uzinduzi wa ujenzi wa nyumba ambao unafanywa na Shirika letu la Nyumba, ni vizuri mkahudhuria kwa sababu na sisi ndiyo hao tunataka watusaidie kujenga *Bunge Village*. Kwa hiyo, ni vizuri mkafika kule Medeli ambako uzinduzi wa mradi wa nyumba wa Shirika hilo utafanyika. Kwa hiyo, nadhani mkitoka hapa sijui kutakuwa na mabasi au usafiri na nadhani kuna mtu atawaonyesha mimi mwenyewe sijui huko Medeli ni wapi, kwa hiyo muende mkashiriki.

Halafu pia niliwatangazia wageni wetu wanaohusika na mambo ya habari kutoka Kampuni ya *Made in Africa TV*, ile inayotangaza habari ya daladala, kiongozi wake Christina Mbunda ambaye mnawita Kiboroto, yuko wapi, yule pale, maarufu Kiroboto. Mheshimiwa kipindi chako ni kizuri sana, kinatoa elimu nzuri sana na Ndugu yako Daniel Kijo, ahsante, kumbe ndiyo ninyi, basi tumefurahi kuwaoneni, mtawaona nje mtakapotoka. (*Kicheko/Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo la msiba, jana wakati Mheshimiwa Balozi wa Marekani alipofika ofisini kwangu, huyu Afisa aliyeongozana naye alinieleza habari ya ugonjwa wa Mheshimiwa Balozi Nh'igula ambaye aliwahi kuwa Naibu Spika katika Bunge letu na aliniambia kwa kweli alikuwa na hali mbaya na amelazwa, tukadhani anaendelea na matibabu lakini hivi sasa navyosoma hapa Mheshimiwa Balozi Nh'igula amefariki. Tulikuwa naye, alikuwa Naibu Spika, mambo mengine ndio na mimi nayaona sasa hivi, kwa hiyo, mengine tutayaangalia huko tutakapokwenda, naomba tusimame kwa dakika moja tumkumbuke.

(*Hapa Wabunge walismama kwa dakika moja kumuombea
Marehemu Mheshimiwa Balozi Nh'igula*)

SPIKA: Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo niliyosema, kama nilivyosema kesho tutakuwa na shughuli ile ya kusikiliza mpango kampeni ya *IGP* kuhusu kutii sheria kwa hiari ili kuweza kupata amani na utulivu katika nchi. Kwa hiyo, tutaanza saa nne na nusu pale katika ukumbi wa Msekwa na mengine yataendelea.

Sina matangazo mengine, nawashukuru sana kwa uvumilivu wenu na nawaombeni radhi sana wale ambao hawakuweza kufikiwa, tutaangalia tena, utaratibu wetu huu haufai kabisa. Kwa hiyo, naahirisha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 8.10 mchana Bunge lillahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,
Tarehe 15 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi*)